ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 21 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya
Wizara ya Afya kwa mwaka 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa majadiliano yanaendelea na michango inaendelea. Jana alibakisha dakika tano Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Jaku amalizie dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana lakini zilikuwa siyo dakika tano, niliposema mapema kama hasa zilikuwa sawa zimebaki kama dakika saba na mbili zilikuwa za kulia kama dakika tisa. (*Kicheko*)

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe naomba munisikilize kwa makini sana maneno ninayozungumza haya. Leo ninataka kutoa darsa.

Waheshimiwa Wajumbe naomba munisikilize kwa makini. Haya si maneno yangu ni maneno ya Mhe. Spika aliyekuwepo kipindi hicho, alitupa tarehe 19 Oktoba, 2012 tujue wajibu wetu Waheshimiwa, lakini kabla ya kuwahoji ninataka niseme maneno yafuatayo.

"Waheshimiwa Wajumbe ninataka niwasihi sana kwamba chombo hichi ndicho kinachotoa uongozi wa nchi, Baraza la Wawakilishi, hichi ni chombo cha wananchi, na wananchi tunawawakilisha sisi kufanya shughuli kwa ajili yao na mamlaka hasa ni yao". Si maneno yangu haya. Huu ni wasia mzito aliotupa Mhe. Spika. Ninaendelea. (*Makofi*)

"Sisi uheshimiwa wetu tunaitwa umetokana na wananchi kwa kukubali Katiba hii, ndiyo tukaitwa Waheshimiwa Wajumbe. Tumeitwa Waheshimiwa Wajumbe kwa ajili hiyo, wananchi wameamua kutuchagua, nendeni huko

mukatuzungumzie masuala yetu. Naomba nirudie tena, wananchi wameamua kutuchagua nendeni huko mukatuzungumzie masuala yetu. Kwa hivyo itakapofika pahala kama hatutimizi wajibu wetu, ninarudia yale maneno ambayo tunasema humu Barazani kwamba tutakwenda kuulizwa mbele ya siku".

Waheshimiwa Wajumbe maneno haya kila mtu ajue mwenyewe kwamba ipo siku tutakwenda kuulizwa namna gani tumetimiza wajibu wetu katika kutengeneza maisha ya wananchi. Hatukufanya hivyo basi. Tutakubaliana Mhe. Mwenyekiti, haya ni maneno na darsa alilotupa Mhe. Spika aliyepita.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia mchango wangu haraka haraka nije na *X-ray department*.

Nilizungumza jana lakini bado kitengo kile serikali lazima ijikubalishe. Ni kitengo muhimu, huwezi kwenda pale ukatibiwa bila ya kufanyiwa uchunguzi. Serikali imeshindwa kutoa shilingi milioni mia nne (400) toka mwaka jana suala hili tumelizungumza humu ndani, lakini mpaka leo hii hakuna utekelezaji. Sijui tuseme kama dharau au tuseme kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, na pale Waheshimiwa tunaokwenda sisi, ninafikiri hatwendi sisi wanaokwenda ni wanyonge hospitali ile. Sisi tukiumwa na mafua hatwendi pale, tukiumwa na kichwa hatwendi wanaoumia ni wanyonge. Serikali iji-*commit* suala hili na siyo masihara. *X-ray* imeshindikana kwa suala sijui, hili haliwezekani.

Leo dawa hamna. Chanjo ya dawa ya mtoto akazaliwa ni mtihani. Mwenyezi Mungu tuendelee kumshukuru vile vile tusaidie na Ramadhani hii kutuponesha na maradhi ya pale hospitali, lakini kwa kweli kama si Mwenyezi Mungu ni mtihani mkubwa kwa hospitali ile. Mambo mazito haya.

Mhe. Mwenyekiti, nije na wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi. Hapa serikali iwe makini kabisa. Hata ninafikiri kuna *query* ya *CAG* hapajapatikana wagonjwa wanapelekwa nje ya nchi. Serikali iandae utaratibu makini. Sijui kuna njia gani ya kuweza kupata kwenda kule. Lakini tafuta utaratibu wa kuleta madaktari wa kutibu. Wakakodi kule wakaneemeka mengi. Serikali iwe na utaratibu makini. Haiwezekani kufanya utaratibu kama huu kwa Mhe. Mohammedraza apate mtoto wangu asipate. Wanaoumia ni wanyonge na pale ni kimbilio la wanyonge ndiyo maana nikawa napiga kelele. Suala la *X-ray* na suala la bajeti ndogo. Mhe. Mwenyekiti, suala hili tuwe makini sana.

Bado ninarudia wimbo ule ule, ninarudia tena wimbo ule Hospitali ya Mnazi Mmoja haijafika kuwa Hospitali ya Rufaa. Musitudanganye Waheshimiwa humu ndani. Huu ni wimbo wa muda mrefu. Hata mkwezi wa minazi kupiga kelele kama hizi lakini hatujafika.

Hospitali ya Mnazi Mmoja leo jenereta haina. Mtu anayekwenda kuzalishwa anachangia, humchukui mtoto wako anakuja kutiwa chupa ya JIK, kama hujapeleka sehemu hujapeleka *drip* huwezi kuzaa.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya *maternity, oxygen* ni mtihani. Dawa hazipo hatuwezi kufika. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ukurasa wa H 17 jiandae na *seven point five* pia tunazihamisha. Wajumbe hili ninakusisitizeni tusaidiane si langu. Bilioni 7.5 tuzigawe, tupeleke kwenye *X-ray machine* na tupeleke kwenye dawa. Mimi hivi sasa jimboni kwangu nina dawa karibu milioni saba za dawa za wananchi. Hatuwezi kufika hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije na suala jengine. Tulizungumza miaka mitatu minne humu ndani suala la banda la wagonjwa jamani. Hii ni dharau Wizara ya Afya munafanya, wala musibishe, nilikuwemo ndani humu, kama hamkuweza kujenga mimi nitatafuta watu nilijenge lile banda. Watu wanaokwenda wanakwenda kwa shida, pale hapapikwi pilau wala biriani wala sadaka haitolewi pale. Mtu anakaa chini, analia kulala chini. Hii ni dharau Wizara ya Afya munayofanya. Banda lile miaka mingapi ninazungumza imekuwa kama ni wimbo wa taifa. Hapa ndipo palipokuwa na majipu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kama imeshindwa kujenga banda, tulizungumza na *hansard* zipo, tukabidhiwe lile eneo. Siku zote libakie hivi hivi. Hii ni dharau. Kama ni dharau twende. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru kwa dhati rafiki zetu wa kweli watu wa China kwa kutusaidia kwa hali na mali. Tunashukuru sana na vile vile nimpongeze mwenyekiti wa Kamati Mhe. Dkt. Mwinyihaji Mwadini Makame, kama kuna mtu aliyefanya kazi katika mazingira magumu basi ni Mhe. Dkt. Mwinyihaji, mimi nimepishana naye anaziba viraka lakini vitazibika wapi, akiziba mia mbili imezibuka, imekuwa kama njia ya Makunduchi zamani. Unaziba mbele ukirudi nyuma tayari imeshazibuka. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Mwenyezi Mungu atakulipa kwa wema wako uliofanya, usitegemee malipo kwa mtu, malipo kwa Mwenyezi Mungu. Na hii ndiyo faida ya kukaa *backbencher* anaiona sasa Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tumefanya kazi kubwa maana yake na malipo tutegemee kwa Mwenyezi Mungu na siyo kwa binadamu. Mimi nimekutana naye huyu. Jumamosi na Jumapili anafanya kazi. Sasa ndiyo uchungu anavyoona Mhe. Dkt. Mwinyihaji.

Vile vile nitoe masikitiko yangu kwangu lakini siwezi kumlaumu labda alikuwa akiiogopa serikali, bajeti hii ulikuwa uikatae mapema kama Mwenyekiti. Hii bajeti Mhe. Mwenyekiti, imekuwa kwenye hatari sana ni bajeti ndogo. Mtu mzima akilia ujue kuna jambo. Hatuwezi kufika hali kama hii tunayokwenda nayo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la Hospitali ya *Mental*. Mhe. Dkt. Mwinyihaji kalizungumza kwa uwazi kabisa. Twendeni kule tukaone Mwenyezi Mungu asije akatujalia sisi, tunaweza tukaupata ugonjwa ule na Mwenyezi Mungu atunusuru. Hali hairidhishi kule. Hukuingia sehemu ya wanawake kule Mhe. Dkt. Mwinyihaji ungekwenda ukalia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku malizia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Naomba kwa Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kama alivyofanya jitihada za kwenda kununua meli kwa heshima kabisa, ijapokuwa wasaidizi wake wapo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, yule wa BLM hivi sasa Mhe. Issa Haji Ussi sijui kama utazipeleka salamu, lakini ninafikiri na yeye mwenyewe anafuatilia.(*Makofi*)

Kwa makini kabisa niendelee kumshukuru kwa dhati pelekeni salamu amefanya kazi kubwa katika sekta ya afya ya Dkt. Ali Mohamed Shein. Hili ninazungumza tena kama jana nilivyozungumza katika nafsi yangu amefanya jitihada kubwa na wizara anaijua, amesaidia mambo ya wazazi, kujifungua bure, *ICU* kujengwa, anataka hata vipimo visichangishwe pale. Lakini havipo vipimo vyenyewe. Hatuwezi kufika namna kama hii. Ni mtihani mkubwa sana huu. Hatuwezi kufanya suala hili.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tuje suala la kipindupindu. Dkt.Dahoma kafanya kazi kubwa sana. Kila siku anatupa takwimu zikoje Dkt. Dahoma. Mimi nikupongeze sana lakini wasaidizi wako Manispaa siyo mimi ninakwambia. Dkt. Dahoma wasaidizi wako Manispaa siyo. Umefanya kazi kwa moyo mkunjufu kabisa lakini wasaidizi wako kuwa nao makini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe Jaku muda wako umemalizika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Ninasema tena sitounga hoja hii mkono wala kichwa wala mguu mpaka nitakapopata maelezo. Na Wajumbe ninakwambieni tena katika ukurasa wa H 17 tusaidiane, bilioni 7.5 hizi tuziondoe, tutakuja kuchekwa humu. Tunapitisha matapishi kwa mikono sisi hatuwezi wakati kazi tunazo. Hii tuiondoshe tuipeleke katika *X-ray machine* na Kitengo cha Dawa.(*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Anafuatia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Mohammedraza Hassanali ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahmaani Rahiim*. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima na sote kutujaalia wazima kufika hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ningekuomba sana nina mambo mengi ya kuzungumza ungenisaidia dakika *extra* kwa uwezo wako uliokuwa nao, ninakuomba sana.

Vile vile nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri na watendaji wake kwa ujumla. Ni watendaji wazuri kwa kuanzia. Lakini kwa nini nikasema hivyo kwa sababu hata mimi nilipokwenda kumuomba tu kwamba kuna matatizo ndani ya Jimbo langu la Chaani kuwa aje akague, basi hakusita na alifika na uongozi wake, tukakagua, tukatembea jimbo zima na utendaji wake wa kazi hata wananchi wangu wa Jimbo la Chaani wanampongeza sana yeye pamoja na wizara yake kwa hatua aliyoifanya ndani ya jimbo langu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mimi nitazungumzia masuala ya afya kwa ujumla na mambo mengine ya machache ya ushauri. Mimi nitaanza na suala la afya na nitaanza hasa na Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hii hospitali kwanza ni chuo maarufu cha kutengeneza ujeuri na matusi. Wewe ukitaka kusomea ujeuri na matusi basi kakae na madaktari na manesi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa nini nikasema hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwanza hasa sehemu ya kujifungua wanawake ni mtihani mtupu mule ndani, utafikiri tupo *mortuary*. Hospitali ile wale watendaji hawafai hata kuwa wafanyakazi kwa sababu mimi ninahisi wanaenda wagonjwa lakini wao wagonjwa zaidi kuliko wale wagonjwa wenyewe.

Mule ndani chumba cha kujifungulia, wale wanaojifungua wanawake kwa taarifa zilizokuwepo wanaachwa kama walivyozaliwa hakuna hata *cover* ya kufunikiwa, hakuna chochote, mashaka matupu na wanavyotendewa haki ilikuwa siyo ya kibinadamu. Hata huo uvunjifu wa haki za kibinadamu wanavunja. Wanawaacha kama walivyozaliwa mtu kajifungua. Na jambo la zaidi lililokuwepo pale sasa hivi kwa taarifa za wanawake wawili watatu kwamba kuna wanaume ndani ya chumba kile wanaingizwa ndani kuwashughulikia wale waliojifungua.

Mhe. Mwenyekiti, hii Mhe. Waziri huu ni mtihani mkubwa, na hii na wewe Mhe. Waziri, mimi Mwakilishi sikubali mke wangu kufanyiwa hivyo kuingiziwa wanaume kwenye chumba cha kuzalia. Hili suala kama lipo na linaendelea basi likomeshwe moja kwa moja, kwa sababu sisi hakuna Mheshimiwa hata mmoja atakayekubali mke wake aingiliwe na mwanamme ndani ya chumba cha kuzaliwa. Hospitali ya Mnazi Mmoja imefika hatua hiyo sasa hivi.

Kuna wanaume si chini ya watatu mpaka wanne wanaingia kwenye sehemu ya uzazi, wakati wale madaktari wenyewe wanawazuia waume zao wasiingie kuangalia wale waliojifungua, wanaambiwa wakae nje wakati mule ndani kuna wanaume madaktari wanawakagua wale wanawake, wakati hawana hata nguo za kufunikwa.

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe wakati wa kujifungua vifaa hakuna, hawapewi hata *cover*. Hivi kweli serikali na bajeti ngapi zimeshazipitisha hapa *billion of shillings*, kweli inashindwa kununua zile *cover* ambazo za kukoshwa mtu anavalishwa kwa kujistiri. Huu umekuwa ni mtihani mkubwa. Kile chumba kimekuwa maudhi, imekuwa watu wananyanyaswa mule ndani, wanatukanwa, wafanyakazi hawa ni ma-*experts* wa ujeuri wa kutukana. Wewe ukitaka kujifunza matusi hasa nenda Hospitali ya Mnazi Mmoja. Maana yake imekuwa siyo hospitali tena, imekuwa matusi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mhe. Waziri ningekuomba sana ufanye ziara ya kushitukiza, na hawa wanaume wanaoingia wanaume ndani ya chumba kile iwe mwanzo na mwisho, kwa sababu kwanza ni Waislamu.

Pili hili suala linakera, nani atakubali mke wake akaangaliwe na mwanamme. Tushafanyia watu wengine vitu kama hivi kama hakuna madaktari basi tutafute wanawake, lakini wanaume haina maana ya kuingia ndani ya chumba cha wazazi. Hili suala lipo na wazazi watatu wamenithibitishia, na mimi kwa ushahidi zaidi ningekuomba sana siku moja ungefanya kongomano kwenye

televisheni ukakaa *live*, wewe na daktari halafu ungeweka namba za simu upigiwe hizo simu uone matatizo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na matatizo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba Mhe. Waziri chumba kile wawekewe waja wazito zile nguo za kufunikwa. Sio mtu atafute au hamna mtu anaachwa kama alivyozaliwa. Huu ni uhuni, hata sijui niite ni maneno gani niyazungumze humu ndani. Huu ni udhalilishaji mkubwa tunaoufanya na tunajua. Leo mtu pale anafika hana fedha ya kujifungua elfu kumi au elfu tano, basi atakhiyari mtu afe mtoto mule ndani lakini ile fedha ilipwe.

Mimi ningeomba serikali mtu kaja pale hana uwezo ajifungue apewe vifaa lakini baada ya hapo waje wazee wake wamlipie. Lakini tusiweke masharti kama hujaja vifaa hivi hufunguliwi na anaweza akafa mtu. Hili suala linasababisha matatizo. Mgonjwa anasema mimi ninaumwa au hivi hasikilizwi. Sijui tatizo ni nini na ukiangalia hospitali hii ndiyo inayoongoza kwa mshahara mkubwa kuliko hiyo bajeti yenyewe. Maana yake mshahara wa wafanyakazi wa hospitali hii ni bilioni karibu saba, wakati matumizi yake ni bilioni tano na milioni mia sita.

Mhe. Mwenyekiti, sasa wafanyakazi hawa wanalipwa pesa nyingi, matumizi makubwa hospitali hii lakini wanaongoza kwa mambo ya udhalilishaji. Mimi ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mungewakagua na kufanya ziara na mungekamata baadhi ya wale watu wanaoumwa mukawauliza, nini wanafanywa. Hii hospitali ni mtihani kwa kweli.

Mhe.Mwenyekiti, vile vile mimi ningekwenda kwenye suala hilo hilo la jenereta lililozungumzwa kwenye kipindi cha nyuma. Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala mengine hasa kama jenereta liliharibika, sijui kama sasa hivi linafanya kazi au halifanyi kazi. Lakini vitu kama hivi vinatakiwa vichukuliwe hatua ya dharura. Kuna majenereta ndani ya Zanzibar, kwa nini lisiende likafunguliwa sehemu yoyote likapelekwa pale. Kuna majenereta yamekaa kule kumi na mbili, ijapokuwa yale ni ya nchi ni *standby*, lakini kwa nini lisifunguliwe moja kwa muda wa dharura watu wanafanyiwa operesheni likatumika.

Mhe. Mwenyekiti, yametumika mabilioni kwenye majenereta yale hayana maana hata kidogo, hayafanyi kazi, yamekaa tu pale. Kwa nini lisifunguliwe moja likapelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tunakaa tunasema jenereta tutanunua wakati majenereta yapo ndani ya Zanzibar yamekaa tu hayafanyi kazi. Tukipachua moja pale kuna tatizo gani kwa muda wa dharura mpaka likaja jengine.

Mimi ningeomba sana kuna vitu vyengine Mhe. Mwenyekiti, muchukue hatua kubwa za dharura, tusidharau. Hii ni bajeti. Mimi ninampongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub ile kulia anaonesha huruma na anawapenda sana wananchi sana, sisemi kama serikali haipendi lakini anaumia na haya masuala. Ule ni mtihani mkubwa kwenye Wizara ya Afya, bajeti ni ndogo na Mawizara mengine yamepita maajabu ajabu ma-*billion of shillings*, angalia *airport* bilioni nne na hamsini na saba karibu. Twende kwenye bandari vitu vingapi vinanunuliwa kwa mabilioni. Kwenye hospitali hapa maana yake hii bajeti haifai hata kujadiliwa kwenye Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri kabla hujapangiwa bajeti hii, kama Waziri usikubali wizara hii ikapangiwa bajeti hii wakati haitoshelezi, wakati ni kitu muhimu katika nchi kwa wananchi maskini. Kuna Waziri gani humu, kuna Mwakilishi gani humu anayekwenda kutibiwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mimi anitajie mmoja aliyekwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wote tutataka kwenda Dar es Salaam, kwenda India, kwenda Dubai, tunawaachilia watu wanyonge. Hizi hospitali zirekebishwe.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile suala la *DNA*. Hii mashine ya *DNA* inasikitisha sana, kwa sababu kwanza nitatoa mfano mmoja. Kwenye kitabu chako kinazungumza wanawake wanaobakwa, watoto wanaobakwa kitabu chako cha Mhe. Waziri wa Afya ni watoto 649, ukienda kitabu cha Mhe. Maudline Castico viangalieni kina wabakaji waliobakwa 497; hivi hii serikali hawa wanaoleta hizi hoja au vitabu hivi huwa wanabahatisha kuandika hii idadi au vipi, vitabu angalieni hapo mtaona, kwenye kitabu cha Waziri wa Afya watoto waliobakwa ni 649, kitabu cha Mhe. Maudline Castico, Waziri wa Wanawake na Watoto ni 497, na hii idadi pia ni uongo watoto wanaobakwa Unguja ni zaidi ya 1000 kwa mwaka, lakini tunabahatisha tu, *DNA* mashine hii ndiyo itakayoweza kumkamata mtu alobaka, lakini leo hakuna, pesa zinanunuliwa tu vitu vya ajabu ajabu, haiwekwi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri, hii mashine ina uzito gani haijaletwa mpaka leo, na kwa nini isiletwe wakati hii ndio inakamata watu waliobaka, watoto zaidi ya 1000 wanabakwa na hili hatulichukulii uzito kwa sababu hakuna mtu aliyefanyiwa humu ndani mtoto wake, tusiombe, lakini akifanyiwa mtu mmoja tu mtoto wake humu ndani tutakuwa wakati na mashine itanunuliwa ndani ya siku mbili tu, lakini kwa kuwa sasa hivi wananchi wanaofanywa hivyo ni wanyonge tunadharau lakini vitu vingine tunavileta havina hata maana vya kufanyika kwa muda huu basi tunaviingiza kwenye bajeti kubwa hapa.

Mimi nam-*support* Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwenye suala hilo na mimi sikubaliani nalo mpaka tuhakikishe kwamba wizara yako inapata fedha kamili za kuhudumikia wananchi wa Zanzibar kwa ujumla waliokuwa hawana uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa utendaji wake na kukuaminini. Lakini ninachotaka kusema kwamba nasema siku zote Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri msimuangushe, nyinyi ndio mnatakiwa mufanye kazi ili yeye apate sifa, kateua Mawaziri, na mkifanya nyie vizuri ndio serikali imefanya vizuri, Mhe. Rais kafanya, lakini mkiharibu nyinyi jina linamuangukia yeye.

Mimi ni sawa sawa na kusema kwamba mpambe ana nguvu kuliko mwenye mali, sasa nyinyi ni wapambe wa Mhe. Rais, mnatakiwa mufanye kazi nzuri, mtapoharibu nyinyi mumemuharibia na mumeiharibia serikali, haiwezekani vitu kama hivi tukaviachilia tu vya maajabu ajabu. Bajeti hii tusikubaliane nayo Wawakilishi sote, bajeti ya afya ni bajeti muhimu kuliko bajeti zote, japokuwa kuna bajeti ni za kuingiza *income* ndani ya nchi lakini tumeenda kuna bajeti zimepita zina mabilioni ambayo hayana maana mbele ya afya, tuzungumze ukweli, hii ndio hali halisi iliyokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mimi ningezungumzia Hospitali ya Kidongo Chekundu ya wale wagonjwa wa akili. Humu ndani tusiombe lakini Kidongo Chekundu tunaona wale ni hawana akili tunawafanya vile vile wendawazimu; hospitali ile chafu kupita kiasi, ina kunguni, ina mchwa, inaingia wizi wanaingia ndani, wanadhalilishwa, tusione watu hawana akili tukawadhalilisha.

Mimi juzi nimemkuta mwendawazimu hapa Mazizini mwanamme mtu mzima kavua nguo kama alivyozaliwa anatembea barabarani. Mimi ningeomba sana wizara yako wakawakamata hawa wakawadhibiti, wawaweke ndani wawahifadhi vizuri wasiwadhalilishe. Hospitali hii ipo taabani, mtihani, hivi leo Mwakilishi au Waziri akija akiwa mmoja mwendawazimu akienda kukaa kule atawekwa, tujichukulie sisi bado hatujaumbika aje kuwa mmoja humu mwendawazimu akienda Kidongo Chekundu atakubali, tuangalie tujifikirie na sisi iko siku tutakuwa wendawazimu katika sisi mmoja tutakwenda kule tuone hali halisi, hebu nendeni kwenye ile hali muone, tusikae tu tukajenga maskuli, majumba, maghorofa ya maofisi mapya, kwa nini tusijenge hizi hospitali?

Mhe. Waziri, Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la *Red Cross* hawa wanasaidia sana mambo ya afya…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, uliniomba dakika tano, lakini naona itakuwa zaidi ya tano. Kwa hivyo, maliza una dakika kama mbili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, dakika kumi na tano zimeshafika? Nina dakika ishirini Mheshimiwa…

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, he! mtihani huu, ndiyo hizo dakika tunazozipunguza na kuna masuala muhimu tunakuwa hatuwezi kujadili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, malizia, kila ukizungumza na dakika zinakwenda. Kwa hivyo, malizia, rudi kwenye hoja zako.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mimi nazungumzia suala la *pharmacy*, ma-*pharmacy* haya yasiuze dawa kwa biashara, wapewe leseni maalumu kwamba wauze dawa bila ya kitu chochote cha daktari wasiuziwe, mtu anakwenda pale anasema tu naumwa na tumbo na kichwa anapewa dawa, hizi *pharmacy* zimekuwa za biashara si za kuhudumikia wagonjwa. Mimi ningeomba sana wizara hii ikawawekea hivi vitu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende kwenye masuala ya fedha. Wale wanaosimamia kipindupindu. Wahudumu wa wagonjwa wa kipindupindu mpaka leo hawakulipwa, wengi wao wanalalamika hawakulipwa. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, wangewalipa hawa watu ambao hawakulipwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wale ambao waliokwenda kusoma kwa wingi madaktari na manesi walioenda kusoma wapelekwe kwa *time to time* wakasome sio wapelekwe kwa mkumbo mmoja tu halafu huku watu wanapungua.

Vile vile hospitali zangu za Chaani, zile Mhe. Waziri, nilokupeleka jitahidi basi japo kituo kimoja kikaanza kujengwa na serikali, hicho kingine kikangojea watu wa msaada ili kazi zikaanza, niko tayari mimi kukwambia kwa vitu vidogo vidogo kushirikiana na wizara, tukakamilisha ile sehemu ikafanya kazi tusingojee msaada.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Waziri, ningekuomba mngetenga maeneo maalumu ya sehemu za hospitali tukenda tukatafuta watu ma-*investors* na

owners, tukenda tukazungumza nao nje ya nchi wakaja wakafanya hapa, ili hapa Zanzibar ikawa kama India watu wa *East Africa* wa *Asia* au *Middle East* wakawa wanakuja Zanzibar. Mimi ningekuomba sana Mhe. Waziri, niko tayari kushirikiana na wewe hata kutumia fedha zangu taslimu, kuondoka tukatafute wale wamiliki wenye mahospitali makubwa zije zifunguliwe hospitali za rufaa ndani ya Zanzibar.

Mhe. Waziri, Mimi nakupongeza sana lakini nina mengi ya kuzungumza isipokuwa nina masuala yangu haya nataka uje unijibu Mhe. Waziri. Suala la kwanza ni lini watamaliziwa fedha zao hawa watu waliosimamia kipindupindu. Suala langu pili ni hawa upande wa *Red Cross* wanaoisaidia Wizara ya Afya, mnawasaidia kwa njia gani, au mnashirikiana vipi wakati wako katika hali ngumu, suala langu la tatu hospitali yangu utaniahidi vipi japo moja tukaanza kwa huo mfuko wa serikali japo kuiweka sawa, ili ikaanza kazi ya Jimbo la Chaani.

Suala langu la nne ni hatua gani utaichukua kwa hawa wanaowadhalilisha wagonjwa wanaojifungua ndani ya hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ujumla.

Suala langu la tano kuhusu hii hospitali ya Kidongo Chekundu mtachukua hatua gani ya dharura kuhakikisha kwamba hawa watu wagonjwa wa akili mnawachukulia hatua nzuri, ili wajihisi na wao kwamba wanaishi katika mazingira mazuri.

Suala langu la sita ni lini utahakikisha kwamba vinajengwa vyoo ndani ya wilaya zetu, au majimbo kwani zile nyumba ambazo hazina vyoo hawana uwezo mjenge vyoo, ili kudhibiti huu uchafu wa kipindupindu na maradhi mengine.

Hayo ni masuala yangu Mhe. Waziri wa Afya. Mimi nakupa asilimia 90, asilimia 10 yangu utapokuja kwenye mjadala wa kupitisha hotuba yako ndio tutakapokuja kufahamiana hapo utaponijibu. Ahsante sana na nakushukuru kwa kazi yako nzuri.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Nadir kwa mchango wako mzuri. Ndugu wajumbe, nilikuwa nawaomba sana, tutumie dakika kumi na tano. Michango ni mingi na kama mnavyozungumza ni wizara nyeti, kwa hivyo dakika kumi na tano kila mtu aweze kuchangia wizara hii, nafasi bado mnazo na kama nafasi bado mnazo mtu anaona mchango wake dakika 15 hazimtoshi, basi ruhusa ipo aandike kwa maandishi apeleke kwa waziri husika. Tunaendelea Mhe.

Suleiman Sarahan Said na Mhe. Mohammedraza Hassanali, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

UTARATIBU

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika usemi wa mwanzo ulinitaja mtu wa tatu, na tokea jana alipoondoka Mwenyekiti hapa alisema vile vile, sijui kumetokea nini, ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia nafasi hii

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahani, subiri kidogo. Mhe. Shihata nafuata utaratibu ambao ulioachwa jana, kwa hiyo kama ulikuwa mtu wa tatu, cha msingi ninachokiona hapa utachangia na jina lako nimelitaja. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetuamsha salama tukafika hapa salama wa usalimini. Mimi nichangie kuhusu hotuba yetu ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jambo la kwanza kabla ya yote, kwa sababu maneno yangu yatakuwa hayamaliziki, basi nitamuomba ndugu yangu Mhe. Waziri wa Afya, yeye *special* aje Hospitali ya Chake Chake aje ayaone, maana nikiyataja hapa yatakuwa hayatoshi, aje tu tukague mimi na yeye tukamalizana hapa. Hilo ni jambo la kwanza ninalomuomba Mhe. Waziri, rasmi. Kwa hivyo, akija hapa aje anijibu tu kwamba nimekubali au sitokubali kuja Chake Chake, basi hilo la kwanza, kwa upande wa Chake Chake Hospitali hilo naliacha yeye atanijibu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nalotaka kuchangia kwa kumsaidia Mhe.Waziri wa Afya, mimi nimesema kwamba katika hospitali zetu zote jambo la kwanza ni kuangalia miundombinu ya hospitali. Hospitali bila ya maji haiendi, hospitali bila ya miundombinu haiendi, hospitali bila ya majengo mazuri pia si hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali zetu maji ni tatizo, na bila ya maji hakuna usafi. Kwa hivyo, ningeshauri sana suala la maji katika hospitali likawa kama ndoto, likawa jambo hili ni lazima lipo wakati wowote, ikawa daktari yupo hayupo mtu ananawa maji, hili la maji ni jambo muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni katika hospitali ambazo hasa zinalaza watu, *generator* ni kitu muhimu sana, mgonjwa anapolala ukiachia *operation*, lakini

mtu anapoumwa na bado na bado na kiza basi hata yale mauti anaona yapo karibu kuliko vile alivyopata umeme hata kama atakufa sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, hilo ningesema, lakini ukiachia hayo umeme pia ni kitu muhimu katika kifaa chochote ambacho kitatumika pale. Kwa hivyo, ningeshauri sana katika afya zetu, sote maana yake sote ndio sisi wenyewe kwa wenyewe, wagonjwa sote, lakini mtu yeyote anapokwenda katika eneo ambalo hali yake itadhibitiwa katika nzuri hata kama atakuwa na matatizo mengine atajihidi kwamba yeye bado yuko salama katika dunia hii. Kwa hivyo, ningeshauri sana mambo ya miundombinu ya maji, umeme, majengo safi yanayonukia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ningeshauri na kitu kimoja hata TV. Mheshimiwa sijaona hata pahala pamoja katika mahospitali yetu kuna TV. Mheshimiwa TV nazo zinapoteza muda kidogo katika ugonjwa, zinapoteza mawazo. Mimi katika hospitali yangu ya Chake Chake hilo nitakuomba nitatia TV. Mhe. Mwenyekiti, kama ikiwa ni lazima angalau kwenye wodi tutaangalia waliokuwa wagonjwa sana tutawatafutia wodi kidogo iliyokuwa ya matibabu ya siri, lakini wale waliokuwa kidogo kaumia mguu, kafungwa *bandage*, kanyanyuliwa mguu anataka aangalie mambo. Watu wote siku hizi wanataka kuangalia mambo, michezo, mpira. Chake Chake hilo nitakuomba, lakini utakapokuja tutaongea zaidi. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nataka niongee kuhusu habari ya mfuko ya Bima ya Afya. Mheshimiwa tulikaa hapa tukapata semina ya mfuko wa Bima ya Afya. Hospitali zetu za serikali zimo katika mfumo au katika mfuko wa Bima za Afya.

Nashukuru ndugu zetu hawa wameziingiza humo, lakini watu wanazikimbia wanakwenda katika Hospitali za *private* na zile bima zinalipa pesa, sasa kama unakuta kitu kama Al-Rahma inalipwa bilioni tatu kwa mwaka, leo Mnazi Mmoja mgonjwa yule yule anatoka Al-Rahma rufaa anapelekwa Mnazi Mmoja, lakini Mnazi Mmoja ile pesa haipatikani.

Kwa hivyo, ningekushauri sana tenga eneo maalumu ambalo litahudumia hawa watu wa Bima ya Afya ili wapate moyo wa kwenda kwenye hospitali zetu za serikali ambapo wewe mwisho wa mwaka utapata fungu ambalo linatoka Bima ya Afya. Kwa hivyo, ningeshauri sana, mara hii walitwambia kwamba sijui karibu bilioni tatu sijui zimekwenda Al-Rahma, lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja imekwenda milioni 200 ah! Sasa milioni mia mbili Mnazi Mmoja na bilioni tatu Al-Rahma inakwenda wapi na wapi, sina hesabu kamili lakini ni

pesa nyingi imekwenda Al-Rahma mara tano au zaidi ya kumi kuliko Mnazi Mmoja, ningeshauri sana Mheshimiwa ukaliangalia kwa kina suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka nikwambie tena narudia kusema Mheshimiwa katika visiwa vyetu, lakini naongea hasa umbali wa Pemba. Mheshimiwa Pemba tumekamatwa na maradhi yasiyopungua matano, tumakamatwa na *cancer* haijulikani inatokea wapi inakwenda wapi, sukari ndio yenyewe, presha haisemezeki, maradhi ya moyo ndiyo yenyewe, figo ndiyo halisemezeki. Nataka nikwambie, wanapokufa watu mia wa Pemba basi thamanini wanazikwa Dar es Salaam, ishirini ndio wanaoletwa Pemba. Ningekushauri sana ikiwezekana na mfuko wetu wa serikali nakuomba msaada kwa wenzetu tutafute madaktari bingwa waje watusaidie pale Pemba, hata mmoja mmoja awepo bingwa wa sukari, *cancer*, angalau mtu apate *advice* ile ya matibabu angalau akitoka pale ajijue naenda wapi. Mwengine anaondoka leo Pemba asubuhi kesho Dar es Salaam anazikwa, angalau mtu ajulikane tu kwamba huyu kwa hali aliyo sio wa kusafirisha wala kitu chochote.

Kwa hivyo ningeshauri sana Mheshimiwa madaktari bingwa ukatupatia. Mimi enzi za nyuma kidogo ninakumbuka tuna Warusi, tuna Wachina, tuna watu gani, tuna Wazungu, tuna Wataliano, ningeshauri hata daktari mmoja mmoja ombeni Mhe. Waziri, wewe nakufahamu ni mtu wa watu sana, omba waje kule Pemba waunde timu pale Chake Chake, itasaidia Pemba nzima.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninataka niseme mimi tena kwa upande wangu, lakini naishauri serikali turudi madaktari wetu wapite kwenye maskuli kwenda kuangalia watoto wadogo wadogo wa maskuli, yaliyokuwa mengine akifika utuuzimani anakuwa hayatibiki tena. Ningeshauri watoto wapitiwe maskulini, wapate kupimwa, hata kama watakuwa wanachunguzwa wanachukua lakini baadaye wanaleta *results*, mtoto huyu anatakiwa akatibiwe, mtoto anakwenda skuli akimaliza skuli anakufa, maradhi hayajulikani.

Sisi wengine tulipata matibabu hayo yalitusaidia tungekuwa hatuko tena duniani sisi wengine, maradhi tuliambiwa hayo ungelikaa mwaka mmoja ungekufa, kwa hivyo watoto wanafanya hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi ningekushauri kwa sababu nimesema mimi katika ilani yangu ya kule kwenye jimbo langu, ilani yangu sio ya CCM, yangu mimi, nataka Mheshimiwa unipe madaktari wa wanawake na wajawazito hata wawili tu, watatembea katika majumba yote yenye wajawazito katika jimbo langu zima. Mwanamke asiende *clinic* atapitiwa nyumbani, atapitiwa nyumbani mama anakosha anaambiwa njoo kidogo, atapimwa mtoto wake na

kila kitu madaktari wanaondoka, gharama nitagharamia mimi, Nakuomba madaktari tu wa mama mja mzito na watoto, lakini kama itaenda kwa nchi nzima sio tatizo litasaidia wengi, hawa mama wengine wanaona tabu, mama wengine hawana uwezo, mama wengine wanakuwa na mashaka mengine, wengine waume zetu wana wivu. Lakini tukimaliza pale tunatembea na Sheha itakuwa wivu utaondoka hasa ukinipatia wanawake. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hilo ninalolisema ikiwezekana tupate hao madaktari angalau watembee kwenye majumba kusaidia hiyo hali. Hilo ilikuwa kidogo niseme.

Mhe. Mwenyekiti, nataka tuangalie sana sekta ya afya. Sekta ya afya unapoumwa unakuwa karibu sana na Mwenyezi Mungu maana hapo tena wewe unakwenda zako akhera. Wewe ukiumwa jua unataka kufa, na aliyekuwa hamjui Mwenyezi Mungu, ngoja aumwe atamjua. Kwa hivyo, ningekushauri Mhe. Waziri kwa ninavyokufahamu unakuwa hata watoto wanatishwa na kila kitu kipo, lakini nakushauri sana mara hii au tunavyokwenda manesi wetu, madaktari wetu, jambo la kwanza wafanyiwe *interview* ile yenyewe kwanza, sio ya kusoma kwamba huyu amesoma *science* nini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kauli moja watu wanasema ukitaka kumjua mwendawazimu subiri ahamaki, akishahamaki wendawazimu wake utaujua, hazuiliki hakamatiki, kuna wengine wana vichwa vizuri vya *science* lakini Mheshimiwa akikasirika anamfanyia yule mgonjwa analotaka mwenyewe, madaktari hawa hawatufai.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeshauri sana wale watakaokwenda kusomea u-*nurse*, wale watakaokwenda kwenye udaktari, tukawapima mwanzo, ukamuhamakisha mpaka akamaliza kuhamaki, vipi ule wendawazimu wake utatokeza au vipi, wakishakusoma hawa mashaka yanakuwa makubwa.
Katika madaktari kumi unapata watano ndio waliokuwa wazuri, watano wabaya, hata wenyewe wanakwambia kwa yule usiende, kutokana na matatizo. Mheshimiwa tuangalie sana hili eneo la afya na hawa manesi waangalie sana.

Mhe. Nadir alilizungumza suala hili. Mhe. Mwenyekiti, manesi nao wana mashaka yao, mtu anapokwenda kuzaa mimi nasema kila siku pale anateremka Mwenyezi Mungu mwenyewe hamtupi mtu, lile eneo ni eneo zito. Mama anachanganyikiwa, lakini tatizo linakuja nesi hata habari hana, anamwita hasa; eh! nesi njoo mimi nakufa. Hata habari hana.

Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri sana hili likawa ni wanawake wenye huruma wakaangalia matatizo yao, lakini pia nataka nikwambie kwamba nakushauri sana hebu omba kifungu chochote upate ajira zile za nusu nusu angalau upate

watu, ambao watafanyiwa *interview* katika mambo yale ya unesi unesi, ambayo hata bado kusoma bado waingie tu na madaktari kusafisha na kufanya hivi, ili utakapokwenda kusomesha ujue huyu tayari ameshakamilika, sio kutafuta watu wenye vyeti tu Mheshimiwa, vyeti tu vitatufikisha pabaya, lazima na khulka ya mtu uitizame, ili hili jambo ulijue hasa kama huyu mtu analiweza. Sio leo unamsomesha akirudi pale akwambie mambo haya miye siyawezi, anaanza kugombana na wagonjwa. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ningeliomba kidogo tuangalie habari ya mambo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine sisi tunapata matatizo ya kila kipindi, ningekushauri tafuta mfuko, omba Serikalini litafutwe eneo la maradhi ya mripuko, sio kuvamia vituo au hospitali, tuwe na eneo maalumu la maradhi ya mripuko. Likitokezea tu tunahamia na madaktari wake waweze kujulikana kidogo ata watano au wanne wa kuanzia, kwamba hawa ni madaktari bingwa wa mirupuko, lakini sio leo tumekaa limetokea tatizo tunaondoa hospitali hii tunang'oa huku watu hawa inakuwa mashaka, tutafute eneo Mheshimiwa hata kama ni mwaka mmoja, kipindi chote cha miaka mitano jengo hili lijengwe. Litafutwe eneo la maradhi ya mripuko ambalo litakidhi haja ambayo itapimwa kwa viwango.

Kwa hivyo ningeomba sana ikiwezekana suala hili likawa ni muhimu sana, kwa sababu kila siku tunakuwa tunavamia hospitali, tunakamata hapa, tunakwenda pale inakuwa haiendi, lakini Mhe. Mwenyekiti mimi nasema ukweli magari, matatizo tunayo na *sabotage* nyengine mimi nakuaminia zipo hasa suala la mafuta, mtu anapiga simu haidhuru Wawakilishi wanasaidia lakini mambo ya hospitali baina ya jenereta, *ambulance* yanakuwa na mashaka, kila siku unaambiwa mafuta hakuna na fungu lipo, fungu linakuwepo basi hata mafuta ya jenereta pia unaambiwa hapana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ningekushauri sana mimi naamini Serikali yetu inafanya kila jitihada za kutafuta majenereta, kutafuta magari lakini hayadumu gari na jenereta la hospitali binafsi Mheshimiwa linadumu miaka kumi, gari la Serikali halidumu miaka mitano hata mwaka mmoja wala jenereta haidumu inauliwa kwa makusudi na watu wengine.

Ningekushauri vitu hivi vitakapoletwa hospitali vikakabidhiwa mtu maalumu, ikiondoka jenereta anaondoka na yeye, ikiwa jenereta haifanyi kazi alete vithibitisho maalumu na magari vile vile, kwa sababu magari ya kumpa kila mtu, madaktari wote, ndio wanavyoziua, wengine wanauza mpaka *spare* ngoja nitaileta hapo utafungua utafunga.

Kwa hivyo Mheshimiwa ningekushauri vitu vile unavyoviona kwamba vina umuhimu wa uhakika si vitu vya kuvichezea, unanunua *Land Cruiser*, *Ambulance* linakaribia karibu milioni mia unampa mtu analichezea halafu unakuja kuilaumu Serikali, na mimi nitailaumu kwa sababu ndio mipango yake, lakini lengo na madhumuni ilikuwa ni kitu hasa kingetufaa sote.

Kwa hivyo ningeshauri vitu hivi vitakapokuja lazima vikabidhiwe ingawa vinakabidhiwa katika hospitali, lakini hata huyo daktari dhamana amkabidhi mtu ambaye atamjua na atamkamata yeye, naomba sana hilo liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, suala ambalo sasa hivi kimekuwa kigezo kikubwa sana na mimi nataka nizungumze limeshazungumzwa sana sijui tena litakuwa na umuhimu gani suala la *DNA*, maana yake hili Mheshimiwa tulilizungumzia sana hata upande wa mama Castico matatizo yameshakuwa mengi sana, ukiachia hayo ninaye Mheshimiwa wangu mmoja humu juzi katika kutoa hoja hii ya kuzungumza habari ya …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan una dakika tatu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mheshimiwa lakini hili lazima kidogo niliseme.

Juzi kuna Mheshimiwa mmoja humu ndani kanikumbusha kwamba juzi katika haya masuala ya kuzungumza kwamba *DNA* lazima kutokana na haya mambo ya ndoa, mambo ya vipimo vya watoto, mambo ya matatizo gani, mama mmoja labda niweze kusema tu mama mmoja alizaa na baba mwengine lakini katika hali ya kutokuaminiana yule mama alimwambia yule mume kwamba huyu mtoto kachukua wicho kwa mjomba wake, yule baba akamwambia mbona hakuchukua wicho wa mbwa ambaye yuko chini ya mlango siku zote.

Kwa hivyo Mheshimiwa nataka nikwambie kwamba hili la *DNA* itatupunguzia matatizo mengi, ikija ndoa hazitovunjika sana, mashaka mengi haya na uaminifu utakuwa mwingi na zogo la watu wengi wa *DNA* limeshakuwa kubwa lazima tufuate Dar es Salaam, naomba tujitahidi sana *DNA* tuipate kwa muda ambao muafakam, mambo ya siku hizi kopa tutalipa usiogope kudaiwa Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo jambo ambalo nitalianza najua nitakukera sasa bora mimi nitamualika Mheshimiwa mwenyewe najua nitamueleza, kwa hivyo cha msingi tu na mimi naunga mkono hoja asilimia mia moja, atakapokuja

kunijibu atakuja Chake Chake asilimia tisini na tisa moja naizuia mpaka atakaponambia tunakwenda Chake Chake kwenda kukagua mambo yetu. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa pumzi, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na viongozi wetu, kwa kujaaliwa kufika hapa kwa utekelezaji wetu wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ndicho kilichotuleta hapa kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo tumo humu ndani kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Waziri, kamati pamoja na watendaji wake wote Madaktari, Manesi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kizalendo.

Nichukue nafasi hii vile vile kuishukuru Serikali nzima kwa mashirikiano tuliyokuwa nayo na Mhe. Mwenyekiti imani yangu kwamba tupo katika mwezi wa ramadhani tunaelekea katika masiku ya *Lailatul kadr,* ambapo sisi Waislam kihistoria tunasema msahafu huu umeteremshwa katika mwezi huu kumi la pili na kumi la tatu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru nimekuwa mzalendo sana kwa kuipenda nchi yangu, kukitumikia chama changu cha Mapinduzi na kuitumikia nchi yangu kwa sababu nina uchungu na nimepata malezi na baba yangu ambaye mpaka leo ananilea mimi ni Dkt. Alhaj Salmin Amour; Rais mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nina imani na sote tuliokuwemo humu ndani basi tumepata neema yake. Usipowashukuru wenzako yeye mwenyezi Mungu hataki kushkuriwa.

Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wenzake ni watu ambao nawaheshimu sana, na ni wenzangu sana na hilo nataka niwahakikishie umma huu Mhe. Mahmoud, Naibu Waziri wa Afya Dkt Juma na wasaidizi wake wote. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba nataka viongozi wetu sisi wakiongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye ni msikivu sana na muongozaji mwenye maadili.

Mhe. Mwenyekiti hivi leo asubuhi nimefika hospitali ya Umbuji saa 2.15 asubuhi hii wakati nimechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Uzini nilikuta kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kutekeleza ilani yake ya chama aliahidi hospitali ya Umbuji Serikali kuijenga katika kutekeleza ilani ya chama miaka sita iliyopita alipoingia katika awamu

yake ya sita, kwa bahati nzuri nilipoingia mimi wamo Wawakilishi na nikakuta ile ahadi ya Rais, na sote ni watekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, nikaomba Wizara ya Afya hospitali ile niijenge mimi kwa niaba ya familia yangu, Hospitali ile ya Umbuji pamoja na wananchi ili vile vile nimsaidie Rais wangu, maana yake yeye ndiye aliyetubeba huku nyuma kwenye mgongo wake katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya nilipokwenda kuwaona wakaniambia Raza hospitali ile kwa bahati nzuri ina mfadhili, kwa hivyo katika hili utuachie, nasema Rais alitoa ahadi nilipokuja kuchaguliwa na wananchi ahadi ile ya Rais kwa sababu ni baba yangu, Rais wangu, nilitaka kwenda kuimaliza miadi ile kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini.

Wizara ya Afya barua zote ninazo, wakanikatalia, wakaniambia ina mfadhili wanaitwa sijui Porio sijui Orio hata ukitaka kutaja lazima ule vidonge vingi ndio utaje Pario sijui nini haya twendeni.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya muda nikaenda tena tulikuwa na mkutano wa hadhara ambao ulifanyika uwanja wa Manzese, kwa bahati nzuri mkutano ule mgeni rasmi alikuwa Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi alihudhuria vile vile Spika wa Baraza la Wawakilishi mzee wangu Mzee Pandu Ameir Kificho, alihudhuria ambaye leo ni Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan alikuwepo pale siku hiyo, na walikuwepo baadhi ya viongozi wa chama na Serikali, akiwemo vile vile Mzee wangu babu yangu Mzee Gavu aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama Mkoa wa Kusini.

Mhe. Dkt. Sira Mamboya aliwaambia wananchi wa Uzini miaka mitatu iliyopita, aliwaambia jamani kweli Raza tumemzuia asijenge hospitali, hospitali hii tayari kuna mfadhili Pario sijui Porio hata sijui Mhe. Waziri utanisaidia baadaye kuisema kwa lugha ambayo unaifahamu wewe. Kwa hivyo Naibu Waziri akathibitisha kuwaambia wananchi kweli tumemzuia Raza asijenge, na hiyo hospitali nakwenda kuijenga kwa wakulima na wakwezi wa Umbuji.

Mhe. Rais alifanya ziara Umbuji katika kufungua barabara pale Umbuji, akaahidi Umbuji pale jamani hospitali yenu mwaka huu tunaimaliza, tunaingia leo nimekwenda asubuhi sisi ni waislamu, nimetoka saa 2.00 na msahafu huu nauweka kichwani yule mbuzi yule anayelia meee meee, basi huwezi kumtibu hospitali ile leo wala njiwa.
Mhe. Mwenyekiti, ramadhani yule ng'ombe huwezi kumtibu, Umbuji tunakwenda kuwatibu wananchi inaniuma mimi, nimetoka sasa hivi na msahafu huu Umbuji haina kiza basi yule mbuzi meee meee huwezi kwenda kumpiga

sindano ya mafua atazidi kuwa na mafua, tuko hapa *on transit,* mimi nilijiambia Adhuhuri isinifike hapa Mwenyezi Mungu atachukua roho yangu na ukipata Adhuhuri jiambie Alaasiri si yako, *we are in transit,* tunaringa na pumzi za Mwenyezi Mungu.

Nakuombeni na hapa nilipo mimi mnaweza kutoka nje mkaambiwa Raza hayupo huo ndio ukweli wa Mwenyezi Mungu, naitumikia nchi yangu, leo tumefika nchi hii Rais kaahidi miaka sita hakuna lililotekelezwa, mimi nataka kujenga hospitali ya kisasa nazuiliwa tena Umbuji.

Leo Umbuji twendeni sasa Wawakilishi sote, yule mbuzi wako mee au yule paka nyau nyau huwezi kumtibu mule, huu msahafu Mhehimiwa, twendeni sasa hivi, lazima tuwe binadamu, hivyo tunatoka hapa tukifika saa saba tunakimbilia kuswali, ikifika saa kumi tunakimbilia kuswali, hatuwezi, *we are in transit.*Mheshimiwa tumekuja hapa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, uhai wetu wa nchi hii ni Chama cha Mapinduzi.

Mimi sivunjiki moyo, nitaendelea kuisaidia Serikali hii, nitaendelea kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, naiambia Wizara ya Afya kwa taarifa nimeshaagizia madawa ya Mchangani, Machui, kote, madawa kutoka nje na karibuni yatafika, wala sitochoka na wala sitovunjika moyo, lakini tunapofika pahala tumkumbuke Mwenyezi Mungu.

Tumekusanya magari hapa mabilioni ya mapesa, leo Serikali haina madawa, taasisi sikatai hohe hahe, lakini tuko sisi mnatuzuia. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema hapa leo tunakwenda kupeleka bilioni 7.5, *fimbo ya Mungu haina sauti*. Unakuja kupeleka pale, watu wanakufa, leo hata mbuzi wako huwezi kumtibu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tuwe wasikivu, Wawakilishi hii bilioni 7.5 mimi kama nina uwezo na kama tuna uwezo wawakilishi tupitisheni hoja tuiondoshe hii Wizara ya Afya bajeti, kama tumesimama kwa Mwenyezi Mungu sisi, Waheshimiwa mnataka nini? *What is next?* Tumekuja hapa kuwatumikia wananchi, tumekuja hapa kuwatumikia wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, Uzini ni jimbo lililoongoza nchi nzima Unguja na Pemba kwa kura, wananchi wa Uzini wanataka *service,* baada ya Oktoba uchaguzi wetu kufutwa watu walikuwa hawalali, wananchi wa mashamba walikuwa hawalali. Lakini mimi nasema jamani namuomba sana Mhe. Rais kama ananisikia kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu awashe gari yake aende Umbuji, hamna chochote ni kiza, sasa hivi nimetoka huko na naomba.

Kwa hivyo naomba kama kweli Waheshimiwa kama tumekuja hapa kwa uchungu wa wananchi, tumekuja hapa kuwatumikia wananchi, tupitisheni hoja ikaondoshwe bilioni 7.5 iondoshwe, tunataka wananchi wa mashamba wapate madawa.

Leo wananchi wa mashamba wote hawana madawa Unguja na Pemba, kuanzia Micheweni mpaka Nungwi, mpaka Makunduchi. *We have to be serious*, nakuombeni sana Waheshimiwa.

Naiomba sana Serikali hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein, Serikali ya Dkt. Ali Mohamed Shein ni sikivu, nasema naomba sana Wizara ya Afya ile hospitali wakaitengeneze.

Leo unakuja kunizuia mimi kwa sababu ni sehemu ya nchi hii, hichi choyo, majungu, fitna tungeliendeleza kwenye maendeleo *wallahi* nchi hii ingelikuwa pepo hapa leo, lakini huyu siye, huyu ndiye, hatuwezi sijui tunataka nini Wazanzibari sisi nchi hii, sijui tumefikwa na nini Wazanzibari. Nchi hii naumia kwa sababu ya Chama cha Mapinduzi, naomba sana tumekuja hapa kutekeleza ilani ya Chama, wananchi wanasubiri, *tusiache mbachao kwa msala upitao*. *Zimwi likujualo halikuli likakwisha, Tusidharau wakunga na uzazi ungalipo*.

Mhe. Mwenyekiti Mtume wetu *S. A .W* alikaa na masahaba wake basi kikazimika kibatari, wale masahaba wake wanamwambia *Yaa Rasulallah*, maana yake Mtume alisema *Inna lillaahi Wainnaa Ilayhi Raajiun*, basi wale Maswahaba wake wanasema *Yaa Rasulallah* kimezimika kibatari unatamka hivyo, akasema na jambo lolote ambalo hulifurahikiwi, wewe ukipotezewa na ufunguo tu sasa hivi hufurahikii, ukitiwa mchanga tu machoni hufurahiki. Jambo ambalo hulifurahikii tuseme *Innaa Lillaahi Wainnaa Ilayhi Raajiun.*Sasa leo Mimi Raza nchi hii bila ya Serikali ya Mapinduzi iliyonisomesha ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Neema yote wamenifikirisha, wananchi leo tuna jengo la hospitali miaka sita nasema tusifanye mzaha tukafanya tashtiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi msahafu huu sipigi buti na nitamshtakia Mungu mpaka kiama, huu msahafu sipigi buti, wala siungi mkono kwa hatua ile kabisa, lakini lazima tuwe wakweli, jembe ita jembe, pauro ita pauro, lakini hatuwezi sote tumekuja hapa kwa kuwatumikia wananchi. Mimi naiunga mkono Serikali nimeshasema madawa nimeagiza, na sitochoka, Wizara zote kwa hali na mali nitazisaidia wala sivunjiki moyo, na hiyo tumeambiwa kwenye msahafu Mwenyezi Mungu alitwambia mtaletewa mtihani katika mali,

katika biashara, katika uongozi. Lakini mwisho Mwenyezi Mungu anatwambia nini, wapeni habari nzuri wanaosubiri.

Mhe. Mwenyekiti, niombe Wawakilishi kwanza kuna vituo vyetu vingi havina madawa, Serikali yetu imefanya mengi lakini hii bilioni 7.5 tuvunjeni hapa bajeti ikarekebishwe.

Wawakilishi tunabeba kwa sababu sisi tumechaguliwa na wananchi kutekeleza ilani ya chama. Mimi hapa nimekuja kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi, nimekuja kutekeleza ilani kwenye Chama cha Mapinduzi, nimekwenda kuchukua fomu ndani ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza ilani ya Chama.

Mhe. Mwenyekiti, niiambie vile vile Serikali kwamba tufike pahala kama tuna jambo lazima kuwe na mjadala, lazima tuzungumzeni tuzungumzeni, lazima tushirikiane.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe mimi nimeyasema, nimekuja na msahafu kwamba yule mbuzi huwezi kumtibu wanavyotibiwa wananchi leo wa Umbuji. Kwa hivyo Waheshimiwa nikuombeni nyote, twendeni tukatelezeni ilani ya Chama, wa kumuogopa yule unayemuendea sijda. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, ninampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, na madaktari wetu na wauguzi wetu wote kwa kazi zao nzuri wanazojitahidi kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nitasema tu kwamba kwa asilimia mia moja ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwajali wananchi wake, na kuona kwamba ipo haja kuwasaidia kwa hali na mali hasa kwenye matibabu bure na mambo mengi katika nchi yetu juu ya kuwajali wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitaanzia katika hospitali binafsi. Ninajua kwamba wenzetu hawa wanajitahidi sana kusaidia jamii, hasa tukizingatia kwamba masafa marefu baadhi ya maeneo hakuna hospitali. Kwa hivyo niseme tu kwamba hili nawapongeza watu wa huduma zote za hospitali

hizi. Pia naipongeza Bodi inayoshughulikia hospitali hizi kwa kufuatia mambo mbali mbali juu ya kuona ubora na utendaji wao katika maeneo wanayofanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ninaiomba sana Bodi hii inapofanya kazi zake inakwenda vizuri lakini pia muda wa kuwapa masharti wale kama pana makosa fulani, uwe mfupi ili vituo vile vifunguliwe na wananchi wetu wapate huduma hizo mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, jengine baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi katika majimbo yao mbali mbali wamo katika jitihada za kutafuta vituo vya afya hasa ukizingatia masafa ya maeneo tuliyonayo. Kwa bahati nzuri Jimbo la Mwanakwerekwe lililopita Mbunge alikuwa Mhe. Juma Sereweji na Mwakilishi alikuwa Mhe. Shamsi Vuai Nahodha. Lakini sasa kwa bahati nzuri jimbo lile limegawiwa limekuja Kijitoupele limekuwa la Mwanakwerekwe peke yake. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri hapa pana kituo alikianzisha Mbunge aliyepita na Mwakilishi wakati huo kipo katika Jimbo la Kijitoupele eneo la Taveta Magirisi.

Kwa kuwa kinamama wetu wa Jimbo hili wanakwenda masafa ya mbali, wanatoka Pangawe, wengine wanatoka Tomondo, wanatoka Kwarara, Kijitoupele, hawa watu kituo hiki cha Hospitali ya Magirisi kikimalizika watapata faraja kubwa sana ya huduma zao hata kinamama na wajawazito na watoto. Niiombe serikali kupitia wizara husika, pamoja na mazungumzo mazuri yaliyofikiwa na Katibu Mkuu na Mhe. Waziri, pia nilimdokeza kwamba hili tuliendee mbio lifanikiwe haraka ili wananchi wetu wapate matibabu ya karibu kwa huduma zao za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za afya katika hospitali zetu naweza kusema kwamba mimi ninashukuru, lakini pia ningeomba moja tu kubwa lolote linalotakiwa liwe zuri basi lugha yako iwe laini na iwe nzuri. Lakini lugha ikiwa mbaya au chafu watu wengi watakukimbia na hawakuelewi, kwa hivyo anasema tu kwamba *sauti nzuri humtoa nyoka pangoni*.

Ninamuomba sana Mhe. Waziri hii ilikuwa watendaji wetu, wauguzi wetu na baadhi ya madaktari wetu, si wote, lakini wawe na lugha nzuri za busara, ili kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu wanapata matibabu mazuri katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika huduma hizo zinazotolewa tunasikia malalamiko mengi yamejitokeza Pemba, hospitali ya Wete, nitamuomba sana Mhe. Waziri hii alitolee kauli wananchi wote wasikie.

Katika hospitali ya Wete Pemba kuna ubaguzi wa kutoa huduma kwa baadhi ya wananchi hasa yanaendana na mambo ya kisiasa. Ninakuomba sana Mhe. Waziri wewe ndiye Waziri unayehusika utoe kauli tuisikie, je, hatua gani zimechukuliwa kwa hawa wanaoendesha vitendo hivi. Ukweli huu upo na unaendelea, baadhi ya wauguzi na madaktari hawawapi huduma sahihi wananchi wetu ambao wako chama fulani. Kwa hivyo hili Mheshimiwa lifanyiwe kazi ili tupate ukweli wenyewe na liondoke kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, unapokuwa askari hasa mwanajeshi na polisi unakula kiapo maalumu cha utiifu. Mwanajeshi utakuwa tayari kuilinda nchi yako na nje ya mipaka yako na uko tayari kufanya hata nje ya mipaka ya Tanzania kwa ajili ya amri utayopewa ya halali inayokubalika. Lakini na wauguzi wa madaktari wetu wana viapo vyao vizuri sana, kwa sababu wawe ni watu wakarimu, watu waadilifu na watu wenye huruma. Ninamuomba sana Mhe. Waziri hili aliangalie.

Kuna jengine ambalo limezungumzwa na watu wengi mpaka jana, *mtu mzima akilia ujue pana jambo*. Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mjumbe wangu katika Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari Utalii yaani imekusanya watu wote hii Wizara ya Wanawake ndio maana nikaamini kumbe Mjumbe wangu alilia kuwa pana haja ya kulia kutokana na mazingira ya jamii yetu inayotulinda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono sana suala la kuwa na hospitali ya rufaa katika nchi yetu, na katika ilani imesema 2016 mpaka 2020 hili litekelezeke liwe tayari. Lakini kwa mtazamo wa hapa na pale Mheshimiwa bado tuko nyuma sana, pamoja na juhudi zinazoendelea halijafikia hata asilimia 80 kama kilivyosema kitabu hiki.

Mheshimiwa kujenga jengo ni sehemu moja, kupata vitendea kazi ni sehemu ya pili, hii sehemu ya pili ndio yenye shida. Kujenga jengo, kwa sababu hata nyumba yako ukijenga unaweza kuijenga ukaiangalia tu ukija kwenye madirisha, milango, unataka mafanicha ukajuta kwa nini ulijenga.

Kwa hivyo niseme tu kwamba tuwe nalo taratibu lakini hili fungu linalopigiwa kelele na wengi na mimi ninaiomba serikali tuliangalie upya. Kwa sababu tunavyoishi tunajuana, *mtegemea cha ndugu hufa maskini*, na anayemtegemea

rafiki ana hiari yake. Kwa hivyo bilioni hizi zilizotangazwa hapa 23.6 tuzipeleke katika madawa na kwengineko ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanapata madawa ya kutosha hasa kinamama, wajawazito na watoto, bado waheshimiwa hospitali zetu zina kero na kero kubwa ya madawa.

Naunga mkono kauli yangu ya mwanzo niliyosema kwamba naunga mkono hospitali ya rufaa iendelee, lakini kwa muda huu wa kipindi hiki cha 2016/2017 tupunguze hizi fedha ziende katika mahitaji maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu vijijini na mijini.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninaloliomba, katika hospitali yoyote panakuwa na sehemu ya kungojea wagonjwa, yaani wenye wagonjwa wanakwenda pale kupumzika na kuona kwamba pana haya ya kuhakikisha kwamba angalau pawe na banda. Au kama serikali inaona tabu kujenga banda katika maeneo ya Mji Mkongwe na waweke turubali au shamiana maalum, wananchi wetu wanaokwenda kutizama wagonjwa wao wapate muda wa kupumzika pale. Kwa sababu Mheshimiwa tusidanganyane, mtu anapokwenda kumuangalia mgonjwa wake hasa mzazi anakuwa akili yake haifanyi kazi na huko ndani kuna mambo. Kwa hivyo akili yake yote mzazi kuondoka pale anaona aaa mwanangu namuacha hapa sijui vipi, bora awe karibu, lakini wajengewe turubali au shamiana, serikali au wizara ina uwezo mkubwa kupata shamiana fulani la kuweka pale kinababa huku na kina mama huku, ili muda ukifika wakaangalie wagonjwa wao kwa salama na amani.

Jengine nitakalolizungumza hapa mimi ninafikiri kwamba suala lililozungumzwa la kipindupindu limetokea katika nchi yetu na tumekishuhudia kwa muda mrefu, hadi leo wagonjwa wa kipindupindu wangalipo.

Niwashukuru sana madaktari na wauguzi wote walioshiriki katika kazi hii, kama mwanajeshi alikwenda kupigana vita ndio mimi mmojawapo tuliambiwa hakuna la kuwapa na Mhe. marehemu Mzee Nyerere isipokuwa ahsante. Lakini na hawa madaktari na wauguzi wetu waliofanya kazi kubwa mpaka leo wanaendelea nayo maana wako *standby* kama majeshi, likitokea wameshafika.

Ninaomba wizara kupitia Wizara ya Fedha iwaangalie kwa jicho la huruma, angalau kuwagaia lile posho lao waondokane na manung'uniko waliokuwa nayo. Mhe. Mwenyekiti, likifanywa hilo Mhe. Waziri atakuwa kawasaidia sana wenzetu hawa, hasa tukizingatia kwamba kazi wanayofanya sawa sawa na mwanajeshi yuko vitani.

Mhe. Mwenyekiti, najua unataka kunambia mda, nasema tu kwamba, baada ya hayo machache ninamuomba Mhe. Waziri Hospitali ya Magirisi itasaidia jamii ya eneo kubwa; Pangawe, Kijitoupele, Kwerekwe yenyewe, Kwarara na kwengineko na Madina yake itawasaidia wananchi wetu.

Baada ya hayo niseme tu kwamba ninaunga mkono kwa asilimia mia moja, sina tatizo na ninawaomba wenzangu hili fungu tunalolipigia kelele kweli tuangalie uwezo wa serikali yetu kwa sasa hivi, kwa sababu tunachotegemea cha nje si chetu, tulichokuwa nacho Mungu atatujaalia ndio chetu tukifanyie kazi kwa ajili ya kupata madawa katika nchi yetu.

Ninashukuru naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi bila kupoteza muda niende katika hoja yangu moja kwa moja nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu kuwashukuru wote na ninawaamkia wote wakati nipo hapa Barazani leo kuichangia hii wizara muhimu ambayo ni Wizara ya Afya.

Kwa kweli kwanza niwapongeze wote waliokuwepo katika wizara hii, rafiki yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo pamoja na Mhe. Harusi kwa uwezo wao pamoja na watendaji wote waliotayarisha hii bajeti. Lakini nataka niseme kitu kimoja na mimi pia kwa upande wangu mwenyewe na wananchi wangu na mimi naungana mkono na wajumbe waliotangulia juu ya hoja ya bilioni 7.5 kwamba sitaunga mkono na tutaungana sote kwa pamoja ili hili fungu lihamishwe, na ninaomba pia na Wajumbe wenzangu wote tushirikiane kwa pamoja tufanye maamuzi ambayo ni sahihi kwa ajili ya wananchi, na yule ambaye hatokuwa na sisi basi tena tutafanya maamuzi kwa pamoja huko.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niende kwenye suala la Mnazi Mmoja. Hii ni hospitali ambayo inatumika na watu wote, hakuna Mzanzibari yeyote katika maisha yake kwa njia moja au nyengine atakuwa hajapita katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Aidha amelazwa, kaenda kumuona mtu au amesikia kitu anaona. Kwa hivyo hospitali hii inagusa watu wengi sana kila jambo.

Mimi mwenyewe niliwahi kulazwa kwa malaria miaka mingi nyuma, lakini ninashukuru siku hizi kuna mambo mengine tofauti, unakuta huyu anatibiwa huku mwengine huku lakini na malaria yenyewe pia inastahiki serikali kupongezwa na kwa watendaji wote kwa kulisimamia. Lakini nataka niseme kwamba Mhe. Waziri utakapokuja kuna vitu vya msingi, suala la *X Ray Machine*, nataka nifahamu lakini pia hii *computerized tomography* yaani *CT*

SCAN, halafu nina taarifa kwamba hata kwenye *laboratory* hizi mashine za kupimia damu *blood count* sijui kama ni kweli, lakini tupate kujua.

Mhe. Waziri pia nataka nichukue fursa hii kuipongeza serikali na Mhe. Rais kwamba maamuzi na bidii na kubuni wazo la kujenga hospitali ya Binguni katika Wilaya ya Kati ambayo itaweza kusaidia na kukidhi haja kwa wananchi wetu wote kwa ujumla, hasa wananchi wa Mkoa wa Kusini na wale wanaotoka Kaskazini iweze kuwasaidia, lakini pia katika kujipanga hili sasa isije ikawa lugha ya taifa, tukaanza nusu tukaenda, tukianza tuanze moja kwa moja, na hili limo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mhe. Waziri umeongea kabisa juu ya suala la kujengwa Binguni. Katika mnasaba huo huo lakini suala la Mkoa wa Kusini kwa ujumla kwenye huduma ya afya hasa katika vizazi kwenye kisiwa cha Uzi katika Jimbo langu watu wa Bungi pamoja na Kikungwi inatokana na uhaba wa vifaa na maeneo ya kwenda kutibiwa bado ni mtihani, na hasa hivi sasa kutokana na ubovu wa barabara sasa hivi ilivyojaa vumbi kwa wagonjwa kutoka Fuoni kuja zao mpaka mjini, hasa pia kwa watu ambao wanataka kwenda kujifungua wajawazito. Huu ni mtihani mkubwa kwa wananchi wote wa Mkoa wa Kusini kutoka Jimbo la Makunduchi, Paje, pamoja na Jimbo langu la Tunguu. Kwa hivyo Mhe. Waziri ni muhimu kuangalia kwa ujumla katika muda wa miezi 6 ni utaratibu gani ambao utaweza kutumika wote.

Nataka niende Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la Mnazi Mmoja ni kitu gani ambacho sisi tungeweza kufanikiwa. Mhe. Mwenyekiti, nimeangalia katika *referral hospital* na maeneo tofauti mifano katika nchi. Lakini ukiangalia kwa undani japokuwa na uhaba wa rasilimali na uhaba wa fedha na nyenzo ambazo inayoipata hospitali ya Mnazi Mmoja kuna suala zima la *management* ambalo ni muhimu.

Hospitali ya Mnazi Mmoja inahitaji usimamizi wa hali ya juu, na ili usimamizi uwe ambao unaostahiki ni usimamizi ambao utaotoka juu ukashushwa mpaka chini. Kuna tatizo la usimamizi katika *Medical Officers*, tumesikia hapa wanazungumza lugha zinatoka ambazo hazistahiki, kuna tatizo pia la watendaji ambao ni wa chini hawafanyi pengine kazi zao kwa muda unaotakiwa na kutokana na majukumu yao waliyopangiwa.

Sasa mimi nataka nimshauri Mhe. Waziri pamoja na watendaji ambao wako juu wananisikia, kuna *tool* inatumika katika biashara inaitwa *balanced scorecard* ni kwenye *management*. Unaweza kuwa daktari mzuri sana umesomea vitu vingi unajua kupasua, unaweza kutumia masuala ya *operation*, lakini katika *management* unakuwa tayari wewe pale hupo sawa. Na hospitali lazima

iendeshwe kama kampuni, kwamba unamsimamia mtu wa juu, wa kati na mpaka wa chini ili usimamizi na kazi zao waweze kufanya. Kwa hivyo unaanza kutoka *broader picture* ya huyu anamsimamia wa hapa, anashuka chini halafu wote wanakuwa wanajua wajibu wao na unaweza kusimamia lile sanduku lote zima kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, hii *tool* imefanya kazi sana katika maeneo tofauti na kuleta changamoto, kuondoa katika makampuni makubwa makubwa duniani. *Balanced Scorecard* imetumika katika taasisi ambazo zilizokuwa sio za kiserikali, imetumika maeneo mengi ambayo ni makampuni yamekuwa *successful* duniani. Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anijibu kwamba hii *tool* aiangalie na watendaji wake, alipokee hili wazo la kuona kwamba atajaribu kuiangalia Mnazi Mmoja ili katika *Check and Balance* wasije wakafanya wakaniletea suala la *SWOT analysis*, hapa hatuzungumzi *SWOT analysis*, tunazungumza kwenye suala moja kwa moja la *balanced scorecard.*

Lakini nataka nizungumze suala jengine ambalo pia ningependa nilifahamu ni suala la *incentive* kwa wafanyakazi wetu ambao ni wahudumu katika hiyo hospitali. Nataka nifahamu Mhe. Waziri kuhusu madaktari wetu na wale ambao wanahusika, suala la *retention.*

La kwanza juzi pale hospitali lakini pia nataka nifahamu kwa upande wa madaktari wetu, hawa tunawaangalia vipi katika haya mafao yao pia na mishahara waliyokuwa nayo. Kwa sababu kuna tatizo pia la Mnazi Mmoja kuja halafu na kuondoka au wanaacha kazi. Mimi ninamjua daktari mmoja kabisa wa macho ni bingwa sitaki kumtaja jina, ameondoka hapa amehamia Dar es Salaam, alipofika aliambiwa mkataba huu hapa jaza jiandikie mshahara wako. Na anamjua Mhe. Dkt. Jidawi kama angekuwepo na kama yupo juu ananisikia anamjua nani ninamuongelea.

Sasa hawa madaktari kama wapo wote hawa lazima tuhakikishe mikataba yao wanalipwa fedha kutokana na uwezo wao, wanapokwenda tusikidharau hiki, ni watu na tusije tukasema kwamba hawa sio wazalendo. Mtu yeyote ambaye anachezea mikojo, matumbo, miguu kila kitu anachinja masaa 13, 14, wiki hakuna siku ya kupumzika hawezi kukwambia sio wazalendo. Hamuwezi kumwita Dkt. Faiza, kina Dkt. Mabodi waliopita na hao wengine wote sio wazalendo, pamoja na kina Dkt. Jidawi. Hawa ni wazalendo wamefanya kazi na wanastahiki kupongezwa, na lazima mengi inataka sisi serikali tuwaaangalie hawa. Sasa lazima Mhe. Waziri utakapokuja ututajie katika hawa madaktari

pamoja na ma-*midwives* na wengine *incentives* unakuwa unaziangalia kwa upande gani.

Lakini ningetaka kufahamu pia suala la usimamizi wa madawa, pia hospitali ambayo yanayotoka na yanatokea wapi na usimamizi wake. Je, mnatumia *tool* gani, mnatumia kwenye *push* au kwenye *pull method* kwenye hospitali.

Pia ningependa kufahamu Mhe. Mwenyekiti,kwamba kwenye suala zima la *solid waste management* hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali zote, hii *solid waste management* inasimamiwa vipi, na je, Mnazi Mmoja ile *generator* ambayo iliyokuwepo…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai samahani kidogo kuna tangazo.

Waheshimiwa Wajumbe, nimepata tangazo hapa kwamba Waheshimiwa wote waliopangiwa kuhudhuria katika kikao cha Wabunge wa Afrika Mashariki wafike juu katika ukumbi wa mkutano. Ahsante endelea Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza naenda sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu suala zima la *centralized solid waste management* kwenye hospitali zote wanatumia *pampers*, masindano haya yote Unguja yanakwenda wapi, yanatupwa wapi vitu ambavyo ni vya hatari. Lakini pia katika vitu vya kawaida ambavyo wanatakiwa wawe na *incinerator* ya kutosha ile ambayo haitoi moshi katika mahospitali mengine. Ningependa nifahamu katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ili kuhakikisha Mnazi Mmoja tunakuwa ni hospitali ambayo inayostahiki tunakuwa nayo vizuri. Suala la *echo*, *ultrasound, x-ray, tomography, laboratory*, *generator* na mambo mengine yote hayo ni mambo ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, na hapa ndipo nataka nizungumze, nimezungumza kwamba suala la *generator* Mnazi Mmoja halifanyi kazi na limekuwa ni kero muda mrefu. Nimejaribu kuangalia upande wangu wa mawazo ni njia gani ya mbadala ambayo Mnazi Mmoja wanaweza kufanya.

Mimi kwa upeo wangu napenda kuishauri serikali tunayo ma-*generator* yetu yaliyokuwa kule Saateni Mtoni yanafanya kazi tunapata pale 25 *megawatt* yapo, *demand* ya Mnazi Mmoja haiwezi kuwa zaidi ya *600 KVA.* Hivyo

watafute njia ya kuchukua lile *generator* la 1.5 *megawatt* kutoka Saateni walete pale walifunge katikati wanaweza kupeleka *backup power* wakapeleka katika *State House* ya Zanzibar, wakapeleka Televisheni Zanzibar, wakapeleka Wizara ya Fedha, wakapeleka na Mnazi Mmoja wakatumia *800 KVA* na bado wakabakiwa na *200 KVA* bila ya wasi wasi na fedha zote ambazo Wizara ya Fedha, TVZ wanazotumia kwa ajili ya mafuta wakatia katika *generator* ile tukasogeza kwenye hospitali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani mtu anafanya *operation minor* au *major* inapotokezea kwa kutumia tochi za simu, hata kwenda kumtia mtu *POP* haiingii akilini kwamba Mnazi Mmoja ikose *backup power*. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hata hospitali za Afrika wanakuwa na *free system* za *power* ya umeme, wanakuwa na *inverters* kwenye *theaters*, kwenye maeneo muhimu umeme unapokatika na hata ma-*generator* mengine wanakuwa nayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuwapongeza wale madaktari wetu wote ambao wamefanya juhudi kubwa hasa hawa madaktari wa Cuba, wazalendo kutoka China na wale wanafunzi ambao wame-*graduate* pale waliosomeshwa walioanza kwenye *medical school* ambao wengi walianza pamoja na kina Dkt. Malik, Dkt. Mabodi huko nyuma, nawapongeza wote wale pamoja na Dkt. Mohamed Jidawi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia hawa wazalendo wote wanaofanya kazi katika kuisaidia hii hospitali, mimi nataka nifahamu kitu kimoja. Hawa Mhe. Mwenyekiti, tuna *issue* ya wagonjwa tunaowachukua hapa kuwapeleka India, ningependa nifahamu katika hao wagonjwa wanaokwenda India kwenye muda wa miaka mitatu ni idadi ya wagonjwa wangapi wamepelekwa, na waliopelekwa India imegharamia kiasi gani, na katika gharama ni kiasi gani, na katika gharama waliochukua ni wangapi ambao waliokwenda katika aina za *operation* waliofanyiwa huko India. Kwa nini nasema hivi?

Najaribu kuangalia kama tutaweza kutokupeleka wagonjwa India, kama tumetumia *extra amount of money,* kama tumetumia dola 500,000 kuwapeleka wagonjwa India kwa mwaka, je, hatuwezi tukaleta wale madaktari kutoka India wakaja hapa wakafanya hizo *operation* hapa na watu wengi wakafaidi zaidi? Kwa hiyo, lazima tujue hiyo idadi kwa sababu katika hii hotuba tuliyoletewa na Waziri sina uhakika humu hupati idadi kamili ya wagonjwa waliopelekwa maeneo ya nje na serikali kulipiwa pesa. Kwa hiyo, kama hao wagonjwa tukileta madaktari ikiwa *appendicitis*, ikiwa *knee replacement*, ikiwa ni masuala ya uzazi, masuala pengine ya kensa hawa tuwalete hapa kama

operation 20 pengine pesa tunazotumia tunaweza tukafanya *operation* zaidi ya 300 katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa pia nataka nimpongeze Dkt. Naufal ambaye anasimamia ile *programme* yote *Zanzibar Outreach Program* na wenzake wote walioanzisha ile *program*. *Zanzibar Outreach Program* ni programu nzuri sana na inafaa pia serikali ikaangalia wigo wa *outreach program* ikawa na programu zao wenyewe madaktari bingwa wanazunguka katika maeneo ya vijijini pamoja na Pemba na maeneo yote kwenda kufanya hizi *minor* na *major surgeries*. Kama inawezekana wawe na *medical bus* yao, wana *tools* zao wanaingia kule wanafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ningependa nifahamu nimeona kwenye *news* kwamba basi lile la kuchangia damu limepata ajali. Ningependa nifahamu hili basi linatengenezeka au halitengenezeki? Kama halitengenezeki Mhe. Waziri anajipanga vipi kuweza kutafuta njia ya kupanga uhaba wa damu kuchangia katika *blood bank*, kwa sababu isije ikatokezea mahala hili jambo likaharibika zaidi kama lilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala zima la wazazi wanaopata ujauzito. Tatizo mama anakwenda vizuri miezi tisa lakini hapa mwisho baada ya miezi tisa kwenye *end point* ndio penye tatizo hapa, kujifungua na maeneo ya kwenda na sehemu tu kufika. Juzi Pemba mtu amekufa kwa kupanda mtumbwi kwenda kujifungua. Sasa lazima tuangalie katika hiki tunafanyaje ili kuwatoa wananchi wetu maeneo walipo.

Mimi kwenye jimbo langu Kisiwa cha Uzi hakuna daktari, hakuna chochote kunapelekwa vidonge vidonge kule wanapewa hakuna lolote. Tena kule maji yakijaa usiku kama umekwama ndio nitolee huna njia yoyote, labda upakiwe uwahishwe kwa haraka. Sasa haya yote katika maeneo ya wananchi wetu lazima tuangalie maeneo ambayo akina mama wanapotaka kujifungua tunawatoa vipi katika maeneo.

Leo Mkoa wa Kusini ile barabara mzazi atapitaje pale mpaka umlete kiti, kiti, kiti, miezi tisa inakuwa hafiki. Mhe. Mwenyekiti, watu wanajifungulia njiani, ni hatari tunachokifanya. Kwa hiyo, tujipange, njia katika uzazi wa mama na mtoto tunalindaje. Pia ningependa nifahamu hizi *child mortality rate* iko kiasi gani, tunasema imeshuka, imeshuka kwa ngapi?

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia uhusiano ni kitu muhimu, sisi nchi yetu ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeungana nchi mbili, lakini Waziri wa Afya

anaposafiri nje ya nchi anajulikana Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi ningependa nifahamu Mhe. Waziri yeye anajenga mahusiano vipi na Waziri wa Afya wa Jamhuri, kwa sababu bado yeye ni Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nje ya Jamhuri mamlaka anayo yule Rais wa Jamhuri ya Muungano na ile serikali. Tunalitambua kwamba inapotokea safari tunaalikwa sisi kwenda Zanzibar kushiriki, lakini kwa mfano Mhe. Mwenyekiti nimesoma kwenye gazeti Waziri Mkuu wa India anatarajiwa kuja Tanzania. Mimi ningependa nimfahamu leo Mhe. Waziri wetu yeye kwanza anazungumza Kihindi, anajipangaje kwenda kunufaika kuweza kumpa marogo. Mimi mwenyewe nazungumza Kihindi kama anaweza twende pamoja tukamuombe, *mtaka cha mvunguni sharti ainame*.

Mhe. Mwenyekiti, na katika masuala hayo wanaposafiri hawa watu wanapokwenda nje hawa mawaziri wengine, sisemi kama mawaziri wa Muungano hawafanyi kazi yao, lakini utetezi wao wakati mwengine kwa upande wa Zanzibar wanajisahau. Mtu anaweza kuchaguliwa kuwa Waziri wa Muungano lakini pengine Zanzibar katika maisha yake amekuja mara mbili. Tumeona Naibu Waziri wa Elimu anaulizwa anakwenda *South Africa* anasema kwamba Zanzibar ni Muungano wa Zimbabwe na Pemba. Haya ni mapungufu tumeona sasa haiwezekani, kwa hiyo lazima mawaziri wetu na sisi wapate hadhi, wajenge utaratibu, afya sio eneo la Muungano, elimu sio eneo la Muungano, lakini eneo muhimu tunatakiwa tufanye kazi kwa ukaribu. Mazingira si eneo la Muungano, lakini mazingira yanatu-*cost* sisi sote kwa pamoja, mtu akiharibu kwenye bahari anaharibika mtu Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tujipange, na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na nilisema kwamba miradi yote ya Wizara ya Afya inatakiwa ipelekwe pale, sio lazima wao wanaojipanga, inapotokea safari ya kwenda nje kama ni siku nne kabla lazima wajue mahitaji kule tunapokwenda kuzungumza na wenzetu tujue wanakwenda kuzungumza nini.

Binadamu yeyote, siku hizi maisha ni kujipendekeza, unapokuwa mwanasiasa lazima unapozungumza na viongozi kutoka nchi tofauti uwe na uwezo wa kusukuma ulimi wako, uwe na uwezo na utashi wa kuweza kuwaambia nini mahitaji ya nchi yako, uwe na uwezo wa kumtongoza waziri uwe naye karibu, akufahamu nini mnaweza kufanya kwa pamoja. Hilo ni jambo la mwanzo, mimi naamini Mhe. Waziri wetu wa Afya yeye anatakiwa aondoke ajipange vizuri kwa kutegemea rasilimali ambazo tulizonazo ndani ya wizara yetu na serikali yetu ni chache. Njia moja ya kutoka ni kujenga marafiki na wahisani kuwategemea waweze kutusaidia, na lazima awe karibu na Waziri wa Afya wa

Jamhuri ya Muungano anapokwenda pahala akipewa mashine za *x-ray* mbili kutoka Korea, moja naam ifike Zanzibar, akienda pahala akisikia kapata hiki akadai cha kwetu pia. Hiyo ni njia moja hawezi akatufikiria sisi kwa wakati wote.

Mhe. Mwenyekiti, najua kwamba Waziri wa Afya yeye kule ana nchi kubwa ana watu milioni 44, lakini na sisi pia tume-*surrender* maeneo yetu ya Muungano mambo ya msingi. Masuala ambayo sisi kama nchi hatuwezi kutoka nje ya nchi kujenga mahusiano, na kwa upande wa afya hatuwezi kwenda hata Kenya kuzungumza na Rais Uhuru. Kwa hiyo, lazima waziri wetu sisi katika mazingira haya tuliyokuwa tunayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kupitia Makamu wa Rais lazima zile fursa zinazotokezea za vijana kwenda kusoma maeneo ya utendaji lazima Waziri wa Afya na yeye ahakikishe na anapokuja hapa atupe ahadi yake atalisimamia bega kwa bega na atamleta huyo Waziri wa Afya tuonane nae sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na wengineo pia wafanye hivyo hivyo ili na sisi Zanzibar wananchi wetu waweze kupata hizo neema ambazo wanafaidi kule Bara na sisi tunakuwa tunazikosa. Sio kwa sababu ya serikali inafanya nini, ni kutokana na kwamba mtu anayechaguliwa anakuwa anajisahau kuja Zanzibar na tumeona.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie nataka niende kwenye hicho ambacho umenikumbushia, katika hili suala la *medical economics* nililolizungumza. Naomba sana wagonjwa wanaotaka kupelekwa maeneo ya nje kwenda kutibiwa hizi fedha tuletewe, tupime, ikiwezekana hawa madaktari tujenge sehemu waletwe hapa Zanzibar wafanye hizo *surgeries*, hizi *surgeries* hata madaktari wetu wanaweza kufanya, lakini vitendea kazi.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, leo nichukue fursa kwa mara yangu ya kwanza muda wangu nimeutumia vizuri niwahi hicho kikao ulichonielekeza cha Wabunge wa *East Africa*, nakushukuru kwa nafasi, mimi naunga mkono hoja asilimia 50 naungana na wajumbe wangu juu ya bilioni 7.5 kwamba hizo zihamishwe na baada ya hapo nitasubiri majibu kamili ya masuala ambayo niliyozungumza.

Ahsante sana kwa fursa uliyonipa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana mahala hapa. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe uliyenipatia nafasi hii na mimi nikazungumza machache katika wizara muhimu hii kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee ziende kwa Mhe. Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, watendaji wote wa wizara hii hasa wale madaktari wetu wanaotuhudumia kila wakati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini napongeza sana na nataka nirudie pongezi kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri kipindi kilichopita alikuwa Naibu Waziri wa Afya na tulikuwa tukimpa maswali mbali mbali katika Baraza hili, kwa kweli nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana kwa majibu ambayo alikuwa akitujibu, yalikuwa ya ufasaha kabisa ambayo utafikiri labda zile *terminologies* pengine anahusika kabisa kwamba ni mfanyakazi katika wizara hiyo. Sasa hili lilikuwa linatufurahisha na namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumsaidia aweze kufanya kazi zake vizuri. Pia nichukue fursa hii kumpongeza Naibu Waziri wake ambaye anafuata nyayo zake kwa sasa, anajitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake na kwa kujali afya za wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, tumeelewa Mhe. Rais ametoa ofa mbali mbali katika Wizara ya Afya ili kuona hasa akina mama na watoto wanapata afya njema na wanajifungua katika uzazi salama.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa upande wangu mwenyewe binafsi nataka nimpongeze Dkt. Ali Mohamed Shein na namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri, mimi mwenyewe niliugua kipindi cha nyuma ingawa bado afya yangu haijakaa vizuri lakini nilipopelekewa maombi yangu na Spika kwa Mhe. Rais basi Mhe. Rais kila aliponiona alikuwa ananiuliza, bado hujaenda, bado hujaenda. Kwa hiyo, na mimi ni miongoni waliosafirishwa na serikali hii, nachukua fursa hii kumpongeza sana Katibu Mkuu ambaye aliweza kunisimamia na Wizara ya Fedha ambayo iliweza kutoa fedha hiyo kwa ajili ya mimi kusafirishwa, nawashukuru *in sha Allah* Mwenyezi Mungu atawajaalia kila la kheri katika majukumu yao.

Pia nataka niseme katika wizara hii Mhe. Mwenyekiti hii ni wizara muhimu sana. Kwa kweli fedha zilizotengwa mimi nasema ni kidogo sana, wizara hii ina majukumu mengi na inaangalia maisha ya wananchi wake, ili tuishi salama basi Wizara ya Afya lazima iwe na fedha za kutosha, tuweze kujihakikishia usalama wetu, isipokuwa hawana uwezo wa kulinda roho ya mtu tu, kwa sababu roho mwenyewe anapoitaka haina ujanja. Lakini matibabu na nawapongeza kwa dhati madaktari wetu wa hospitali ya Mnazi Mmoja kwa

kazi kubwa na juhudi kubwa ambazo wanazichukua katika kutuhudumia, Mwenyezi Mungu atawalipa kila la kheri.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka niungane na wajumbe wenzangu waliopita, kwa sababu kulihamisha hili fungu la bilioni 7.5 tukalipeleka katika ununuzi wa vifaa ni jambo muhimu sana. Napenda nichukue fursa hii niwaombe wanawake wenzangu kwa kuwa hili fungu hatulihamishi, kama tunaliondosha ndani ya wizara, tunalihamisha kulipeleka katika ununuzi wa vifaa muhimu ambavyo ninavyojua mimi daktari hawezi kumtibu mtu kama hajaona vipimo sahihi ndio yeye vitamuongoza katika kutibu maradhi ya mgonjwa. Sasa nawashauri tu kina mama wenzangu tuunge mkono hili la uhamishaji wa fungu hili na tulipeleke pale kwenye ununuzi wa vifaa na dawa ili liweze kusaidia katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini mimi pia nina wazo jengine ambalo nataka niwaombe sana wajumbe wenzangu, na kama watanikubalia basi mimi nitafurahi sana. Mhe. Mwenyekiti, nataka tumuunge mkono Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kama yeye anavyochukua juhudi za kupenda afya za wananchi wake, na mimi nataka niwaombe wajumbe wenzangu ili tuwapende sana wananchi wetu ambao wametuchagua na wakatuleta hapa. Naomba turidhie posho letu la siku moja likatwe ili zipelekwe fedha hizi katika kutafuta dawa, hii Mhe. Mwenyekiti kwanza kipindi hiki cha mwezi wa Ramadhani tukitoa pesa hii ndani ya mwezi huu Mwenyezi Mungu anatulipa fungu kubwa, kwa sababu tuko katika ibada, lakini pia tutajihakikishia wananchi wetu na wao watathamini tunachokifanya kwa sababu wataona tunawatakia wao wawe na afya njema. Mhe. Mwenyekiti, naomba wajumbe wenzangu tuliridhie hili ili kwa kuweza kuhakikisha maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamepiga makofi inanipa ishara nadhani watakuwa wamekubali, wakiwa wamekubali nitafurahi sana na *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu atatulipa kheri, kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema ile ufanye wema hata uwe kama chembe ya mchanga Mwenyezi Mungu atatulipa, *in shaa Allah* Mwenyezi Mungu ndani ya mwezi huu atulipe kheri na wema mkubwa juu ya kufanya hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mchango wangu kwenye programu hii ya kinga na elimu ya afya. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niseme wizara ina jukumu kubwa la kuendelea kutupa elimu juu ya kujikinga bila ya kwenda katika tiba yenyewe.

Mhe. Waziri ameonesha katika kitabu chake kama moja ya kinga ni kufanya mazoezi na mambo mengine. Lakini Mhe. Mwenyekiti, siku hizi kumejitokeza mtindo ambao mimi kwa kweli siufurahii, siku hizi tunapokwenda kama kwenye semina ilikuwa kuna ugawaji wa pipi nyingi tunawekewa kwenye visahani, na mwenyewe Mhe. Waziri wa Afya anakuwa yupo. Sasa mimi ningeomba Mhe. Mwenyekiti, hii takrima ya peremende kwa sasa ipungue, kwa sababu ni moja ambayo inatusababishia matatizo, na kuna maradhi mengi ambayo sasa hivi yanajitokeza lazima sisi wenyewe tuweze kutafakari na kuona vitu vyengine havifai kuliwa. Sasa yaani tumejenga utamaduni watoto wetu ma- *chocolate*, mapipi ndio tunawapatia sana wakati tungewapatia matunda tungeweza kuwajenga vizuri kiafya.

Mhe. Mwenyekiti, pia juu ya hili nimuombe Mhe. Waziri aendelee kufanya utafiti wa kina ili kuweza kuyaepuka yale maradhi ambayo yasiyoambukiza. Mhe. Mwenyekiti, niombe afanye utafiti kwa sababu tuna wafanyakazi wetu ambao wanashughulika kule katika *x-ray,* je hawa tuna uhakika gani kama na wao hawapati athari juu ya vile vitu wanavyovitumia katika kazi zao ili tukaweza kuwanusuru na kutokupeleka yale maradhi ambayo yanaweza kuepukika.

Mhe. Mwenyekiti, hata watumiaji wa kompyuta tungefanya utafiti huo na wao kwa sababu muda mwingi wanazitumia hizi tukaweza kuona labda kama kuna mambo yanawatatiza basi tukaweza kuwaepusha nayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika ile programu ya afya ya uzazi wa mama na mtoto.

Mhe.Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema nampongeza Mhe. Rais kwa hatua hii ambayo ameichukua, lakini ndani ya hili Mheshimiwa katika kitabu chako umetueleza kama ili wanawake waweze kujifungua vizuri umeandaa utaratibu wa kuweka kina mama hasa katika Wilaya yangu ya Kaskazini B nimeona kwanza nasema hongera juu ya hilo, lakini pia mimi nilitaka kujua labda hao kina mama katika Wilaya ya Kaskazini B wapo katika vituo vyote ili tuweze kuwafata kina mama hawa tuweze kubadilishana mawazo na kuendelea kuhakikisha wale kina mama ambao wanawashughulikia basi wanaweza kuwashughulikia vizuri, nilitaka ukija unieleze kama hawa kina mama wako katika vituo vyote vya Wilaya ya Kaskazini B nilitaka kujua hilo. Nitoe hongera sana kwa mambo haya ambayo mnayafanya yanaendelea kutupatia usalama zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoomba bajeti hii ni ndogo naomba sana serikali Wizara ya Fedha iangalie. Mhe.Mwenyekiti, nina kituo cha Donge, pale kina mama wanakitumia sana kwenda kujifungua na kwa kipindi hichi hawana daktari, naomba sana Mheshimiwa uliangalie kwa jicho la huruma ili kina mama wale wasisumbuke nyakati za usiku wanapokutwa na shida ya kutaka kujifungua.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe wenzangu sana kuiangalia Wizara ya Afya kwa jicho la huruma sana na hasa ukizingatia wizara hii kuwa inapambana na majukumu mengine ambayo hawakuyatarajia tuliangalie suala la kipindupindu lilivyojitokeza ambapo serikali iliacha kufanya majukumu yake mengine na ikaweza kulishughulikia hili; hivyo tuone basi umuhimu wa wizara hii, na kwamba saa nyengine inapanga mambo inakuwa na malengo lakini inashindwa kuyatekeleza hasa pale linapotokea tukio kama hili la dharura la kuweza kuhami wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu wote waiunge mkono hoja na tuendelee kuiombea na kutaka kila la kheri ili iweze kupatikana katika wizara hii ili afya zetu ziendelee kuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Panya Ali Abdalla, anafuatia sasa hivi Mhe.Miraji Khamis Mussa na Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mhe. Mihayo ajitayarishe pamoja na Mhe. Dkt Makame Abdalla Ussi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nishukuru na mimi kunipa nafasi kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya Wizara ya Afya.

Pili niwapongeze sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri na Watendaji wote wa wizara hii kwa jukumu kubwa sana walilopewa na Mhe. Rais la kumsaidia, lakini pia naomba pia niwape pole sana kwa sababu wana eneo moja zito sana, lakini *in shaa Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu naomba awape nguvu, awape busara na hekima ili waweze kutumikia nafasi hizi na lile lengo la serikali liweze kutimia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaomba nianze na Chumbuni, kwa sababu mengi yamezungumzwa kupitia kwa ujumla wake, naanza na Chumbuni kwa sababu nina mwezi wa tisa sasa ninakosa huduma kwa wananchi wangu, jambo ambalo

linanikereketa sana na lazima nisimame hapa kuwasemea wananchi wangu, sitofanya busara kama sitawasemea. Kwa sababu sisi viongozi wa Jimbo la Chumbuni tulizunguka sana kwenye ilani na tukaahidi kusaidia huduma za afya katika Jimbo la Chumbuni, ikiwemo kuboresha kituo kile kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, tumeahidi pale kupeleka *ambulance* moja, tumeahidi kujenga ukuta ambao sasa uko katika hatua nzuri, lakini tumeahidi pia katika kipindi chetu cha miaka mitano kujenga banda ambalo litasaidia kuendeleza huduma katika kituo kile.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa katika kadhia ya kipindupindu imehamia Chumbuni, kwenye kituo cha wananchi wa Jimbo la Chumbuni sina tatizo na uwekwaji wa wagonjwa wa aina hii ya kipindupindu kwa ghafla hii iliyotutokea, lakini muda mrefu na sijaona mpango wa serikali na tunakoelekea huko ziko non'gonon'go ambazo akija Mhe. Waziri, ni busara akaja akanifafanulia vizuri kama ile hospitali wameichukua basi ajibu ili wananchi wa Jimbo la Chumbuni wajue, lakini sisi tuna busara sana wakichukua ile tutajenga nyengine, lakini serikali itamke kuwa hii hospitali tunaichukua sisi, yako maeneo ya serikali tutaendelea kushauriana nao ili ile dhana yetu ya kujenga banda moja pale basi tuanzishe utaratibu mwengine lakini sio kuendelea kukosa huduma kwa muda itakuwa sio haki. Kwa sasa hivi sisi tunasubiri lakini majawabu hayapo, kwa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja atupe *plan* ya serikali kwenye kituo cha afya cha wananchi wa Jimbo la Chumbuni.

Mhe. Mwenyekiti, Naeleza haya kwa masikitiko ya kuonekana huduma nyingi sana tunazikosa, kulikuwa kuna *plan* tayari serikali imeandaa na jengo lipo limejengwa karibuni la kujifungulia mama zetu pale. Sasa leo huduma ile imesita na sisi tuliharakiza kuagiza *ambulance* kwa sababu itakapotokezea tatizo tuweze kufanya *transfer,* sasa hizo *ambulance* za kipindupindu zinakuja hapa lakini tunajua sio zetu na hatujajua mpango wa serikali, lakini tukasema sisi tusaidie eneo hilo. Kwa hiyo waziri nakuomba sana kaka yangu mimi sitazuia fungu katika eneo lolote katika bajeti yako lakini nijibu vizuri sana ili wananchi waridhike, na tujue basi serikali ina nia njema na thabiti ya kuwatumikia wananchi wake hususan wa Jimbo la Chumbuni katika eneo la afya.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba niondoke hapo niungane na wenzangu sasa kuelekea katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hii Hospitali ni Hospitali ambayo tunaitegemea Wazanzibari sote na sehemu ya watanzania waliopo katika eneo hili la Zanzibar. Lakini katika *department* ziliokuwepo pale karibu zote zina matatizo, kama hakuna tatizo la wataalamu basi kutakuwa kuna tatizo la vifaa,

kuna tatizo la dawa. Hospitali hii ndio kimbilio la wanyonge wa Zanzibar hii, sasa leo ukienda *ICU* siku ya mgonjwa wako kufika kule unaambiwa *oxygen*, na mbaya zaidi siku moja kuna mtu ana mgonjwa wake ambaye anatarajiwa kuingia mle akaambiwa *oxygen* hamna, *oxygen* iliyokuwepo imewekwa akiba kwa ajili ya Waheshimiwa ah! sasa tumepata mashaka *oxygen* unaweka akiba kwa ajili ya Waheshimiwa, mnajua tutaumwa lini sisi, wale wanaoumwa wanakosa huduma ya moja kwa moja, sasa lazima *oxygen* hii ipatikane katika *ICU* yetu pale, tunajua ni gharama kubwa lakini kauli ya serikali ambazo zinatoka hapa huwa serikali haiogopi hasara, haiogopi gharama, kwa hiyo naomba sana katika eneo hili tujipange Mhe. Waziri ili kunusuru sehemu ya watu wetu ambao wanalazimika kuingia katika chumba hichi pale ambapo linatokezea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nihamie sasa katika kitengo cha hisia. Katika kitengo cha hisia hapa tumejenga jengo zuri lakini karibu miaka minne sasa tunategemea madaktari kutoka Spain waje pale wafanye tiba au *operation* wiki mbili tatu wanaondoka wanatuachia sisi wagonjwa ambao vidonga vyao havijapoa. Miaka yote hatujaona hata mpango wa serikali kutuwekea mtaalamu katika eneo hili, ni tatizo kubwa sana.

Leo hii wenzangu wamezugumza tunataka kwenda kwenye rufaa, katika hali ya kawaida hapa ulipo kuna asilimia 9 hiyo rufaa unaipataje, unawahamasisha vipi watu; kwa hiyo eneo hili lina changamoto kubwa, halina wataalamu lakini hata hayo maeneo mengine, ukienda katika eneo la kuyatambua hayo maradhi wenzangu wamezungumza hapa, maana hakuna eneo muhimu kama la ugunduzi wa maradhi.

Leo *x-ray* tunayoitegemea hiyo ya zamani nayo inakwama, ile ambayo ilikuwa ipo kubwa pale muda mrefu tu serikali imeitengeneza sasa hivi imeiacha, kwa hiyo huduma ile upatikanaji wake sio mzuri. Sasa lazima eneo hili la ugunduzi wa maradhi ndiyo linalomfanya daktari atibu, kwa hiyo leo tunazungumza hapa sisi, tunaiambia serikali lakini baadae hakuna muendelezo wa kitu chochote kwenye eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, wataalamu, leo ukishapiga *x-ray* umsubiri mchina mpaka anafasike kuja kukusomea *x-ray* yako, ingawa tuna mmoja tu pale, sasa lazima akija waziri aoneshe *plan* ya serikali, hatuwezi kutegemea mtu mmoja kwenye eneo muhimu la ugunduzi wa maradhi, serikali lazima itenge bajeti ya kuongeza wataalamu, hata ukienda *ENT* unamkuta daktari mmoja tu na hili waziri hanisuti, leo haumwi huyu, leo huyu hana likizo, maana akienda huko hiyo huduma inasita hospitali gani, kuna mtu mmoja mmoja, uende maabara

kule na huko utamkuta mmoja peke yake, hata wale wataalamu wa kusema leo serikali inasomesha iwe na mkakati madhubuti ya kuongeza wataalamu hamna. Sasa akija waziri atwambie mpango wa serikali katika kuongeza wataalamu hatuwezi kuwa na Hospitali kubwa ambayo wanyonge wanaitegemea, ukienda katika *department,* aidha hakuna au kuna mtu mmoja mmoja, tunaonesha nini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana maana hapa serikali ukisema sana hivi kuna wengine wanainuka wanakwambia uombe radhi, na sisi tunataka kusaidia wananchi wa nchi yetu. Mimi sitakuja kuinuka na kuomba radhi niko tayari kupata adhabu, lakini lazima serikali tuiambie kwenye eneo muhimu hasa hili la afya, tunawaombeni sana viongozi, na pia tunaiomba serikali kuu kupitia Wizara ya Fedha, mwenzangu kasema hapa, lazima fedha tuwatilie kwa wakati.

Tunaendesha kampeni za kuongeza madawati kule, lakini tunawasahau watu katika afya zao watasoma vipi, kampeni hizi ziende, Mhe. Panya hapa kasema kawaomba wajumbe wachangie, na mimi niko tayari kuchangia na yule mmoja kawaomba wanawake, lakini kwa sababu na mimi mke wangu mwanamke pia nitaku-*support,* lakini tuhakikishe fedha hizi tunazihamisha kwenda katika eneo muhimu la kununua *x-ray*, tukaongeza dawa na *plan* ya serikali basi tutakuja kuwa-*support* kwenda katika rufaa, lakini alau hapa waoneshe nia ya kuelekea huko sio sasa, sasa hatujafikia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nihamie Hospitali ya Wagonjwa wa Akili (*Mental Hospital*). Jamani lazima na huruma, wenzetu hawa hawakwenda pale kwa kutaka, mazingira yao magumu kweli kweli. Namuomba sana Mhe. Waziri, tusiwaongezee *assignment,* maana wanakwenda pale wana kichaa kichwani mwao, maana ndio ugonjwa huo, unakwenda kumuongezea kichaa chengine, maana unakwenda kule unakuta katika mazingira magumu baada ya yeye ku-*relax,* huduma hakuna tunategemea nini, namuomba waziri ajitahidi sana eneo hili ni eneo gumu kweli kweli. Ukienda kutembelea kule utaona huruma sana, huyu mwenzetu kalia humu lakini wewe unakwenda *field* ukalia kule, tujitahidi sana.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende katika eneo la damu salama. Damu salama nako hakuna huduma ni eneo muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, na namuomba sana Mhe. Waziri, leo hii tunapozungumza hapa kuna mwanachama ambaye ana kipande hasa cha kupata huduma ile na anachangia ana mgonjwa wake damu hakuikuta, leo hii ninapozungumza hapa, anachangia na damu hakuikuta. Sasa anaanza sasa kwenda kutafuta watu wa ziada kwenda kumtolea damu ambayo itachunguzwa saa ngapi, mgonjwa kule anataka damu kwa wakati, lazima tuendeleze kampeni ya kuchangia damu lakini tuweke juhudi za

makusudi ili eneo hili nalo lisiwe na kasoro kubwa ni hatari, tuwasaidie wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuelekeza maelezo yangu kwenye Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi na naomba sana Mhe. Waziri umenisikiliza sana kule tokea Chumbuni lakini na hapa nisikilize tena. Eneo hili linalalamikiwa sana, wana jitihada nzuri, wanafanyakazi vizuri, wamedhibiti vitu vingi, mimi nawapongeza sana. Lakini bado kuna wafanyabiashara wanalalamikia sana, si kwa kutengeneza maslahi yao lakini kwa kutengeneza utaratibu mzuri katika kuingiza biashara kutoka nje ya nchi, kuna kampuni iliwahi kuwasafirisha watu wanne, watatu ni wafanyakazi pale lakini mmoja ni mmiliki, kwa sababu huwezi kuwasafirisha watu kama na wewe mwenyewe hujawapeleka, akenda katika kiwanda kimoja Marekani kwenda kukagua, kwa sababu anasema huwezi kuingiza mzigo wa aina fulani mpaka uwapeleke watu nje, ni jambo kubwa sana kwa wafanyabiashara wanaotafuta maisha, wamepelekwa watu kurudi mfanyabiashara huyu kakosana na *supplier* katika ku-*deliver* mizigo kaamua kwenda Poland, leo anaambiwa tena wapeleke Poland.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tuangalie serikali imeanzisha bodi ile *ZBS* ambayo inaenda kuangalia viwango vya *product* zote zinazotoka nje na tuna ma-*agent* kote duniani kwa nini tusiitumie ile kuvitambua viwanda, kuwatambua hizo *grades* ambazo zinatengenezwa ili wakashirikiana na bodi kuondosha kadhia hii; wafanyakabiashara kama mimi ambao tunachunga pesa za wakulima, leo unaenda kuingia katika biashara fulani kuwasafirisha watu wanne maana watu wanapoteza dola elfu kumi kwa hatua ya mwanzo.

Kwa hiyo Mhe. Waziri, naomba sana nipate majibu kwa sababu bodi wana uwezo mzuri, moja ya nafasi waliyopewa ule mzigo ukiingia hapa wanaukagua na wanapewa majawabu, na jawabu likiwa silo wanakwenda kuuangamiza, wamefanya kazi kubwa nasema na nawapongeza sana. Lakini kunako eneo hili hatuoni kama kuna ukaribu wa kuwakaribisha wafanyabiashara katika maeneo muhimu haya, hasa la hawa wanaoleta *chicken porter, sausage*, *chicken*, kwa hiyo eneo hili Mhe. Waziri liangalie sana linaleta manung'uniko makubwa, watu wanataka kufanya biashara, bodi tunaiiomba sana iangalie utaratibu mwengine ambao utakuwa una manufaa kwa wote, mzigo ukifika waangalie, hauna viwango wauangamize kama utaratibu, lakini leo hii tunapelekwa Marekani, mfanyabiashara anakosana na supplier upelekwe Poland, *supplier* unakosana naye tena upelekwe Brazil, sioni kama itakuwa ipo haja ya msingi katika wananchi wetu tumewaambia wajiajiri katika eneo hili tunawakandamiza kwa hali

ngumu kweli kweli. Naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja anipe maelezo ya kina kwenye eneo hili

Mhe. Mwenyekiti, lakini na mimi nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia 75, 25 naweka nikipata majawabu mazuri nitaondosha. Sitoi pahala shilingi lakini na asilimia 75 za kuunga mkono ili nitengenezee vibuti viwili vitatu kwa kuzuia fungu mpaka nipate jawabu nzuri.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi asubuhi hii ya kuweza kuchangia.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutufikisha hapa tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru sana Waziri wa Afya pamoja na *team* yake yote kwa hotuba yao nzuri ambayo imetupa changamoto mbali mbali katika vituo vyetu vya afya.
Mhe. Mwenyekiti, mimi niende katika ukurasa wa 39 unaosema huduma za kupandisha hadhi hospitali za wilaya na vijiji. Mimi naelekea katika Hospitali ya Abdalla Mzee iliyopo Mkoani.

Hospitali ile mara nyingi tunaambiwa inapandishwa hadhi lakini hadhi yake inakuwa ni ndogo, tunajua kwamba sasa hivi tunajengewa jengo kubwa, zuri ambalo litakuwa na huduma mbali mbali, lakini wasi wasi wetu ni ukosefu wa madaktari katika hospitali ile.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali iliyopo Mkoani pale tunaletewa wafanyakazi ambao wanatoka katika masomo wanakuja pale kwa muda wa miaka miwili. Baadhi yao ile miaka miwili haifiki wanatoa dharura na wanaondoka, wananchi wanapata tabu sana kwa sababu wanatoka wananchi kutoka Wete, Chake Chake wanakimbilia pale hususan wale wagonjwa ambao wamepata ajali za kuanguka wakaumia katika mifupa. Daktari aliyeko pale ni Dokta Kirau peke yake, Kirau huyo mmoja atafanya kazi kwa watu wangapi kwa siku moja. Namuomba Mhe. Waziri aliangalie kwa kina juu ya kuipandisha hadhi zaidi ile Hospitali ya Mkoani sio jengo tu, bali ni wafanyakazi pamoja na vifaa vya kisasa, ili wananchi wapunguke na ile kupata tabu ya kusafirishwa mara kuja Hospitali ya Mnazi Mmoja au apelekwe nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile sasa nije katika hospitali yangu iliyopo Chambani. Ndani ya jimbo langu ninavyo vituo vya afya vitatu, lakini kituo kimoja

ambacho kipo Ukutini kituo kile kilitolewa ahadi kwamba kitakuwa ni hospitali ya rufaa kwa mama wajawazito pamoja na watoto, itaunganisha Chambani, Chonga na kituo kilichopo Mtangani, lakini mpaka sasa ukienda hata yule daktari aliyepo ni mmoja tu, na huyo mmoja atashughulika kwa mama wajawazito, ashughulike mpaka na wagonjwa wa kawaida. Huu ni uonevu, yule ni binadamu kama binadamu mwengine. Tumuombe Mhe. Waziri atupelekee madaktari wa kutosha, na kama hakuna madaktari basi ni lazima sasa hivi serikali ifanye juhudi za kutosha kuwasomesha wale watu ambao wako katika vijiji na wanaweza kuhudumia vizuri wananchi.

Kwa mfano, tulikuwanao pale watoto wetu ambao walikuwa ni *red cross* katika Hospitali ya Abdalla Mzee, wale walikuwa wakifanya kazi vizuri, wakijituma wakati wowote hawakujali kama muda huu mimi ni wa kuondoka au laa, wao wanafanya kazi kwa kujituma. Lakini kwa bahati mbaya wale watoto ndio waliondolewa pale na mpaka hii leo hawapo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika hospitali ya Wambaa. Wambaa ni mbali na kituo kilichoko kule ukikiangalia Mhe. Waziri si kwa kuwa na daktari mmoja hatoshi, kituo kile kina watu wengi, kimechukua mpaka kutoka Tumbi na kwenda Wambaa si sehemu ndogo sana. Mhe. Waziri namuomba atuongezee madaktari.

Sasa nakuja kwenye kituo kilochopo hapo hapo Ukutini, kituo kile hakina kifaa hata kimoja cha mama na watoto, mtu kama kaletwa pale kuja kujifungua imetokea *emergency* tu basi ni tatizo, na watu wengine wanatoka sehemu mbali mbali.

Nimuombe sana Mhe. Waziri aniambie au awaambie wananchi wangu wa jimbo la Chambani lile lengo lililokusudiwa pale litatendeka mwaka gani? Kila siku zikiendelea basi tuna ukosefu mkubwa sana, tuliambiwa meno yatang'olewa pale lakini hatuoni kitu, tuliambiwa wagonjwa watakuja wakipimwa mpaka sukari pale lakini hata hicho kifaa hapana. Lengo la wananchi ni kupata mafanikio katika majimbo yao sio kuwekewa majengo tu. Mhe. Waziri atakapokuja hapa awaambie wananchi wa jimbo langu la Chambani vipi atawasaidia katika huduma hizi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika jimbo langu hilo hilo nimepakana na Wilaya ya Chake Chake, Wilaya ya Chake Chake imeanza Mpakani na kutoka Mpakani mpaka kufikia Mtambile ndio kwenye kituo cha afya. Mhe. Waziri pia paliwekewa ahadi na serikali pale kwamba patajengwa kituo cha afya. Hivi sasa wananchi wako tayari kutoa sehemu ya kujengwa kituo cha afya. Kwa

hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana na wananchi wangu wa jimbo la Chambani awaambie kwamba hili kweli litajengwa na mwaka gani endapo litafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tuje katika wafanyakazi, wafanyakazi wetu baadhi yao wana matatizo ya kutokuwa pamoja kwa mashirikiano na masheha walioko katika shehia, wanafanya maamuzi wao wenyewe bila kushirikiana na wale masheha wetu. Tunaamini kwamba masheha na wao ni watu wa serikali, linapotokea tatizo kwa daktari aliyemo katika shehia basi ni lazima alisimamie kwa kina pamoja na ile kamati ya afya. Lakini baadhi ya vituo vyetu haionekani kama sheha wanashirikiana vizuri na madaktari wale waliopo. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atapokwenda kwenye vituo vyetu basi awaelekeze vizuri madaktari wetu ili waweze kushirikiana na masheha waliomo katika vituo vile.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja hii kwa asilimia 85, asilimia 15 mpaka Mhe. Waziri atakapowaeleza vizuri wananchi wangu wa jimbo la Chambani kuhusu upatikanaji wa vifaa Shehia ya Ukutini pamoja na madaktari wa kutosha kwa alivyojipanga katika hospitali yetu ya Wilaya ya Mkoani.

Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nami kwa kunipa fursa hii kwa kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Afya. Kwanza kabisa nichukue fursa hii ya dhati kupongeza na kupongeza ile nia ya dhati ya Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein ya kutaka mabadiliko hasa katika sekta ya afya.

Tunafahamu sana Mhe. Rais ana nia thabiti kabisa ya kutaka kuleta mabadiliko na dhamira yake ya kutaka kuwasaidia Wazanzibari wanyonge ambao wanapata fursa ya matibabu katika maeneo tofauti.

Pili, nimpongeze Mhe. Waziri sambamba na Naibu Waziri kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya na changamoto kubwa wanazokumbana nazo, kwa sababu katika sekta hii nayo ina mitihani mingi sana. Sasa tunafahamu lakini tunasema msipothubutu watu watawachezea, hivyo ni vyema kule ambako kuna dosari zinaonekana na kasoro zikafanyiwa kazi kabla maeneo yale hayajakubuhu.

Tatu, niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati ambao waliona ni busara kabla ya kuja kuwasilisha ripoti yao waende wakatembelee hasa katika maeneo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na katika eneo la Bohari Kuu. Leo bila ya wajumbe hawa tusingejua kwamba kwa kipindi cha miezi sita sasa Bohari la Dawa halina dawa za kutosha, tuwapongeze sana.

Hapa hapa Mhe. Waziri hii ni changamoto kwake kwamba tujue wakati tunawasilisha bajeti hii tayari hatuna *stock* ya kutosha ya dawa jambo ambalo tutakuwa ni *disaster* kwa kipindi cha miezi mitatu, minne inayokuja. Maana huwezi kupata huduma kwa kumuhudumia mtu kwa kumpa kidonge cha *panadol* tu.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika michango yangu ambayo nimeikusudia kusema. Nianze kama wenzangu walivyotangulia kusema nami nianze na huduma za afya katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Tuna dhamira njema sana ya kuwasaidia Wazanzibari lakini katika hili penye ukweli tuseme, huduma za afya katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni mbovu, huduma za afya katika hospitali hii hazikidhi haja, hakuna hata kitu kimoja ambacho kinamshawishi leo Mzanzibari mnyonge anayekwenda pale kupata huduma. Bahati nzuri wapo watu ambao wanajitahidi lakini *management* ya Mnazi Mmoja sio nzuri, hii lazima tuseme, kama tuna *management* mbovu, hatuna huduma tutakayoweza kuifanya pale.

Bahati nzuri mimi na Mhe. Waziri huwa tuna mawasiliano, siku moja niliwahi kwenda pale tulikuwa na mgonjwa ni jambo la kusikitisha unakwenda *OPD* hakuna *gloves*, anapokuja mgonjwa kapata *injury* kidogo hata yule mtu anayehudumia anaona tabu kumshika kutokana na damu anayotoka. Sasa hatuwezi kuwafanya watu wakawa wanahudumia watu katika mazingira kama haya, *motivation* katika maeneo ya kazi pia ifanyike, lakini vile vifaa vyao ambavyo wanavihitaji wavipate katika muda stahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri kufanya mawasiliano na Mhe. Waziri akashusha ile *roda* kumbe bahati nzuri yule mtu aliyekuwa na nafasi *gloves* anazo lakini kakaa nyumbani kwake tu, kwa sababu ni *week end* kafunga ofisi. Sasa haiwezekani, inafikia kipindi serikali inaangamiza vifaa, inachoma moto kwamba vimepitwa na wakati hali ya kuwa kumbe vyengine vipo havitoki kwa wakati. Tumuombe sana Mhe. Waziri na tuiombe serikali *management* ya Hospitali ya Mnazi Mmoja mbovu, kama hatutajirekebisha hili hatutakuwa na sababu ya kuipandisha hadhi hospitali hii, kama hatutakuwa na *management*

nzuri ya uongozi wa hospitali ile jambo ambalo hawa watu wakaweza kuwa *creative* na kuweza kutoa hizi huduma nyengine.

Sambamba na hilo nami niungane na wajumbe wenzangu waliopita, leo tumetenga kiasi cha shilingi bilioni saba na takriban shilingi milioni mia tano na kidogo kwa dhamira ya kuipandisha hadhi hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Lakini hatuwezi kupandisha hadhi hospitali hii hali ya kuwa hata picha kwenye *X-ray* tu hakuna.

Mhe. Rais ana dhamira njema sana ya kuwasaidia Wazanzibari na keshasema huduma ya afya iwe bure, lakini kama huna shilingi 35 elfu mpaka 40 picha hujapiga Hospitali ya Mnazi Mmoja, utaambiwa picha hakuna leo, kesho hakuna siku utakayokwenda na pesa mkononi ndio siku utakayoweza kupiga picha. Sasa tuambiwe hizi picha zipo, hii *x-ray* nzima au mbovu, haya mambo yote Mhe. Waziri lazima tujue ili kuweza kujipanga sasa kuweza kuipandisha hadhi Hospitali hii ya Mnazi Mmoja, la si hivyo itakuwa vichekesho. Kwa sababu tutakapoipandisha hadhi hii itakuwa bora mtu akatibiwe kwenye kituo ambacho akienda atakutana na daktari atamdanganya kuliko kwenda sehemu asipate huduma.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana wenzetu wa Wizara ya Afya wajitahidi katika kuwahudumia wananchi katika sekta hii, maana sekta hii ni moyo wa Wazanzibari, tutakaposhindwa kuwa na huduma nzuri za afya tayari hatutakuwa na kitu kizuri cha kuwahudumia watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumzie katika eneo letu la Pemba hasa katika sekta ya afya. Tunasikia mengi, yanasikika mengi hakuna haja mpaka leo muajiriwa wa serikali anayefanya shughuli ya umma kuhudumia wananchi anagoma eti kisa mambo ya itikadi za kisiasa, hatuna sababu ya kuendelea kuwatizama.

Mhe. Waziri na Katibu Mkuu wao ni watu makini hakuna sababu ya kuendelea kukaa na watu ambao wanaleta *sabotage* za kuacha kuwahudumia watu katika sekta ya afya, si jambo jema. Hawa wanaogoma si vyema lakini hatuwezi tukaendelea kuwafumbia macho, ni vyema hatua stahiki za haraka zikachukuliwa kwao kwa dhamira ya kupata kuwasaidia watu kwenda kupata huduma nzuri zinazostahiki katika nchi yao.

Watu wana matumaini sana na serikali hii ya Dkt. Ali Mohamed Shein. Sekta hii ya afya inafarijika sana kumpata Rais ambaye anayetokana na *field* ya afya, lakini leo watu wachache wanafanya mambo haya makusudi kabisa kumfelisha

Mhe. Rais. Sisi tuliokuwemo humu hatuwezi kukubaliana na hali hii, lazima wenzetu wa serikali waweze kulifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema sasa nami niungane na wenzangu kulichukua fungu lile la shilingi bilioni saba na milioni 500 kuweza kwenda kununulia madawa, vifaa vya *CT Scan* na *X-ray* kwa dhamira ya kwamba sasa iwe imetosha, maana *X-ray* ukienda kuitafuta kwenye hospitali za *private* utaambiwa shilingi 50,000; kuna baadhi ya maeneo utaambiwa shilingi 180,000, kwengine ukitaka kupiga *X-ray* kichwa utaambiwa kama huna shilingi 200,000 hujapiga *X-ray*, hatuwezi kuona wananchi wanyonge wakabaki kuwa wanadhalilika na kuteseka kwenye taifa lao. Hii ni Serikali ya Kimapinduzi lazima tuboreshe huduma hizi za afya kwa dhamira ya kuwaokoa wananchi wanyonge, kama hatujafanya hivyo hatutakuwa tumewatendea haki Wazanzibari, kama hatujaboresha sekta hii ya afya hatutawatendea haki Wazanzibari kwa ujumla.

Mimi niombe sana, na natambua sana serikali yangu hii sikivu, na kwa kutambua jitihada za Mhe. Waziri na Naibu Waziri hasa kwa kuzingatia huyu ni mtoto wa Mwanamapinduzi, atakuwa na dhamira thabiti kabisa ya Mzee wake, Mzee Thabit Kombo. Kwa kufanya hivi ndio tunaweza kutetea watu, hatuwezi kutetea watu kwa kuwanufaisha watu wachache.

Mhe. Mwenyekiti, hilo nilikuwa nataka kulizungumzia hivyo. Lakini jengine pia leo tunajiandaa na huduma ya bima ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana serikali kwa kulifikiria hili kwa dhamira ya wafanyakazi wetu wa serikalini na wao waweze kupata huduma ya afya kwa kutumia bima zao atakayeweza kuzilipia. Naipongeza sana serikali na wizara kwa kutumia jitihada hiyo, lakini pia huduma hii leo pale Mnazi Mmoja wapo watu wanaokwenda na huduma ya afya lakini kama hajatoa pesa *extra* bado hajahudumiwa. Kwa sababu yule mtu ambaye anatoa huduma ile anaona huyu mtu hajaja na pesa yake mkononi kaja na kipande chake apate huduma, apate na dawa, si kitu kizuri kwa watu kama hawa.

Mhe. Mwenyekiti, hili mimi nalisema kwa sababu wiki moja iliyopita nilimpeleka mtu kwa kutaka kupata huduma kama hii na alikuwa anatumia bima ya afya basi hakupata huduma hii kwa ukamilifu, kila anapokwenda anapigwa danadana akienda huku anapigwa huku si kitu kizuri, dhamira yetu ni kuwa tunataka kufanya huduma hii kuweza kuwasaidia wafanyakazi wetu.

Tunajua kabisa serikali hii ina changamoto nyingi ambazo inakabiliana nazo, lakini naiomba sana serikali na Mhe. Waziri na wizara yake, kwa ujumla pamoja na Katibu Mkuu, ni vyema sasa kama tuna dhamira ya kuweka huduma hii ya bima ya afya katika hospitali zetu za serikali hasa hospitali yetu ya Mnazi Mmoja tukaboresha na tukaweka kitengo hiki maalumu kitakachoweza kuwahudumia watu watakaokwenda pale na tiba ya huduma ya bima ya afya, *otherwise* watu wote watakaopata bima ya afya watakwenda tu, watakwenda *Global*, watakwenda *Al-Rahma* na kuikosesha mapato hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Tunafahamu kwamba leo wenzetu wa bima ya afya wanatwambia wana-*spend more than 1.7 billion per year* kuwalipa Hospitali ya *Al-Rahma* kwa huduma ya bima ya afya tu, na ukizingatia watu wengi wanaokwenda kule ni wale ambao wametokana na Taasisi za Serikali ya Muungano wa Tanzania ambao tayari walikuwa na huduma hii hapa. Si sahihi kiwango hichi cha pesa kingekuwa kinafika katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kingetumika vizuri na hospitali hii ikapata kujiendesha si kiwango kidogo 1.5 bilioni pesa nyingi sana. Sasa Mhe. Waziri ni vyema tukaboresha huduma hii ya Bima ya Afya na angalau tukaipa msukumo ili sasa wafanyakazi hawa wa serikali na wenyewe wafarijike na huduma pamoja na Serikali ya Mapinduzi iliyokuwepo madarakani.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nizungumze suala la madawa. Jambo la kusikitisha sana vituo vyetu vya afya bado hatuna madawa ya kutosha. Jambo ambalo linatia unyonge kwa mtu ambaye tayari keshapewa matumaini ya kwamba anapata huduma ya afya bure kumbe ukibahatika bure ni kumuona daktari tu lakini kila kitu kinalipiwa. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nina imani sana kwa hii sio dhamira ya Mhe. Rais. Mhe. Rais bado ana dhamira njema sana isipokuwa bado kuja watu watakuwa wana dhamira ya kufanya uharibifu ya kuhakikisha Mhe. Rais katika sekta hii ya afya anafeli.

Sasa mimi niwaombe sana bahati nzuri mara hii tutapambana sana katika maeneo haya, kama ikiwezekana hata kwenda kwa Mhe. Rais msione tabu kuwawajibisha watu wachache ambao wanailetea uharibifu serikali hii ya Mapinduzi ambayo ina dhamira ya kuwasaidia watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la vituo vya afya kuna Wilaya zimegaiwa tulikuwa tuna Wilaya ya Magharibi leo tuna Wilaya ya Magharini A na B, na bahati nzuri Wilaya ya Magharibi A imebahatika kuwa na kituo cha afya kikubwa cha Mbuzini ambacho bado hakijakamilika kilitokana na Mfuko wa Halmashauri. Lakini kwa maongezi ya muda mrefu wenzetu wa wizara ya afya tayari

mlikuwa mshachukua jukumu la kukisifu kama kuwa Hospitali ya Wilaya kama ambavyo Mhe. Rais alitoa agizo lake.

Tunatambua sana kama mna mambo kama mtakimalizia kituo hiki na Hospitali hii kuwa ni Hospitali ya Wilaya ya Magharini A tutawapunguzia sana wananchi wengi huduma ya kutoka huko katika maeneo ya mbali na kwenda kusongamana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tuwaombe sana wenzetu wa Wizara ya Afya mtakapokuja hapa mje na majibu mazuri ambayo Halmashauri ya Magharibi A watapata kujifariji na hata watu wa Wilaya nzima watapata kunufaika na majibu ambayo mtaweza kutoa. Bila ya vituo vidogo vidogo kwenda kuvimalizia hatuwezi kuwa na huduma stahiki ya msongamano katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, maana leo tunalazimisha watu wote hata anayeugua kipele aende katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kitu ambacho sio sahihi.

Mhe. Rais kaahidi kuhusiana na hospitali hii lakini miaka inakwenda siku zinakwenda, tofali zile zinaanza kuyoyoma. Sasa ni vyema tukaenda kuiboresha mapema na kuimalizia kwa pale ambapo imebaki ili wananchi wengi waweze kupata huduma katika maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, miezi miwili nyuma tulikuwa na hali mbaya ya magonjwa ya mripuko hasa ugonjwa hatari wa kipindupindu, tukawaweka watu katika mazingira magumu katika kila sehemu. Wenzetu wa Mnazi Mmoja hospitali pale kulikuwa na watu maalum ambao wanahudumia wale watu na wengine walioko kule kwenye Hospitali yetu ya Chumbuni. Lakini wenzetu wa Chumbuni wanapata posho hata kwa kiwango kidogo kidogo. Lakini hawa wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wametupwa mpaka leo hawajapata chochote na wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Ukweli Mhe. Mwenyekiti, hiki si kitendo sahihi, tumuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja katika majumuisho yake hapa aweze kuwaambia watu hawa wa Mnazi Mmoja ambao walikuwa na jukumu lile la kuwahudumia watu wale ambao watakuwa wanabainika na kusadidika kuwa na ugonjwa hatari wa kipindupindu angalau wapate fidia nao wafarijike, hizi ndizo *motivation* ambazo tunazitaka kwa wafanyakazi wetu wa serikalini wazipate ili nao wapate nguvu za kutaka kufanya kazi.

Leo tukiwakosesha hawa watu hawa wachache ambao wanahudumia jamii ya watu wengi zile pesa ndogo ndogo ambazo ni za ziada katika majukumu yao tunakuwa tunaweka katika hali ya unyonge sana. Tuwaombe sana wenzetu wa wizara tuiombe sana serikali, ni vyema katika fungu hili tulilokuwa nalo angalu

twende tukawafute machozi ili na wao wafarijike na huduma ambayo waliokuwa wanaipata, wamefanya kazi kubwa, wamefanya kazi ngumu mpaka kuweza kufika hapo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mihayo una dakika tatu.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Nimalizie na jengine kama ambavyo tumeweza kusema ni vyema tukaweza kutumia kile kiwango cha fedha ambacho kilikuwa kimepelekwa kule kuweza kukamilisha ile huduma ya *x-ray* pale.

Lakini jengine Hospitali zetu za Kivunge kule haziko katika hali nzuri ni vyema sasa serikali ikaamua kuziwekea mazingira stahiki. Huduma hii ya Sekta ya Afya tukishindwa kuwahudumia hawa watu ambao wanawahudumia wengi tutakuwa tumewaweka katika mazingira mabaya. Mimi niiombe sana serikali kwa kutambua sana serikali hii sikivu ya Chama cha Mapinduzi, na kuitambua sana serikali hii na wizara hii kwa kuthamini Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020.

Tunaamini sana ni vyema katika kipindi hiki mkaweka Sekta hii ya Afya ikaboreshwa kwa dhamira sasa watu wakafarijika na huduma hii ya afya. Leo watu wote wanakimbilia kwenye *Private hospitals* tunaziacha Hospitali zetu za serikali, leo tuna vituo vingi vya afya ambavyo havina dawa kila mtu anaona tabu kwenda, ni vyema mtu anaona akienda sehemu akadanganywa akapata sehemu akatumia gharama kubwa jambo ambalo tunalifanya watu waitukane serikali yao kwa mambo ambayo hayana msingi.

Mimi nina imani sana kwa gharama ya kuhudumia vituo vyetu hivi vichache vya afya kwa uthubutu wa serikali hii kama ambavyo imeanza kuwa na dhamira ya uthubutu wa kuweza kufanya harambee ya madawati katika sekta ya elimu tunafanya hivi na sekta ya afya. Haiwezekani leo tuna *Dispensary* na hospitali ndogo hazizidi 150, au 200 katika Unguja nzima na tukaweza kukosa madawa, haiwezekaniki.

Mimi niiombe sana serikali, natambua jitihada kubwa sana unazofanya, lakini tukiweza kukamilisha na kuweza kuisaidia sekta hii ya afya tutaweza kumuweka katika mazingira mazuri Rais wetu ambaye ana dhamira njema sana na *field* yake ya udaktari. Bahati nzuri Rais wetu amehudumu katika maeneo mengi sana ya sekta hii ya afya. Sasa tusimtie doa Mhe. Rais kwa jambo ambalo yeye mwenyewe analipigania ndani ya moyo wake.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, natambua sana. Lakini sitaunga mkono hoja asilimia mia mpaka pale Mhe. Waziri atakapokuja na majibu mazuri ya kina, yenye kutia faraja wananchi wanyonge kwa Wazanzibari. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi leo niwe mmoja kati ya wachangiaji wa Hotuba ya Wizara ya Afya.

Wizara ambayo kwa kweli inabeba kila kitu kwa maana ni Sekta Mtambuka, ukienda Mawasiliano Wizara ya Afya ipo, ukija humu ndani Baraza la Wawakilishi Wizara ya Afya ipo, ukienda Habari Wizara ya Afya ipo na mote kwengineko Wizara ya Afya ipo.

Napenda sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako niwapongeze sana wote wale wanaoiongoza hii wizara kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote pamoja na viongozi wengine na sisahau pia kuwapongeza na wafanyakazi.

Wizara ya Afya ni ngumu kumuhudumia mgonjwa ambaye pengine anatoa hata harufu si jambo dogo, ni jambo kubwa na linataka ustahamilivu sana. Pia niunge mkono hotuba aliyoitoa Mwenyekiti wa Kamati, hotuba ile imeshitua mambo mengi sana yaani kama ingekuwa ni kesi basi yule ingekuwa hiyo *qualification* aliyoikusudia basi ameipata. Kwa kweli kuna matatizo sana ya huduma inawezekana kukosekana kwa fedha, inawezekana kukosekana kwa utaalamu. Lakini kitabu hichi kimelenga kutatua hayo matatizo ambayo yapo.

Sasa kidogo baada ya pongezi nitoe historia kidogo halafu nieleze yale ambayo ninayoyataka. Kabla ya Mapinduzi huduma za afya zilikuwa chache mno, waliokuwa wanapata huduma hizo ni wale mabwanyenye tu na aila zao basi. Madhila hayo pamoja na madhila mengine ndio yaliyosababisha yafanyike Mapinduzi mwaka 1964.

Pia wakati huo huo wa Ukoloni kutokana na kukosa kwa huduma za afya kwa wananchi masikini huko vijijini na kwengineko hata waliokuwa hawamo kwenye matabaka mjini. Kuliwafanya watibiane kwa kutumia njia za kienyeji kupandisha mashetani, kuandikiana makombe, miti shamba na kadhalika. Hayo yote baada ya Mapinduzi matukufu ya 1964 yaliyoongozwa na Jemedari wetu Mkuu Mzee Abeid Aman Karume yametoweka. Bidii kubwa ilifanyika kusambaza huduma hizi za afya vijijini na kila pahala na wananchi wengi

walipata huduma, na zile itikadi nyingi sana hata kama zipo basi mgonjwa hakubali kutibiwa kienyeji peke yake lazima atakwenda hospitali, hayo ndio mafanikio.

Sasa usambazaji wa huduma za afya uliofanyika kwa kweli unastahiki kupigiwa mfano, kuna zahanati nyingi sana vijijini na mijini, kuna vituo vya afya vingi, kuna Hospitali za Wilaya na Mikoa na kuna hospitali pia za Taifa ndio hiyo ndio ambayo moja ambayo tunataka kuifanya iwe Hospitali ya Rufaa.

Sasa lakini pamoja na juhudi zote hizi mimi naweza kusema kwamba kipaumbele kikubwa kilichokuwa kinafanyika ni kutibu badala ya kukinga, na hili si tatizo la hapa tu, hili ni tatizo la dunia nzima, mpaka mtu apate ajali pengine ndio atibiwe. Baada ya kufanya yale mambo ambayo yatawezesha zisitokee hizo ajali au magonjwa basi tunasuburi zitokee. Pengine si kwa makusudi ila kwa bahati mbaya, hatukatai.

Sasa kutokana na hayo sasa kumekuwa na mripuko wa magonjwa mengi, kuna gonjwa kubwa sana la UKIMWI, Malaria siitaji sana kwa sababu hiyo tumeweza kiipiga vita. Kwa hiyo, kumbe tunaweza na mengine haya kuyapiga vita pia. Kuna ugonjwa wa saratani, kuna sukari, kuna mafigo, maradhi mengi tu yamejitokeza wakati huu. Sasa ni wajibu wetu kwa kweli kuangalia, hasa tukiangalia sasa tunakwenda kwenye Hospitali ya Rufaa kuna mambo ambayo kwa kweli tunapaswa tuwenayo, na moja katika hayo ni kufanya zile *specialities* za magonjwa mbali mbali ziwepo.

Mimi nitauliza swala nitataja hizi ambazo mimi nimeziorodhesha wataalamu wa afya wanajua zaidi kuliko mimi, lakini nitataja hizi orodha labda Mhe. Waziri atakuja kusema ni wangapi wapo sasa hivi. Kwa sababu bila ya kuwepo hawa hiyo Hospitali ya Rufaa nadhani haitakamilika. Kuna ma- *specialty* wa *cancer* wapo wangapi, wanatosheleza haja, halafu kuna hii *cardiology* na *heart Surgery* hawa wapo kwa sababu haya magonjwa yapo, kuna sukari hii na *endocrinology* nikikosea *spelling* basi wao wanajua na nawaomba watambue tu nimekusudia nini.

Kuna matatizo ya masikio, pua na koo yapo hata sasa hivi ukipita mitaani kuna wengine wanalalamika yanawabana matonsisi yaani haya mambo yapo. Kuna *gastroenterology* na *GI Surgery* yapo vipi haya**.** Halafu kuna, *geriatric*, kuna *Gynecology*, kuna *nephrology* na *neurology* kuna na *ophthalmology*, kuna *Orthopaedic* kuna *psychiatric* kuna *palmology* kuna mambo ya *rehabilitation* sio kwenye mashimo ya mchanga tu, kuna *rehabilitation* kwenye afya. Kuna

rheumatology kuna *urology* kwa kutaja machache, mengine wanayajua wenyewe.

Sasa tungepata kujua tunaelekea kwenye Hospitali ya Rufaa katika wataalamu hawa niliowataja wao tunao wangapi, na tuna mpango gani wa kuwapata hao wengine ili tuweze kukamilisha ule utaratibu mzima wa kuwa na Hospitali ya Rufaa. Naelewa kabisa kwamba kuna wale waathirika wanakuwa ni wagonjwa nao wameathirika kwa sababu ya madawa ya kulevya.

Nimepata kuwasikia pale Hospitali ya Kidongo Chekundu pale wanakuja wanakaa pale chini wanazungumza wenyewe wanasema hawa madawa tunayopewa ya kukata makali ya ulevi yanatuumiza kwa sababu tunakuwa hatujiwezi unakuwa mtu umeregea pale huwezi kufanya lolote. Sasa wanakwepa wengine hawaendi.

Sasa ningeomba ufanyike uchunguzi wa kutosha kuona hizi dawa zinafaa kama zinavyotakiwa au ziko haja au kuzi- *replace* ukaleta za aina nyengine ambazo zitawahamasisha waende kwa wingi ili waepukane na madawa. Kwa sababu kuna wengine wanataka waache lakini wameshazoea hawawezi kuacha kirahisi rahisi.

Baada ya kuzungumza hayo sasa nadhani hapo nimefahamika kidogo. Sasa niingie kwenye hizi takataka za hospitali. Hizi taka kwa kweli ni hatari sana tukiaacha ziendelee kama zilivyo zitatuulia watu kwa wingi sana. Sasa ukija kuongezea na maajali ya magari yanayotokezea barabarani na mabadiliko ya *climate changes* inayotokezea magonjwa yanakuja mengi na hii nayo itatuathiri sana.

Kuna hospitali zipo kwenye majumba ya watu kwenye jumuiya za watu zikiwemo mfano Al-Rahma nyengine ziko hizo Mwembeladu pale na kwengineko. Hawa wanachoma mataka ya hospitali kwenye *surroundings* za watu harufu moja kwa moja. Zile harufu zinazotoka kwenye moshi ule ni hatari ni *heavy metal* Kuna matatizo ya baadae watu wakawa wagonjwa, badala ya kutibu tunazalisha wagonjwa wawe wengi zaidi na hali ya matibabu haitoshelezi. Kwa hivyo, ninashauri sana hospitali hizi zifuatiliwe hata karatasi wasichome. Hawa watu wa Al-Rahma walikuwa wanachoma pale chini kwenye kuta lao, harufu moja kwa moja. Watu wamelalamika na sasa hivi wamehamia juu ya nyumba yao ndiyo wanakochoma taka zile, makaratasi yote yanahamia kwenye makaazi ya watu, ikija mvua watu kwa sababu ya matatizo ya maji wanakinga maji yale hujui wanakunywa nini.

Tafadhali sana hospitali hizi zishughulikiwe wakachome taka zao Bungi au wakachome taka zao kwengine au wapatiwe *incinerator* ambazo zitakazoweza kuchoma taka kwa kitaalamu zaidi. Hawawezi kuchoma hivi hivi wataua na mimi nina wasi wasi kwa kipindi ilipowekwa Al-Rahma wakaanza kuchoma madawa tangu siku hizo nina hakika watu wameshaathirika. Lakini maradhi haya hayajajitokeza lakini yatakuja kujitokeza majirani pale, maradhi makubwa sana. Tena maradhi yenyewe yaje haya ya kuambukiza watakuja kufa watu kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, ninaishauri Wizara ya Afya ifanye *inspection* ya hali ya juu kabisa wale watu wanapewa bima kubwa sana, wenzangu wamesema hapa fedha nyingi za bima zinatumika kuwalipia wale wanaokwenda kuwaua watu kwa kuwapa moshi mchafu. Mwanzo mwanzo huko waliwahi kutupa vidonge, masirinzi ya damu yale yakazagaa ovyo ovyo, siku hizi wameacha mambo hayo lakini bado wanaendelea kuchoma taka taka.

Mhe. Mwenyekiti, na si hayo tu na hospitali nyengine ndogo ndogo zote wanachoma njiani na nje, wanachoma ofisini pale moshi unakwenda kwa wakaazi. Hata *disposal* yake huko wanakokwenda huko Bungi waangalie sana namna wanavyo-*dispose*, taka taka za aina tofauti, mabaki ya binadamu yale yanataka yawekwe kivyake, yahifadhiwe kivyake yawe-*disposed* kivyake, yakichomwa tu mchanganyiko ni pale pale tunaharibu. Madawa yanayobaki haya yaka-*expire* yanazikwa kiaina yake, kwa sababu kama utayazika tu ovyo ovyo unaweza ukaharibu *underground* yote hapo mtaani, unaweza kufanya *pollution* kwenye *underground water*, matokeo yake tukaja tukanywa maji machafu yaliyokwisha athirika.

Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwa ufupi sana Wizara ya Afya ina kazi kubwa sana kuwalea binadamu waliopo hapa Zanzibar na kwengine watakaokuja nao ili wawe na afya bora waweze kufanya mambo yao kwa ufanisi, bila ya afya hakuna kitakachopatikana afya haina mbadala. Hivi sasa kuna wenzetu wanataka watembee wapo kitandani hawawezi hata kunyanyuka kwa sababu ya afya. Kwa hivyo, mimi niseme kwamba pamoja na matatizo yote, wenzetu hawa wamerithi. Kipindi kilichopita mimi ninakumbuka sana wamebadilishwa mawaziri mara mbili, hivi sasa tuna mawaziri mapya. Nina waamini wana lengo kubwa sana la kutatua haya matatizo hivyo tuwaunge mkono. Mimi ninaunga mkono hoja ya kuhamisha pesa zile tuhamishe tuzipelekwe kule, lakini tuangalie tukihamisha huku hawa waliotengeneza hii bajeti ni wataalamu, ni sawa na hapa tunataka kufanya hivi. Pengine hilo wanalolitengeneza litasaidia huko mbele kuendeleza haya yanayotokea. (*Makofi*)

Mimi ninashauri Wizara ya Afya ikakae na Wizara ya Fedha ambayo ni jungu kuu halikosi ukoko, watoe fedha za ziada ziingizwe kwenye zile tuzilizozielekeza hapa ili litatuliwe hilo tatizo tulilolisema. Huku waachiwe hata kama ikibidi kupunguziwa kidogo basi si mbaya wapunguziwe, lakini tusiseme kwamba bajeti hii haipiti kwa sababu ya kwamba pesa hizi tunataka ziende huku, tutakuwa tunajikwamisha wenyewe, tena tutakuwa tunajikwamisha vibaya sana. Maana bajeti hii ikirudi maana yake *time* tunaanza kuipoteza sasa tuje tukae tena tufanye nini. Tafadhalini sana tuwaunge, mimi ninaunga mkono asilimia kwa mia lakini wanihakikishie hapa kwamba watakwenda kukaa na Wizara ya Fedha wapate kifungu cha ziada ijapokuwa *emergency* kisaidie kwenye hayo matatizo ambayo wawakilishi wameyataka. (*Makofi*)

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimuonea huruma rafiki yangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alipolia, kwa kweli sote tunalia lakini maana yake kilio chetu hakitokezi, lakini mwenzetu kalia dhahiri. Tunataka huduma za wananchi zipatikane kama inavyotakiwa wananchi wawe na afya wafanye mambo yao kama inavyostahiki ili maendeleo yapatikane. Kwa hivyo, nashauri sana Wizara ya Afya mna moyo mkubwa wa kuendeleza wizara hii, tafadhali tufuate yale yale aliyoyapendekeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati halafu tena jengine tufanye utafiti wa kutosha kuhusu haya mambo ya afya. Tusione taabu kutoa fedha ukafanya utafiti wa kutosha na utafiti upo wa aina nyingi. Kuna *primary assesment*, unakwenda tu una-*assess* unaondoka unakwenda kuleta *recommendations* zako. Kuna utafiti wa *investigation* tu, halafu kuna utafiti huo wa *researc*h. Sasa huo wa *research* ni mkubwa lakini nao pia utasaidia, tufanye hizi za *primarily* na mambo mengine mengine tupate *recommendation* ambayo itafanya *research* kubwa ifanyike kuondosha matatizo haya.

Baada ya hapo ninataka sana nimalize ndani ya wakati nisizidi, bora nipunguze. Niingie tena kwenye hii…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umebakiza kama dakika mbili, naomba sana ujali wakati.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti: Zinatosha hizo kabisa ahsante sana.

Kwenye ukurasa huu wa saba, hii namba mbili ongezeko la maradhi. Mimi naomba sana tufanye utafiti wa kina tujue kiini cha ongezeko la maradhi, maradhi yanaongezeka sana. Kuna maradhi hapa sasa hivi mtu ana afya yake anavaa shati linabana sawa sawa kwenye mabega, baada ya muda unamuona kabaki kitumbo kwenye mabega huku kumekonda kote. Haya ni matatizo kwa

hivyo tufanye utafiti wa kutosha kuona haya maradhi mapya hasa kiini chake ni nini.

Halafu jengine ni kwamba hapa pameelezwa kuwa kuna ongezeko la bidhaa ambazo hazikidhi haja. Mimi ninadhani hapa tupate *inspection* ya kutosha ili tuondokane na hili tatizo la kuleta vyakula ambayo hayakubaliki.

Kwa kumalizia nende haraka haraka ukurasa wa 13. Hapa kidogo pamenipa wasi wasi, watu elfu kumi na sita, mia tano na ishirini na tisa waliokuwa hawana ishara ya malaria walifanyiwa *investigation*. Lakini inatisha kuona kwamba asilimia 40 na zaidi ya asilimia 40 wana vimelea vya malaria, na sisi tunasema malaria tumeshaitokomeza na ipo *below one percent*. Je, hii takwimu yenu kidogo inatosha? Muufanyie uchunguzi sana takwimu hizi kidogo inaweza ikawavunja moyo hata wale wahisani ambao wametusaidia tukawaambia tuna 0.5% ya maambukizi.

Kwa hivyo, baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa muda wako umetosha ahsante sana. Na ninakushukuru kwamba hukuni-*interact* ukaniambia kwamba muda wako dakika mbili, umeningojea mpaka nikamaliza, nika-*pause* kidogo ndiyo ukaniambia.

Mhe. Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia na ninawaomba wenzetu wote tuiunge mkono waende wakajirekebishe kwa vile ambavyo tumesema bajeti iendelee. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame. Sasa afuate Mhe. Salma Mussa Bilal na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajitayarishe Mhe. Abdalla Maulid Diwani na kama muda utaruhusu tutampisha Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis. Lakini pia niwaombe wajumbe kwamba wachangiaji ni wengi na kama mulivyozungumza hii wizara ni nyeti, naomba sana sana waheshimiwa ambao hawakupata kuchangia lakini fursa wanayo, naomba michango yao wapeleke kwa maandishi.(*Makofi*)

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya.

Mhe.Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyenipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele kwenye Baraza lako Tukufu na kuweza kuchangia hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao kwa kuweza kukaa pamoja na kuweza kutuandalia kitabu hiki

cha bajeti yao ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nianze kuchangia mchango wangu, naomba nianze moja kwa moja na mimi kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, wengi wameshachangia, lakini nilikuwa nimeshaleta na mimi labda lazima niwe na mchango angalau mdogo wa kuweza kutilia nguvu hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwapongeze wizara hii hasa kupitia Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuweza kuweka kampuni ya ulinzi pale kwenye hospitali. Wamefanya vizuri kwa sababu ulinzi unasaidia mambo mengi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko kabisa ninaiomba wizara, ninadhani walipoitafuta ile kamapuni labda pengine hawakuwapa mipaka ya kazi yao. Kampuni ile badala ya kufanya ile kazi yao hasa imekuwa usumbufu kwa wananchi na watu mbali mbali ambao wanakwenda katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, mwananchi hatoki tu huko akasema anakwenda labda kutembea au kufanya jambo lolote. Mwananchi anapokwenda pale anakwenda ana shida, anaumwa, ana mgonjwa lakini inakuwa usumbufu mkubwa, wale walinzi wana usumbufu mkubwa pale. Mwananchi ana mgonjwa wake anapewa cheti anaambiwa nenda kanunue dawa, anarudi na dawa anazuiwa mlangoni, anapata matusi na anapata maneno yasiyokuwa na maana.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ilikuwa na nia nzuri lakini namuomba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake hebu muwaite wale viongozi wa ile kampuni, wawaite wafanyakazi wao, wawape mipaka ya kazi zao pale. Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi unakwenda pale kwa heshima na taadhima, unaambulia matusi na maneno yasiyokuwa na maana. Mhe. Mwenyekiti, kwa suala hili naomba sana ni nia nzuri lakini imekuwa karaha sana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba pamoja na nia nzuri ile ya kuweka walinzi, hebu naomba Mhe. Waziri wafanye utaratibu na kuweka kampuni ya usafi pale katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Serikali ina nia nzuri ya kuweka Hospitali ya Mnazi Mmoja katika kuipandisha daraja kuwa Hospitali ya Rufaa. Lakini hospitali ile wenzangu wameshasema kwamba hata hizo asilimia tuzipe ngapi ya kwamba kweli iwe Hospitali ya Rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ile hospitali haparidhishi hata kidogo kuhusu usafi wa ile hospitali. Labda itakuwa kipindi hiki kwa sababu kuna bajeti itakuwa pengine kumeimarishwa imarishwa kidogo ili tukenda kutembelea

tuone kwamba labda usafi umeimarishwe. Lakini pale hospitali Mhe. Mwenyekiti, hapafai hapafai. Unampeleka mgonjwa tena mtoto ana maradhi, mtoto ndiyo mtoto akishapata nafuu kidogo badala ya kupona yale maradhi aliyonayo anaondoka na maradhi mengine pale hospitali. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa makusudi Mhe. Waziri au wizara ifanye juhudi za makusudi labda kuweka na kampuni ya usafi ili ile hospitali iweze kuridhisha hali ya pale.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameshalizungumza suala la maradhi ya kipindupindu. Maradhi haya ya mripuko yametokezea na kila mtu ameyaona, kila mmoja alikuwa na taharuki, sisi wa mitaani, sisi hawa madaktari, si wenye wagonjwa wao. Tumepoteza watu wengi. Kwa makusudi wizara imebidi itoe wafanyakazi wa ziada kutoka katika vituo mbali mbali kuwapeleka Chumbuni na maeneo mengine ya vituo vile vya maradhi ya kipindupindu kwa ajili ya kusaidia ile hali ya pale ya kuhudumia wagonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, madaktari wale walikuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu, mazingira hatarishi. Wanahudumia wale wagonjwa, wagonjwa wanakuja pale hali mbaya. Mhe. Mwenyekiti, wale manesi wanashindwa hata kula akifika nyumbani chakula kinawashinda kutokana na hali halisi iliyokuwepo pale kwenye kambi mbali mbali za kipindupindu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mpaka leo wale manesi na madaktari ambao walikuwa wanafanya kazi katika mazingira hatarishi wapo baadhi wamelipwa posho zao, lakini wapo baadhi mpaka leo Mhe. Mihayo Juma N'hunga amesema pale kwamba wale lazima tuwape motisha, wamefanya kazi katika mazingira magumu.

Sasa hivi hali imepungua ipo haijaondoka, lakini hali imepungua wale ndiyo waliochangia walisaidia ile hali kupungua pale, walihudumia vizuri kwa moyo wa kujitolea. Lakini baadhi ya wahudumu mpaka leo bado posho zao zile za kufanya kazi katika mazingira hatarishi hawajapata. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia watendaji wako hebu tuwafanyie, tuwatendee haki wote waliokoa lile jahazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo na mimi ninakwenda katika Kituo cha Afya Umbuji. Kituo cha Afya Umbuji ni kibovu, hakifai kabisa. Mhe. Mohammedraza Hassanali alipozungumza mimi nilikuwa sipo, kwa hivyo na mimi nina haki kwa vile kipo katika Mkoa wangu, kituo hakifai. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri leo ikinyesha mvua kile kituo hakikaliki, kipindi chote cha mvua inabidi huduma zisimame za Kituo cha Afya Umbuji. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammedraza Hassanali alitaka kukijenga kile kituo mkamzuia, mkasema sijui kitajengwa mpaka leo kipindi cha miaka mitatu kile kimemalizika na tunaanza tena kipindi hiki, bado kile kituo na humu sikukiona naona kwenye kitabu na sijui kama sijaangalia vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ninataka Mhe. Waziri ukija hapa uniambie ni lini Kituo cha Afya cha Umbuji kitaweza kufanyiwa kazi. Wananchi wanasumbuka sana, madawa yanaharibika, vifaa vinaharika mle ndani wakati wa kipindi cha mvua. Na halafu huku tunaambiwa kuna upungufu wa madawa, kuna upungufu wa vitendea kazi lakini vile ambavyo vipo pale vinaharibika kwa mvua. Hivyo Mhe. Waziri naomba sana ukija hapa uniambie ni lini. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda tena katika Hospitali ya Binguni. Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa na nia nzuri sana ya kuwapunguzia masafa au ya kuwasogezea karibu huduma ya afya wananchi wake, na ilishaamua kwamba inataka kujenga Kituo cha Afya Binguni cha Wilaya. Tulikuwa na kamati pale Mkoa wa Kusini kulifuatilia hili, tumefuatilia kiwanja, tumefuatilia upatikanaji wa hati na kila kitu kipo sawa na tumekabidhi Wizara ya Afya. Lakini hadi leo bado hospitali ya Wilaya ya pale eneo la Binguni bado ingali hadithi ya kwenye vitabu tu au hadithi ya kwenye meza tu. Ninaomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hebu atueleze amefikia wapi au ana mpango gani kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kati pale eneo la Binguni.

Wananchi walishaanza kulivamia lile eneo, wameondolewa lakini wakiona kimya wanaona serikali ndiyo kawaida yake tu. Wanaona hakuna kitakachoendelea. Kila siku tunagombana na watu pale kuwa wanaingia tunawatoa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri naomba utusaidie sana. Tunaomba sana mpango huu uendelee basi kama bado haijawa tayari basi angalau kuna yale maeneo ya mipakani tu kule tuzungushie alama, sio uzio. Uzio ni gharama kubwa, yale maeneo ya mipakani tukayajenge ikiwezekana kona za kuonekana hasa ili wananchi wasiendelee kulivamia lile eneo, kwa sababu tunatengeneza chuki baina ya serikali na wananchi wetu. Wananchi wanapanda vipando vyao, haidhuru wanavamia, wao hawayajui hayo, wao wakiona kimya wanavamia, na wakikatazwa wanajenga chuki. Kwa hivyo, tupunguze chuki, angalau tukaweke japo zile kona kubwa za kuonekana kunyanyuka hasa au tutowe matoleo tuyapandike mule, kwamba hakuna ruhusa mtu kuingia kwenye eneo au kujenga katika eneo au kufanya lolote katika eneo, angalau tupunguze chuki na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo ninde kwenye Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Suala hili lilishazungumzwa sana, lakini na mimi nataka nilitilie mkazo

kidogo, kwa sababu nina ushahidi. Simo kwenye kamati wala sikwenda kukagua, lakini nilikua nina *issue* ambayo ilinibidi lazima niende.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hospitali ile ni chafu sana, pamoja na kwamba wale wanaopelekwa pale ni wagonjwa wa akili, lakini wagonjwa wa akili wanawekwa katika mazingira magumu ambayo ni hatarishi. Mtu anakwenda pale akili zake hazifanyi kazi vizuri, halafu anakwenda pale hospitali hairidhishi hata kidogo.

Pia Mhe. Mwenyekiti, ulinzi wa wale wagonjwa ni mdogo sana, wale ni wagonjwa wamejengewa ukuta mkubwa, lakini sasa siku hadi siku wagonjwa wanaopelekwa pale wanatoroka, wanapanda ukuta ule wanachupa, kule anakochupa hajulikani ataangukia nini, kama gae ama msumari, kwa sababu akili zake hazifanyi kazi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wizara iongeze ulinzi katika eneo lile la hospitali ya wagonjwa wa akili, ili wale wagonjwa waweze kuwadhibiti vizuri na wasipate kutoroka pale hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hilo pale hospitali ya wagonjwa wa akili, kuna wagonjwa wa akili na kuna walemavu wa akili. Walemavu wa akili wanatakiwa kutumia dawa...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salma Mussa, samahani kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, mazungumzo yamekuwa mengi sana. Kwa hivyo,ule mchango anaoutoa mjumbe sifikirii kama waziri husika atakuwa anausikia. Baadae kutakuwa kuna mabuti mengi sana hapa, kwa kutokusikiliza yale majibu yanayotoka kwa waziri husika. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima na taadhima tuwemo ndani ya Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea, nilisema kwamba pale hospitali wanakuwepo wagonjwa wa akili, lakini wanakuwepo na walemavu wa akili. Walemavu wa akili Mhe. Mwenyekiti, wanatakiwa kutumia dawa kila siku ya Mwenyezi Mungu na dawa za *mental* ni ghali sana.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwa makusudi awapatie tahafifu hawa wagonjwa walemavu wa akili, ili waweze kumudu kutumia zile dawa na kuweza angalau kusogeza maisha yao kwa kupata hizi dawa kwa unafuu.

Mhe. Mwenyekiti, kidonge kimoja cha dawa ya walemavu wa akili kinanunuliwa shilingi 3,000 kwa kidonge kimoja, na anatakiwa mgonjwa wa

akili atumie dawa kila siku ya Mwenyezi Mungu na hali zetu ni ngumu, wananchi wetu hali zao ni ngumu. Ili aweze kuishi vizuri basi dawa ile ndio uzima wake na ndio uhai wake. Humjui mgonjwa yule ataishi muda gani.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri, hebu tuangalie jinsi ya kuwasaidia hawa walemavu wa akili. Mgonjwa wa akili anakwenda anapata dawa unamtibu anapona. Lakini mlemavu wa akili inakuwa yeye uzima wake ni zile dawa tu anakula maisha yake. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe Waziri hebu tuwaangalie tutawasaidiaje wale walemavu wa akili.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho, katika kitabu hiki kuna eneo la uzazi salama. Anasema kwamba tumewahamasisha sana akina mama kidogo kuwe salama basi ni kuzalia mahospitali. Nashukuru wanawake wengi au wananchi wengi wameitikia wito wa kwenda kuzalia hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kina mama na wanawake wengi wanavunjika moyo kuja kuzalia hospitali, wanaona bora wazalie majumbani kutokana na matatizo na matusi wanayopata kwa wahudumu wetu. Kumekuwa na maneno machafu sana. Mimi mwenyewe shahidi, nilimpeleka mgonjwa wangu pale...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi mwenyewe shahidi, wanakwenda pale wagonjwa wanapata maneno ya matusi mno, machafu mno. Mgonjwa anasema nyinyi si mmetuambia tuje tuzalie hospitali halafu tunakuja huku tunapata adhabu kama hii, basi hatuji bora tuzalie nyumbani. Wanafika kusema hivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nakujua wewe ni msikivu, ni muumini wa maendeleo, nakujua hasa unavyotaka maendeleo. Kwa hivyo, naomba sana tuangalie vizuri hawa watendaji wetu. Viongozi wana nia nzuri, lakini watendaji ndio wanaoangusha hospitali ile isifikie hatua nzuri, na watendaji ndio wanaosababisha mambo mengi pale yasiwe. Kwa hivyo, naomba tuwafuatilie vizuri hawa vijana wetu, tuwaelimishe vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia wasikae tu wizarani, lazima muwe mnapita mnafanya ziara za kushtukiza, ili mkaone hali halisi ya kule. Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache na mengine siwahi kuyaandika. Lakini kwa hayo machache na mimi naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Kwa kuwa najua Mhe. Waziri ni msikivu atafuatilia yale yote ambayo nimemshauri au nimemuomba.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salma Mussa Bilal, sasa namuita Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mhe. Abdalla Diwani na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis ajitayarishe.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii nitowe mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Afya. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na afya na mimi namuomba aniwezeshe niweze kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuchaguliwa kwake kuwa waziri, kutoka Naibu Waziri mpaka kuwa waziri. Lakini pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa jitihada yake katika kipindi kifupi ambacho amechaguliwa amefanya ziara nyingi za kuona wizara yake ikoje na hata kufika katika Jimbo langu la Mgogoni kuona kituo changu kikoje, namshukuru sana na nampongeza.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika hotuba hii ambayo ina uhai wetu sote tuliomo humu na tulio nje ya humu ambao kuwa inasema afya. Mhe. Mwenyekiti afya ni tunu, tunu hii ni lazima tuwe nayo na lazima tuitunze ili iendane na haya iliyokusudiwa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja, kwanza sadaka huanza nyumbani. Niende kwenye kituo changu cha afya kilichopo katika Shehia ya Finya. Naipongeza serikali kuona kwamba tulikuwa tuna kilio cha muda mrefu kutaka kituo cha afya, na baadae kikaweza kutekelezwa kilio chetu hiki kwa kutuwekea kituo cha afya ambacho ni kikubwa sana kwa kiasi fulani. Kituo hiki kilijengwa kwa lengo la kutoa huduma mbali mbali, zikiwemo za mama mjamzito kuweza kujifungulia, kung'oa meno, kutoa huduma za mama na mtoto pale na wagonjwa wengine wa nje.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna baadhi ya huduma sasa hivi zinaendelea na nyengine hazipatikani. Kama vile huduma ya uzazi. Huduma hii haipatikani kutokana na kwamba hakuna daktari ambaye anakuwepo pale au analala pale na ukosefu ni nyumba ya daktari. Jengo lipo na Afisa Mdhamini baada ya kuwasiliana na wahusika alisema, tatizo ikishapatikana nyumba ya daktari, kwa hivyo huduma zitaweza kupatikana na wahusika wapo.

Mhe. Mwenyekiti, naona na Mhe. Waziri na yeye suala hili aliangalie kwa upeo wake, kwamba kituo hiki ni muhimu sana kuwa na nyumba ya daktari. Nyumba ya daktari itasaidia sana wazazi ambao wanakimbilia kule Wilaya ya Micheweni au Wete, hapa itasaidia kituo hiki kiko katikati, wazazi wataweza kujifungulia hapa kwa muda ambao umefikia bila ya matatizo. Ni shuhuda mimi mwenyewe kuwaona wazazi pale wanazaa kwenye magari, wanatoka Micheweni kukimbizwa Wete hawafiki wanazaa kwenye majumba na huku wakiazima nguo na vitu vyengine.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana msaada huu upatikane kwa nyumba ya daktari, kiwanja tayari tumeshakipata. Kituo cha Afya Finya, tayari kiwanja kipo tunaomba msaada huu upatikane wa kupata nyumba ya daktari, tutashirikiana na wananchi tuliokuwepo hapa na waliokuwa nje ya hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapa niende kwenye Hospitali ya Wilaya ya Micheweni. Kwanza sina budi nimtakie rehema kiongozi wetu muasisi Marehemu Abeid Aman Karume, kwa zile fikra zake alizozitoa kwamba sehemu zote zile ambazo kuanzia Ukoloni zilikuwa ni duni, baada ya Mapinduzi zilikuwa ziwe ziko juu nazo miongoni mwao ilikuwa ni Wilaya ya Micheweni. Micheweni ilikuwa nyuma sana wakati wa Ukoloni. Lakini leo Micheweni ukienda ukiiona utafikiri ni Ulaya.

Kwa hivyo, zile fikra zake zinaendelezwa, naishukuru sana serikali imezijali, na ndio kama vile maneno yalivyosema yeye amekufa, lakini fikra na busara zake bado zipo, na kweli naziona kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika hospitali hii ilioko Wilaya ya Micheweni. Katika hotuba yake Mhe. Waziri alionesha katika ukurasa namba 40, kwamba ameifanyia matengenezo, ameweza kujenga ujenzi wa wodi ya kinamama na kinababa. Suala hili nalipongeza sana. Ameweza kukarabati nyumba za madaktari, anasema amekamilisha. Lakini hapa pana changamoto. Mhe. Waziri hapa pana changamoto kwamba hizi nyumba tokea zilipoanza kujengwa hospitali ni ndogo. Sasa imekuwa na huduma zinaongezeka, leo panaanza vyumba vya operesheni, patahitajika madaktari wa aina mbali mbali, hizi nyumba bado ni ndogo. Lazima ushirikiane na serikali kuongeza makazi ya wahudumu watakaokuwepo hapa. Hivi sasa chumba kimoja anakaa daktari mmoja, hii haiwezekani kwa mfanyakazi kukaa chumba kimoja hiki. Nyumba unaiona pale ina vyumba viwili ndio hivyo hivyo, hawezi kukaa na mtoto hata wa kumlea, au kuwa na mgeni mtu kama yule, kitu ambacho ni vigumu kuweza kukaa maisha peke yako pahali.

Daktari kama yuko pale basi anahitaji kuwa angalau na mdogo wake au mtu mwengine, anapokuwa kazini awe na msaidizi mwenziwe nyumbani inashindikana. Kwa sababu daktari mmoja au muhudumu mmoja pale ana chumba kidogo, hili ni tatizo naomba tuliangalie sana. Lakini vile vile Mhe. Waziri hapa ameeleza kwamba wameanzisha hiki chumba cha upasuaji. Nawapongeza sana na nilisikia sauti ya Mhe. Naibu Waziri akisema kwamba alitoa siku tatu chumba hiki kiwe kimemaliza, sasa sijui kama kimemaliza au vipi. Lakini sasa ndio yale yale kwamba kuwa na jengo haitoshi, tuangalie vipaumbele, operesheni hii itakayofanywa hapa inahitaji watu kama wa huduma ya usingizi, je, wapo ambao kuwa ni muhimu, wataalamu wa *X-Ray* wapo, wataalamu wa *ultrasound* wapo, kuwa na jengo tu haitatosha.

Kwa hivyo, na hili tuliangalie watu wetu ambao wanataka kwenda kusoma au tuwapeleke kwa makusudi, ili isijekuwa tunataka operesheni, lakini tunaambiwa tumsubiri mtu wa usingi au mtu wa *X-Ray* kutoka katika hospitali nyengine au sehemu nyengine yoyote ile. Suala hili litatusaidia sana kama tutaona kwamba tunapowasomesha wanafunzi wetu wale basi na suala hili tunalipa kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuipongeza wizara kwa kuanzisha na kuendeleza ile sheria ya uanzishaji wa Bima ya Afya. Hoja hii mimi nilikuwanayo katika kuchangia kwangu kabla sijakiona kitabu hiki, nilikuwa niishauri wizara ianzishe Bima ya Afya. Lakini leo nimepata faraja kuona kwamba hii sheria itakuwepo na inaendelezwa kufanyiwa kazi. Naomba sana iendelezwe kwa hali kubwa sana iweze kufanyakazi muda sio mrefu.

Vile vile Wizara ya Afya imeanzisha hizi Kamati za Afya katika Shehia. Sijui wanaziangalia vipi hizi kamati katika shehia na zinafanyakazi vipi. Suala hili nina wasi wasi sana kwa sababu utekelezaji wake sijauona. Kwa hivyo, nashauri ili tuweze kufanyakazi vizuri basi tuwe tunazipa mafunzo, yanapokuja yale mambo ya ndani ya shehia ya kiafya basi tuwe tunazitumia.

Kwa mfano, kama kugawa vyandarua basi tuziite zile kamati watajiona kwamba na wao tunawapa kazi, kuliko kuziita tu Kamati za Afya, hizi hazifanyi kazi vizuri. Kwa hivyo, jambo ambalo litasaidia ni kuzishirikisha kikamilifu pale ambapo yatatokea mambo kama hayo. Pia zitasaidia hata kuweka usafi katika maeneo yetu ya makaazi, tukiwapa elimu nzuri wataweza kusaidia kwamba usafi nao ni afya.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika hotuba hii na mimi niungane na wenzangu katika suala la fungu la bilioni 7.5, fungu hili kulipeleka katika

kununua vifaa muhimu ambavyo tunahitaji katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba hatuwezi kutibu bila ya kujua maradhi au chanzo cha maradhi kiko wapi. Kwa hivyo, hivi ni vitu muhimu sana au kama si hivyo, basi iweze serikali kutafuta nyongeza ya bajeti hii ili iweze kununua vifaa vinavyohitajika katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja.

Mimi nakubaliana nao sana kuhusu suala la kuipandisha daraja, lakini sio liwe jengo tu, wafanyakazi nao wabadilike sana ili mtu atakapokwenda pale ajuwe kwamba amekwenda, kwa sababu kutibu ni kazi kubwa sana inahitaji huduma na upendo mkubwa ili kila mmoja awe na hamu ya kwenda pale, isiwe tunajengo tu la kusema hospitali ya rufaa lakini ukifika ni maudhi, suala hili la kuuguza ni kubwa sana na ni jambo la kujituma katika moyo.

Mhe. Mwenyekiti, niendele na mchango wangu kwenye Kisiwa cha Pemba kuhusu uhaba wa madaktari. Mhe. Mwenyekiti, suala hili la uhaba wa madaktari Pemba unaukumba sana, kutokana na kwamba wananchi wanapotaka kuajiriwa basi anakubali kwenda kufanyakazi Pemba, akiwa daktari ameshasoma na tayari kupelekwa kufanya kazi Pemba, lakini daktari yule ukifika mwaka mmoja au miaka miwili tayari anaomba uhamisho, na Katibu Mkuu ndiye anayetoa uhamisho huo, bila ya kuzingatia kwamba mtu yule alimpeleka Pemba kwa sababu kuna tatizo. Sasa kama tutaendelea na mtindo huu basi siku zote tutakuwa tuna majengo matupu bila ya daktari.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ninapokuambia katika kituo changu cha Finya kinafikia hadi kufungwa. Ni juzi tu nilikuwepo mimi naangalia milango imefungwa, daktari aliyekuwepo ameshastaafu yumo ndani ya likizo ya kustaafu na wengine wako kwenye semina, hakuna wengine. Hiki ni kituo cha serikali kunahitajika huduma siku za kazi, sio kwamba ni Jumapili. Hii yote inachangia na kwamba madaktari walikuwepo pale baada ya siku mbili au tatu wanarudishwa huku Unguja. Mhe. Waziri naomba mliangalie sana suala hili, msikubali kumuhamisha mtu ambaye kuwa ameshapelekwa Pemba ili kufanyakazi katika hospitali zetu za Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili nao hawa madaktari tuwaweke vizuri, basi Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aliangalie sana suala la wale ambao wako katika vituo vya mbali, kama vile Makoongwe, Ukunjwi, Mkia wa Ng'ombe, Maziwa ya Ng'ombe tuwape motisha ya posho maalum, ili mtu hata akipangiwa kwenda kukaa kule basi anajua mwisho wa mwezi ana posho maalum la mazingira, wafanyakazi wengine hawataki kupangiwa, siku zote wanataka hospitali za mjini. Kwa hivyo, yule ambaye amekubali kwenda kukaa porini kule, kukaa na

wananchi walioko kule kijijini basi na yeye tumuweke vizuri awe na ushawishi na hata mwengine akubali kwenda kule si hivyo kila mmoja akipangiwa yuko tayari kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la afya mashuleni, namuomba Mhe. Waziri utaratibu wa afya mashuleni uendelee kurudi kama vile tulivyokuwa tunasoma sisi kulikuwa na utaratibu maalum wa kupita na kuchunguza afya zetu na sasa uendelee, hivi ndio muhimu zaidi kwa sababu maradhi ni mengi sana suala la kuja kupewa vidonge tu hili suala mimi naliona sijui lina mantiki gani. Huwa najiuliza hawa wenzetu baada ya siku tatu unasikia mtoto tunapewa dawa, miezi miwili tunapewa dawa kunafanywa uchunguzi.

Nataka waziri atakapokuja anijuulishe kwamba uchunguzi gani unafanywa kwamba dawa tulizotibu zimefanya kazi lakini miezi mitatu tunarudisha tena madonge, siku wanayokula vidonge vile watoto wale ni wagonjwa badala ya afya tunatia ugonjwa. Naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hebu nipe ufafanuzi na wananchi wajue kwa sababu hiki kilikuwa ni kilio changu siku nyingi sana hiki.

Mhe. Mwenyekiti, wakati anatoa hotuba yake alisema wamepiga marufuku nguo za ndani kuingia na nyengine zimeshaharibiwa. Je, hizi zilizomo za ndani za mitumba zinafanywa nini ambazo ziko masokoni sasa hivi? Atakapokuja Mhe. Waziri anijibu hili.

Mhe. Waziri ameeleza jinsi walivyotibu maji humu lakini nina mashaka kwa utaratibu wa sasa hasa kwamba visima vyetu sasa hivi vinatoa maji moja kwa moja havipitii tena kwenye matenki. Baadhi yao mnatumia utaratibu gani katika kutibu maji haya, maji ambayo yanatoka kwenye kisima moja kwa moja yanaingia kwenye bomba na kuingia kwa mlaji. Naomba sana utakapokuja utueleze utaratibu mnaoutumia katika kutibu maji haya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile namuomba waziri atakapokuja kwa sababu katika kitabu hiki alieleza suala zima la mtoto anapozaliwa asipewe chochote zaidi ya chuchu la mama kwa muda wa miezi sita. Je, kumefanywa utafiti maendeleo ya hatua hii na kuna mafanikio gani na matatizo gani ambayo kuwa yanapatikana kutokana na mtoto anapozaliwa asilishwe chochote hata maji mpaka afike miezi sita, kuna mafanikio gani na kuna matatizo gani. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze.

Pia naomba Mhe. Waziri atakapokuja alieleze Baraza hili kwamba kuna wafanyakazi waliostaafu, waliokufa na waliokimbia kazini jumla yake

nimepata watu 85 hapa. Je, hatua gani aliyoichukua katika kuziba pengo hili wakati wenyewe tunaijua wizara ina upungufu wa watu, ni hatua gani aliyoshirikiana na serikali kuona kwamba pengo hili limezibwa.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni machache lakini mwisho natoa shukurani. Natoa shukurani kwa yale mataifa na serikali za nchi tofauti ambazo kuwa bado zinaonyesha moyo wa kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea afya njema wananchi wake, hii itaonyesha wazi kwamba bado serikali ya Mapinduzi Zanzibar inakubalika kitaifa na kimataifa. Kwa hivyo, nawashukuru wote wale mashirika na nchi mbali mbali ambazo kuwa zinaendelea kutusaidia na naomba waendelee kuzisaidia hivyo.

Baada ya kusema hayo mimi naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia bila ya pingamizi yoyote *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii adhimu kuchangia Wizara ya Afya. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima wa afya kupata nguvu ya kusimama leo kwenye Baraza lako hili tukufu, vile vile nawapongeza sana viongozi wanaosimamia wizara hii kaka yangu Mahamoud Thabit Kombo, kaka yangu Dkt. Juma Wakili na Wakurugenzi wengine nawambia hongereni sana na *inshaallah* kwa nguvu zenu hizi lawama za afya zimepata muarubaini wake. Kwa jinsi ninavyowatambua watu hao utendaji wao wa kazi ulivyotukuka na *inshallah* Mwenyezi Mungu uwape nguvu hizo.

Mimi katika mchango wangu moja kwa moja nitaanza juu ya vituo vya afya. Kwanza nitazungumzia kituo changu cha afya cha Jumba la Vigae pale Jang'ombe. Kituo kile mwanzo kilikuwa kinafanya kazi lakini yakatokea matatio ya kupasuka ikasimamisha lile zoezi, lakini bahati nzuri sasa hivi kupitia pesa za mfuko wa Maendeleo ya jimbo, Mbunge na Muwakilishi wamesharekebisha hali ya juu na tunasubiri Wizara ya Afya tu sijui lini watakuja kukitembelea kile kituo na kupata ruhusa kuweza kufunguliwa. Kwa ajili ya kutiwa vifaa, kuanza kazi ya kusaidia matibabu katika maeneo yetu ya Jang'ombe na maeneo jirani.

Baada ya hapo vile vile nitakwenda katika suala zima la Kituo cha Umbuji, Umbuji limekuwa jipu zogo la muda mrefu sana tokea mimi sijakuwa na nia ya kuingia Baraza la Wawakilishi, mpaka nimekuwa Baraza la Wawakilishi sasa hivi tayari kuna zogo. Hebu basi serikali amueni uamuzi wa kidume mpeni huyu ajenge, unajua huyu Baiya maana Baiya anapenda sana kufanya mambo ya sifa sifa ajenge kile kituo ili nyinyi muondokane na lawama hizi. Hapa

hapana chochote, hapa kuna chuki za kisiasa baina ya watu na watu, kwa hivyo imekuwa jipu kwa maana hiyo kampuni mmeona ngumu nileteeni mie Jang'ombe itengeneze mradi Jang'ombe wa hospitali, lakini Hospitali ya Umbuji mpeni Mhe. Raza akijengeni kituo kizuri ambacho kitasaidia wapiga kura wetu na wananchi wa Jimbo zima la Umbuji na majimbo jirani.

Nafikiri Mhe. Waziri unisikilize katika hilo, naomba utakapokuja hapa hebu twambie kwamba hiki kituo mumpe Mhe. Raza akijenge kwa sababu hiyo kampuni imeshatajwa zaidi ya miaka kumi sasa hivi hakuna kinachofanyika. Kama zilikuwa ni siasa tu za chuki baina ya watu na watu kutaka kuonyeshana umwamba tuondokeni kule twendeni sasa kuwatumikia wananchi kidhati kabisa. Kama alivyosema mwenzangu tumekuja hapa kwa nguvu za wananchi wanaangalia je, tunawatetea kweli au tunaendekeza maslahi yetu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba sana najua wewe msikivu na Katibu wako pia nafikiri hili suala litakuwa limepata muarubaini wake.

Lakini nazungumza juu ya ripoti ya *CAG* kuhusu Wizara ya Afya 2013/2014, nilikwambia kwamba kuna matumizi ya 2.9 bilioni kwa ajili ya kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Ni pesa nyingi si haba *Alhamdulillah* kwa nguvu zetu kupeleka wagonjwa wale kwa sababu tunawapenda wananchi wetu, lakini pesa hizi matumizi yake hayajaonyeshwa zimetumika vipi. Lakini vile vile pesa hizi 2.9 bilioni ikiwa kweli tutajitahidi tuseme tulete wataalam kutoka huko tunakopeleka wagonjwa wetu India, na tulete vifaa husika tuone kwamba vitafaidisha watu wengi.

Kwa hivyo, 2.9 bilioni sijajua jumla ya wagonjwa wangapi, lakini pesa hizi kama zimetumika vizuri kuleta hao wataalam ambao wanaostahiki kuwapelekea wagonjwa wetu India na kuletewa vifaa vikaweko hapa Mnazi Mmoja nafikiri wagonjwa wengi sana watafaidika na tutaipunguzia gharama serikali kuwapeleka wagonjwa ili kwenda kufanya matibabu kule wakati tuna wataalam wa kutosha na vifaa tiba vya kutosha. Kwa hiyo, 2.9 bilioni nafikiri Mhe. Waziri aangalie kwa hilo.

Vile vile lakini kuanzia mwaka 2014/2015 ni wagonjwa wangapi wamepelekwa India na wangapi wanasubiri kupelekwa India? Kwani kila siku hili zogo lipo katika mitaa yetu na ambao wanasubiri kwenda India mpaka wengine wanafika kufa hapa hapa, Mwenyezi Mungu anawachukua. Lakini kuna taratibu gani zinazofanya wagonjwa hawa nashukuru sana kuna daktari yule alisifiwa sana utendaji wake, lakini bado kuna lawama na ile bodi nzima ya kuwasafirisha hawa wagonjwa wetu. Nafikiri tutakapokuwa makini sana tutaondosha hizi changamoto nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuhusu ripoti ya matumizi iliyopita tuliambiwa kuna 73.9 bilioni zimetumika, lakini hizi matumizi haya hayajaonyesha vielelezo vyake na wala hazijafuata matumizi ya pesa za serikali. Sasa sijui waziri katika suala hili ananiambia suala gani, kwa sababu hili ni tatizo tayari pesa ya serikali inatumika kimjomba mjomba tu kwa sababu kama ingelikuwa inatumika kitaratibu kungelikuwa na utaratibu mzima wa shughuli za serikali. Je, ununuzi lini unafanyika au ugavi unafanyika lini? Hizi pesa hazionyeshi matumizi yake katika jadweli tuliyopatiwa kwenye taafira ya *CAG*. Naomba Mheshimiwa utakapokuja utusaidie sana katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza juu ya suala zima la Hospitali ya Mnazi Mmoja watu wengi wameizungumza Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini mimi nitakwenda moja kwa moja katika suala zima lile la kitengo cha ajali. Watu wanapata ajali wanaopelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja wakifikishwa pale jioni, huwa hapana matibabu mpaka siku ya pili asubuhi. Daktari anakuwa haonekani, mara huyu hayupo, kama daktari yupo utaambiwa usafiri wa kwenda kumchukua nyumbani haupo, na ile ni taasisi nyeti Mhe. Waziri najua kaka yangu Mahamoud Thabit Kombo mwerevu kuna lawama juu ya hivi vifaa kwa ugunduzi wa maradhi *CT scan, x-ray*, Mnazi Mmoja mgojwa anaumia anakaa pale zaidi ya siku mbili hajapata vitu kama hivyo sio lengo.

Kwa nini serikali baada ya kutokea dhahama ya kuzama meli ilibini njia mbadala kukata baadhi ya shughuli zake na matumizi yake ikenda kununua meli ya MV. Mapinduzi, kwa mapesa chungu nzima tushindwe kukata pesa zetu katika sehemu fulani tukahakikisha kwamba hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ina vifaa tiba, ina madawa ili kuwasaidia wananchi wetu kwani imekuwa kilio cha muda mrefu sana. Kilio hiki ni sawa sawa na kilio cha samaki machozi yanakwenda na maji hujui kama watu wanalia. Mfano, mdogo hapa Mhe. Muwakilishi jana kalia ule ni ujumbe tosha kwenu nyinyi watu wa mbele, mfahamu kwamba watu wanaumia na watu mnawaumiza, tuondokane na kufanya kazi kimazoea.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani kidogo Mhe. Abdalla Maulid Diwani ndugu wajumbe naomba kwanza tuwatambue wageni wa Mhe. Naibu Spika, ambao ni Wabunge kutoka Bunge la Afrika ya Mashariki, ndugu wajumbe kutoka Bunge la Afrika ya Mashariki karibuni sana. *(Makofi)*

Pia nilikuwa naomba sasa hivi nimpishe Naibu Spika, katika hiki kiti aendelee Mhe. Naibu Spika, karibu.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, na mimi naomba nichukue fursa hii adhimu kuwakaribisha Wabunge wa *EALA* ndani ya Baraza letu Tukufu. Lakini vile vile niwaambie tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba tulikuwa na Mkutano, ambao mkutano huo ulikuwa ni mkutano mzuri sana, tumezungumza mambo mengi sana, tumejadiliana lakini natarajia sana kwamba Wabunge wetu watarudi tena kwa ajili ya maslahi ya Wazanzibari.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba muwapokee wapo hapo mbele yetu na *inshaallah* tutakuja kuonana nao tena, karibuni sana.

Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nazungumza juu ya suala zima la Kitengo cha Ajali Mnazi Mmoja na matatizo ya vifaa. Nafikiri Mhe. Naibu Spika, watendaji basi wa-*copy* yale mazuri aliyofanya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano John Pombe Magufuli anafanya ziara za kustukiza mara kwa mara katika kazi muhimu ili kuwapa matumaini wananchi wetu. Pia na nyie Wizara ya Afya Mhe. Mahamoud, Mhe. Dkt. Wakili tokeni mwende hospitali ya Mnazi Mmoja mkagundue yale mambo msikae ofisini tu mkasubiri kuletewa. Mwende *field* muangalie hali halisi kinachofanyika pale *at least* na nyie muweze kupata muarubaini wake tuondokane na kufanyakazi kimazoea.

Lakini napata wasi wasi juu ya suala zima la kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ni Hospitali ya Rufaa, sijui kwa kigezo gani mtangulizi wangu alizungumza kwamba je pale tuna wataalam wale uliowataja. Kuna wataalamu wangapi wa moyo, wangapi wa figo, wangapi wa pua, wa koo na maradhi yote, je wataalam wale unao wa kutosha ili itupelekee kuanzisha kuwa Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja au nafuata ushabiki tu, kwa sababu wenzetu wana Hospitali ya Rufaa Muhimbili na sisi tunataka ku-*copy* kule twende, mimi nafikiri bado hatujawa tayari katika hicho. Kwa hivyo, tume- *mark time* hapa, tuhakikishe kwamba tunatengeneza miundombinu mizuri, tunasomesha madaktari wetu kwa wingi na kuweza kufanya kazi pale na si suala hilo tu.

Mhe. Waziri ulizungumza juu ya wafanyakazi kuondoka au kukimbia hao wenzetu wanafanya hii SMZ au hospitali zetu ni shamba la bibi. Tunatoa wataalam wengi wanakwenda kuwasomesha nje ya nchi, lakini baada ya kuja hapa hatuwapi stahiki zao maslahi madogo lazima waende wakatafute maslahi ya ziada. Kwa hivyo, tuone uchungu sana tunatumia pesa za Wazanzibari mamilioni ya mapesa tunasomesha watu kwa kuja kuisaidia Zanzibar, lakini

kutokana na mioyo yao mepesi ya uzalendo wanatafuta kwenda sehemu nyengine kwa kuendelea kuifanya Zanzibar ni shamba la bibi.

Kuna madaktari bingwa wengi sana wa nchi hii wanafanya kazi nje ya nchi hii, ni aibu kwa sababu sisi wenyewe tunawahitaji madaktari wale lakini hatunao kwa sababu hatuwezi kuwa-*facilitate* pale. Kwa hivyo, wanatukimbia kila siku tukisomesha baada ya muda mdogo wakija hapa wanangalia maslahi madogo wanaondoka. Nafikiri tuunde timu maalum ya kuhakikisha kwamba madaktari wale tunawasomesha na tunawadhibiti angalau watufanyie kazi katika nchi yetu ili iweze kuondokana na mazogo haya ya kukosa wataalamu.

Vile vile kuna suala zima kwamba nyumba za Mchina pale, zilijengwa zile nyumba *special* kwa ajili ya madaktari kuwapa kipaumbele. Mhe. Waziri inasikitisha sana nyumba zile wamekaa wanasiasa, wana majumba matatu matatu wanakodisha majumba yao wanakwenda kugombania kile kisungura kidogo pale Mombasa, ambacho kilikuwa kwa ajili ya madaktari wetu tunaowaleta kutoka nje ya nchi, au madaktari wetu bingwa pale Mnazi Mmoja kuwaweka sehemu yenye hadhi yao hawapati fursa hiyo.

Mhe. Waziri inasikitisha sana nyumba zile wamezikalia miongoni mwa wanasiasa ambao wana majumba matatu, manne nyumba zao wao wanafanyia biashara, lakini wanakaa kwenye nyumba zile ambazo hawastahiki kutokana na nguvu zao tu au fursa walizokuwa nazo wanapeana tuondokane huko. Mhe. Naibu Spika, kila kitu kinachofanywa iwe wapewe watu wanaostahiki kufanya, sio kila mtu kutokana na nguvu zake anajiona yeye nani ana utawala mkubwa ana-*force* anachukua ile rasilimali ambayo haimuhusu kuitumia.

Mhe. Nabu Spika, vile vile Mhe. Waziri jambo la usafiri Mnazi Mmoja, *standby transport* pale imekuwa tatizo. Unapokwenda pale Mnazi Mmoja una mgonjwa wako ukimpeleka pale ukiambiwa daktari hayupo, basi unaambiwa daktari ukimpigia simu anakwambia mimi niko mbali kwangu na usafiri sina, kama huna pesa ya mafuta au huna gari huwezi kwenda kumchukua daktari. Mhe. Waziri nakuomba sana lazima zibakie gari pale japo *ambulance* lakini ijulikane pale inapotokea tatizo watu wawe wapesi kwenda kumfuata daktari kuja kuokoa maisha ya wananchi. Maisha ya wananchi wengi yanapotea kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Nathubutu kusema kwa asilimia 50 au 60 kwa uzembe wa madaktari wetu au uzembe wa serikali kwa kukosa vifaa na mambo mengine, na madaktari kufika kwa wakati unaostahiki.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakusihi sana kaka yangu Mahamoud hii wizara ni ngumu, kwa sababu inagusa moja kwa moja maisha ya watu. Lakini kwa

uwerevu wako wewe basi naamini kwamba jipu limepata mtumbuaji nitafurahi sana Mhe. Mahamoud Thabit Kombo, utakapokuja useme kwamba sasa hivi unatumbua majibu. Kuna hata changamoto za kisiasa ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na hilo suala nimeshakueleza *private,* lakini nathubutu kulitamka tena humu ndani ya Baraza hili tukufu, kuna wafanyakazi wameondoshwa kwa masuala ya siasa tu. Kwa sababu eti wanakiunga mkono Chama cha Mapinduzi, hii serikali yetu, chama chetu inakuwaje Mhe. Mahamoud mpaka dakika hii hujalichukulia hatua. Hili suala nilikwambia lakini bado watendaji wanakomolewa, Mhe. Waziri naomba sana utakapokuja uniambie umefikia hatua gani katika suala hilo.

Kwa kweli kama ulivyosema kwamba muda sio rafiki nisizungumze mengi, *message* yangu ni ndogo tu nathubutu kukwambia kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia kama thamanini. Zitakazobakia nakaa nazo mwenyewe hizi ishirini mpaka baada ya kupata maelezo yangu haya ikiwemo maelezo ya Kituo cha Umbuji na maelezo ya wafanyakazi wanaonyanyasika pale Mnazi Mmoja na mengineyo basi tutaendelea. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimepata *note* nyingi sana kutoka kwa wale wajumbe ambao walikuwa kwenye kikao, wanataka kuzungumza ili wachangie japo kidogo, kwa hivyo nitawapa dakika tano tano kila mtu ili angalau yale muhimu naomba sana muyazungumze yale ambayo ni muhimu kwenu nyinyi mengine tayari yameshazungumzwa. Sasa tutampisha Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis na baada ya Mhe. Mwantatu nitampa nafasi Mhe. Hassan, baada ya Mhe. Hassan atapata Mhe. Shadya Suleiman, atafatia Mohammed Dimwa na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze mchango kwa kuwapongeza Mhe. Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa juhudi kubwa wanazozionesha kuhakikisha afya zetu zinaimarika na kwa kweli nawapongeza sana sana. Mhe. Naibu Spika, ninafikiri nitapunguza pongezi niende moja kwa moja katika michango ambayo nimekusudia.

Nianze na programu ya kinga na elimu ya afya. Niipongeze sana wizara kupitia programu hii kwa juhudi kubwa wanazoonesha za kukinga maradhi mbali mbali au magonjwa mengi yakiwemo malaria, kwa kiasi kikubwa malaria imepungua, siwezi kusema kwa asilimia thamanini, lakini kwa kiasi kikubwa tunaona kwamba malaria yamepungua kutokana na juhudi za wizara hii. Lakini vile vile gonjwa la polio hili kwa miaka mingi hivi, sasa naona limepungua kwa

asilimia inaweza ikafika hata asilimia 90 au 85. Kwa sababu polio ilikuwa ikiathiri sana zaidi watoto chini ya umri wa miaka 5 na kwa sasa hivi suala hili sio tatizo kubwa kwetu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kupunguza tatizo la magonjwa ya surua, surua kwa sasa hivi si aghlabu sana kutokezea ipo lakini imepungua kwa asilimia kubwa. Na hili vile vile Mhe. Spika, lilikuwa linaathiri sana hasa watoto kupata matatizo hasa ya ulemavu wa macho au tatizo la macho. Kwa hivyo, niipongeze sana wizara kwa juhudi kubwa wanazochukua kupitia programu hii ya kinga.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika huduma za mama wajawazito, mwenzangu aliyenitangulia alinifisidi kidogo na mimi vile vile nawapongeza wauguzi wetu pamoja na madaktari kwa juhudi kubwa wanazochukua ili kuhakikisha afya ya mama na mtoto inaimarika vizuri. Vile vile katika programu imeeleza kwamba wamehamasisha wanawake ili wajifungulie katika mahospitali, na ni kweli wanawake wameweza kuhamasika vizuri na wengi wetu nikiwemo na mimi wenyewe tunajifungulia huko huko katika vituo vya afya na kuelimisha wenzetu wengine.

Lakini kama ilivyotanguliwa kusema kuna changamoto bado ndogo ambazo zinatupata wanawake tunapokwenda kujifungua. Kuna baadhi ya wauguzi hawa wafanyakazi wanakuwa hawana lugha nzuri kwa wanawake wanapokwenda katika haya mahospitali kujifungua. Hili ndio linalovunja moyo au linalowafanya wanawake wengi kurudi nyuma kwenda katika hivi vituo au katika hospitali kujifungua. Lakini sasa Mhe. Naibu Spika, kutokana na hotuba ya Mhe. Waziri imeelezwa kuwa Baraza la Uuguzi wameshakamilisha muongozo na kanuni za maadili za wauguzi. Kwa hivyo, kupita muongozo huu na kanuni hizi ni matumaini yetu kuwa viongozi wa wizara watalisimamia vyema suala hili ili liondoke au kero hii kinama ituondokee.

Mhe. Naibu Spika, niende sasa katika hospitali ya Mental. Kwanza niipongeze wizara kwa juhudi kubwa inayochukua kuwawezesha au kuwapatia vijana wetu ambao wanatumia madawa ya kulevya kuwapatia dawa *methadone* ambayo inawarejeshea hadhi yao. Kwa kweli vijana hawa hii dawa imewasaidia sana na wanaendelea vizuri na wameweza kujitambua na kufanya shughuli zao. Mimi mmoja ni shuhuda wa hili, mimi mwenyewe nimewaona si vijana wawili wala watatu wala wanne ambao walikuwa na hali mbaya, baada ya kupata dawa hizi afya zao zimeimarika na wanaendelea vizuri. Kwa hili Mhe. Waziri niombe kuipongeza sana wizara .

Mhe. Naibu Spika, vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa hili limewezekana, basi aangalie upatikanaji wa dawa kama mwenzangu aliyetangulia alizungumza dawa kwa wale wenye tatizo la kifafa, na wale wenye tatizo la akili, hawa Mhe. Naibu Spika, huwa wanatumia dawa muda wote na uhai wao wote. Lakini kwa mfano wale wanaotumia dawa ya *phenobabiton*, kidonge kimoja ni shilingi 30 pengine wanatumia vidonge 60 kwa mwezi, fikiria kwa mwaka atatumia kiasi gani na uhai wake wote atatumia kiasi gani. Na huyu asipopata dawa hizi anakuwa tena afya haiko sawa. Mwenye kifafa atapokosa dawa hizi inaweza ikapelekea akapata tatizo jengine la akili, ama la ulemavu wa viungo, kwa hivyo hii dawa ni muhimu kwake kuitumia.

Aidha, kwa hawa wenye matatizo ya akili wanapokosa kutumia hizi dawa kama hapati usingizi, ndio hapati kabisa na kama anakuwa anazurura ndio anazidi kuzurura na kama anatoka madenda ndio anazidi kutoka madenda. Lakini uhai wake na uzima wake ni kupata hizi dawa. Hivyo basi, nimuombe Mhe. Waziri afanye jitihada zake zote kama alivyowezesha hawa wanaotumia madawa ya kulevya wakapata hizi dawa, na hawa wenye matatizo ya akili na kifafa angalau wafikiriwe kupatiwa hizi dawa bure, tena ziwe zinapatikana ili kuwapunguzia ukali wale wazazi, kwa sababu kuna wazazi wengine wana watoto wawili, watatu, wanne na wana tatizo kama hilo na hali ya maisha yetu tunaijua. Kwa hivyo, Mhe. Waziri afanye juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba hizi dawa tunazipata na ziwe zinaweza kuwaendelezea maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika kitengo cha mazoezi na viungo bandia, *Orthopaedic Workshop,* kitengo hiki kiko pale hospitali ya Mnazimmoja. Kitengo hiki ni muhimu sana kwetu sote wakiwemo wenye ulemavu na wasio ulemavu, kwa sababu hawa huwa wanafanya kazi zao za kufanya mazoezi kwa wale wagonjwa wanaohitaji mazoezi, lakini vile vile kitengo hiki miongoni mwa matibabu wanayoyatoa ni kufanya marekebisho na matibabu kwa wale wenye miguu rungu. Vile vile kitengo hiki kinatengeneza viungo bandi, miguu bandia, mikono bandia na viungo vyengine bandia wanatengeneza.

Lakini kinachosikitisha kitengo hiki pamoja na kazi zote hizo ambazo wanafanya hawapatiwi bajeti yoyote miaka yote. Je, nimuulize Mhe. Waziri katika hali kama hii tunawatengenezea mazingira gani watendaji hawa wa kitengo hiki, vipi wataweza kufanya kazi zao. Mhe. Waziri katika uwasilishaji wa hotuba yako Mhe. Naibu Spika, alieleza Mhe. Waziri kwamba wameongeza mfanyakazi mmoja wa kitengo hiki. Lakini kama kitakuwa kitengo hakina bajeti huyu mfanyakazi tunayemuongeza pale atakwenda kufanya nini?

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri afanye kwa makusudi katika bajeti hii ambayo tunategemea leo tutaipitisha na itapita inshaallah vizuri bila ya wasiwasi atenge fungu kwa ajili ya kitengo hiki ili awawezeshe hawa wafanyakazi angalau wawatie moyo. Kitengo kile kwanza hayo mazingira kiliko kinavunja moyo, wafanyakazi wanaweza kufanya chochote halafu tukaja tukawalaumu. Kwa sababu kwanza Mhe. Naibu Spika, ni wenye uwezo mkubwa tu wa kutengeneza hivi vifaa. Na ukitazama gharama wanazochukua wananchi au watu ambao wanaokwenda Bara kutengeneza viungo hivi ambapo akitengeneza hapa anaweza akapata pengine miguu 2.

Mguu unaotengenezwa hapa 250,000 akisafiri anaweza akatengenezewa kwa 500,000 lakini hapo hapo kuna gharama za usafiri na gharama nyengine za chakula. Na si kama anapofika tu pale unatengenezwa inabidi akae pale pengine siku 3 wiki, pale anatumia gharama, sasa kwa kupunguza gharama zile tunaonaje kitengo hiki. Kitengo hiki kikafanyiwa makusudi kitaingiziwa hii bajeti ili kupunguza haya makali kwa hawa wetu wenye tatizo hili.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na jitihada wanayoifanya ya kupitia katika maduka ya dawa kuangalia namna gani huduma hii inatolewa. Lakini bado kuna taarifa au manun'guniko kwa baadhi ya maduka ya ndani yanatoa huduma hizi ambapo wauzaji wake hawana sifa. Kwa hili nimuombe Mhe. Waziri na watendaji wake wafanye jitihada za makusudi kugundua hiki kitu ili kiondokane kama vile wanavyofanya kwa maduka ya mjini mjini kuondosha yale au kufunga. Basi kwa haya maduka ya ndani wafanye hivyo.

Baada ya hayo Meh. Naibu Spika, niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii, mimi Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Jimbo la Welezo. Kwanza naanza kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii kwa kuteuliwa kuwa waziri, *however* alikuwa Naibu Waziri. Kadhalika napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii shemegi kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu. Kadhalika naomba kuchukua fursa hii kumpongeza aliyekuja na wazo hili la kuanzisha Hospitali ya Mnazimmoja kuwa hospitali ya rufaa. Ni wazo zuri, wazo la busara lakini kama binaadamu tuna wasiwasi hali ya hospitali ya Mnazimmoja si nzuri.

Sasa Mhe. Waziri aje kutwambia kwamba kuwa hospitali ya Mnazimmoja ya rufaa hii hali ya sasa ambayo Mnazi Mmoja iko hali mbaya, Katika wizara

inayolalamikiwa sana Zanzibar kuliko wizara yoyote ile ni Wizara ya Afya, hasa hospitali ya Mnazi Mmoja kwa sababu ina majukumu mazito kwa maslahi wa wananchi. Jukumu la kwanza kututibu, jukumu la pili kutulinda tusipate maradhi.

Sisemi ameshindwa lakini kuna mambo ambayo mapungufu ni mengi, si siri Mhe. Naibu Spika, kuna uzembe katika hospitali ya Mnazi Mmoja ya hali ya juu, kuna dharau na unapowakuta watendaji ukiwauliza wanakwambia tatizo ni pesa. Kila mtendaji wa hospitali ya Mnazi Mmoja uzembe na dharau, lakini wanakwambia pesa.

Mhe. Naibu Spika, kuna maneno ya kiongozi mkubwa wa nchi hii karibuni tulikuwa tunaongea alisema

'Wizara ya Afya ni taasisi ambayo naomba kunukuu, inaingiziwa pesa kwa kiwango kikubwa, lakini viongozi wake bado wanakwenda mbio tu na kupenda kuoneshwa kwenye TV'.

Na Mhe. Rais ana matarajio makubwa na wizara hii, lakini bado hali ya Wizara ya Afya Mnazi Mmoja hairidhishi. Mhe. Naibu Spika, sasa naanza kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, miezi miwili iliyopita naonesha jinsi gani Mnazi Mmoja pana uzembe ambao unatusababishia vifo na wala siku zetu bado. Alipelekwa mzee wangu mpaka saa 8 alikuwa mzima yuko hai, kufika saa 9 alitiwa *oxygen* akaletwa mtoto, kuletwa mtoto ikabidi atolewe yeye *oxygen* atiwe mtoto, yeye akatiwa mipira ya pua miwili kufika 10.30 mzee wangu yule alitangulia mbele ya haki. Baada ya kuwauliza wakaanza kutetemeka wakanambia tatizo ni gesi, kwa sababu alikuja mtoto *priority*, mtoto nakubali ikabidi atolewe yule mzee atiwe mtoto, mzee alipoteza maisha kwa sababu tatizo ilikosekana gesi.

Mhe. Naibu Spika, si siri najua tauhid, ninaujua Uislam lakini mtu huyu angekuwa yuko hai kama gesi Mnazi Mmoja ingekuwepo, lakini ilibidi afariki. Nilipouliza nikaambiwa ukosefu wa gesi, lakini nimesema ni uzembe na dharau. Pesa hizi angekuwa anataka mkubwa kusafiri Mhe. Naibu Spika zingepatikana, lakini pesa za kununua gesi kunusuru maisha ya watu ati zimechelewa kuandikiwa na kutoka. Huu ni uzembe na hii ni dharau, ni wazi kwamba Mnazi Mmoja kutokana na uzembe na dharau wanatuua siku zetu bado.

Mhe. Naibu Spika, unapokwenda Mnazi Mmoja maslahi ya watumishi ni mabovu hayaridhishi, aliyemaliza *degree* na *master* Mnazi Mmoja daktari

anapitwa na dereva wa baadhi ya mashirika ya Zanzibar anapata mshahara mkubwa. Na kingine naomba kukisema kuna upendeleo katika kutoa maslahi kwa watumishi, hayo wamenambia wenyewe leo asubuhi, kwa sababu nimefanya *research* kubwa na naendelea kufanya *research* kubwa, kwa sababu siridhishwi na huduma za Wizara ya Afya ambazo zinaendelea kuwaua wakulima na wakwezi bila ya sababu.

Mhe. Naibu Spika, kuna hospitali inaitwa Al-Rahma, Al-Rahma tumei-*register* kama hospitali, lakini ukiangalia huduma inayotoa Al-Rahma haikidhi kuitwa hospitali. Mfano, anapotaka kufa mtu mbio hukimbizwa kupelekwa Mnazi Mmoja kutibiwa ili asifie Al-Rahma. Namuomba Mhe. Waziri Al-Rahma aitizame vizuri ina watu *unqualified* hawafanyi kazi vizuri, ipo pale taasisi hii kutafuta pesa kwa maslahi yao ubinafsi. Ninamuomba aifanyie uchunguzi akiweza aifute mpaka itapokuwa kweli hospitali ya kutoa huduma. Muda sina ningeeleza jinsi gani kutokana na utafiti wangu Al-Rahma inaua kila siku bila ya sababu.

Mhe. Naibu Spika, naendelea kuzungumzia uzembe na dharau ya Mnazi Mmoja. Leo asubuhi saa 1.20 nilikuwepo Mnazi Mmoja hospitali ni chafu, kwa hili pia utaambiwa pesa hata kumsimamia *orderly* kusafisha hospitali pia kunataka pesa, huu ni uzembe tu wa *administration* ya Mnazi Mmoja hawawezi kuwasimamia watendaji kusafisha hospitali ya Mnazi Mmoja ni chafu. Wote viongozi wa pale wana *private* hospitali zao, ukiziangalia *private* hospitali zao ni safi na zinaridhisha.

Chengine Mhe. Naibu Spika, maabara usiku hazifunguliwi, mashine za *x-ray* zote usiku zimefungwa na usiku wanakwenda wagonjwa wa *serious* ambao kutokana na kutokufunguliwa kwa huduma hizo zinawasababishia vifo. Naendelea kueleza uzembe.

Mhe. Naibu Spika, kitu kingine ni nidhamu kila pahali panahitaji nidhamu, kwa sababu tunahudumia wananchi lakini watendaji wa Wizara ya Afya, madaktari baadhi yao na manesi hawana nidhamu, wanamjibu mtu wanavyopata. Manesi na madaktari baadhi yao ukiwapa rushwa wanakuwa na nidhamu dhidi yako. Mambo haya hayafanywi katika mahospitali yao ya *private*, wanapoajiriwa wanafanya vizuri, lakini wanadharau hospitali ya Mnazi Mmoja kwa sababu ya kukitia doa Chama cha Mapinduzi kinachoongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nasema sio wote ni baadhi yao. Mhe. Naibu Spika, ninaiomba sana nidhamu hii lazima ukaisimamie. Wale *security officer* uliowaweka pale hawafanyi vizuri wananyanyasa watu.

Mheshimiwa kwa kumalizia chakula hospitali ya Mnazi Mmoja hasa *mental hospital*, chakula wanachopewa ni kibaya, hakina nidhamu, usafi mbovu, wale watu wananyanyasika. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa wazo kwa kumalizia. Hospitali ni kitu muhimu, matibabu ni kitu muhimu kwa mtu yeyote duniani. Tatizo ni kubwa kwa hospitali za Zanzibar, kwa sababu linatusababishia vifo siku zetu bado. Ninakuomba sana Mhe. Waziri amwambie Mhe. Rais aunde kamati ya kutafuta vyanzo vyengine vya pesa tuweze kuiendesha Mnazi Mmoja, kwa ya kunusuru vifo vya uzembe kwa wakwezi na wakulima. Pesa Zanzibar zipo, zinawezekana kupatikana lakini tuzitafutie vyanzo tuache kutegemea wafadhili kutuendeshea Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, jengine la mwisho kabisa watendaji wa Mnazi Mmoja kutokana na jeuri yao na kutokuwa na nidhamu, naomba Mhe. Waziri wavae beji ili tuweze kuwajua ni nani, tukaweze kuwakatia rufaa na kuwashitaki katika taasisi zinazofaa.

Mwisho sheria inayohusu *nurse* na madaktari lazima uwaelimishe wananchi wapate kuijua, kwa sababu wanavyotufanyia jeuri, dharau tuweze kuwalalamikia ikibidi afungiwe au kufukuzwa kazi. Natoa kesi moja, daktari juzi anamjibu mtu utanifanya nini, nikifukuzwa Mnazi Mmoja cheti changu kitanipa ruhusa ya kupata kazi nyengine. Mhe. Naibu Spika, hili si jibu la mtoa huduma daktari au *nurse* kwa raia wa kawaida mwenye kuumwa, amefanya amemzidishia kuumwa, amepanda *pressure* mpaka amekufa kwa jeuri ya daktari na *nurse*. Mhe. Naibu Spika, sheria hizi wananchi wetu ni lazima sasa wazijue waweze kuzitumia…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha…

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mimi na wengine tuko tayari kuwatetea wananchi hao, wakwezi na wakulima kwa dhuluma na vitendo vibaya wanavyofanyiwa hospitali ya Mnazi ya Mmoja. Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache muda ulikuwa mdogo naomba kuwasilisha. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hassan ningekushauri mengine unaweza ukapeleka kwa maandishi na ukapata majibu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Naunga mkono hoja asilimia 50 na asilimia 50 na-*reserve* mpaka nitakapojibiwa masuali yangu mengi, ili niweze kupitisha kwamba uzembe uwe mwisho Mnazi Mmoja. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa angalau dakika hizi kidogo na mimi nikachangia katika bajeti hii ya Wizara ya Afya, bajeti muhimu sana katika maisha yetu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya, lakini nimpongeze vile vile Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa kuweza kutujibu majibu yetu vizuri sana na kwa makini. Niwapongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote pamoja na watendaji waliomsaidia Mhe. Waziri kuweza kui-*frame* bajeti hii na kuja kusoma hapa kwa umakini mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nianze tu kusema mtu mzima akilia ujue kuna jambo. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Jaku amelia sana jana, na mimi nataka nimpongeze sana na nataka nianze hapo hapo.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chako hiki cha bajeti kwenye kifungu cha *up reading,* Mnazi Mmoja Hospital nasema hatujafikia wakati, pesa ni ndogo sana tutampa kazi sana Mhe. Waziri ya kufanya kazi hizi. Kwa hiyo, tungeiomba serikali kwa macho yote, kwa mioyo yetu yote iongezewe bajeti Wizara ya Afya ili ikafanye kazi zake. Wizara ya Afya ni wizara muhimu sana kwetu, bila ya afya hatufanyi kitu chochote, wenyewe wataalamu wa afya wanasema kinga bora kuliko tiba. Kwa hiyo, tunaomba sana tuanze na hili.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja na mimi niongeze kwenye hospitali hii ya *Mental Hospital*. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama utakumbuka *hansard* zangu za mwaka 2012 nilisema hapa kule nyuma kama hatuwezi kufyeka basi tukapande ule mpunga wa *NERICA*, kwa sababu unaota vizuri sana tutaweza kuondoa yale magugu mazito yaliyokuwepo pale. Lakini sasa ndio maana mpaka wale wezi wanaweza kuparamia na kuweza kuwadhuru wagonjwa wale.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ile ni chafu sana tungeomba sana wizara itupie macho pale wale ni wagonjwa tu kama wagonjwa wengine. Lakini mheshimiwa pale tulipoangalia Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii alipokuwa akisema pana p*sychiatric nurse* 22, lakini kazi zao zipi hazijuulikani. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja utwambie una mkakati gani wa kuweza kuona kuimarisha hospitali ile. Lakini halikadhalika na kuona basi unaweza kuwagundua hawa *nurse* ambao hawafanyi kazi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile alisema Mhe. Mwenyekiti kuwa daktari dhamana wa pale hafanyi *round*, sasa nini maana yake kuwa hafanyi *round*, hataki

kuwaona wagonjwa, amechoka kazi au vyenginevyo? Tunaomba hili utwambie ili tujue vizuri.

Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Mnazi Mmoja vitu vingi sana viko chakavu ikizingatia halikadhalika na yale majengo yake. Mhe. Naibu Spika, kwanza tunataka tupate vipimo bora, tunataka tupate vitu bora lazima kwanza majengo yetu yawe makini, yawe bora na yawe safi ndio tutapata kitu bora.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikizungumzia *orthopaedic clinic* kile kitanda cha siku nyingi na nikawahi kusema hapa, kile kitanda chake kinaweza kikamsaidia mtu au kikamsababishia kupata *tetanus* kwa sababu kimechakaa na cha muda mwingi. Kwa hiyo, ningemuomba Mhe. Waziri afanye ziara pale akakione ili basi kuwaonelea huruma wale wafanyakazi wanafanya kazi katika hali ngumu sana.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye maabara yetu ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, maabara hii ni maabara muhimu ili kupata kujua tunaumwa nini, ili kupata kujua tatizo letu nini lazima tuwe na maabara bora. Mwenyezi Mungu ametujaalia tumeweza kupata mfadhili pale *East African Support* ambazo anatusaidia *reagent* na zile zile *reagent* pale nimegundua ni zaidi ya milioni 60 inaweza kutumika kwa mwezi mmoja, sasa kwa bajeti hii iliyokuwepo hatuwezi kwenda popote. Kwa hiyo, tungeiomba serikali ijitahidi sana kuweza kuimarisha maabara ile, kuwapa *reagent* za kutosha ili tuweze kupata *quality improvement of pathology laboratory*. Tukiwa tunapata pale na tukiwa tuna *insurance* kubwa pale yakuwa na *standard* ya vipimo vyetu ndio tutaweza kujua jinsi gani maradhi haya yanaweza kuondoka. Waswahili wanasema ukiweza kugundua maradhi kwa asilimia 50 basi na dawa moja kwa moja umepata.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye *mortuary* yetu, *mortuary* yetu ni ndogo sana kutokana na ongezeko la binadamu,a Zanzibar *mortuary* ile haifai. Tunaomba sana serikali iweze kuongeza au kupata sehemu nyengine ya kuweza kujenga *mortuary* ile.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye bohari kuu ya madawa, lakini niseme tu changamoto ni nyingi sana nao tunawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo wanazozifanya. Wamefanya kazi kubwa, lakini tuseme tu wizara iwaone kulipa katika yale malimbikizo yao ya pesa za kazi ngumu.

Mhe. Naibu Spika, *x-ray department* tunawapongeza sana kwa kufanya kazi kubwa muhimu na kubwa sana kwa maisha yetu. Lakini kitu kimoja ambacho

tumekiona ni majengo chakavu yameendelea kuwepo. Pia kubwa jengine zaidi hata lile posho la maziwa pale *x-ray* limeoondoshwa. Kwa hiyo, tungemuomba Mhe. Waziri aje atwambie ni sababu gani, sababu ya ukata wa bajeti hii tunayokwenda nayo au kuna sababu nyengine ambazo wanazifanya wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye *ICU* nayo imekosa dawa muhimu sana, tungeomba sana Mhe. Waziri aje atwambie kwa nini *ICU* inakosa dawa muhimu. Mhe. Naibu Spika, nazungumza haraka haraka nakwenda kwenye *maternity*. Niwapongeze sana wakina mama au *nursing made wife* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya pale. Wamefanya kazi kubwa na mimi niwapongeze wanafanya kazi kwenye hali ngumu sana, niwapongeze sana. Wakati mwengine yale maneno machafu yanakuja na sisi wenyewe, lakini na wao wajitahidi sana kufanya kazi ile, kwa sababu mgonjwa *total* anapokwenda nae anakwenda mtanikoma, na wafanyakazi vile vile nao sasa binadamu wana sehemu kwa hiyo tujitahidi kwa pande zote mbili kuweka mustakabali wetu sawa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye madaktari, niwapongeze sana kwa kazi kubwa sana wanayoifanya na juzi nilikuwa shuhuda pale…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimwia umebakisha dakika tatu malizia.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nitakwenda haraka haraka nimekwenda kuwaona madaktari nikawa najiuliza kwa nini madaktari wengi wanakwenda kwenye njia za upinzani? Kumbe hali halisi ni hii, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hata vifaa tiba wanakosa. Kwa hiyo, tunakuomba sana Mhe. Waziri ujitahidi kwa hili. Lakini Mhe. Naibu Spika, niwapongeze sana ndugu zangu wa Bodi ile ya Hospitali Binafsi wamefanya kazi kubwa sana na wamezifungia hospitali nyingi. Hili sio la kusikitika kuna mtu wa maabara ni *nurse assistant* hawezi hata kusajiliwa kwenye bodi ya *nurse* anaenda kuwa mtu wa vipimo anajigeuza *lab technician*, ni hakika lazima waweze kufungiwa kitu hiki ni kibaya sana na anaweza akaua mara moja.

Mhe. Naibu Spika, niende tena kwenye bodi hii ya vipodozi na kumlinda mlaji. Niwapongeze sana wamefanya kazi kubwa sana, na ninawashukuru popote pale, nawambia wamefanya kazi vyema sana kwa mustakabal wa kutulinda sisi wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe pendekezo tu katika kifungu H 02 fungu la hospitali ya Mnazi Mmoja, hii imeandikwa ilikuwa na *program* moja, lakini mimi nilikuwa nataka nipendekeze kwa Mhe. Waziri na serikali nzima ziweko

katika *program* mbili. Baada ya kuwa na *programme* moja, *programme* ya kwanza iwe ya uchunguzi na hapa Mhe. Waziri nataka uangalie jinsi ya kurudisha kile cheo cha *Chief Director of Diagnosis Centre.* Lakini kingine kuweka huduma za matibabu kiweko mbali kabisa, hii itasaidia kurahisisha katika kuleta mustakabali na mwenendo mzuri. Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana na ninasema naunga mkono hoja na mengine nitapeleka kwa Mhe. Waziri, naunga mkono hoja kwa asilimia 95 na 5 naomba nizichukue mwenyewe. Nakushukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu katika wizara hii muhimu sana kwa maisha yetu Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri na kwa sababu Mhe. Waziri ni mtendaji mzuri sana, ni mtu ambaye anafuatilia, ni mtu ambaye hadharau kitu unachomwambia. Hilo kwa kweli namshukuru sana, sana lakini naomba tu isije ikawa ile "mgema akisifiwa….

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli siwezi nikaacha shukurani na watendaji wote wa Wizara ya Afya kuanzia Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wengine. Wanawatibu wazee wetu, watoto wetu kwa kweli tunafarijika sana. Isipokuwa tu nilikuwa nina ushauri kwa Mhe. Waziri tunapomaliza bajeti hii leo tukijaaliwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutaipitisha bila ya matatizo. Naomba sana zile nasaha na ule ushauri hasa ule wa waheshimiwa waliozungumza kwa ukali sana, naomba ukakae na watendaji wako uwaambie haya sio maneno ya waheshimiwa, haya ni mambo wameambiwa na wananchi wao. Kwa hiyo, hebu tujirekebishe ili wananchi wetu kupitia wawakilishi wao wawe na imani kubwa katika hospitali zetu zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati, kwa kweli jana mimi nilikuwa sipo, lakini nilifuatilia mjadala kuanzia tokea Mhe. Waziri anasoma mpaka Mwenyekiti anasoma hotuba yake. Kwa kweli katika kipindi kifupi sana kwanza Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii ni mtu wa kuiga sana, maana yake kamati zote hazikupewa nafasi za kuweza kwenda kutembelea katika wizara mpaka kupitisha bajeti. Lakini inaonesha kwa kuwa aliona Mwenyekiti mzoefu alifanya ziara ya ghafla na akaibua mambo mengi na akaishauri vizuri wizara yake na yeye alijaribu kuiga, na kwa kweli inaonesha kweli kamati kwa muda mfupi walikwenda wameona changamoto nyingi sana.

Jana nilisikia Mhe. Jaku kalia, lakini hata Mwenyekiti wa Kamati kama mlikuwa mnamuangalia machoni mwake yeye hakulia, lakini machozi yalikuwa yanamtoka. Sasa hii ndio hali ya wizara yetu na hospitali zetu. Sasa hata tukisema vipi kwa bajeti hii, kwa fedha hizi tulizomtengea Mhe. Waziri wa Afya kwa kweli bado, bado, bado sana. Mimi nilikuwa nina ushauri kidogo kuna baadhi ya mambo ambayo yanayohitaji huduma za dharura.

Mhe. Naibu Spika, tutakaa kikao kama wawakilishi kuna mambo sisi kama Baraza la Wawakilishi tutaandaa utaratibu na tutakaa na Mwenyekiti wa Kamati ili atuelekeze. Mfano, tukisema kuna fungu kiasi fulani kutoka katika mazingira yetu ya Baraza la Wawakilishi, sio ya bajeti kwa sababu bajeti hatuwezi tukatia mkono. Lakini yako mambo mengi ambayo tunaweza tukasema basi hapa hebu tunaweza tukasaidia kitu fulani. Kwa hiyo, tutakaa na Mwenyekiti wa Kamati tushauriane na sisi katika bajeti hii Mhe. Mwenyekiti tutatia baraka zetu vile vile. Lakini hilo ni la dharura, lakini hebu tuangalie mambo ya kudumu.

Mhe. Naibu Spika, kuna eneo hapa nililiona katika ukurasa wa 10 anaeleza kukamilisha sheria ya uanzishwaji ya mfuko wa bima ya afya. Mhe. Naibu Spika, moja katika muarubaini wa kuondoa changamoto za hospitali zetu, sio ya Mnazi Mmoja tu na pale Kidongochekundu ni suala la kuharakishwa kuanzishwa na hii sheria ya bima ya afya na serikali yetu. Mimi nashukuru serikali yetu sasa hivi kwa kweli wamo katika *speed* kubwa kuanzisha jambo hili. Pamoja na wafanyakazi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watu binafsi tuhamasishe wajiunge katika mfuko wa bima ya afya. Mhe. Mwenyekiti, matatizo mengi katika haya yataweza kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, tulipokaa na watu wa Mfuko wa Bima ya Afya walitwambia hospitali ya Al-Rahma ndio ambayo waheshimiwa wanaisema sema, kwa kweli katika kipindi kilichopita walikusanya fedha nyingi sana, karibu bilioni moja nafikiri na milioni mia sita kupitia Mfuko wa Bima ya Afya. Hospitali ya Mnazi Mmoja shilingi milioni mia mbili na hamsini, wakati wagonjwa wengi wanapata huduma nyingi tena kubwa kubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa hiyo, mimi nadhani ili wananchi wetu kuhakikisha kwamba tunapata huduma bora, serikali yetu iharakishe hii sheria ya kuchangia Mfuko wa Bima ya Afya na wananchi wetu mpaka wakulima, wavuvi kwa sababu suala hili huwezi ukalijua umuhimu wake mpaka ile siku ambayo unaumwa au anaumwa mtoto wako. Kwa hiyo, naamini hii tutakuwa tumei-*boost* bajeti ya Wizara hii ya Afya. Maana hata tukisema tunazuia huku mfumo wetu wa bajeti Mhe. Naibu Spika tukishaipitisha bajeti kuu ya serikali siku ile ya mwanzo pale tena

huwezi ukafanya kitu chengine, sana unachomoa mkono huu, unaunga mkono huu. Huwezi ukatoa fedha katika wizara nyengine ukaweza kuziingiza pale.

Mhe. Naibu Spika, sasa kusema kwamba unanyokoa eneo moja katika fungu la wizara hii hii ambalo pia halitoshi wende ukaliweke katika eneo jengine bado sasa tutakuwa tuko pale pale tunagaragara, tutakuwa hatujapiga hatua mbele. Lakini suala ambalo la kuweza kuongeza fedha ni huo ushauri ambao niliohisi kuweza kuuchangia.

Mhe. Naibu Spika, kabla hujaniambia nikae kitako dakika zangu zimeisha, nilikuwa tu nataka nimshauri Mhe. Waziri. Humu katika kitabu chake ameeleza moja katika malengo yake ukurasa huu wa 10 ni ukarabati wa jengo la macho katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Naibu Spika, nafurahi sana hii kauli kwamba ukarabati wa hospitali ya macho Mnazi Mmoja. Kwa hiyo, hii inaashiria kwamba kile kitengo cha macho kilichokuwepo katika hospitali yangu ya Jimbo la Kwamtipura, hospitali ya wananchi ina maana kile kitengo cha macho kimo katika maandalizi ya kuhama.

Sasa mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri wale watendaji tumeshirikiana vizuri sana, wametoa huduma nyingi sana za macho kwa Wazanzibari wote katika kituo chetu cha jimbo cha hospitali ya Kwamtipura ambao wengi wanaita Mikunguni. Nilikuwa naomba hata kama mkihama basi tubakishieni pale kile kitengo alau iwepo branchi pale ambayo ile huduma ya macho itaendelea kupatikana pale. Kwa hiyo, wengine watakwenda hospitali ya Mnazi Mmoja na wengine watakuja hospitali yetu pale. Lakini pia nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia una dakika tatu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya Mhe. Naibu Spika, dakika zangu tatu nilikuwa pia naomba kwa kuwa hii kutokana na mashirikiano makubwa tuliyopata kutokana na madaktari wale kitengo cha macho, basi ningeliomba kile kitengo cha macho kikija kikiondoka kikihamia kwao Hospitali ya Mnazimmoja, basi mtuletee na kitengo cha kung'oa meno, kwa sababu huduma hizi Mhe. Naibu Spika, na kwa kweli hospitali yetu inahudumia watu wengi wanaotoka mashamba na sehemu za ng'ambo, kwa kweli kitaweza kutusaidia sana.

Sasa cha kumalizia kabisa dakika yangu moja iliyobakia Mhe. Waziri, ameeleza changamoto nyingi, kuna changamoto ya wataalamu na kuna changamoto ya vitendea kazi. Mimi nilikuwa naomba au Mhe. Waziri, akija

aniambie je, katika hizi changamoto za watumishi, je kuna maombi yoyote waliyopeleka utumishi mpaka sasa hivi wamekwama hawajapatiwa nafasi za uajiri. Kwa sababu tukiangalia kuna vijana wengi wamesoma, kuna vijana wengi wana utalaamu mbali mbali, lakini wamo wanahangaika kazi hawana na huku waziri anasema ana changamoto ya watumishi katika wizara yake. Sasa hili nilikuwa naomba aje atuambie je, kuna maombi gani waliyoyapeleka utumishi hawajawajibu, lakini Hospitali ya Abdalla Mzee Mhe. Naibu Spika, Hospitali nzuri kubwa ya kisasa, lakini Mheshimiwa jengo halitibu, vinavyotibu ni vifaa na wataalamu. Je, kule Abdalla Mzee Hospitali kuna mpango gani makusudi ulioandaliwa, ili na wenzetu kule Pemba wakapata huduma iliyo bora kama ilivyo Mnazimmoja.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hasa akija akiniambia kwamba kitengo cha macho kikihama kitabakishwa sehemu na vile vile kitengo cha meno katika hospitali yangu, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa wale wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia aidha ikiwa kwa kuzungumza au kwa maandishi, lakini vile vile nimepata majina ya Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri ambao na wao walitaka kuchangia, lakini kwa bahati mbaya sana kutokana na muda wetu hawatopata fursa hiyo. Lakini ningeomba sana niwataje, ili waingie kwenye *hansard* kwa nia ya kwamba walikuwa wanataka kuichangia Wizara ya Afya. Naanza na kumtaja:

1. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mhe. Lulu.
2. Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali - Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri
3. Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum - Mhe. Juma Ali Khatib
4. Mhe. Waziri mwengine asiyekuwa na Wizara Maalum - Mhe. Said Soud
5. Mhe. Naibu Waziri wa Habari na Utalii - Mhe. Chum Kombo Khamis
6. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafuzo ya Amali - Mhe. Riziki Pembe Juma na
7. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Mhe. Dkt. Khalid na
8. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji na Wanawake, Watoto, Vijana, Wazee - Mhe. Castico

Kwa hiyo, fursa nitampa Naibu Waziri wa Afya pamoja na Mhe. Mohammed Aboud, Waziri wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na baadaye nitampa Mhe. Waziri, ahsanteni. Naomba nianze na Mhe. Aboud na baadae atakuja Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili nami kwa niaba ya serikali niseme maelezo machache. Lakini pia nataka nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake kwa kazi nzuri katika kipindi kifupi sana. Naamini sana sote humu ndani mashahidi namna ambavyo katika muda mfupi tumemuona Mhe. Waziri alivyoweza kui-master vizuri wizara hii na alivyoanza vizuri yeye na Naibu Waziri wake, kwa hiyo tuwapongezeni sana kwa kazi nzuri na naamini kutokana na uvumilivu wao na umakini wao na usikivu wao wameyasikia sana maelezo yetu waheshimiwa wajumbe, lakini pia wana mtindo wao wa kwenda moja kwa moja kwa wananchi kusikiliza maoni yao na kupitia vituo mbali mbali vya afya na hospitali zetu kujuwa yaliyopo, kiundani wanayajua mengi sana katika sekta hii. Kwa hiyo wanayoyafanya tuwape moyo, ili wazidi kuyafanya kwa dhamira ile ile ya kuimarisha na kutoa huduma bora katika sekta hii ya afya. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika, lakini pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwanza kupitia kamati na Mwenyekiti mwenyewe kwa maelezo yake na wajumbe wake kwa kazi nzuri waliyoifanya na namna ambavyo wameshauri. Lakini na wajumbe wote waliochangia kwa namna ambavyo wana upeo mkubwa na uwezo wa hali ya juu katika kuwasilisha hoja. Lakini kwa imani kubwa waliyonayo kwa wananchi wetu, zote pande mbili serikali na wajumbe nia na dhamira ni kuimarisha na kutoa huduma bora za afya.

Tazito letu la msingi ni hilo mulosema na ni hali halisi ya uchumi wetu ndio unaotukwaza kutekeleza yale ambayo yote mloyasema tuyatekeleze.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo mliyoyasema yote ni mazuri na dhamira ya serikali ni hiyo kuhakikisha utendaji katika sekta hii unafanyika kwa asilimia mia moja, lakini hali halisi ya kifedha ndio unakwamisha utekelezaji huo na ndio maana serikali sasa inachukuwa hatua mbali mbali za kuimarisha uchumi kwa msingi moja katika eneo muhimu ambalo linapewa kipaumbele ni katika sekta hii ya afya, elimu, maji na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo ninataka niwaondoe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe kwamba hayo yote mloyasema serikali inayaelewa na inayafanyia

kazi, nilichokifanya katika kueleza katika Baraza hili ni zaidi kuweka mkazo, ili na sisi tuongeze kasi ya utekelezaji, ili tukidhi kiu yetu na kiu ya wananchi, tunajuwa sana sana matatizo wanayoyapata wananchi katika sekta hii ya afya. Lakini dhamira yetu ni njema kama ilivyo yenu, hoja yetu kuu ni kuimarisha hizo huduma za afya. Pale tunaposema tunaimarisha hospitali ya Mnazimmoja, dhamira yetu si kuimarisha peke hospitali ya Mnazimmoja lakini kuziimarisha hosptiali zote. Hospitali ya Mnazimmoja kwa utaratibu wetu wa hapa Zanzibar ndio kituo kikuu cha afya katika hospitali zetu mbali mbali zinaposhinda kwa namna moja au nyengine, basi wagonjwa hupelekwa mnazimmoja kwa mtazamo wetu sisi inakuwa kama ni hospitali ya rufaa kwa maaana inahitajika kitaifa kwa watu wote.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo jitihada zetu ni kuimarisha hospitali hizo nyengine, ili ziweze kutoa huduma bora huko ziliko na kadiri inavyowezekana kuimarisha na hospitali ya Mnazimmoja.

Kwa hiyo dhamira ya kuimarisha hospitali ya Mnazimmoja inaenda sambamba na kuziimarisha hospitali zote zikiwemo hospitali ya Micheweni kule Pemba, hospitali ya Wete, hospitali ya Chake Chake, hospitali ya Mkoani, hospitali za hapa Unguja, za Kivunge, Makunduchi na kwengineko ili ziweze kutoa huduma.

Mhe. Naibu Spika, lakini tunajuwa sote kwamba wengi wetu hapa tunaitumainia sana hospitali ya Mnazimmoja. Ndio maana inabidi kwa njia moja ama nyengine ipewe upendeleo maalum ili tuziimarishe huduma hizo ziweze kutoa huduma bora. Sasa lipo eneo hapa naamini Mhe. Waziri atalizungumzia zaidi lakini na mimi kwa kiasi ninavyoelewa niseme, kuhusu kuimarisha hospitali ya Mnazimoja na kupewa fedha hizi 7.5 bilioni. Hizi Waheshimiwa Wajumbe zimetengwa kwa dhamira ile ile ya kuimarisha hospitali yetu na hiki kilio chenu mnachokisema cha kutoa hutuma bora za afya ndio dhamira yake si vyenginevyo na kwa bahati nzuri fedha hizi, pia tunahamasisha wenzetu, kwa wafadhili wetu na marafiki zetu ambao kwa miaka mingi wamesimama na sisi katika kuimarisha huduma za afya.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano wenzetu wa Norway wametujengea pale jengo la mama na mtoto, jengo jipya la kisasa ambalo litakuwa na vitanda mia moja na vifaa mbali mbali vya uzalishaji na pia kutakuwa na vitanda sita kwa ajili ya huduma ya *dialysis*. Sasa katika zile bilioni 7.5, milioni mia tano kama mchango wa SMZ unaingia katika msaada huu mkubwa katika ujenzi wa hospitali pale Mnazimmoja.

Kwa hiyo tunaposema *upgrading*, tunapotoa milioni mia tano katika kutoa huduma bora za uzazi, nyote mnaelewa namna gani tunapoteza maisha ya watoto wetu wakati wa uzazi, tunapoteza maisha ya mzazi mwenyewe, kwa hiyo kinachofanyika pale ni kutoa huduma bora, za kisasa kwa umakini zaidi ili kuepusha vifo, ili kuepusha magonjwa na watu wetu wapate huduma bora.

Mhe. Naibu Spika, lakini tunalo tatizo kubwa ambalo wagonjwa wengi wa sukari hupata athari hiyo ya mafigo na ndio maana kunakuwepo sasa na kitengo hicho cha *dialysis* pale ndani kitakachosaidia kutoa huduma bora.

Kwa hiyo tunapoweka mchango wa milioni mia tano ni kuongeza nguvu kwa wenzetu wa Norway ambao wanatusaidia katika lengo hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini zile bilioni 7 zinakuwa vipi. Ile ni mchango wa ule mradi wa ORIO ambao SMZ inatoa asilimia hamsini na wenzetu wa Holand wanatoa asilimia hamsini, pale tena pana ujenzi maalum wa wodi ya watoto na *clinics* zake, kwa maana ya kwamba kutakuwa na *x-ray*, *ultrasound*, hata *ICU* ya watoto itakuwa mule mule ndani, *incubator*, ma-*generator* ya kusimamia kituo hichi; kwa hiyo zile bilioni saba SMZ inatoa bilioni 3.5 na wenzetu wa Holand wanatoa bilioni 3.5, ili tujenge wodi hii ambayo ipo pale pale karibu na ile wodi ya mama na mtoto, kutakuwa na jengo jengine.

Kwa hiyo tuna majengo mawili pale Mnazimmoja mpya, ya kisasa, yatayotoa huduma bora kwa watoto wetu, kwa mama zetu kwa maana ya kuimarisha huduma ya afya. Kwa hiyo fedha tulizonazo ndogo tungepaswa tutoe zaidi kwa ajili ya kuimarisha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naelewa *concern* ya wajumbe wanavyozungumzia suala la fedha hizi ziende kwenye madawa, lakini tuone umuhimu watakayopata watoto wetu, mama zetu na kadhalika. Kwa hiyo suala la madawa bado serikali linayafahamu na bado tunazungumza na wafadhili wetu, marafiki zetu, licha ya mchango mkubwa wa serikali katika madawa, ili na wao marafiki zetu waanze kusaidia na namshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya amefanya jitihada kubwa katika eneo hili, amewaalika wale *traditional friends* wetu wanaotusaidia katika hili na aliwakaribisha hapa siku yake ya usomaji wa bajeti. Nia na dhamira ni kuongeza nguvu katika kuchangia huduma ya madawa. Kwa hiyo suala hili sio lenu peke yenu Waheshimiwa Wajumbe, ni letu sote kwa pamoja, dhamira ni kuimarisha huduma bora za afya yakiwemo madawa na kila la muhimu linalofanywa.

Mhe. Naibu Spika, lakini ninataka niseme kwanza ushauri wenu hususan suala hili la mfuko wa Bima ya Afya hili jambo limefanyiwa kazi kubwa sana ndani ya serikali, Mhe. Waziri, atakuja kulieleza kwa kina. Lakini yako mambo ya msingi ambayo mlituambia na takriban yote ya msingi, sisi wajibu wetu kuyapokea na kuyafanyia kazi kwa bidii kubwa, ili yalete tija na utanisi. Sulala la maslahi ya madaktari ni jambo muhimu sana, ni lazima madaktari wetu wapate motisha, hali zao za maisha, majukumu ya kazi yao na hasa tukitumainia tunahitaji wafanye vizuri zaidi kuliko wanavyofanya sasa.

Kwa hivyo kuwatizama kimaslahi na kuwapa nyumba na haki zengine nadhani tungeipongeza serikali, tusiilaumu serikali kuwashughulikia madaktari kwa jambo hili, maana madaktari wetu wanafanya kazi kubwa lazima tuwapongeze.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi nipokee kwamba tubadilishe ile mindset yetu kwa madaktari na wahudumu wote wa Wizara ya Afya wanapowashughulikia wananchi wetu kwa maana ya wagonjwa wanaokwenda pale, lazima nidhamu iwepo, unyenyekevu uwepo, heshima iwepo, kwa sababu saikolojia kubwa unapompa mgonjwa huduma ukafanya vizuri kwa maelezo mazuri, maneno mazuri si ya kifedhuli moja ni tiba kwa upande wao.

Kwa hiyo jambo hili kama serikali tutashirikiana pamoja tuone namna gani tunachukuwa hatua za ziada katika kuhakikisha watoa huduma hawa kwa wananchi wanatoa huduma bora, lakini kwa nidhamu na kwa kufata taratibu zao za kisheria.

Mhe. Naibu Spika, liko jambo pia limezungumzwa na Mhe. Hassan kuhusu Hospitali ya Al-Rahma. Kwanza mimi nataka nichukuwe fursa hii kuzipongeza sana zile hospitali binasfi zinazofanya vizuri kwa kutoa huduma, zimeitikia wito wa serikali, zinafanya vizuri na Al-Rahma nayo ni moja katika hospitali ambayo inajitahidi kufanya kazi na kwa kweli ndani ya serikali tunaongozwa kwa mujibu wa sheria, sheria nambari 4 ya mwaka 1994 ambayo inasimamia utoaji wa huduma kwa hospitali binafsi, iko Bodi maalum inayosimamia hospitali binafsi, Bodi hiyo haijaleta serikalini tuhuma ambazo Mheshimiwa amezieleza.

Kwa msingi huo sisi tunaamini hospitali hii inafanya kazi vizuri na wengi tuliomo humu ndani tunakwenda pale, tunaona huduma zao kwa kiasi fulani wameitikia wito wa serikali na tunapaswa kuwapongeza hawa na wengine wanaoshiriki katika kutoa huduma ya afya, tunahitaji zifanye nzuri. (*Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninataka nimpongeze sana Mhe. Dimwa kwa kuona jambo hili, kwa kuona umuhimu wa hospitali hizi binafsi zimetusaidia sana tusizivunje moyo, tunapozizungumza hapa kwa tuhuma na shutuma kubwa tunavunja moyo kwa kiasi fulani, ni lazima tuone umuhimu wao na pale penye kosa basi tulizungumze kosa lile kwa mujibu wa zile sheria, maana wao hawana wa kuwasemea hapa, hawawezi kutoa majibu hapa, sasa sisi wajibu wetu kama serikali linapotoka hili tulieleze. Kwa msingi huo kama lipo tatizo la msingi kwa mujibu wa sheria iliyopo, waheshimiwa mungepeleka malalamiko haya kwa Wizara ya Afya wakajua tatizo ni lipi la msingi.

Mhe. Naibu Spika, malalamiko yamezungumzwa sana, zipo *sabotage* katika hospitali za Pemba na kwengine, nazo ni vile vile kama hujapata ushahidi wa kutosha ukawapelekea wenzetu wa Wizara ya Afya ni tabu sana kufanya maamuzi yaliyokuwa hayana mashiko.

Kwa hiyo tunapoona upo ushahidi fulani, kuna jambo fulani limefanyika kinyyume na utaratibu, amedhalilishwa mtu, hakupewa huduma stahiki, haya mambo tunapaswa kama wajumbe tuyaripoti kwa mujibu wa sheria, ili hatua zikichukuliwa zichukuliwe kwa misingi ya sheria. Kwa sababu shilingi ina pande mbili ina upande huu na upande huu, kosa lifanyike likifanyika tulione hatua zichukuliwe kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, sisi tunatoa agizo maalum kwa watendaji wetu wa Wizara ya Afya, wahakikishe wanatoa huduma bora, kwa nidhamu, kwa kuwanyenyekea watu wetu, ili wagonjwa wetu wapate huduma stahiki.

Baada ya maelezo haya Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Afya kwa asilimia mia moja na nawaomba Wajumbe wenzangu tuwapeni nguvu wakaanze, naelewa ni kidogo wangehitaji kupata kingi lakini ndio kilichopo. Kwa hiyo, tuwaunge mkono kwa hiki kidogo tukipitishe wakaanze kazi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii, nakushukuru na kukupongeza wewe pamoja na Spika kwa uongozi wenu mahiri kwetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa umuhimu wa pekee naomba nimshukuru kwanza Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia na kutupa nafasi hii ya

kuwepo hapa kwa kuwawakilisha wananchi ambao wanatuamini na wanaendelea kutuamini, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya chini ya uongozi mahiri wa waziri Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Mwakilishi wa Jimbo la Kiembe Samaki na kwa mashirikiano mazuri na wahusika wa wizara hii inawathibitishia wananchi pamoja na Wajumbe wa Baraza hili kwamba tutaendelea kufanya wajibu wetu kwa kuhakikisha tunatekeleza kwa dhati agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwatumikia wananchi wote, pahali popote na bila ya ubaguzi wowote. Kila mmoja wetu ana wajibu wa kusimamia na kutekeleza wajibu wake katika nafasi aliyo. Wananchi tunawaomba watuamini pia watupe mashirikiano kwa kuwafichua wale wote watakaobainika kwa njia moja au nyengine kukiuka miiko ya utumishi kwa kutofanya wajibu wao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya wakiwemo madaktari mabingwa wazalendo na wale wageni wanafanya kazi kubwa ya ujasiri kwa kuyalinda na kuyaokoa maisha ya wananchi kwa kila kitu na bila ya kujali maisha yao. Changamoto katika Wizara ya Afya ni nyingi, lakini wenzetu hawa wanafanya kazi za ziada na katika mazingira magumu na wakati mwengine katika mazingira ya kukatisha tamaa hasa pale yanapotokea majanga ya maradhi ya mripuko na ya kuambukiza, ambapo kwa mara chache hutokezea kuathiri na hata kupelekea kupoteza maisha yao.

Nawapongeza na kuwataka waendelee na moyo huo bila wa kuwatumikia wananchi bila ya kuweka maslahi mbele, kwani kazi wanayoifanya ina malipo madogo duniani, ina lawama kubwa na changamoto nyingi. Nawaomba waendelee na juhudi zao kazi hii ina malipo makubwa kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba sasa nichukue fursa kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa michango yao katika hotuba yetu hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya ya mwaka 2016/2017. Shukurani za pekee naomba pia nizitoe kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi wake mzuri aliyoutoa punde tu kuhusu Wizara yetu ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa nianze kujibu baadhi ya michango iliyotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kama ifuatavyo na naomba nianze na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mwakilishi wa jimbo la Chaani.

Mhe. Nadir Abdul-latif aliuliza ni hatua gani zitachukuliwa kwa wodi ya wazazi Mnazi Mmoja hasa kwa udhalilishaji, na zaidi aligusia kujifungua bila ya kuwa na nguo. Mimi naomba nimjibu kwamba, kwa kweli mzazi anapofikia katika ile *critical stage* ya kujifungua basi bila ya kuambiwa kwamba vua nguo yeye mwenyewe nguo kwake ni tatizo. Inawezekana wazazi hawa au baadhi ya wazazi ambao wamemueleza baada ya kufika kwenye wodi na ikabidi kitendo cha kujifungua kimeshafika basi yeye mwenyewe anaikataa nguo kutokana na machungu na maumivu makali anayokuwanayo. Mimi sifikirii na haijawahi kutokea *nurse* au *orderly* au dokta akamwambia zivue nguo ziweke kule kaa juu ya kitanda cha labour ukiwa uchi, hiyo haijawahi kutokea. Lakini kutokana na hali halisi aliyokuwanayo pale basi nguo kwake ni mzigo. Hili naomba lieleweke. *(Makofi)*

Jengine anasema ni sababu gani zinazosababisha wanaume waingie ndani ya chumba cha kuzalia *(maternity room)*. Mhe. Nadir hili nataka nimjibu kwamba mule wanaoingia sio wanaume ni madaktari, walio wanaume kweli kweli na ambao wamesababisha mimba ile ije izaliwe pale huwa wanafikia mlangoni wanapokewa mizigo, wanapokewa mikoba inaingizwa ndani, lakini mwanamme yeyote utakayemuona ana suruali ndefu anaingia mule basi muangalie hana *uniform*, huyo ni daktari, ni *nurse* au *orderly*. Mara nyingi katika wodi ya wazazi basi *orderly* mwanamme hapewi nafasi mara nyingi mule ma-*orderly* ni wanawake, lakini wanaopewa nafasi ya kuwemo mule ni madaktari na ma-*nurse* kwa ajili ya uzito wa tatizo lenyewe la uzazi.

Naomba niendelee na suala la Mhe. Suleiman Sarahan wa Chake Chake. Kwanza Mhe. Suleiman Sarahani kwa niaba ya wizara yangu naomba tumpongeze na kumshukuru sana kwa jinsi anavyofuatilia katika Hospitali ya Chake Chake. Wakati nilipofanya ziara mwezi uliopita nilipata taarifa kwamba anafuatilia kwa njia ya simu, anafuatilia kwa njia ya kwenda yeye mwenyewe. Nampongeza sana na nilipata taarifa kwamba yeye katika hospitali ile ana cheo kumbe ni mlezi wa Hospitali ya Chake Chake.

Pia tunampongeza kwa moyo wake wa kujitolea kuweka ahadi ya kununua televisheni katika hospitali ile. Inshaallah Mwenyezi Mungu amjaalie, ambariki na yeye Mwenyezi Mungu amlipe zaidi. Suala lake lilikuwa linahusu ukarabati wa hospitali pamoja na vituo vya afya. Suala hili pia aliliuliza Mhe. Mtumwa Peya kwa kituo cha Makoba.

Mhe. Naibu Spika, wizara imejipanga mpango maalum kwa kufanya ukarabati wa baadhi ya hospitali zetu na vituo vya afya na tunaanza baada ya bajeti hii, tunaomba tuwe na subira tutafanya ukarabati huu hatua kwa hatua kwa jinsi

bajeti itakavyoturuhusu na kuweka baadhi ya vifaa kwa baadhi hospitali kama *generator*.

Kuhusu utaratibu wa kuchunguza afya za watoto maskulini, ili kubaini matatizo mapema. Mhe. Suleiman Sarahani hili pia aliliuliza. Mimi naomba nimjibu kwamba huduma hii ipo lakini kwa baadhi ya magonjwa kama macho, masikio na kadhalika. Tunalipokea shauri lake hili tutajiandaa kwa ajili ya kuchunguza zaidi katika maskuli hawa wanafunzi wetu.

Pia aliuliza kuhusu madaktari mabingwa wa maradhi ya kansa, figo na kadhalika kuweko katika hospitali zetu za Pemba na zaidi Hospitali ya Abdalla Mzee. Mimi nataka nimhakikishie kwamba karibuni tutafungua hospitali yetu kubwa ya Abdalla Mzee Mkoani na mambo haya yote wakiwemo madaktari mabingwa tunatarajia watakuwepo na hawa wanaweza wakafanya huduma nzuri kwa hospitali za Pemba nzima.

Mhe. Naibu Spika, wa tatu alikuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) suala lake lilikuwa linahusu zaidi huduma za afya katika Hospitali ya Wete kutolewa kwa ubaguzi kutokana na siasa. Mimi napenda nimjibu suala lake la kuhusu ubaguzi katika sekta ya afya, inawezekana lipo, lakini kwa sababu wanaolalamika kuhusu jambo hili hawako tayari kutoa ushahidi, tunaomba tupatiwe ushahidi maalum wa kisheria, kwa sababu sheria ya madaktari ni kutoa huduma bila ya ubaguzi wowote na ndivyo Mhe. Rais wa Zanzibar anavyotusisitiza. Tunaomba ushirikiano wenu ili tupate ushahidi, ili sheria za utumishi zichukuliwe na kufuata mkondo wake kwa muhusika atakayekutikana na tatizo hili.

Mhe. Mtumwa Peya yeye alizungumzia kuhusu upungufu wa dawa katika vituo vya afya. Upungufu wa dawa katika vituo vyetu vya afya mara nyingi huu unatokana na upungufu wa dawa katika Bohari yetu Kuu. Kwa sababu mgao wa dawa katika vituo vyetu vya afya unafanywa kwa mahitaji ya kituo husika, kila baada ya miezi mitatu kituo husika kinapeleka orodha yake ya mahitaji yake ya dawa na kwa bahati nzuri dawa ambazo zipo zote huwa anapewa ama za miezi mitatu au miezi sita. Sasa inapotokea tatizo kama hili kwenye kituo ikawa dawa fulani haipo kwa mfano panadoli kama alivyotolea mfano, basi inakuwa dawa ile pengine hata huko kwenye Bohari Kuu inakuwa haipo. Hata hivyo, kupitia Mfuko wetu wa dawa ambao tuliomba Waheshimiwa Wawakilishi muingie katika kuuchangia basi tunategemea tatizo hili litamalizika na vituo vyote vitapata dawa kama inavyotarajiwa.

Jengine ni kuhusu eneo la Pangatupu kupatiwa kituo cha afya. Mhe. Mtumwa Peya namuomba apate nafasi aje wizarani tukae na wataalmu tufanye utafiti juu ya kuona *population* ya watu iliyoko katika kituo hiki cha Pangatupu, ili tuone kama kuna umuhimu kweli wa kupatiwa kituo chengine kule au watatumia katika kituo cha karibu, ili shida ya kutafuta huduma ya afya iwaondokee hawa wananchi wa Pangatupu.

Mhe. Panya Ali Abdalla huyu ni Mjumbe wa Viti Maalum. Kwanza Mheshimiwa tunampongeza kwa dhati kwa ushauri wake kwa wajumbe kwa kuchangia posho ya siku moja kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Dawa. Lakini pia tunawapongeza kwa dhati Wajumbe wa Baraza hili mana tumeona sura ya kukubali kwa shauri hili.

Pia tunamshukuru Mhe. Panya Ali Abdalla kwa michango yake mbali mbali kwa jitihada zake wakati tukipita katika baadhi ya vituo kufanya ziara zetu huwa tunapata habari zako, kwamba unapita katika baadhi ya vituo hivyo na kuona jinsi wanavyofanya shughuli zao.

Suala jengine ni Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Mheshimiwa ametushauri kufuatilia katika sehemu za mahoteli vinakopikwa vyakula na anasema kwamba huko mara nyingi huwa vinapikwa vyakula vilivyoharibika au vinapelekwa vyakula vilivyoharibika.

Mimi namhakikishia ushauri wake huu tutauchukua lakini mpango huu katika Wizara ya Afya upo wa kupita katika mahoteli yetu na sio kupita tu, bali wanaangalia afya mpaka ya wapishi, wanaangalia sehemu za jikoni kunaridhisha au hakuridhishi na baadae ndio wanatakiwa watoe huduma hiyo. Lakini tunachukua ushauri wake wa kupita pengine kuna sehemu ambayo tulikuwa hatujaipitia au tumepitia muda mrefu kwa hiyo wanafanya wanavyotaka.

Mhe. Naibu Spika, nije kwa Mhe. Bahati Khamis Kombo yeye amesema kwanza kuhusu uhaba wa madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee. Mimi naomba tumhakikishie kwamba uhaba huo wa madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee karibu utafikia hatima. Kwa sababu jengo la hospitali hiyo liko katika *final position* kumalizika na litakapomalizika mwezi unaofuata hili jengo linahitaji wafanyakazi wasiopungua mia mbili na sasa hivi wizara imo katika mchakato kutafuta uwezekano wa kupata uajiri wa wafanyakazi hao, wafanyakazi hao wakiwemo madaktari, ma-*orderly* pamoja na wafanyakazi wengine. Kwa hiyo, hili tatizo lina kikomo chake na huenda ikawa ni karibuni.

Kuhusu wafanyakazi kutoka Unguja kufanya kazi miaka miwili tu Pemba na hawafikii miaka miwili wanaomba kurudi na tunawaruhusu warudi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili ni suala ambalo sisi wenyewe Waheshimiwa humu tunalichangia, na naomba niwashauri Waheshimiwa wenzangu kwamba tuache utaratibu huu. Mfanyakazi anapohamishiwa Pemba sijui kuna kitu gani lakini hata ile miaka miwili huwa haitimii anaomba arudi Unguja. Wizara inamkatalia kwa sababu anajua mkataba wa miaka miwili aliyopewa haujafikia au haujamaliza, lakini ni sisi Waheshimiwa ambao tunaingilia kati wizara na kupeleka maombi na kusema pengine huyu mumewe atamuacha, au huyu ana matatizo haya, basi tunatengeneza mistari ya kuwafanya watendaji pale Wizara ya Afya wawaruhusu, ili warudi Unguja bila ya kutegemea. Hili ni tatizo tunaomba lisiendelee kwa kweli linaathiri. Hata sisi tumeshaliona kwamba linaathiri tunaomba waachwe wafanye kazi kwa kadiri ya mkataba ulivyowaruhusu.

Mhe. Bahati aliendelea na suala kuhusu ukosefu wa madaktari Chambani, Mtangani, Wambaa. Wizara iko katika hatua ya kuhakikisha mapungufu hayo yanafanyiwa marekebisho hatua kwa hatua kwa kupata madaktari watakaofanya kazi katika sehemu hizo hasa pale baada ya kumaliza katika hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, basi watakaoajiriwa kufanya kazi kule na wengine watapelekwa katika vile vituo ambavyo vina uhaba mkubwa wa madaktari.

Kuhusu Hospitali ya Ukutini kuwa ni hospitali ya rufaa kwa waja wazito hii ni ahadi ya Rais. Ahadi za Rais ni ahadi za serikali zina kitengo maalum katika wizara yetu. Hili tayari liko katika mpango linashughulikiwa naomba Mheshimiwa apate nafasi aje, ili tubadilishane mawazo na kuona hali ya kufikia ufanisi katika suala hili, lakini utekelezaji wa suala hili upo unafanyiwa mipango.

Mhe. Naibu Spika, mwengine ni Mhe. Shehe Hamad Mattar yeye amesema kituo cha afya Finya kina matatizo ya nyumba ya daktari.

Mheshimiwa kweli kituo cha afya Finya kina tatizo la nyumba ya daktari. Kituo kipo, kizuri, kinafanya kazi vizuri, lakini kina tatizo la nyumba ya madaktari na hii sio kwa kituo cha Finya tu vipo na baadhi ya vituo ambavyo vina tatizo hilo. Lakini kituo hiki tatizo lake halikuwa ujenzi wa nyumba ya daktari pia palikuwa pana *miss understanding* baina ya watu au jamii.

Nakumbuka nilipofanya ziara mwezi uliopita katika kituo hiki cha afya nilikuta kuna kutokufahamiana baina ya jamii iliyopo, sheha pamoja na jumuiya ya

mtaa ule ambayo ina mkono fulani inasaidiwa na wakaazi wanaokaa Bara lakini wamezaliwa katika kijiji cha Finya. Nilikuta tatizo hilo kwamba hawaelewani na wao ndio waliokuwa wakivutana kwamba nyumba ijengwe, isijengwe, wapi kila mtu anajivutia upande wake. Sheha anasema hashirikishwi lakini Jumuiya ya Finya na wao pia walikuwa wanasema hawakushirikishwa ipasavyo, kila mtu alikuwa anajivutia upande wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri tulikwenda pale pamoja na Afisa Mdhamini baada ya kutueleza tukaitisha kikao Kamati ya Sheha ile Jumuiya ya Finya pamoja na jamii waliokuweko karibu wakafika, baada ya kuzungumza nao tukakubaliana na kulitatua lile tatizo basi moja kwa moja waliahidi kwamba sasa wako kitu kimoja na baada ya kuondoka kwangu mimi kama Naibu Waziri kuendelea na ziara yangu wao watakaa pamoja na watapanga na walinihakikishia kwamba sehemu ya kujengwa nyumba ya daktari ipo, ila tatizo walikuwa hawajakubaliana. Kwa hiyo, naamini suala hili kwa mashirikiano yao litafanikiwa.

Jengine ni kuhusu suala la Mhe. Ali Khamis Bakar wa Tumbe, amesema kwa sasa kituo cha Tumbe kina jumla ya wafanyakazi watano. Amesema kuna uhaba wa wafanyakazi katika kituo chake cha Tumbe. Tatizo hili sio la Tumbe tu ni sehemu nyingi kwa kweli kuna uhaba wa wafanyakazi na hili hata wafanyakazi wetu wanalilalamikia sana, kwa sababu wanafanya kazi kupita kiasi kazi za kufanywa na *nurse* sita kwenye wodi wao wanazifanya kwa *nurse* mmoja. Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo lipo na wizara inalishughulikia kuona kwamba sehemu hizi ambazo zina mapungufu ya wafanyakazi zinapatiwa wafanyakazi wa kutosha. Lakini hata hivyo, kwa *population* ya watu waliopo pale Tumbe na orodha ya wafanyakazi waliopo basi huduma katika kituo cha Tumbe naamini zinatolewa ipasavyo kwa sababu kuna *clinical officer* mmoja, kuna *public health B* mmoja, kuna *public nurse B* mmoja, kuna *Laboratory Technicians* mmoja na *orderly* wawili.

Kwa jinsi ninavyokielewa kituo kile na wafanyakazi hawa waliopo kama wanaingia kazini kama ipasavyo, basi naami kwamba huduma zinaendelea vizuri.

Hata hivyo, wizara itakaa na kuliangali suala hili wanzako wakipatiwa katika vituo vyao na wewe katika kituo chako cha Tumbe *Inshallah* Menyezi Mungu atajaali utapata. Ushauri wako tunaupokea tutafanyia kazi kuhusu kuchunguza mchele unaoingia nchini pamoja na ma- *pampers*. Ulitaka tufanyie kazi ya kufanyia uchunguzi vifaa au vyakula vinavyoingia nchini, hili linafanyika kwa kweli lakini kwa sababu umetushauri basi na sisi tutalifanya kwa ufanisi zaidi.

Baada ya Mhe. Ali Khamis Bakar (Dokholo) naona michango iliyobakia ni ya Mhe. Waziri kwa uwezo wake mkubwa Mwenyezi Mungu aliomjalia na *inshallah* Mwenyezi Mungu atamjaalia amuongeze katika meza hii ili aweze kuifafanua ile michango ya Waheshimiwa wengine walioitoa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: *Bismilah Rahman Rahim*, Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ambapo mwisho kabisa nitatoa hoja.

Kwanza kabisa nachukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa hapa wa afya njema na wazima kabisa.

Pili Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe shukurani zangu za pekee kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu la Wawakilishi wote kwa ujumla wao. Kwa nini natoa hizi shukurani za kipekee, mimi nina uzoefu katika Baraza hili limekuwa katika vipindi viwili tafauti hichi cha tatu, na katika vipindi vyote sikupata kuona Wajumbe wa kutoka Chama kimoja cha CCM jinsi wanavyochangia kwa moyo wao wote kwa ajili ya wananchi wao. (*Makofi*)

Jana bahati nzuri nilipita Maskani moja na Maskani ile imenambia baada ya kilio kile cha Mhe. Jaku Hashim Ayoub kukiona wamenambia sasa CCM inafanyakazi kwa ajili ya wananchi, tunaona wao walikuwa wamekusudia kwamba kazi imekuja mara mbili zaidi. Kwa sababu hapo mwanzo walipokuwa wakituona tuko vyama vingi, bado vipo vingi lakini sio kama pale mwanzo. Lakini sasa wanasema hawa ma- *backbenchers* waliokuwepo kwa kweli wanakufanyeni serikali muwe macho saa zote. Mimi naomba kuwapongeza *backbenchers* wote. (*Makofi*)

Mimi binafsi nimelichukulia hili, kwa sababu wizara hii ni jukumu zito sana hata kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu sisi tuna cheza na roho za watu siku zote na maisha ya watu na wakifa watoto 30 katika *maternity word* waziri anapata ripoti mezani kwani kwake waziri yule anabeba dhamana ya vifo vile ndio maana ya kile kiapo tunachokula na tukashika msahafu mbele ya Rais ndio maana yake hiyo. (*Makofi*)

Nyie kwa kuwa mmeshika msahafu hapa mbele ya Mhe. Spika, tumeapa sote hapa na kila mmoja kwa dini yake ameshika kitabu hapa na nyinyi mnachukuwa dhamana hiyo hiyo na ndio maana Mwenyezi Mungu atatusaidia sote kwa pamoja kuweza kulifanikisha hili tufanikiwe kwa lengo moja kwa nia

moja na kwa dhamira yetu moja ya kuwahudumia wananchi wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jana mimi nilipata tabu sana, kwa sababu kilio kilikuwa miongoni mwa Mwakilishi mmoja humu lakini mimi nilifuta machozi watu karibu 31 kule nje. Kwa sababu wale wote walilia nae Mhe. Jaku Hashim umeliza watu wengi sana. Naomba hilo nilitamke wazi kabisa. Kwa nini, kwa sababu amegusa nyoyo za wananchi moja kwa moja. (*Makofi*)

Mimi kwa hili niko nae moja kwa moja na sichukulii lolote kuwa ni baya. Lakini nachukulia yote hayo ni mazuri mnayojaribu kutusidia sisi Wizara ya Afya katika kufikia malengo kutimiza kwa wananchi na ndio lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ndio lengo la Jemedari wetu Mkuu Mahiri Dkt. Ali Mohamed Shein akisaidiwa na Mhe. Makamu wa Pili Mhe. Balozi Seif Ali Idd na Mawazi na Manaibu Waziri wote waliokuwemo humu pamoja na watendaji wetu wote.

Mhe. Naibu Spika, najaribu kuangali muda na michango ni mingi sana na michango mingine ilikuwa inakuja kwa maandishi na mengine nimepata dakika za mwisho. Lakini nitajitahidi kwa kadiri nitakavyoweza kumgusa kila mmoja inakavyowezekana nitaomba mnivumilie muwe wastahamilivu. Lakini ambapo nitakuwa nimemuacha yeyote yule nitaomba radhi sana asichukulie kwamba tumemuacha kwa kuwa tumedharau au tumemdogosha! Sisi wizara yetu milango iko wazi tunataka kufanya kazi na Wawakilishi wote. (*Makofi*)

Naomba niwashukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Mohammed Aboud ambaye amenisaidia sehemu kubwa katika ile bilioni saba mliokuwa mkiishikilia yeye ameitolea ufafanuzi mzuri kabisa ambayo mimi nitatoa ufafanuzi zaidi kidogo juu ya hilo.

Naomba niwashukuru wale Wawakilishi wote ambao wamekuwa wakituunga mkono katika ziara zetu kwenda Majimboni kwao kuangalia vituo vyao. Mimi kama Waziri wa Afya pamoja na Naibu Waziri wangu ambaye ameeleza majibu mazuri ametoa ufafanuzi mzuri sana hapa leo. Sisi naomba tukuahidini kwamba tutakwenda pamoja bega kwa bega kwenye vituo vyenu vyote kama si mimi Mhe. Naibu Waziri. Tumegundua tukienda kwenye vile vituo tukienda pamoja na nyinyi tunaweza kutatua mambo mengi zaidi kuliko tukienda peke yetu, hilo tumeligundua.

Kwa sababu wale wananchi wamekuchague nyie kwa hiyo mkiwepo nyie pia wanafunguka zaidi na tunakuwa hatuna taarifa mbili tunakuwa na taarifa moja

tu. Hivi mkenda nyie peke yenu mnapa taarifa tofauti na sisi tukienda peke yetu sie tunapata taarifa tofauti. Lakini tukienda pamoja namshukuru sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy tulikwenda pamoja na sote tukapata taarifa hii moja na taarifa ile tumeweza kuitekeleza na Mhe. Nadir, yule mtoto wako mdogo mwenye matatizo ya moyo anakwenda India tayari nimeambiwa leo ameshatiwa kwenye orodha. Huo ndio utakuwa mfumo wetu Mungu akitujaalia huko tunakoelekea kufanya kazi. (*Makofi*)

Mimi Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri nimeshakaa *backbencher* nimekaa katika ile awamu ya kwanza kabisa niliyoingia Barazani nilikuwa katika Kamati ya *PAC*. Nadhani sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa ndie mwenyekiti wakati ule walikuwa Mhe. Abaas Juma Muhunzi ndie Mwenyekiti wetu kutoka Chama cha Upinzani na pia nimeshakuwa katika Kamati ya Katiba na Sheria naelewa nini kukaa nyuma kule na naelewa kuna nini ukikaa mbele.

Sasa wakati nayapokea haya, naomba kwanza kabisa niwatambue wachangiaji wote kwa kuwajata na kama nitakuwa nimemwacha yeyote yule naomba tafadhali anikumbushe, kwa sababu mengine ni mengi ya kimaandishi. Naomba kwanza kabisa nimshukuru sana na kumtambua:-

Mhe. Dkt Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini pamoja na kamati yake nzima ya Ustawi wa Jamii. Mchango wao hawa hii hotuba ya Mwenyezi ya Kamati kwa kweli Mhe. Mwinyihaji Makame ume-*cover everything* kila aliechangia amegusa hotuba yako. Sikupata kuona hotuba mahili kama hii ya kamati ambayo inawasilishwa kwa ajili ya wizara.

Hii kamati baada ile hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa ndani ya Baraza la Wawakilishi hapa ya pili tutakuwa tunaifanyia kazi hii. Waraka huu ni wa kuufanyia kazi mwaka mzima. Naomba nikuahidi Dkt. Mwinyihani Makame Mwadini umetusaidia pamoja na kamati yako nzima, umegusa kile eneo ambalo tuna tatizo, tuna upungufu umetokea katika bajeti, umetokea upande wa fedha kwa wingi zaidi, ili tuweze kutimiza malengo.

Lakini fedha yetu wenyewe ndio hiyo bilioni mia nane bajeti nzima ya serikali bilioni mia nane na kitu, ikigaiwa kwa wizara kila mmoja alikuwa akisimama kwa wizara mwenye kudai maji, barabara katika ule mgao sisi tuliomba mia, lakini tumepata hamsini na sita hizo mnazoziona. Kwa sababu mgao ni wa *cash budget* na kinachopatikana na hiyo kutokana na ule muongozo ambao unapangwa wa kiuchumi kutokana na lile ndilo tunalopangiwa.

Sasa tukishirikiana kwa pamoja kwa umoja wetu hichi hichi kidogo Mwenyezi Mungu atatujaalia kitakuwa na baraka na kitakuwa kingi tutaweza kutimiza malengo mengi sana. Lazima tukubali kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi 5 tu zinazotoa matibabu bila ya malipo duniani wengine wote wanalipa na hali yetu mnaijua ilivyo. Kwa hiyo, tukienda kwa mashirikiano tutafika.

Naomba niwatambue sana katika michango wanaofata:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy,
Mhe. Suleiman Sarahan Said
Mhe. Mohamedraza Hassanal
Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
Mhe. Simai Mohamed Said (Mpaka basi)
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Bahati Khamis Kombo
Mhe. Mihayo Juma N'hunga- Ahsante sana pia kwa mchango wako wa maandishi wa ziada ulioniletea.
Mhe. Dkt. Mhe. Makame Ali Ussi
Mhe. Salma Mussa Bilal
Mhe. Shehe Hamad Mattar
Mhe. Abdalla Maulid Diwani
Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
Mhe. Hassan Khamis Hafidh
Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa)
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo
Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri asiyekuwa na Wizara)
Mhe. Said Soud Said (Maziri asiyekuwa na Wizara)
Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
Mhe. Waziri wa Fedha
Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na
Mhe. Rashid Makame Shamsi

Kama kuna yeyote nimemuawacha basi sio kwa kukusudia bali imetokezea bahati mbaya.

Naomba moja kwa moja nianze sasa kutoa ufafanuzi katika yale maeneo ambayo yameguswa maeneo mbali mbali.

Kwanza kabisa nitaanza na masuala yaliyoguswa moja moja, suala la Hospitali ya Rufaa.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya kuna mkono kule nafikiri kuna mmoja hujamtaja

Waheshimiwa: Wengi!!

Mhe. Naibu Spika: Ah! Kumbe wengi sasa kwa sababu ni wengi haitawezekana nyote sasa hivi kuwataja. Nafikiri Mheshimiwa uwaombe radhi kama ulivyoomba radhi na baadae au walete *list* ya majina wote waliochangia ambao hujawataja ili waweze kuingia kwenye *hansard*. Utawataja hata mwisho wa kutoa hoja yako. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vi-*note* vyao vingine vilifika mwisho na vi-*note* vyengine hata majina havikuwa navyo. Kwa hiyo, inakuwa kidogo shida.

Naomba niwataje baadhi ya ambao ninao vi-*note* vyao.

Mhe. Said Omar Said
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Asha Abdalla Mussa
Mhe. Hamza Hassan Juma - hii nyongeza nimeshakutaja
Mhe. Mohamed Mgaza Jecha - Ahsante sana mchango wako mzuri kweli
Mhe. Mihayo Juma N'hunga
Mhe. Ali Salim Haji
Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al- Wardy

Naomba wale wengine wote niliokuwa sijawataja waniandikie nipate ki-*note* hapa, ili niweze kuwataja hapa kwa ajili ya kuingia kwenye *hansard*. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Kwanza kabisa katika hotuba ya Mhe.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya samahani pia nilikuwa naomba wale watendaji wako waje huku baadae nawaomba kabisa sio sasa hivi wakati wa vifungu.

Mhe. Waziri wa Afya: Katika masuala yote yanayohusiana na Hospitali ya Mnazi Mmoja, naomba nichukuwe yote kwa ujumla niseme hivi kwamba:

Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kweli kuna matatizo ya *X-Ray* kwa sababu ile ilioko sasa hivi ni *Mobile Unit*. Ile *X-Ray* nyengine imekufa kifaa kinachoitwa *fluoroscopy* kifaa cha kitaalamu hicho ndio inayotoa picha na ika-*process* zile picha na picha kutoka upande wa pili. Sio kwamba haipigi picha lakini haiwezi ku- *process* zile picha. kifaa kinagharimu kama milioni thalathini na tano, kwa kuwa tumeona kuna mradi mkubwa wa Kuweit unakuja na pesa zenyewe ndio hizi kidogo tumekaa tumechemsha bongo tumeona hakuna haja ya kuingiza shilingi milioni thalathini na mbili kwenye kifaa hichi, wakati mradi wa Kuweit mkubwa wa Dola milioni arubaini na mbili yaani bilioni thamanini na nne hizo unakuja ambao utajumuisha vifaa vyote *city scan*, *X-Ray* na vifaa vyenginevyo.

Sasa sisi tumeona kwamba tusitumie kitu hichi kwa sababu mradi ule sasa hivi tuko katika *final stage* mawasiliano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na *Kuweit Fund* na *BADEA* pamoja na *Saudi Fund* pamoja na Qatar wote wamo pamoja hao. Kwa kuwa mawasiliano hayo yanaendelea tumeona tusilifanyie hivuo.

Kwa kuwa *pressure* nayo ya wagonjwa imezidi kwa sababu huduma zile tunatoa bila ya malipo na Mhe. Rais pia amesisitiza katika agizo lake basi tutajitahidi sana naomba mtuwachie hilo hiyo *fluoroscopy* na hiyo milioni thalathini na mbili sisi tutatumia mbinu zetu pamoja na wafadhili wetu wa maendeleo tutazitafuta zipatikae, ili ile *X-Ray* kubwa itape kufanya kazi. Hilo naomba kuliweka wazi kabisa. Nnaamini hatutoshindwa sisi kwa milioni thalathini na mbili kwenda mbio tukazipata naamini hivyo na hasa tulikuwa wapiga debe wakubwa katika ile harambee yetu tuliyoifanya ya chama chetu, nadhani mnakumbuka. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwenyekiti wa kamati alizungumza kuhusu bajeti iongozwe ni kweli. Lakini naomba niseme kwamba ile Bima ya Afya wale wote waliochangia masuala ya Bima ya Afya ya Zanzibar ndio itakayokuwa mkombozi wa Bajeti, itakuwa mkombozi wa mnyonge, itakuwa mkombozi kwa hata mwenye uwezo, itakuwa mkombozi wa kuongeza huduma ndani ya hospitali zetu, itakuwa mkombozi wa kutoa huduma iliyokuwa bora zaidi kwa

wananchi.Naomba sana mutuachie tushawasilisha waraka wa kwanza na wa pili serikali juu ya Bima ya Afya. Bado hatujakubaliwa kwa sababu kuna marekebisho yanatakiwa yafanyike kwa faida ya wananchi na faida yenu nyinyi nyote ambao ni Wawakilishi wa wananchi.

Sasa tunaomba sana hivi sasa wataalamu wetu watano wameukalia huo waraka na siyo wa Wizara ya Afya tu, wanatoka pia katika wizara nyengine. Waraka huo Mhe. Rais, ameshatuhimiza anautaka haraka iwezekanavyo kwa sababu ndiyo itakuwa ndiyo mkombozi wa huduma ya afya. Hilo munalolisifu kwamba Al-Rahma leo anapata bilioni mbili, *NHIF* wanafanya hivi kwa sababu wenzetu walianza kabla ya yetu na sisi wakati wetu wa kuanza ndiyo huu. Tunaomba hilo mutuunge mkono Bima ya afya itaanzishwa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Rais katika hotuba yake pale Hoteli ya Bwawani siku ya Mei Mosi siku ya wafanyakazi duniani alilirejea tena suala hilo na suala hilo sisi tunaliendelea mbio. Pengine mwezi ujao sisi tutakuwa tushawasilisha kwenye vikao husika vya serikali ili iweze kuletwa hapa Barazani na ikapitishwa kama sheria maalum, kwa sababu ni mfuko wa afya ambao utakuwa kama hiyo mifuko mengine; Mfuko wa Barabara, mfuko wa masuala mengine yote hayo na huo utakuwa ni Mfuko wa Bima ya Afya ambapo wale wenye kipato ama wenye uwezo na wale wanaochangia kupitia *ZSSF* wataweza kuchangia kwenye mfuko ili kunyanyua pia hali za wale waliokuwa wanyonge wa chini. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ninatumai Mhe. Naibu Spika, atatusaidia sana tutakapofika katika hali hiyo. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wengi mumesema wakati wake bado Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa rufaa. Waingereza wanapenda kuuliza, *If not now then when?* Kama siyo sasa hivi ni lini. Wenzetu Dar-es-Salaam pale Hospitali ya Muhimbili walipoweza kuanzisha ikawa ikajitenga kabisa na Wizara ya Afya, ikawa na Bodi yake, ikawa na *chairman* wake wameweza kujiendesha vizuri zaidi kuliko vile walivyokuwa mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba Hospitali ya Mnazi Mmoja ipo tayari kujitenga kwa sababu zifuatazo:-

Sababu ya kwanza kabisa ikijitenga sasa hivi itaweza kujitegemea wenyewe, tukiisubiri ikuwe mpaka ianze kwenda mbio, hayo hayatotokezea, siku zote tutakuwa tunarudi nyuma, kila siku tutakuwa tunarudi nyuma. Lakini leo tukiiruhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja isimame kwa miguu yake wenyewe,

itaweza kwa sababu ilikuwa inatambaa, sasa hivi itasimama kwa miguu yake na itaweza kwenda mbio.

Lakini la pili, sheria yake inakuja tarehe ishirini na saba, naomba muiunge mkono.Katika sheria hiyo naomba nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu ametusaidia sana. Tulikuwa tumeweka wa serikali watupe, nikisema wa serikali watupe, yaani wafanyakazi wa serikali watupe. Mwanasheria Mkuu akatuuliza si mutakuwa vile vile. Safari hii tumeweka wafanyabiashara wawili ndani yake, tena wafanyabiashara maarufu ambao katika nchi tunataka tuwaingize wawemo katika uongozi wa Bodi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa hivyo, tukianza sasa hivi kufanya Bodi ya Hospitali Mnazi Mmoja. Hospitali hii itaweza kufanya kazi vizuri zaidi, itaweza kusimama kwa miguu yake yenyewe, itaweza kutoa adhabu pale panapokuwa na mapungufu, haya yote yaliyotajwa itaweza kutoa adhabu, itaweza kukopa, itakuwa inakopesheka, itaweza kufunga mkataba wa ubia na hospitali nyengine kubwa kubwa ulimwenguni, itaweza kwenda kufanya *discussion* huko na *MIOT* na *APOLLO* na wengine wote. Kwa sababu hawa wote tuna mikataba nao sisi Wizara ya Afya hivi sasa na tunapeleka wagonjwa wetu huko. Mumezungumza wengi kwamba kwa nini wale madaktari bingwa tusiwalete Zanzibar, hawatoweza kufanyakazi kwa sababu hakuna *facilities* za kufanyia kazi.

Hata ukileta wale madaktari kama vile vipimo na *facilities* huna, huwezi kutoa yale matibabu. Mgonjwa wako lazima itabidi aende India akatibiwe. Kwa sababu India haendi kwa ajili ya matibabu tu, anakwenda kwa ajili ya *the whole range of product*, kuanzia vipimo, kuanzia mashine zile zilizokuwepo. Kila kitu anafanyiwa baadae ndiyo anafanyiwa matibabu. Matibabu yanakuja mwisho. Mwanzo yanaanza na vipimo.

Sasa leo wale *MIOT* tuna mkataba naye, *APOLLO* tuna mkataba naye na mahospitali mbali mbali, kila siku wanakuja mlangoni kwetu kutafuta mikataba na sisi. Mpaka Wizara ya Fedha wakati mwengine wanatuzuia zuia, wanatwambia aah! Musisaini mikataba mingi ina athari yake hii kwa sababu hawa watakuja kupokea wagonjwa wenu halafu wakuleteeni *bill* tu mwisho wa mwezi mutashindwa kulipa.

Lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja tukiipa uhuru wake wake kamili, itaweza kusainiana mikataba na zile hospitali zetu, watakuwa na mfuko wao wa kibiashara. Wale wa kule watakuwa na imani zaidi ya kuleta mashine zao za vipimo Hospitali ya Mnazi Mmoja ili waweze kutoa zile tiba na wale wataalamu, ndipo hapo wataweza kuja. Hawatoweza wale wataalamu kuja bila

ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa huru. Naomba sana wengi mumeipinga ile sheria bila ya hata kuiona. Wengi sana mumeipinga ile sheria hata bila ya kuiona. Ninakuombeni sana sheria ile Mwanasheria Mkuu atawasilisha kama *draft* ya mwanzo ndani ya Baraza, itajadiliwa na sisi tumeshatayarisha maelezo yake ili Hospitali ya Mnazi Mmoja itabadilika itaweza kukopa, itakuwa shirika kama mashirika mengine yanayoweza kujitegemea. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi ninaamini itakapowezeshwa Hospitali ya Mnazi Mmoja itashindana na mashirika kama *ZSTC*, kama *ZECO*, kama *ZAWA* na wengine wote. Maana itakuwa na Bodi yake yenye uamuzi na Mwenyekiti wake. Kwa hivyo, naomba sana.

Lakini la mwisho kabisa kwenye hilo hilo la Hospitali ya Mnazi Mmoja itaweza kufunga mikataba na Vyuo Vikuu mbali mbali, kwa sababu Vyuo Vikuu mbali mbali sasa hivi vinaendesha hospitali zao kama *University Hospital*, inajulikana kama *University Hospital*. Kwa hivyo, tutaweza kufunga mikataba pia na *institutions* nyengine. Wanakuja munaona wapo Wazungu wengi pale sasa hivi Hospitali ya Mnazi Mmoja wanafanya kazi, lakini mukituuliza sisi tunafaidika nao nini, aah! Wao wanakuja kufanya *field* wanatiliwa *marks*, wanarudi nchini kwao wanapata digrii zao. Sisi hatufaidiki moja kwa moja. Wanakuja kufanya *field* tu pale, lakini tukiwa na mikataba na *Universities* zao hata watoto wetu kutoka majimbo mbali mbali watafaidika kuja kusoma pale.

Tunamshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein tayari ameshaanzisha kozi ya digrii ya *medicine* imeshaanza ndani ya *SUZA*. Na ile kama itakuwa inaweza ikapatiwa uhuru wake, itakuwa ni *University Hospitali* ambao *SUZA* watatumia pale kwa ajili ya kuwafundishia wanafunzi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa Zanzibar sasa hivi tumeshaanza, nani alikuwa na ndogo kwamba Zanzibar siku moja ingezalisha daktari wake. Tayari daktari zaidi ya sitini wake wenyewe ambao wamesoma hapa hapa, wamezaliwa hapa hapa hawakwenda popote wameshazalishwa ndani ya Zanzibar yenyewe, tuna madaktari wetu wenyewe. Na tunatarajia baada ya mwaka mmoja au mwaka mmoja na nusu madaktari tisini wengine watazalishwa.

Mhe. Naibu Spika, na hichi chuo chetu cha *SUZA* sasa hivi kinakwenda kwenye programu maalum ili kiweze kuthibitishwa katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa hivyo, kitakuwa ni chuo ambacho kinajulikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na matibabu ama utabibu ama udaktari ikiwa fani mojawapo kuu ndani yake.

Mhe. Naibu Spika, limezungumziwa suala la vitendanishi, maabara. Hilo ni moja kwa moja ni suala la fedha. Kila fedha inapopatikana huwa vinanunuliwa. Imezungumziwa pia suala la dawa zile muhimu. Naomba tuseme katika dawa bado kuna *shortage*. Hivi sasa tunazungumza na wenzetu hawa wahisani wa maendeleo. Naomba nikupeni siri lakini sasa si siri tena, maana tunaizungumza hapa.

Huko ulimwenguni katika Shirika la Afya Duniani, sisi Zanzibar tunasifiwa kwenye malaria, tunasifiwa sana. Kuweza kuja chini ya asilimia mia moja kutoka kwenye asilimia thamanini tulipokuwa na kuja chini ya asilimia moja katika kipindi kifupi. Sisi tunapongezwa sana na tunasifiwa na ni mfano ambao unatumika ulimwenguni kwa upande wa Zanzibar. Pili, upande wa Tiba tunasifiwa, tumeweza kuidhibiti na kuipunguza kwa hali ya juu.Tunasifiwa sana kwenye *HIV/AIDS* kuweza kuipunguza kwa kiasi kikubwa sana.

Lakini pahala pamoja ambapo bado tunatakiwa tufanye kazi kubwa ni katika vifo vya mama na mtoto. Bado hatupo vizuri. Lazima hili tuseme ukweli na hili linatokana na zaidi kufikisha zile huduma za haraka. Hivi sasa kuna mpango maalum tunafanya na *UNFPA* na wametuletea mtaalumu maalum wa kufikisha hizi huduma haraka zaidi na kuwahusisha wakunga wa jadi hatuwadharau. Mimi huwa ninawaita Mpatakuva, Mzalia nyuma na wote wengine. Wale tunataka tufanye kazi nao pamoja na kuwajumuisha katika *system* ili kupunguza vifo vya mama na watoto. Kwa sababu bado akina mama mitaani na vijijini Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, utakuwa shahidi ulikuwepo kwenye kikao umeona kwamba, bado akina mama kwenye Jimbo lako la Chaani wengine wana imani nao wale wakunga wa jadi. Wakunga wa jadi bado wana imani yao na yote kwa sababu wanatoa lugha nzuri, wanawakaribisha vizuri, wanawapokea vizuri, wanawabembeleza. Walitueleza yote yale, tulisoma siku hiyo vizuri sana.

Mhe.Naibu Spika, na ndiyo maana wale wote waliozungumzia habari ya lugha sisi tunaendelea kujitahidi lugha ya manesi wetu iwe nzuri, lugha ya wakunga wetu iendelee kuwa nzuri na kuna kozi maalum ya masuala ya maadili *(work ethics)* ambayo imetolewa hapa Mbweni *College*, hapa Chuo cha Afya Mbweni ambayo inaendelea kusisitiza utoaji wa lugha njema kwa mgonjwa ili lugha njema peke yake ni nusu ya matibabu.Ukimpa mgonjwa lugha njema ni nusu ya matibabu. Kwa hivyo, nalo linaendelea.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pia alieleza kuhusiana na kuvuja kwa paa, maabara, akaeleza pia katika hili suala la kuvuja paa. Kama nilivyosema hapo awali na ma-*documents* yapo, Hospitali ya Mnazi Mmoja

walipokuja kufanya *study* wale wenzetu wa *BADEA*, KUWAIT, Qatar na Saudi Arabia ile jumuiya yao ya pamoja, wote tuliwaambiwa twende Binguni wakasema aah! Sisi haja yetu hii Hospitali ya Mnazi Mmoja na tutaifanyia kazi Hospitali ya Mnazi Mmoja. Walipokuja pale wamefanya tathmini ya kila kitu. Kuanzia mashine, kitanda, paa, Mnazi Mmoja kuifanya ya kisasa mpaka *flow* mpaka vitanda ndani mpaka kila kitu na picha zake zipo nimekuja nazo bahari nzuri.

Mhe. Naibu Spika, walipokuwa wanafanya tathmini ile mpaka jenereta Mhe. Simai Mohammed Said, wameliingiza pia. Jenereta limo katika huo mradi wa KUWAIT na ndiyo la *500 KVA megawatt* ambalo litakuwa linafanya kazi kote. Hofu yetu sisi kwa rai yako tukenda kuchukua sasa hivi jenereta lile la Mtoni na tukaweka pale, tutakuja kushindwa kwenye mafuta. Kwa sababu yale majenereta nayo yanakwenda kwa mafuta na bajeti yetu ndiyo munaiona hii. Lazima tutafute *solution* nzuri ambayo baada ya kupatikana mradi huo fedha zote sasa zitakuwa zinakwenda kwenye kuendesha hospitali na wakati huo Mwenyezi Mungu akitujaalia Hospitali ya Mnazi Mmoja itakuwa huru ina Bodi yake, inakopa, inakopesheka, ina uongozi wake. Kila kitu kinakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia, lilizungumziwa kuhusu posho la wafanyakazi mbali mbali pamoja na wale wafanyakazi waliokuwepo kwenye kambi za kolera. Naomba niseme hivi. Naomba sana tutofautishe, kuna maposho ambayo yamo katika Sheria ya Utumishi, yale ni ya serikali. Yale yanaendelea kulipwa kila tunapopata fedha, lakini posho za hizi kambi ni fursa maalum. Kwa sababu wale wana-*attend* vitu maalum. Sasa tunapokuja kudaiwa halafu tukashitakiwa na wengine wakaja kutushitaki mpaka Barazani, itakuwa kwa kweli hawatutendei haki. Na ile fursa ile inaweza ikafutwa na Waziri husika wa Afya. Ninarudia tena ile fursa ile inaweza ikafutwa. Mpaka sasa hivi katika maposho tushalipa kama milioni mia moja na hamsini, tumeshalipa tayari. Posho hili limeanzia mwezi wa Septemba, Oktoba, Novemba na Disemba. Tunachodaiwa ninafikiri sana ni baina ya Januari, Februari na Machi pamoja na Aprili kidogo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, *WHO* Shirika la Afya Duniani kutuonea huruma kwamba kidogo tuna kasoro na wao wametusaidia milioni thalathini na mbili wanatupa wao. Jamani hamuwafagilii! Milioni thalathini na mbili, maana wapo wenyewe humu ndani ambazo wanatupa wao na tunazitumia hizo kwenye posho.Tukumbe tena mutapojiwa Waheshimiwa Wawakilishi na hawa vijana wetu, wote tunaofanya nao kazi pamoja na wanapata mshahara wao wa kawaida ni wafanyakazi wa Wizara ya Afya, munapojiwa kwa ajili ya posho ya hii kambi, tukumbuke kwamba ni fursa, sisi tumeshatoa ahadi na sisi ni

waungwana na Serikali ya CCM ni waungwana, tutaendelea kuitimiza hiyo ahadi. Na watatimiziwa ahadi zao mpaka wakamilishiwe lakini ni fursa. Naomba nirudie tena hilo ni fursa, siyo kama maposho mengine yaliyokuwa kwenye Sheria ya Utumishi. (*Makofi*)

Mhe.Naibu Spika, limekuja suala la Hospitali ya Kidongo Chekundu.Suala hili ni kubwa na yeyote mimi ninakubaliana na nyinyi *hundred percent*, yeyote kati yetu anaweza kwenda pale. Pale wameshakwenda watu mabingwa duniani. Mukenda kutembelea leo pale kuna mmoja ya wagonjwa na atakuwa ananisikiliza sasa hivi kwa sababu yeye anaangalia *TV*, kila siku ananiambia Mheshimiwa, nimekuona siku fulani unazungumza kitu fulani. Yeye ni msomi wa hali ya juu ana digrii mpaka ya *Master* yupo pale, anazungumza Kiingereza kizuri sana. Kila siku anatoka nje kwenda kutafuta gazeti na taarifa za habari kusikiliza. Mimi siku niliyokwenda pale ziara kaniambia Mheshimiwa, nimekuona siku fulani unazungumza kitu fulani kwa lugha ya Kiingereza tena *very good commanding language of English*. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema naomba hili suala la Hospitali ya Kidongo Chekundu, kwa sababu kuna mradi mkubwa. Huu mradi wa *BADEA*, KUWAIT, Saud Arabia pamoja na Qatar jumla yake yote ni Dola milioni arobaini na mbili. Kwa mahesabu ya haraka haraka Dola milioni arobaini na mbili ni kubwa kuliko bajeti yetu nzima ya Wizara ya Afya, kweli si kweli?

Bajeti yetu nzima munaiona kwenye kitabu hapa. Bajeti hii si ya Hospitali ya Mnazi Mmoja tu, inahusisha hospitali zote tatu, kwa sababu hizi zote katika fungu moja la Hospitali Mnazi Mmoja. Yaani Hospitali ya Mwembeladu pamoja na Hospitali ya *Mental*. Na kwa taarifa yenu kama mutataka ramani zipo nitakuonesheni, tutazizungusha. Hospitali ya Kidongo Chekundu yaani ile Hospitali ya *mental* inajengwa *mental wing* na lile eneo lote jengine litatumika kwa kujenga *facilities* nyengine mbali mbali pale. Itakuwa ni hospitali ya kisasa. Vichwa sisi vinatuuma sasa hivi vinakwenda mbio ili vijana wetu wasome kwa wingi waweze kujaza zile nafasi. Kwa sababu tutakuwa na *shortage* kubwa sana ya nafasi wakati mradi huu ukishamalizika. Watatakiwa watoto wetu zaidi ya mia ambao watakaofanya kazi pale. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na halikadhalika kwa Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba. Nadhani waliokwenda watakuwa wameiona. Mimi nilikuwepo kule wiki iliyopita, bahati nzuri nilikwenda pale na tumeitembelea. Hospitali ya Abdalla Mzee itahitaji wafanyakazi si chini ya mia tatu. Pale pana *theatres* nne. Kwa hivyo, sisi sasa hivi tunakwenda mbio kuhakikisha kwamba vijana wetu wanamaliza kwa wakati, hao niliowataja, kuna masuala mengine yameandikwa

kwa maandishi wanaotoka China, India wapo *very well qualified*. Sasa hivi mtu akija tu na *medical degree* hakai anapata kazi hapo hapo. Miongoni mwa kwa kada tunamshukuru sana Mhe. Rais, pia, miongoni mwa kada ambayo anatupa sisi *priority* ya juu kabisa ni kada ya afya. Kada ya daktari akitua tu Mhe. Suleiman, akitua tu hapo hapo anakwenda kwenye Utumishi, anakwenda kwenye ule mlolongo wa *GSO* kuchunguzwa anapewa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na ninamshukuru sana hapa Mhe. Rais, naweza kusema leo ni kwa ufahari kabisa, kila siku sisi tukikutana na Mhe. Rais, kuzungumzia wizara hii basi wizara hii ipo ndani ya moyo wake. Kwa sababu yeye mwenyewe ametokea kwenye wizara hii hii. Naomba sana mutuamini sisi tuliokuwemo humu lakini mumuamini Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein wizara hii haikuiacha nyuma hata kidogo.

Kwa hivyo, katika mradi huo wa Hospitali ya Kidongo Chekundu ile *mental wing* huenda mradi unazungumzia patabomolewa mote, kwa sababu pale pashaanza kuzama, maji ya mvua yakija yanaingia kwa wanaotokea kwenye majimbo hayo watakuwa wanajua, maji ya mvua yanaingia mpaka hivi *level* ya magoti yanafika. Kwa sababu yale majumba yameshakuwa yapo chini na eneo lile ni la maji maji kidogo. Kwa hivyo, kila baada ya muda, tunaamini sana mradi huu utajenga majengo yote yale ku-*repair* na kadhalika. Homa yetu wale wagonjwa tutawapeleka wapi kwa muda wakati ile *repair* inafanyika halafu tuweze kuwarudisha. Hayo ndiyo tunayofikiria na kuyapanga hivi sasa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia, lilizungumziwa suala la maji yanayotiririka. Hayo tunaendelea ni masuala endelevu. *Bill* ya umeme. Hilo tunaendelea kulipa na ninashukuru serikali inatusaidia pale tulipokuwa tumekwama, kama madeni yanakuwa nyuma tunaendelea kulipa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu magari. Magari tunayo ya kutosha. Magari naomba nitamke kwamba tunayo ya kutosha, hatuna kasoro ya magari. Tunatakiwa kuyatumia vizuri, lakini hatuyatumii vizuri na hatuyapangilii vizuri. Na sasa hivi tumeshaanzisha utaratibu maalum na kuna Kamati maalum imeandaliwa ya kusimamia matumizi ya magari. Sisi tuna magari zaidi ya 180, ndio. Zaidi ya 180 katika *asset register* ya magari. Lakini utakuta hili liko huku na hili liko kule, lile bovu limepelekwa kwa fundi halijafuatiliwa. Hayo sasa hivi ndio mambo ambayo naomba mtupe nafasi. Toka nichaguliwe mimi miezi mitatu haijafika, imefika miezi mitatu tayari? Maana nimepokea mishahara miwili tu, kwa hivyo, najua. Miezi mitatu haijafika, basi mtupe muda zaidi haya ni

mambo ambayo tumeingia, tumeanza kuyaona na tunayafuatilia, yale magari tunataka sasa hivi yatumike vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kwa magari zaidi 180 ni mengi sana kwa Wizara ya Afya. Naogopa tukisema kwamba tunataka Mhe. Mwenyekiti wa kamati hii, kama ulivyoeleza kwenye hotuba yako, tunaogopa sasa hivi tukisema tunataka magari zaidi, tutashindwa kwenye pesa za mafuta, kwa sababu magari hayaendei kwa maji, yanakwenda kwa mafuta. Kwa hivyo, tukiomba *asset* zaidi basi kuna *running cost*, kuna *operational cost* tutakuja kuumia.

Kwa hivyo, tunataka haya magari yetu sasa hivi tuyatumie vizuri zaidi na tuyapangilie vizuri zaidi na tuwe na usimamizi maalum. *Weakness* yetu naikubali mbele yenu, *weakness* yetu kubwa ni usimamizi, ndio maana mnaona sasa hivi tunaweka wasimamizi kila sehemu kuna usimamizi. Kule wenzetu Bara mmesifu wanafanikiwa kwa sababu kuna usimamizi mahiri, sisi tunaoneana muhali, sasa huu muhali tunataka tuuweke pembeni na tuweke usimamizi mbele.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea pia lilizungumziwa suala la pale *mental* kuhusu suala la ukosefu wa ulinzi, ukuta umetobolewa. Yote hayo tunayafahamu, na tumo katika kuyafuatilia. Lakini narudia tena ule ukarabati mkuu utakaokuja, basi utarekebisha masuala yote hayo. *Fumigation* inaendelea kufanyika. Unajua Mhe. Naibu Spika, kila tunapopeleka vifaa pia napo tunaathirika kwa sababu wengine ni *aggressive*, yale magodoro wanapoyachana inakua ni sehemu ya maradhi yao. Kwa hivyo, hayo tunaendelea nayo tunawashukuru wale wafadhili wote wanaotufadhili kwenye chakula, sitaki kuwataja wengine wamo humu ndani wanatufadhili kwenye chakula, kuna ndugu yetu, ndugu Bopar ambaye anatufadhili kila mwezi pale kwa chakula cha mchele tunamshukuru, na sisi bajeti yetu kila inapopatikana tunapeleka chakula pale na tunaendelea kwa wagonjwa wale kuwapatia vyakula. Wanapatiwa vyakula mara mbili kwa siku, hivi sasa ni mara mbili kwa siku.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu gari za dawa, nimeshaeleza. Kuhusu *ICU* kukosa dawa za *emergency*. Suala hili hutokezea *shortage* kwa muda tu, lakini pale madawa yale muhimu yote huwa tunahakikisha yanakuwepo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu hospitali binafsi. Nashukuru na wao wenyewe wapo hapo juu sasa hivi wanatusikiliza. Nadhani mtakua mmeona katika kipindi cha hivi karibuni, hatutaki kutangaza, lakini kila tutakapotumbua majibu na sisi sasa hivi tutakuwa tunatangaza, tutafanya hivyo sasa. *(Makofi)*

Tumeshazifungia hospitali zaidi ya nane, nadhani hilo mnalijua mmeona kwenye *TV* na sassa hivi tutakwenda kwenye *pharmacy*, tutawatuma wajumbe wetu. Tena wenye *pharmacy* madamu wananisikiliza basi wanisikilize vizuri kwa kupitia chombo hiki. Kwenye *pharmacy* tutawatuma wajumbe wetu. Kuna *drugs* ambazo zinaitwa *over the counter drugs* unapewa bila, *prescription*, lakini kuna *drugs* ambazo ziko *clearly defined*, hutakiwi kupewa bila ya cheti, yaani bila ya *prescription*, Tutawatuma wajumbe wetu waende wakanunuwe hizo *drugs*, wakipatiwa bila ya *prescription*, basi *pharmacy* ile tutaifunga.Kwa hivyo, jitayarisheni, wenye *pharmacy* wajitayarishe wasitowe vidonge hivyo bila ya *prescription*, kwa sababu zimegaiwa kisheria hizi. Nikisema *prescription*, nakusudia cheti cha daktari na cheti cha daktari dhamana, usije ukamtafuta mtu mtaani akakuandikia cheti ukenda kununua dawa utakuwa unafanya kosa jengine. Kwa hivyo, hilo nalo tunakwenda nalo ni hatua hii ambayo tunaifanyia kazi hivi sasa.

Kuhusu suala la Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba itakapofunguliwa.Suala hili nimeshalitolea maelezo kwamba sasa hivi tuko katika kukusanya *database* na *scheme of service* tunaifanya ya wafanyakazi kwa ajili kujiunga moja kwa moja itakapoanza Hospitali ya Abdalla Mzee.

Mhe.Naibu Spika, kuhusu filamu za *X-Ray* nimeshalitolea maelezo. Kambi za Kipindupindu tayari nimeshazisema. Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende kidogo kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Jaku Hashim, naomba nikuhakikishie kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein amekusikiliza vizuri sana, naomba nikuhakikishie hilo. Pia, naomba nikuhakikishie kwamba Dkt. Ali Mohammed Shein ni sehemu ya hili Baraza la Wawakilishi na anafuatilia sana tunayozungumza hapa ndani. Alikusikiliza yote, amekuelewa yote na sisi atatupa maagizo.Lakini ninachotaka kusema ni lazima tumpongeze kwa kununua ile meli kwa sababu ilikuwa inahitajika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mgonjwa mnyonge akitokea Pemba anataka kuja *referral* atakuja vipi leo bila ya kutegemea usafiri wa nchi na meli ni usafiri wa nchi. Kwa hivyo, ilikuwa wakati ule imepelekwa pesa kwenye meli na safari hii Mwenyezi Mungu akitujaalia tutapata pesa tutapeleka kwenye *X-Ray* na mambo mengine yote, na kwa kuwa nipo mimi nitaendelea kushirikiana na nyinyi ili kufikisha hizo huduma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu masuala ya chanjo, pale palipokua na mapungufu kwenye masuala ya chanjo. Jana mimi niliwaalika wale *development partners* kwa makusudi mazima ili waelewe matatizo yetu na wapate kuwasikia nyinyi mnazungumza nini. Wengine walikuja na wakalimani wao pale, ili wapate

kujua moja kwa moja matatizo ya jimboni na mimi nilifanya kwa makusudi kuwaalika. Maana tumeshazowea wale huwa tunawaalika wakati wa kuzindua Baraza na siku ya mwisho. Lakini sisi tunawaalika kwa sababu tumetaka wayapate yanayotoka kwa wananchi moja kwa moja, ili mimi ninapokwenda kupitisha bakuli langu kwao kwenda kuomba msaada, iwe rahisi kutusaidia na wao wameshakubali watatusaidia kwenye maeneo mbali mbali, hususan kwenye mama na mtoto wanatusaidia kwa sehemu kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu cha bajeti mtaona bilioni 20 zinatokea kwao moja kwa moja na zile bilioni 20 za kwao ziko tayari wao wanazo mkononi ni *cach budget*, kwa hivyo, wanazo tayari, sisi mpaka tuzitafute...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, nakuomba kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, tunaona kwamba muda wa kumaliza unakaribia na bado Mhe. Waziri, anafanya majumuisho na vile vile, nia yetu leo kumalizana na wizara hii. Kwa hivyo, basi nimuombe Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kutengua kanuni ili tuweze kuendelea na shughuli yetu hii. Mhe. Waziri, karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli zetu za leo, na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Afya, yumo katika kufanya majumuisho na pia kwa kuwa tunahitaji muda wa kukaa kama kamati, hivyo niliombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando, ili tuweze kumaliza shughuli zetu kama zilivyopangwa kwa leo. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa. Wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. Mhe. Waziri karibu, lakini ningekuomba sana tujaribu kuangalia wakati.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, haya ni mengi kweli kweli, lakini nitajitahidi kwenda kwa *speed* na mengine sitoyataja, kwa sababu najua buti nitapigiwa *anywhere*, kwa hivyo, bora niyajibu wakati wa buti. Kwa hivyo, nitakwenda haraka haraka, na nitamkwepa zaidi Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Simai Mohammed Said, kwa sababu wapate kupiga buti zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa kuchangia dawa jimboni kwake. Kuhusu banda la kupumzikia nje wagonjwa pale Mnazi Mmoja, kama mtapita sasa hivi mtaona kidogo kuna mabadiliko kuna ma-*benches* pale kama matano yanatengenezwa, *garden* ile sasa hivi

imeshakatwa majani na mambo yanakuja kidogo kidogo. Sasa hivi tumeamua tutafanya wenyewe, kwa sababu nyinyi mnapiga makelele humu ndani, lakini hamtoi chochote, baada ya hapa tukiondoka hapa pangupakavu hakuna chochote kinachotolewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kasema tuambieni kama tayari. Mimi nimeshamuambia mara chungu nzima njoo tukae ofisini pamoja, tuambie wewe unaweza kufanya nini hapa na bado narudia kauli hiyo, njoo tukae Mhe. Jaku Hashim, kama unataka bado muda upo, sijajenga banda bado. Bado muda upo njoo niko mimi, tena wewe *size* yangu mimi,usije ukalia tu kule wizarani. Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba tumeanza hatua ya kuweka sawa, pale watu wanakaa vizuri, tumeanza kujenga ma-*benches*, na wiki ijayo tunatarajia kupata pesa kidogo ambapo tutaanza kuwekeza, kuna hodhi pale la maji tumeshachimba, tunataka kuanza na vyoo, kwa sababu wale wanaokuja pale wanapata tabu sana, wengi wanatokea mashamba, wanapata tabu sana ya vyoo. Wakati mwengine baraza yetu ya Wizara ya Afya nzima inakua inajaa usiku watu wanaokuja kuwauguza wagonjwa wanalala pale. Kwa hivyo, hilo naomba muondowe hofu.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, kwa haraka haraka sasa hivi. Namshukuru sana, mashine ya *DNA* tumeanza *process* ya kufuatilia, yale yaliyotajwa tajwa juzi yaliyokuwepo melini kama ile meli imezama au imekuja, yale sitaki kuingia kwenye msingi ule. Lakini naomba mtuachie tumeingia juzi, naomba mtupe muda tufuatilie halafu tuje kuwasilisha na tunakwenda sambamba na Mhe. Mwanasheria Mkuu, anatuongoza katika hili. Kwa sababu jambo hili kumbukeni jambo hili ni la kisheria, lina mambo ya kisheria sheria. Wenzetu Bara kule walichokoza chokoza kule, basi mambo chungu nzima yameibuka, nadhani mnajua. Maana wengine watoto wamekuja kuwa.... Haya. Naomba niendelee. *(Makofi)*

Kwa hivyo, suala hili tunaendelea nalo, tunapokea mawazo yako Mhe. Nadir Abdul-latif, yote ya kongamano ya kwenye *TV* ya kukaa na madaktari na kadhalika yote tunaendelea nayo. Kuhusu *generator* nimeshalitolea ufafanuzi. Hospitali ya Kidongo Chekundu tayari nimeshalizungumza. Kuhusu hospitali zako za Chaani, japo kituo kimoja kianze. Kituo hiki tulikwenda pamoja kwenye ziara tumezungumza na hivi sasa tunazungumza na wafadhili jinsi ya kubadilishana, tukitowe kituo chengine tukitie cha kwako na cha kwako tukiweke kwenye ufadhili utakaokuja kuwa baadae, kwa sababu tunajua kuna tatizo kubwa kwako wewe na lile tatizo tumeliona na tatizo la mchwa nililishughulikia mimi mwenyewe kabla ya wewe kuchaguliwa katika jimbo lile nikiwa mimi ni Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Spika, yako mengine mengi nitakuja kuyataja baadae ambayo wameyaleta kwenye ki-*note*. Mhe. Suleiman Sarahan Said, kuhusu maji safi, kwa Bara wanaita maji taka au maji machafu. Kuna programu maalum ambayo tunashughulika sasa hivi na *UNICEF*, tunawashukuru sana na *WHO*, hiyo programu inaitwa *WASH*, yaani *(Water and Sanitation Hygiene Program*), ambayo tunashughulika nayo, tutakwenda mpaka kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwenye skuli, na tutakwenda kwa Mhe. Haji Omar Kheir, kwenye Tawala za Mikoa, inakwenda kila pahala.

Kipindupindu sababu yake kuu kabisa sio Wizara ya Afya, watu wengi wanasema ni Wizara ya Afya, ni kule kwenye maji machafu ndiko kilipoanzia hapo, yaani maji ya kunywa kuchanganyika na maji ya kinyesi, sikutaka kutaja lile jina jengine. Kwa hivyo, hilo tunalishughulikia kwa programu hiyo, naomba mtupe muda tu, tunaendelea na programu hiyo, mtaona watu wamevaa vikoti vya *blue* wanakuja majimboni kwenu kuzunguka kwa ajili ya kuliangalia hilo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kuweka *TV* hospitali. Kuna baadhi ya maeneo sisi huwa tunaruhusu kuweka *TV* katika hospitali, lakini kuna baadhi ya maeneo huwa haturuhusu. Kama kule *mental hospital* tumeweka *TV*. Tena nikuambieni siri wanafurahi kweli kweli wenyewe na hivi karibuni...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, nakupa dakika 15 umalizie.

Mhe. Waziri wa Afya: Dakika ngapi?

Mhe. Naibu Spika: Dakika 15.

Mhe. Waziri wa Afya: Hii! Haya. Habari ya *mental* nakwepa sasa, maana kulikuwa kuna *story* nzuri sana nilitaka kuielezea, lakini nakwepa hapa. Nakwenda moja kwa moja kuhusiana na mahitaji ya daktari bingwa wa maradhi mbali mbali kama vile sukari, *cancer*. Daktari wa *cancer* tunaye mmoja, wa sukari tunaye, lakini tutaendelea kuzungumza na wenzetu ndugu zetu wa China. Juzi alipokuja yule *Governor* aliahidi mambo mengi sana, alifanya mazungumzo na Mhe. Rais. Kitu kimoja mimi nilichogundua Mchina akiahidi jambo bwana harudi nyuma, maisha, anatimiza ahadi yake. Toka mwaka 1964 madaktari wake wanakuja Zanzibar mpaka leo hawajakosa hata mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mhe. Saada Ramadhan na yeye alichangia kwa maandishi, namshukuru sana. Kuhusiana na kituo cha Chumbuni, wenyewe wapo Chumbuni wapo, eee!

Nasemaje Kituo cha Chumbuni leo kinatufaa taifa zima, kile ni kituo cha afya kilichokuwa chini ya Wizara ya Afya. Naomba tuwashukuru sana kwa kujenga ukuta, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, Mhe. Mbunge wa Jimbo la Chumbuni mmejenga ukuta mzuri sana. Kituo kile kimetuokoa sisi kweli kweli, ni lazima niwaambieni ukweli, ile ndio iliyokua kambi kuu ya Kipindupindu kwa Zanzibar nzima. Safari hii sisi tumepata takriban wagonjwa 5,000, haijawahi kutokezea katika historia ya Zanzibar, wote waliougua Kipindupindu, na kituo kile kilituokoa kwa sababu kilibeba wagonjwa wengi sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme hivi pale hajaambukizwa mtu, hizi ni stori tu kwamba mgonjwa katoka ana harisha huku ana tapika, kamuona mwenzake kafa kitandani jirani, yeye akanyanyuka. Kwanza mgonjwa wa Kipindupindu kunyanyuka kitandani hawezi, *guarantee* nakuambieni, madaktari wale pale juu mtawauliza. Ile miguu yake inakuwa haishiki *potassium* na zile *components* za *sodium* zinakuwa zimeondoka kwa sababu *dehydrated* amekosa maji, hawezi kunyanyuka. Kwa hivyo, zile ni stori tu kwamba mgonjwa kanyanyuka ndani katembea mwenyewe, kenda kuwaambukiza watu mitaani, hapana, sio kweli. Pale pana utaratibu maalum, kwa sababu kile kituo kimekaa vizuri na kimezungukwa kidogo pako wazi, kuna utaratibu maalum wa ku-*dispose* kile wanachotapika au wanachokitowa, kinatiwa *chlorine* kuna njia maalum ya ku-*dispose*.

Kwa hivyo, nawaombeni sana muendelee kutumia kituo cha Saateni hakiko mbali, kuna kituo chengine jirani jina limenitoka kidogo, kiko upande wa Magogoni kuna kituo pale, sio Kihinani, Kinuni. Limenitoka jina kidogo, lakini kuna kituo ambacho tulifungua nyumba ya daktari hivi karibuni katika Sherehe za Mapinduzi Zanzibar, tulifungua nyumba ya daktari. Kwa hivyo, tunaomba mtumie vituo vile sisi tutawaongezeni *facilities* pale nzuri zaidi, tutaongeza dawa pale ili wananchi wako waendelee kutumia kituo kile mpaka tumalize suala la Kipindupindu, tukimaliza tutarudi tena, maana Kipindupindu ndipo kinapoanzia kule, wananchi wako ama wananchi wetu wakiendelea kutumia maji machafu, basi kambi yetu ndio ile ile hatuna pengine. Kwa sababu ile kambi mpaka Umoja wa Mataifa wenyewe wameikubali kwamba ni kambi iliyokaa vizuri sana kwa ajili ya Kipindupindu. *(Makofi)*

Ndio maana tulifunga yale mahema, naomba mtukubalie sana hili. Kama Mhe. Hamza Hassan, alivyotukubalia kwake tukatumia katika huduma ya macho mara hii na kule mtukubalie, ile ndio kambi pekee. Sisi wenyewe tumewapeleka Tunguu, tumekwenda nao Binguni na tumekwenda sehemu mbali mbali, tumekwenda nao mpaka kwenye kiwanja chetu sisi wenyewe

Binguni, hiyo tunataka kujenga hospitali ya rufaa wakasema hapana, hapa hapafai, tunataka hapa hapa Chumbuni, na wao ni Umoja wa Mataifa wana uzoefu mkubwa kuliko sisi, Mwenyezi Mungu atuepushe mbali sisi hatujawahi kupata Ebola, wao mpaka Ebola, hawa waliokuja hapa Ebola wameshawahi kuidhibiti huko wanakotokea. Kwa hivyo, tunaomba sana hili mtukubalie. *(Makofi)*

Mhe. Mohammedraza Hassanali, sisi ndio kwanza tumeingia katika wizara hii, imezungumzwa kulikuwa kuna siasa za nyuma kuhusiana na kituo cha Umbuji. Mimi nitaitisha hili *file* la Umbuji, ni jambo jipya kwangu mimi, nitalichukua nakuahidi nitakwenda na wewe mguu kwa mguu na tutamualika na rafiki yetu Mhe. Abdalla Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Wananchi Jang'ombe, tutakwenda pamoja pale tufanye ziara rasmi, tupige kidogo mambo pale ili kile kituo tukishughulikie.

Mhe. Naibu Spika, tuna wafadhili wawili wakuu sasa hivi, tuna *Orio* ambapo vituo takribani 19 na tuna Milele ambao tunaendelea nao, tunawashukuru sana ndugu zetu wa Milele kwa kutupa *support* yao. *(Makofi)*

Mhe.Naibu Spika, Mhe. Tatu Mohamed Ussi, alizungumza kubwa kabisa kwamba wafanyakazi tukiwapeleka masomoni, basi tusiwapeleke kwa mkururu, tupange. Tunalipokea na tunalichukua. Ni kweli kuna idara nyengine Wakurugenzi wao wako hapa wanasikia walipeleka kwa mkururu wakajisahau. Kila anayekuja kumuomba, akija kwa Mkurugenzi. Mkurugenzi na mie, akizungumza kwa sauti hiyo tu kidogo, basi Mkurugenzi ana-*sign* mtu anakwenda kusoma. Mkurugenzi kujishtukizia anaona wafanyakazi 25 kati ya wafanyakazi 28 wameondoka kwenda kusoma wamebakia watatu. Sasa tumeshawaambia Wakurugenzi wetu wote wa-*review* programu yao ya kusoma wasiruhusu wafanyakazi kutoka mpaka wananchi wakawa wanapata taathira au wanapata athari katika kupata huduma za afya.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu bohari ya madawa. Suala hili nimeshalieleza Mhe. Naibu Waziri wa Afya, pia alilitolea ufafanuzi mzuri tu kabisa. Kuhusu kuchukua wafanyakazi waliokuwa wanatoka vijijini kule. Tumeianza programu hii Kijini, Mwakilishi wa Kijini yupo, Naibu Waziri, Matemwe, tumeanza programu hii imefanyakazi nzuri sana, tumeanza programu hii Kiongwe nimekwenda kuangalia mimi mwenyewe, Kiongwe Bumbwini kule, unakwenda mwisho kabisa Bumbwini, inakwenda vizuri sana kwa sababu wale watoto wa pale wanakaa majumbani kwao na kadhalika. Sehemu nyengine tumeambiwa kina baba wawaowe wale watoto wanaokwenda pale, wawe wanawaowa ili wawe wanabakia kule kule. Lakini katika programu mbili

zilizofanyakazi vizuri sana ni hizi. Kwa hivyo, na sisi tutaendelea na programu hii ya kuwashajihisha watoto wanaotoka vijijini, kuwapeleka kwa kupitia Chuo chetu cha Afya na baadae kuwarudisha kule kule wanakotokea.

Mhe. Naibu Spika, tunawashukuru sana ndugu zetu wa *UNFPA* wanatupa fedha za kuwa-*sponsor* kwa ajili ya programu hiyo, kwa hivyo, programu hiyo tunaichukua na tunaendelea nanyo.

Mhe. Naibu Spika, michango iko mingi sana sidhani kama nitaimaliza, lakini naomba kwenda kwenye Hospitali ya Rufaa ya Binguni, naomba kumjibu Mhe.Simai Mohammed Said, hili lipo ramani unayo hapo nimekuonyesha tunaendelea kujadiliana linajadiliwa katika ngazi ya Serikali na limo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ni ahadi aliyoitoa Dkt. Ali Mohammde Shein mwenyewe na yeye ni muungwana katika miaka iliyopita yote mitano ametimiza ahadi zake zote katika sekta ya afya. Na ninaamini katika miaka mitano yake hii ijayo atatimiza ahadi zake zote na mimi hapa nilishasema kwamba sisi tunamuahidi tutakuwa nae bega kwa bega tutakwenda mbio mpaka na hili nalo tulitimize.

Kwa upande wa uboreshaji wa huduma za Afya katika Mkoa wa Kusini, hili ni zoezi ambalo linaendelea upande wa Makunduchi pamoja na huduma mbali mbali za mama na mtoto wa *RCH*.

Mhe. Simai, pia aliuliza idadi ya wagonjwa waliopelekwa nje nchini India wagonjwa hao waliosafirishwa... Mwaka jana tulipeleka wagonjwa takriban 380, bili yetu tunayodaiwa pale ni kama bilioni 1.2 zimebakia, lakini tunamshukuru sana Dkt. Khalid na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ndugu Khamis Mussa na watendaji wao wote kila wanapopata fedha wanatutilia tunawalipa India, Dkt. Khalid watu wa India wamefurahi sana na wewe na wanaendelea kukupongeza pamoja na watendaji wako wote tunaendelea kuwalipa, pamoja na uongozi uliopita waliokuwa wakitusaidia tunaendelea kulipa zile bili zetu.

Sasa hivi tumepunguza sana kupeleka wagonjwa India kwa sababu huduma nyingi zinatolewa hapa hapa tunaweza kutoa sisi wenyewe, na kama hazitolewi hapo basi tunampeleka Dar-es-Salaam, tunampeleka mtu India ambaye yuko *very very critical* na lile tatizo halipatikani tiba yake hapa Zanzibar.

Kuhusiana na Benki ya damu, suala la ukusanyaji wa damu linaendelea isipokuwa ile gari iliyopata ajali linatengenezeka na gharama ya utengenezaji mpaka sasa hivi tuliyopewa sisi ni milioni 23, hili tutalifuatilia zaidi pengine

tukienda sisi wenyewe tukashuka chini zaidi tunaweza kidogo tukapata kwa unafuu, kwa sasa lipo Gereji ya ndugu yetu Alhaj Juma Buda liko kwenye gereji yake kwa ajili ya matengenezo na tunatafuta hizo fedha na tumemwambia na yeye atupe *discount* yake ya kuchangia katika Wizara ya afya.

Mhe. Ali Sulaiman Ali, aliuliza suala la Hospitali ya Wete kutoa ubaguzi limeshajibiwa na Mhe. Naibu Waziri.

Suala la kufungia hospitali za binafsi tumeshazifungia. Naomba nitoe maelezo kidogo tu kwa ufupi kuhusu bodi zetu za afya, muhimu sana Waheshimiwa Wawakilishi mkiwa na malalamiko nyie wenyewe au wananchi wenu kuna bodi ya madaktari, kama lile lalamiko linahusiana na daktari wao ndio wenye *mandate* ya kisheria ya kupokea malalamiko dhidi ya daktari, yaani linaitwa Baraza la Madaktari. Ukiwa na malalamiko dhidi ya wauguzi kuna baraza la Wauguzi wenyewe wapo hapa *Prof.* Amina Abdulkadir ndio mwenyekiti na wana ofisi yao pale pale pembeni ya Wizara ya Afya unafikisha malalamiko yako pale, wao ndio wenye *mandate* ya kisheria ya kutumbua majipu, hili naomba nilitamke na liwe wazi ili wote wawe wanalifahamu.

Mhe. Naibu Spika, sasa kwa kumalizia, yako mengi kweli kweli, lakini kwa kumalizia naomba yote yote yako mengi yaliyobakia yote tunayapokea, naomba Mhe. Naibu Spika, tuwakaribishe Wawakilishi waje ofisini kwetu wasitusubiri tunapokuja humu ndani ndio wakaleta mengine mapya hatukuwahi kuyaona. Mengine hatujawahi kuyapitia ma-*files* yote, mimi na Naibu Waziri, tumechaguliwa tarehe moja sote tarehe 9 mwezi wa *April*, hatukuwahi kuyapitia yote na Wizara hii ni kubwa, naomba waje ofisini kwetu tushirikiane nao Waheshimiwa Wawakilishi, tutawapa mashirikiano ya kutosha. Wale wote haya yote mengine sikuwahi kuyajibu kutokana na muda, wale wote ambao sikuwajibu kwa njia moja au nyengine si kwa makusudi, lakini *inshaalla* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutawajibu kwa maandishi wote, watendaji wapo tutayakabidhi haya maandishi.

Lakini pili kuna ya utendaji humu ndani tunaahidi mimi na Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wetu wote Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mshauri wetu pamoja na watendaji wa Wizara nzima ya Afya tutakwenda nao sambamba kwenda kuyatekeleza, Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache niliyoyasema na mengi kuyabakisha ni dhamira yangu na madhumuni kwamba Waheshimiwa Wawakilihi, watanikubalia ombi langu hili nililowaomba na naomba kutoa hoja sasa ya kukubaliwa hivyo vifungu na Baraza lako likae

kama kamati ili kujadili bajeti yetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Afya, ameshatoa hoja, wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na ndugu wajumbe wote, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara yetu ya Afya kwa mwaka 2016/2017, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya Matumizi ya Wizara yangu. Naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU H O1 - WIZARA YA AFYA

Kifungu H 0101 Afisi Kuu

Mhe. Naibu Spika: Hatujafika kwenye kifungu, tunakwenda kwenye vifungu vidogo, hatujafika huko bado.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, siko huko naomba ungenisikiliza, sihoji huko mie nahusu Makadirio na Katiba na Kanuni zinaturuhusu za Baraza, nahoji ama nikusomee kifungu cha 98 Mhe. Mwenyekiti, Makatibu wanaweza kukusaidia pengine nakusikiliza uamuzi wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Spika: Una hoja wapi kwenye hichi tunachokipitisha?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nina hoja hapo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Eee!

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nina hoja hapo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Hoja ipi hiyo?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Eheee! Mheshimiwa, hapa kwa kuwasaidia Wizara ya Afya hapa wanategemea kukusanya pesa, lakini tunachokikusanya hakipo hiyo pesa yenyewe haipo, ndio nikatoa ushauri ile bilioni saba ile igaiwe angalau zipatikane hizi pesa wapate kukusanya, *extra* yenyewe Mheshimiwa haipo, tutakusanya nini?

Mhe. Naibu Spika: Nimesemaje, ndio maana nikakwambia kwanza subiri hatujaingia kwenye hicho kifungu kidogo, wewe umeingia kwenye fungu kubwa, subiri kwanza una haraka ya nini, subiri.

Kifungu H0101	Afisi Kuu Pemba	78,000,000
Kifungu H0102	Idara ya Mipango	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ninachozungumza hiyo huduma ya *X-ray* ni ya kusuasua katika Hospitali ya Mnazi Mmoja wala si ya rufaa hatujafika bado, mapato haya tutakusanya kwa miujiza, ndio ushauri wangu niliposema jana katika kuchangia zile bilioni saba zile tuzigawe, hizo milioni 500 zilizokwenda kwa wazazi na watoto sawa, huu ndio ushauri wangu, huduma haipo ya *X-ray*, *X-ray* iliyopo ya *mobile* baadhi ya vipimo havipatikani, kwenye paja hapa huwezi kupiga, kwenye mgongo haipatikani, kwenye kichwa haupatikani.

Na hichi Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu shahidi mimi nina udhu wangu hivi sasa mwaka jana nilisema *X-ray* haipo, lakini hili sijui tuseme ni dharau au kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti: Aaa! Wewe uliza hilo suala unalotaka kuuliza, hadithi nyingine usilete.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nishauliza basi Mwenyekiti, haya mapato yatakujaje?

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Jaku, kwa kuuliza na ana haki ya kuuliza kwenda kifungu hiki. Kwanza jina la kifungu ni malipo naomba Mhe. Jaku, afahamu ni malipo ya *X-ray* na uchunguzi wa damu na Makatibu watatusaidia hapo, kwa hivyo, hizi fedha milioni 8 tunachukua hichi kifungu cha kwanza kabisa, mfano milioni 8 kwa mwaka 2016 za kuingiza zinaweza zote zikatokea katika uchunguzi wa damu.

Lakini la pili naomba Mhe. Jaku, atukubalie sio siku zote itakuwa *X-ray* hamna mfano hii Idara ya Pemba imeandikwa hapa Afisi Kuu Pemba, sio siku zote sisi tutakuwa hatuna *X-ray*, pale *X-ray* Pemba ziko nne zitaletwa katika hospitali ya Abdalla Mzee itakapofunguliwa na tunatarajia Septemba wale wanamaliza mradi wao, Novemba pengine Mheshimiwa katika Sherehe za Mapinduzi pale kuna ufunguzi rasmi, kwa hivyo, pale patakuwa na *X-ray* na wale wagonjwa mbali mbali ambao watakaokuwa katika hizi huduma za *National Insurance* watakuwa wanalipa hizi pesa, kwa hivyo, hizi sio nyingi sana madam zimeshapangwa naomba tuzikubali na hizi huduma nyengine nazo katika fungu hili hili tutaendelea kuchangia.

Tuende kwenye jina Malipo ya *X-ray* na Uchunguzi wa damu, sio *X-ray* peke yake.Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahante sana Mhe. Waziri, tupo katika kujenga hoja wala hatukuja kulumbana, mimi nakusaidia wewe wala mimi sitofaidika na kitu, hiyo *X-ray* Pemba hali ndio kama hiyo, ndio nikasimama hapa, usingeniona kusimama hapa, ndio ushauri wangu niliotoa Mhe. Waziri, hizi bilioni saba tuzigawe wananchi wetu wana imani na Chama chetu cha Mapinduzi ndio walichokichagua kwa kishindo tukafika hapa, hatuwezi kuwekea rehani maisha ya wananchi wetu, hizi pesa watazipata wapi. Twende kidogo kidogo tu wala hatukuja kushindana, hakuna mbora hapa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana, mimi Mhe. Naibu Spika, sishindani na Mhe. Jaku, labda yeye hajanifahamu, sishindani nae hata kidogo, na anajua yeye anawatetea wananchi na sote hapa tupo katika kuwatetea wananchi na mbora anajulikana huko mbele ya *Allah*, maana kwa hivyo tunavyofanya kazi naamini na sisi pia tuna fadhila zake ndani yake tunapata.

Mhe. Jaku, kwa kupitia kwako wewe Mhe. Mwenyekiti, hapa nitachukua mfano wa kifungu, twende kwenye H0101 nachukua kifungu cha mwanzo kabisa, 1422051 ni milioni 8, tunakubaliana kwanza hapa, hichi ni kipato kimewekwa wala hatubishani, sasa yeye kaishika hii bilioni saba, bilioni saba haipo hapa, bilioni saba hapa haipo kabisa, ni kwengine kabisa anakozungumzia ambayo maelezo yake yatakuwa mengine, hichi ni kipato. Katibu atatusaidia hapo mezani, hichi ni kipato cha milioni nane, milioni nane kwa mwaka mzima kwa Pemba wanaweza kuingiza, huduma zinazotolewa pale milioni nane *is nothing*, tukiwapunguzia watu watapumzika zaidi, bora tuwawekee ili watu wapate kwenda mbio watimize, watakapokuwa hawajatimiza tutaweza kuwahukumu kwamba kwa kiasi gani hawajatimiza.

Kwa hivyo, mimi sibishani na Mhe. Jaku, hata kidogo, niko katika kumfahamisha na ninafahamu anatutetea sisi Wizara ya Afya, anawatetea wananchi wa Zanzibar, anatutetea sisi tupate fedha nyingi zaidi. Lakini akiziondoa hizi milioni nane, mathalan nimechukua mfano huo akiziondoa hizi milioni nane atakuwa hata sisi hatutetei anatupunguzia kwa sababu hichi ni kipato kwa Serikali. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti…

Mhe. Mwenyekiti: Hii mara yako ya Mwisho Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Namshauri Mhe. Waziri, atakusanya kipi wakati hicho kitu hakipo, si itakuwa miujiza, unategemea kitu ili ukamate kitu, sasa hicho kitu chenyewe hakipo kinasua sua, atafute njia ya kukitengeneza ili apate hayo mapato. Mhe. Waziri, nafikiri umenifahamu ili utengeneze kitu au upate maziwa mengi ni ng'ombe umlishe vizuri, hichi kitu hakipo, utafute njia unijibu, utatafuta njia gani.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mhe. Jaku, umeshauliza Mhe. Waziri, mjibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti na mimi labda niendelee kumfahamisha tu kidogo awe muelewa Mhe. Jaku. Kwanza ninachokisema Mhe. Jaku, haya ni mapato, yaani makusanyo. Makusanyo yoyote huwa yanatokana na chanzo cha kukusanyia, hapa pana vyanzo viwili; kuna chanzo kitakachopatikana kwa hudum ya *X-ray*, *X-ray* ikifanya kazi kunawezekana kupatikana mapato.

Chazo chengine ni uchunguzi wa damu, nikenda mie nikitaka kupimwa damu, chochote kinachohusiana na uchunguzi pale nacho ni chazo kitakacholeta mapato ndani ya ile hospitali na chazo cha mapato kinapopangwa hakitakiwi kwamba lazima kifike kile ambacho kimepangwa, inawezekana ukapanga mapato ukayafikia yale uliyoyakadiria, ukayapitiliza au usiyafikie. Kwa hivyo, kwa hili Mhe. Jaku, hapa hata kama *X-Ray* haipo bado yatakusanywa mapato kwa uchunguzi wa damu ndani ya hospitali, na mimi na yeye tukenda tukipeleka kidole tu kutafutwa malaria, maana yake umechunguzwa damu kama shilingi elfu mbili, elfu moja.

Kwa hivyo, napenda kumfahamisha Mhe. Jaku, kwamba hii sehemu ya mapato, Bima ya Afya pale ipo na kila kitu vipo vinapatikana, kwa hivyo, hii sehemu ya mapato angengoja labda tukaingia hiyo sehemu anayotaka pengine masuala

anayotaka yeye, lakini kwa hili halina mjadala wala haliwezi likakosa haiba ya kuwa lisiwepo kwa sababu *X-ray* haipo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aaaa! Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichokizungumza...

Mhe. Mwenyekiti: Aaa! Sijakupa ruhusa Mhe. Jaku.

Kifungu PH0102	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	110,011,000
	JUMLA YA FUNGU	**188,011,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU H01 WIZARA YA AFYA

Kifungu PH0101	Program Kuu ya Huduma za Kinga na Elimu ya Afya	

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana, wakati nilipokuwa nikichangia na nilikuwa nikiuliza masuala hapo nyuma nilikuwa nimekerwa sana na kuuliza kwangu, kwa nini shindano ya kinga ya *BCG* imekosekana kwa kipindi chote cha mwezi wa tano hadi leo, naomba ufafanuzi kidogo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Dimwa, kwa kuomba ufafanuzi hapo, naomba niseme kwamba sasa hivi kuna programu maalum ya chanjo ambayo tuna-*deal* na hili Shirika linaitwa *GAVI*, wao ndio wanao-*distribute* hizi chanjo na tuelewe kwamba sisi kama Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mara nyingi huwa fedha zetu tunapata kwa wahisani wa maendeleo moja kwa moja ambao wanatununulia hizi chanjo na hii ni miaka mingi sana. Nadhani kihistoria mtakuwa mnakumbuka huko nyuma kisiasa tushawahi kuathirika kutokana na masuala haya haya ya chanjo. Sasa kipindi hiki kidogo wakati wa uchaguzi kulitokezea na *delay*, lakini *delay* sasa hivi ishatatuliwa na wanaendelea kutuletea hawa jamaa kama kawaida. Kwa hivyo, naamini ile athari iliyokuwa imetokezea kipindi kile cha uchaguzi ilikuwa ni *very temporary*, sasa wataendelea na hili suala linaendelea. Sikuwahi kumjibu pale Mheshimiwa, ndio katika yale niliyokuwa nimeomba radhi kwa sababu yalikuwa maswali mengi sana.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri, ila hakunambia lini kama zipo tayari au yeye anasema tutaendelea tu, kwa sababu tuna maradhi ya *airborne disease* ambayo kama *tuberculosis* na mengine ambayo yanaweza yakawapata watoto wetu wakiingia katika *atmosphere* hii nyengine. Lakini aniambie tayari, lini au vipi, kwa sababu hajanambia anasema tunaendelea tu na kama atajibu hilo tunaendelea basi tuendelee.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Dimwa kuomba ufafanuzi wa ziada. Hivi majuzi tu tumetoka kwenye mkutano wa *WHO* wa kimataifa na hii ndio iliyokuwepo katika ajenda kuu moja wapo. Nchi zinazoendelea zinatoa fedha kuwasaidia wale nchi zisizoendelea na mara hii wanataka na sisi tuanze kuchangia, bado kuanza uchangishaji rasmi na *stock* ya sasa hivi tunayoitegemea ambayo hiyo wame-*prove* kutokana na hiyo *shortage* iliyokuwepo, *stock* nimeletewa sasa hivi hapa na karatasi zake inatarajiwa kuwasili Zanzibar tarehe 17 Julai, 2016, *stock* ya *DCG*. Katika ule utaratibu wetu tutakaotoa tutajitahidi kumshirikisha Mheshimiwa na yeye aje kutembelea kule kwenye maeneo yetu apate kuna yale mafriza yale makubwa yanayoweka madawa hayo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na niishukuru sana serikali yangu kwa kufanya jitihada kubwa sana kwa kuleta, lakini inaelekea hasa Mhe. Waziri, alikuwa hana hicho kitu ndio maana amenijibu hivyo. Nina *Hansard* hapa mbili tofauti; ikiwa moja ya Mhe. Naibu Waziri na moja Mhe. Waziri, ambayo alitupa ufafanuzi lakini pamoja na *account* ya kuchangia, lakini nasema tu tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, Mimi katika mchangio wangu wa hotuba katika maswali yangu kumi na tatu niliyouuliza nimejibiwa moja, lakini kwenye swali langu moja yanaingia maswali mawili. Mhe. Naibu Waziri, kajitahidi kunijibu lakini katika kunijibu sikuridhika. Alipokuwa akinijibu sikuwemo ndani lakini nilikuwa ninasikiliza kwa juu. Suala hili mimi nililikemea sana na nilizungumza kitu nina ushahidi, mtu yeyote Mnazimmoja kwenye chumba cha uzazi kwamba, mtu anapofanyiwa *operation* nchi za wenzetu mimi mwenyewe binafsi nilifanyiwa *operation* ya mguu, lakini unapoingia kwenye *theatre* unavalishwa guo la *plastic* ambalo linakuziba, mfano unafanyiwa *operation* kwenye mguu chini basi litakuziba mpaka kwenye magoti utapasuliwa ile sehemu husika, lakini sehemu iliyobakia umestirika. Kama unapasuliwa kwenye tumbo ipo nguo *special* ya *plastic* ambayo kwenye tumbo inakuwa nafasi anachanwa ile sehemu unafanyika

operation lakini mtu kastirika. Lakini Mhe. Naibu Waziri, ananijibu namsikia juu kwamba, wanawake wenyewe inapofika ile *time* kwamba wao wenyewe nguo hawaitaki. Hii kauli, mimi nataka nimuulize yeye mwanzo Mhe. Naibu Waziri, hivi kweli hiki kitu anachokizungumza kakizungumza anakifahamu ama anazungumza tu kwa hasira.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, uliza swali.

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Mimi swali nililouliza kwa nini serikali haitoi nguo zile na watu wanawekwa uchi, nazungumza moja kwa moja afahamu, haiwezekani watu wadhalilishwe hawana nguo wakati uwezo wa kuvalishwa *plastic* upo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hiyo lugha unayoitumia siyo.

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Lugha ipi?

Mhe. Mwenyekiti: Wewe mwenyewe unafahamu huwezi kutumia lugha hiyo hapa, Kanuni zinakataza.

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Lugha ipi sijaifaham katika niliyozungumza, nitumie nini, wanakaa bila stara, samahani. Kiswahili kigumu Mhe. Mwenyekiti. Sasa swali jengine alizungumza vile vile hawa madaktari wa kiume, mimi nilizungumza wanaingia ndani na wakati watu hawana stara wapo kama wanavyozaliwa, kwa nini wanaingia madaktari wa kiume, hakuna madaktari wa kike.

Mhe. Mwenyekiti: Umeshauliza swali, mwache Waziri ajibu. Naibu utajibu haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza naomba nimshukuru mtoto wangu Nadir, kwa kukerwa na suala hili. Lakini nataka niendelee kumuhakikishia kwamba katika wodi za *maternity* zote basi hakuna amri maalum ya kwamba anayeingia mzazi avue nguo. Kama hicho kakiona na kwa bahati nzuri hapa alipokuwa anachangia alisema kwamba hakuona kasikia na watu wawili watatu. Inawezekana hawakumueleza vizuri, lakini utaratibu ukiingia mule unaingia na nguo zako, *nurse* anakupokea anakuonesha kitanda cha kukaa ili uchungu ukikolea akusaidie jinsi ya kwenda kwenye chumba cha *labor* na hapo mote unakuwa na nguo zako mpaka ukifikia hatua ya kwamba unaenda kujifungua wewe mwenyewe kwa hiari yako, mimi nakueleza kwa

sababu hiki kitu kimeshanifika. Mimi ni mwanamke, mimi ni mama na nimeshajifungua, wewe Nadir hujajifungua unasikia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, nafikiri Mhe. Nadir, anachokitaka anauliza serikali zile nguo ambazo watu wanavalishwa wakati wa kufanyiwa *operation* ndio anazoona kwamba hazipo, yeye ninafikiri hoja yake kubwa. Kwamba kuna nguo ambazo yeye anahisi hazipo, kwa hivyo, watu wanakwenda kufanyiwa matibabu bila ya kuvalishwa hizo nguo. Ninafikiri ndio hoja yake kubwa.

Mhe. Naibu Waziri: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini nguo zile wanavalishwa wagonjwa au wazazi wanapofanyiwa *operation* tu hawavalishwi wakati wa kujifungua. Kama ni hizo alizokuwa anaziuliza, hilo swali kalibadilisha mwanzo lilipokuja halikuja katika sura hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, hapa tutapiga makofi sana, hili suala la kum-*support* ni jambo ambalo sio zuri ku-*support* halipendezi.Mimi nilichozungumza ndivyo ulivyomuuliza wewe ndivyo nilivyozungumza. Sibadilishi kauli na kauli ninayoizungumza mimi kwamba anadhalilishwa mwanamke kuingia mwanamme ndani. Wewe umeona wapi mwanamme anaweza kumsaidia mtu kwenye kuzalisha.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Nadir, ni hoja mbili tofauti.

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Ndio kazijibu na kakosea na mimi ndio swali langu nililouliza. Mimi hili suala kwa sababu ni muhimu na mimi si mwanamke, mimi ni mwanamme na mimi baba vile vile nina watoto. Lakini walionambia na mimi nina uhakika nao wamefanyiwa hivi, kwani mimi lazima niingie mule ndani kwenye ushahidi mwengine. Yeye Mhe. Naibu Waziri, aniambie keshakwenda mara ngapi kuangalia mule ndani kwa ile hali iliyokuwepo, aniambie hivyo basi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati wote mazungumzo yanaendelea nilikuwa najaribu kutafuta hoja ya msingi. Naomba nitoe maelezo haya ili Mhe. Nadir, anifahamu na kama atataka mimi nimeshafanya ziara *maternity* mimi mwenyewe binafsi, si mara moja, si mara mbili, si mara tatu, si mara nne ya Mnazimmoja na nimeshakwenda ndani mimi mwenyewe na leo nimefunga saumu na nasema ukweli kabisa. Na shahidi ni Bi. Tatu fundi ambaye ni *sister in charge* ya wodi ile, yeye mnaweza kumuuliza atakupeni ushahidi. Nimefanya ziara nimeikuta hiyo hali, hao niliofanya ziara mimi wakati huo mimi nimeikuta hiyo hali hawakujali hata kama kuna mwanamme

ndani, hawakuwa hata na hiyo akili ya kujali kwamba kuna mwanamme humu ndani au hakuna mwanamme. Na wakati mimi nifanya ziara ya kikazi hiyo sikuangalia hivyo vitu vyengine kwa sababu lililonipeleka pale mimi ni moja tu. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, Mhe. Mwenyekiti, *in charge* ya wodi nzima ya *maternity* yetu ya Mnazimmoja na Dr. Zakaria mwanamme, mwanamme kamili. Sasa hivi tumeletewa mtaalam na *UNFPA* kutusaidia katika *monitory and supervision* ya *infant and maternal mortality*, yaani vifo vya mama na mtoto vimetoka Umoja wa Mataifa, naomba Mhe. Nadir, unikubalie hili, tumeletewa kutoka Umoja wa Mataifa anaitwa Dr. Hemed Mahfoudh mwanamme na wanasema wanawake wenyewe na mpo humu ndani wengi mtathibitisha hilo. *The best delivery* anayopata mwanamke ni anayofanyiwa na *delivery* mwanamme. Mimi mwanamme ninakwambieni *the best service* anayopewa mgonjwa wa kiume ndani ya wodi ni *nurse* mwanamke.

Kuna *research* imefanyika kwamba wanaume wanakuwa katika *delivery room*...

Mhe. Mwenyekiti: Jibu swali moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Afya: Ndio ninajibu niko katika kujibu. Katika *delivery room* wanapokuwa wanaume hata vifo vya mama na watoto vinapungua na wanaume wanaolazwa kwenye wodi hizi za kawaida wanapokuwa na maradhi mbali mbali manesi wakiwa wa kike wanapona haraka wanatoka kwenye zile wodi haraka. Ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-atif Yussuf Al-Wardy: Ninachotaka kusema sisi Waislamu wengi Zanzibar na tukisikiliza wazungu mwisho watakuja kutwambia tuje tuoane wanaume kwa wanaume na tutaoana humu. Kwa sababu tukisema tu tunaletewa mwanamme *doctor* ende kwa mwanamke kwenye mambo ya *operation*, mambo ya kuzaa na tunakubali, kwani wanawake hakuna. Mimi ninachozungumza hoja yangu iko pale pale kwamba mwanamme ni udhalilishaji kuingia chumba cha mwanamke anayejifungua na hakuna nguo ya *plastic* ya kuvalishwa anawekwa kama alivyozaliwa. Mimi naomba tuendelee lakini wafahamu na wajue hiki kitu sio vizuri kwa mujibu wa dini yetu ya Kiislamu, mimi Mwislam na nitapigania dini yangu mpaka nitakufa. Ahsante.

Kifungu kidogo SH 010101 Program Ndogo ya Kinga na Elimu ya Afya 2,721,644,000

Jumla ya Programu Kuu ya Huduma za Kinga na Elimu ya Afya **2,721,644,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyoe)

Kifungu PH 0102 Program Kuu ya Huduma za Tiba
Kifungu kidogo SH 01

Mhe. Mihayo Juma N'hunga: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wakati ninawasilisha nilijitahidi sana kumuomba Mhe.Waziri, atakapokuja kwenye majumuisho yake angalau agusie Kituo cha Afya Mbuzini ambacho wizara imeshakubaliana na ahadi ya Mhe. Rais, kuwa kituo kile kimalizike ili sasa kiweze kuhudumia wilaya. Sasa nilikuwa naomba majibu ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana sana Mhe. Mihayo, ni kweli hilo aliuliza ameuliza kwa kuzungumza na ameuliza pia kwa maandishi na maandishi yake ameandika kwa heshima na taadhima, maana ameanzia kwa maneno hayo mazuri kabisa ninayo hapa. Naomba nimthibitishie kwamba na sisi pia tumeshapokea barua kutoka kwa Mhe. Rais mwenyewe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein akitwambia sisi na kutukumbusha kwamba pale ana ahadi.

Hivi sasa tayari tumeshafanya mawasiliano na wafadhili mbali mbali na Mkuu wa Wilaya yake ametuletea barua ya kutukumbushi na kituo kile ni muhimu sana, tumeshaanza kufanya mazungumzo na wafadhili mbali mbali tukimpata mfadhili mkononi keshakubali na anatatoa fedha, basi na sisi tutachangia sehemu yetu tutakwenda kutengeneza kituo. Naomba atuvumilie lakini hilo lipo na Mhe. Rais mwenyewe pia analifahamu na ameshatuandikia kwa maandishi kabisa tunayo. Ahsante sana.

Mhe. Mihayo Juma Nunga: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini huu ni mwaka wa tatu sasa tangu ahadi hii imetoka na kucheleweshwa kwa kituo hiki kunazidi kuifanya hospitali ya Mnazimmoja kuendelea kupata huduma ya watu wengi na kuzidiwa. Sasa kupata majibu ya Mhe. Waziri, naomba tuendelee.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia niliomba sana kwamba lile fungu kubwa la bilioni saba tuligawe ili liweze kupatika huduma za vifaa ili hospitali yetu hii ya rufaa ambayo tunaitegemea isije ikatokea usumbufu mgonjwa kutoka Kijijini anakimbilia Mnazimmoja na ikawa kule hakuna kifaa cha kumpimia. Nikaomba fedha hizi tuzigawe ili iweze kupatika huduma hii ya vifaa ikiwemo *X-ray* na mambo mengine.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naona hilo fungu haliko moja kwa moja, lakini naomba nitoe ombi maalum na Mhe. Panya, atukubalie. Kwa kuwa wenzetu wa Wizara ya Fedha tumeshapanga nao na kwa kuwa hizi bilioni saba hatutumii sisi moja kwa moja kuipandisha hadhi. Kwa sababu ile itapanda hadhi kutokana na huo ukarabati mkuu utakaofanyika. Fedha hizi zinatumika katika miradi ambayo itasaidia kupandisha hadhi ya yale majengo mawili ya pale kilichokuwa kiwanda cha madawa zamani ambayo moja imekuwa ni wodi ya watoto na moja ni wodi ya wazazi na kupitia miradi mbali mbali hiyo miwili, fedha hizi zitakwenda kuchangia kule kumalizia yale majengo kama ni ahadi yetu kwenye ule mkataba baina sisi na *ORIO,* yaani Serikali ya Uholanzi.

Kwa hivyo, kwa hapo tutakapomaliza majengo yale hadhi ile itakuwa imechangiwa sana kupanda Mnazimmoja. Tusipofanya hivyo hivi sasa tutakosa sisi faida kwa sababu ile *grant* lazima dola tutowe dola, kila wakitoa wao na sisi inabidi tutoe. Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Panya, atukubalie kuna maelezo mengi ambayo ninayo ya kuyatoa hapa na mambo ya ramani na kadhalika, lakini naomba atukubalie kwamba fedha hizi sio sisi tunatumia moja kwa moja kwa Mnazimmoja, zinakwenda kufidia kwenye lile jengo ambalo linajengwa sasa hivi kilichokuwa Kiwanda cha Madawa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli maneno ya Mhe. Waziri, nimeyasikia lakini tatizo linalotupata maradhi huwa hayasubiri akatokee mfadhili huko maradhi yanapokuja yanataka kuhudumiwa kwa wakati ule yaliyotokea. Sasa kama tulivyoona katika wimbi lile la Kipindupindu halitatusubiri atokee mfadhili aje atufadhili kwanza, lazima itabidi sisi wenyewe tupigane ili tuone huduma ile lazima inapatikana.

Sasa Mhe. Waziri, bado mimi naendelea kukuomba suala la kupata vifaa katika hospitali ni muhimu kwanza kuliko kutengeza hayo mengine. Kwa sababu hii hospitali tayari tumeshaiweka ya rufaa na kwamba sisi tegemeo letu lote tutakapotoka vijijini kasi yetu tunakimbilia Mnazimmoja. Sasa kuja

Mnazimmoja na huduma pia ikawa haipo ni tatizo Mheshimiwa, ninakuomba sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Panya, anataka ahadi kwako anakuomba. Sasa mjibu ombi lake.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante na mimi naona raha sana kuombwa na Bi. Panya na mimi huwa namuomba hivyo hivyo. Mheshimiwa, naomba tena na mimi nimuombe na yeye pia. Pale katika hii hospitali mpya vinakuja vitanda 100 katika wodi ya watoto ambayo itatupunguzia kule kwenye mabao wanakolala watoto sasa hivi, kwa sababu wakati mwengine wanalala watoto wawili mpaka watatu kwenye kitanda kimoja, inatilisha huruma sana wazazi wanakuwa wanakaa pembeni. Kama siku ya Sikukuu hivi mkiona mama Shein anatoa vitu pale vya Sikukuu au Bi. Asha Balozi mtakuwa mnaona nyinyi kitanda kimoja wamekaa mama na watoto wawili, yaani mama na mama na mtoto na mtoto wanakaa kwenye kitanda kimoja. Sasa hili naomba sisi tuendelee kule, lakini wakati huo huo mimi nimeshatoa ahadi kwamba tutafuta zile milioni thalathini na mbili, ninaamini hatutoshindwa kwa ajili ya kupata ile *fluoroscopy* ambayo pesa ile imetaka kutolewa kwa ajili ya *X-ray* ili tufidie kule kwenye *X-ray*. Lakini huu Mradi wa *ORIO* ukiathirika kidogo tu na wale wameshakaa kimtego mtego wenzetu, ukiathirika kidogo tu tutakuja kuumia.

Mradi huo uendelee na Mradi wa Norway ambao unaendelea vizuri nao umalizike kwa sababu tuna wagonjwa wengi wa *kidney* pale watakuwa wanasafishiwa mafigo, mkojo unasafishiwa pale, wagonjwa wale wanaokwenda *dialysis* itakuwa inafanyika pale pale katika chumba kile. Tunatarajia kwa kuanzia tutakuwa na vitanda sita, kwa hiyo, wagonjwa sita kwa wakati huo wataweza kufanyiwa. Kwa hiyo, pesa hizi kwa kuwa wenzetu Wizara ya Fedha tumekaa nao na tutakaa nao tena namuahidi Mhe. Panya, tutakaa nao kwa sababu katika ushauri wake alisema tukakae nao tena Wizara ya Fedha kujaribu kupanga nao ili kuweza kuyaondosha matatizo hayo. Tutakaa nao tena muda ulikuwa mdogo baina ya uchaguzi na bajeti, muda mdogo sana, sio ule muda wa kawaida tuliozoea tunaliza Oktoba mpaka sasa hivi. Kwa hiyo, tutakaa nao na hilo tutalitafutia ufumbuzi, namshukuru Mhe. Panya, kwa kutukubalia. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mheshimiwa, sijakubali kwa sababu 'mtumai cha ndugu siku zote hufa masikini'…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, kuna majibu ya ziada kutoka kwa Mhe. Waziri wa Fedha, naomba tumpe nafasi akujibu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Waziri, naomba kumueleza mama yangu Bi. Panya kwamba hizi bilioni 7,000,000,000 lazima kwanza tuzichambue, bilioni 7,000,000,000 zenyewe kuna *grant* ya Waholanzi 3.5 *billion*. Kwa hiyo, sio pesa za SMZ hizo 3.5 billion kwa ajili ya mradi huu. Lakini katika makubaliano ni kwamba lazima iwepo na *matching fund* ya serikali ya 3.5 *billion*, ukisema unazitoa hizo zako 3.5 *billion* ina maana na hizi 3.5 *billion* za *ORIO* huzipati. Kwa hiyo, ningemuomba tu tukubaliane, hayo mambo mengine tutizame utaratibu mwengine, lakini hili fungu tusilikatishe. Nakushukuru sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante napenda nikubaliane na Mhe. Waziri wa Fedha na kwa sababu namuamini sana, lakini napenda aniahidi mbele ya Baraza hili utaratibu gani atautumia ili tuweze kuhakikisha mgonjwa anapata kipimo ndipo daktari anapata kumtibu. Anihakikishie utaratibu atakaotumia ili tuhakikishe wananchi wetu wanaendelea kupata tiba sahihi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusikitika Mhe. Panya, leo haniamini mimi, kasema anamuamini Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, hata nikitoa kauli natumaini atakubali kauli langu la si hivyo, itabidi Waziri wa Fedha ndio atoe kauli. Mimi kauli yangu inakwenda sambamba na Waziri wa Fedha kwa sababu mwisho wa mwezi nakwenda pale kwake yeye ananikabidhi mimi nakwenda kuwatumikia wananchi kama anavyosema Mhe. Jaku. Kwa hiyo, Mhe. Panya, kama ataniamini kwa kauli yangu basi tutakwenda sambamba na Mhe. Waziri wa Fedha, kulitimiza hilo. Ahsante sana lakini imenigusa kidogo kusema kwamba anaamini kauli ya mwanawe Waziri wa Fedha, mimi ya kwangu haiamini.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Waziri wa Fedha, nawaamini mawaziri wote kusema kweli ndani ya Baraza hili, lakini umuhimu wa hili jambo na tunalifanya kwa maslahi ya wananchi wetu, nyote mnaelewa, si kama labda tunapinga tu. Tunataka tiba sahihi kwa sababu daktari hawezi kumtibu mtu kama hapana kipimo, kupima ugonjwa unaohitaji kupimwa, maana yake ndio atapata kumtibu mtu. Sasa Mhe. Waziri wa Fedha, kwa kuwa wewe ndio mwenye ufunguo, naomba uniahidi wewe ili tupate tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Hii Mheshimiwa, nimeitoa *extra* kwa sababu yako Mheshimiwa, lakini nafasi yako ilikuwa imeshamalizika umeshauliza mara tatu, lakini nimwachie Mhe. Waziri, atoe hiyo ahadi.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Panya Ali Abdalla, atuamini sote mawaziri tuliomo humu, na serikali yetu kwa ujumla, inafanya haya yote kwa ajili ya wananchi wake na huduma za tiba zinaendelea,jitihada zinazofanywa sasa hivi ni kuimarisha zaidi huduma hizo. Kwa hivyo, atuamini kadri hali itakavyowezekana ya kuhudumia wananchi wetu basi serikali haitasita kuchukua hatua hizo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema hospitali hasa ya Mnazi Mmoja hairidhishi usafi wake, yaani ni chafu. Mhe. Mwenyekiti, naamini Serikali yetu ya Mapinduzi uwezo wa kununua *JIK* tunao, lakini kuna uzembe na dharau kwa usimamizi. Hospitali madirisha machafu, hospitali *floor* chafu, hospitali ngazi chafu, leo saa moja na dakika kumi niko pale. Mhe. Mwenyekiti, ndani ya madirisha ya hospitali amezaa ndege, ni uzembe wa usimamizi. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri, kwanza akubali kwamba hospitali ni chafu, hilo la kwanza. Jambo la pili, aniambie kweli uzembe wa usimamizi upo na jambo la tatu, aniahidi ataanza lini kuisimamia kuisafisha hospitali. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hassan, kwa *concern* yake na kwenda kutazama vitu vyote hivyo. Baadhi ya vitu yeye ni ndugu yangu, rafiki yangu sitaki kubishana nae, kwanza sitaki kumkatalia moja kwa moja ningependa twende pamoja akanioneshe hiki hapa kibanda cha ndege kimejengwa ndani, kwa sababu nitapenda kukiona hiki kibanda cha ndege, mimi nakwenda sijabahatika kukiona.

Lakini la pili, ni kuhusu *supervision*, *supervision* sasa hivi tuna *strengthen* tunaongoza nguvu kubwa sana tumeanza na *maternity ward*, tunaongoza na nguvu kubwa sana na wafadhili wetu wote kwa Mnazi Mmoja wa maendeleo safari hii tumewaambia tunataka kuelekeza nguvu zetu kwenye *supervision* zaidi kwa sababu ndio jambo la kulishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la tatu, yule aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu pale Mnazi Mmoja ameondoshwa sasa hivi yupo wizarani, *Director General.* Naamini Mhe. Rais, hivi karibuni atateuwa pale, atateuwa jembe moja kubwa la kufanya kazi, ninaamini sana kwa sababu tumo katika *process* likishapatikana hilo jembe basi mambo yote yatakaa sawa. Hivi sasa hivi tunakwenda sisi na wafanyakazi wa pale na *medical superintendent* ndio tunafanya kazi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa, naomba niseme kwamba hali ya usafi ipo vizuri, *maternity* juzi nilikuwepo mimi mwenyewe inaendelea vizuri na ma-*orderly* waliokuwepo pale wanafanya kazi nzuri ya usafi, na hatujaishiwa na *JIK*, *JIK* ipo, kama atataka twende pamoja ili akanithibitishie pale mimi niko tayari kufatana nae, lakini naamini vitu vyote hivyo viko sawa kwa sababu juzi nilikuwepo mimi mwenyewe pale. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, *just* nataka nimwambie Mhe. Waziri, huwa sizungumzi kwa kughushi, nasema tena leo saa moja na dakika tano niliamkia Mnazi Mmoja, nimeondoka saa mbili na dakika kumi. Kuingia kila pahali, vyoo kumejaa madude mabovu yaliyokufa kama viti, sijui na makorokoro gani, yaani mimi sizungumzi kwa kughushi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, anaposema atachaguliwa jembe mwengine karibu, yeye waziri ndio msimamizi mkuu kwa mujibu wa katiba na sheria, Mkurugenzi Utumishi yupo. Kwa maana hiyo kwa kuwa yule amepelekwa kwengine ndio hakuna mtu mwengine wa kusimamia kufanya usafi. Nafikiri majibu haya yanakuwa sio sahihi, ni majibu ya kisiasa zaidi. Kwa hiyo, ninachomuomba kama mwenzangu tunachomwambia akasimamie, kaaminiwa na Mhe. Rais, tunamjua ni mtoto wa mwana Mapinduzi asilale akafanye kazi ya kusimamia wana Mapinduzi wakwezi na wakulima wawe salama nchi hii ili CCM milele daima iendelee kuongoza. Namuomba tu, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana, sana, Waziri wa Afya na nimshukuru ndugu yangu Mhe. Hassan, kwa kufuatilia kwa karibu sana hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. Ninachotaka kumwambia kwamba ushauri wako tunaupokea, tutaufanyia kazi, tutakaa karibu zaidi na waziri husika kila ambalo linasemwa na Waheshimiwa Wawakilishi, hapa tutakwenda tulifanyie kazi vizuri ili tuhakikishe usafi unakuwepo katika hospitali zetu zote, tuhakikishe madawa yanapatikana, tiba inapatikana nia na dhamira ni kupitisha bajeti hii tukafanye kazi. Nawaomba tu Waheshimiwa, waturuhusu tukafanye kazi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mheshimiwa, kwa kauli ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nimekubali tuendelee, lakini pia naomba Mhe. Waziri, sisi ni jukumu letu kusimamia, sote tunafanya kazi moja ya kusimamia wananchi wa Zanzibar hasa ukizingatia sote tunatetea Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, tunaposema tusikilizwe, isiwe njia ya kutaka waziri au nani kujenga hoja na wajumbe haipendezi. Naomba kuwasilisha, ahsante.

Kifungu SH 010201 Programu Ndogo ya Huduma za Hospitali
18,438,180,000

Jumla Kuu

18,438,180,000

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu PH 0103 Programu Kuu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala
Kifungu SH

Mhe. Mwenyekiti: Naanza na Mhe. Abdalla Diwani, baadae Mhe. Ali Salum na baada ya hapo Mhe. Nadir.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante mimi katika mazungumzo yangu nilipochangia hotuba hii nilizungumza juu ya kadhia ya matumizi ya shilingi bilioni 73.9 ambazo pesa zile zilikuwa kwa ajili ya miradi ya kifua kikuu, uzazi wa afya ya mama na mtoto na kupandisha daraja hospitali zetu, nilikuwa na matumizi lakini bila ya vielelezo vyovyote vilivyoonesha kwa mujibu wa kitabu kile kilichosomwa cha bajeti cha Wizara ya Fedha ile bajeti ya serikali. Je, waziri katika hilo ananiambia vipi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Mhe. Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Jang'ombe kwa kuliona hilo. Ni kweli kutokana na uandishi wa kitabu cha bajeti yenyewe na jinsi ilivyoandikwa. Lakini hiyo *breakdown* ninayo hapa kama atahitaji kopi naweza kuiwasilisha mezani. Ahsante Mheshimiwa, na nilikuwa nayo wakati nimekwenda pale lakini kwa sababu masuala yalikuwa mengi sikuweza kulitolea ufafanuzi.Lakini nashukuru sana kwa kuliona hilo. Ahsante.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana basi ikiwa ni haki yetu kuiona basi tulikuwa tunahitaji tuione ili tuweze kuthibitisha na sisi kama utanipatia nitashukuru zaidi nitajua kweli umesimamia utaratibu wako ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba uniletee hiyo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante tuendelee.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri na mimi nilikuwa katika wale waliochangia kwa maandishi tukasahauliwa kidogo na mchango wangu mimi ilikuwa nina michango miwili; mmoja upo hapa na

mmoja tutakuja kwenye banda wakati Mheshimiwa, alipokuwa Naibu Waziri alinipa ahadi nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilichangia suala la madaktari, lakini nataka nimshukuru Mhe. Waziri, amelijibu hili kwamba wizara yake imejipanga vizuri, mtu yeyote ambaye ameshamaliza kusoma basi akirudi tu hapa anaenda kuajiriwa. Lakini mimi nilikuwa na mawazo tofauti nikataka tusaidiane baina yake yeye na Waziri wa Utumishi na Ajira, pamoja na kwamba wameweka hiyo *loophole* ya kwamba mtu akija na kuajiriwa, kuna tatizo la kimaslahi, unaweza ukaweka ajira lakini mtu kutokana na maslahi akawa hayuko tayari kuajiriwa kwa sababu ya mafao.Sasa nataka nimsaidie Mhe. Waziri kwamba tumpongeze sana Mhe. Rais kwa kauli zake na ahadi anazozitoa kwa Wizara ya Afya kwamba alifika kutamka kuwa atafanya jitihada kuwasomesha vijana ili tupate madaktari bingwa wazalendo.

Niishukuru sana Bodi ya Mikopo na Elimu ya Juu kauli ya Mhe. Rais, wameifanyia kwa vitendo, wamepeleka wanafunzi 34 Uturuki, 34 China tangu mwaka 2010 tulikuwa tuna jumla wanafunzi 68 wenye fani tofauti za udaktari. Kwa bahati vijana hao wanarudi Zanzibar Julai, 16 na kila kijana mmoja amegharimu shilingi 65,000,000 kama ni gharama za hiyo elimu, kwa hesabu ya jumla jumla na jawabu niliyoifanya hapa karibuni bilioni 4,420,000,000 pesa za wavuja jasho, pesa za Tanzania, pesa ambazo zinahitajiwa na kila mtu. Kwa hiyo, hofu yangu kama hatukupanga mipango mizuri baina ya wizara na Wizara ya Utumishi vijana hawa wakija wakikimbia, maana yake tunai-*cost* Bodi ya Mikopo kutokupata marejesho, kwa sababu mwanafunzi anatakiwa afanye kazi ndipo aweze kufanya marejesho baadae tupate kuwasomesha vijana wengine. Sasa nataka kujua mipango madhubutu waliyoipanga ili tusije tukakosa vijana hao kuajiriwa na kuweza kurejesha mikopo ile kwa kuweza kusaidia vijana wengine. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe. Ali Salum, ni kweli nampa heshima zote kama Mnadhimu wangu, ni kweli aliuliza masuala mawili; moja ni hilo alilolisema na la pili, lilikuwa ni kuhusiana na banda lile la kupungumzikia. Kuhusiana na hili Mhe. Mwenyekiti, yeye pia akiwa Mjumbe wa Bodi ya Mikopo atakuwa analielewa zaidi kwa hesabu zinazotolewa huko na masomo yanayotolewa huko.

Lakini kwa upande wa Wizara ya Afya, naomba nimshukuru sana tena kwa mara nyengine Dkt. Ali Mohammed Shein amekuwa akilisimamia zoezi hili la kupata ma-*specialists* vijana wetu waliokuwa wamesha-*graduate* wamepata *MD* kwenda kusoma zaidi masomo ya juu zaidi. Lakini pia hivi juzi tu

tulipotembelewa na Gavana kutoka *Jung Soo Province* Jimbo lile kutoka Serikali ya Watu wa China alipotembelea na kufanya ziara yake Ikulu suala hilo lilizungumzwa tena na kuombewa nafasi. Tumekubaliana nao kwamba watakuwa wanakwenda vijana 30 kila mwaka nchini China katika *sponsorship* yao moja kwa moja kwenda kusoma na itakuwa ni fani ya *medicine*. Na lile nililojibu mwanzo ilikuwa ni *doctor of medicine* akija anapata pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mafao hili linaingia moja kwa moja kwenye ule utaratibu mzima wa utumishi wa *salary scales* za serikali, sio kwetu sisi moja kwa moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya, kwa maelezo yake. Suala la ajira kwa vijana wetu wanaokwenda kusoma nchi za nje, Mheshimiwa katika serikali ambayo imesomesha watu wengi Zanzibar tumejitahidi sana kusomesha vijana wetu, wamekwenda katika fani mbali mbali. Katika eneo ambalo Serikali yetu hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inaipa kipaumbele ni eneo la madaktari wenye fani hizo ambazo maalum tunazosema. Haiwezakani hata siku moja daktari aje hapa amalize masomo yake tusimuajiri, walimu wa sayansi tunawaajiri tunawapa *priority*, madaktari tunawapa *priority* wakisharudi kusoma. Lakini tatizo lilokuwepo na ukweli wenyewe ndio huo kwamba wengine hawarudi huku kufanya kazi na sisi.

Sasa suala hili la uzalendo ni wenyewe vijana wetu tunaowapeleka kusoma huko, la msingi hapa kwamba sisi watakaokuja hapa wamerudi kwa hiari yao, na wanarudi baada ya kumaliza masomo, serikali haiwezi kuwatupa hata siku moja, tutawaajiri wote wanaokuja na madamu tumewapeleka kwa gharama tutawaajiri katika serikali yetu wala hatujaweza kuwaacha hata siku moja. Tatizo lilokuwepo vijana wetu tuliowapeleka kama huko Uturuki sina hakika mwenyewe Mhe. Waziri wa Afya, pengine atakuwa anajua, lakini sisi pale Utumishi tukiletewa tu ana *qualification* tunamuajiri moja kwa moja.

Sasa tatizo kama hawarudi sasa wanakwenda kufanya kazi kwengine, maslahi hayatoshi kwetu sote hapa, lakini sasa ni suala la uzalendo na kuipenda nchi yako. Tunachoomba sisi vijana wetu wakirudi kusoma, warudi wafanye kazi na sisi ili waweze kuwahudumia wananchi wenzao.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimewasikia mawaziri wote mimi sina tatizo sasa, lakini niseme kwamba bado tuna haja ya kuangalia maslahi bora, kwa sababu nasema kwamba tusipoangalia maslahi bora, maana yake na hapa tayari kuna fedha za serikali tumeshaziondosha. Sasa tukisema maslahi

hayatoshi ni kweli hayatoshi na ndio maana hata na sisi wawakilishi tunachosikitisha kwamba maslahi tuliyokuwa nayo hayatutoshi tunataka tulingane angalau na maslahi ya wenzetu kama wabunge lakini hatufiki kwa sababu ya uwezo wa serikali ni mdogo. Lakini angalau jitihada nayo inakuwa inaonesha matumaini. Mimi sina tatizo kwa sababu aliyemaliza namuheshimu sana Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichangia vile vile, namshukuru kwanza Mhe. Waziri, alinijibu vizuri vituo vyangu viwili vya Jimbo langu la Chaani ambavyo vimefungwa kwa muda mrefu; kile kimoja hakifanyi kazi vizuri, ni kibovu na kile kingine hivyo hivyo amekiona. Sasa mimi nilitoa ushauri kwamba katika mfuko wowote ambao yeye anahisi akatoa kile kituo kimoja kati ya viwili akakitengeneza na mimi nimemwambia niko tayari kutoa vifaa kama vitanda na mashine ambazo za vipimo kwa upande wangu ili kikafanya kazi kimoja, hicho kimoja tukangojea huo msaada kwa sababu msaada wenyewe hatujui lini vitajengwa vile vituo. Sasa mimi ningeomba Mhe. Waziri, anijibu vipi tunaweza kufanya angalau kituo kimoja kati ya vile viwili kifanye kazi vizuri na kiwe katika hali nzuri na mimi niko tayari kushirikiana naye na nishamwambia, naomba anijibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana. Ni kweli Mhe.Nadir, tulifanya mazungumzo na ni kweli tulifanya ziara pamoja ya vituo vyake vyote na ni kweli alitupa *support* kubwa sana wakati tunafanya ziara, kwa sababu kamati yake nzima ya afya ya shehia ilikuwepo. Kwa bahati kituo chake kimoja kipo tayari katika orodha ya miradi ya *ORIO* na kwa bahati nzuri mradi wa *ORIO* wakimaliza pale Mnazimmoja *extension* ya ile wodi ya watoto wakishamaliza pale ndio watakwenda kwenye vituo kumi na tisa, kabla ya kumaliza pale hawendi kule. Na kwa bahati mbaya yeye anakihitaji kile kituo haraka iwezekanavyo na wananchi wake wameeleza madhila yao kwa sababu wanakwenda kutibiwa kwenye nyumba ya daktari, hivi sasa hivi wanakwenda kwenye nyumba ya daktari kutibiwa na ambayo nyumba imejengwa kwa madhumuni ya daktari.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunachokifanya sisi sasa hivi, tunajaribu kukichomoa kwenye mradi wa *ORIO* kukitia katika mradi wa *MILELE* na kuzungumza na ndugu zetu *MILELE* ambao tunatarajia watatukubalia ombi letu hili, wakitukubalia itafanyika haraka zaidi, wakitukatalia itabidi tusubiri ile ile ratiba ya *ORIO* ambapo wakishamaliza Mnazimmoja watakwenda kwenye hivyo vituo kumi na tisa, ila sisi tutahakikisha kituo cha Mhe. Nadir, Chaani kule kinakuwa miongoni mwa kituo cha mwanzo kabisa kuwemo kwenye mradi wa *ORIO*. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mwenyekiti, mimi nimefurahi sana na majibu ya Mhe. Waziri, lakini hiki kimoja cha katikati kama hicho kimoja kwamba atakitia kwenye hiyo *MILELE* au *ORIO* ni vizuri sana, lakini kuna chengine pale ambacho kinataka *repair* ndogo ndogo tu ambazo za kufanya *repairing* ile sehemu; mimi ningeomba sana hichi kimoja madhali hakimo katika masuala ya msaada basi tukakirekebisha kile ambacho hakito-*cost* hata milioni arubaini na tano au hamsini katika kukitengeneza na mimi nikaingiza vifaa ambavyo vya muhimu vinavyotakikana. Ningeomba Mhe. Waziri, hili, hilo moja nishalifahamu, lakini hichi cha katikati naomba unijuilishe.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Nadir, hapa anacheza ule mchezo wa zamani wa kumweka mtu kwenye kona hivi. Tatizo letu ni bajeti Mhe. Mwenyekiti, na kwa wataalamu wetu kwa eneo lile kwa *catchment area* ile wametuambia kituo kimoja kitaweza kukidhi mahitaji ya eneo lote zima. Kwa sababu *distance* baina ya kituo kimoja, yaani masafa yale baina ya kituo kimoja na kituo cha pili si marefu; kama panahitajika *repair* ndogo ndogo sio kwa bei hiyo tunaweza tukafanya utaratibu tukaweka kwenye ku-*repair*. Lakini kwa *repair* kubwa kubwa kwenye kufika milioni arubaini na hamsini bajeti hiyo tutashindwa, sisi lazima tutegemee ile miradi ambayo imeshapangwa tayari na imeshaingizwa katika mlolongo mzima.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yale aliyoyaeleza Mhe. Waziri wa Fedha, na hivyo vituo kumi na tisa bado pia vimo kwenye mpango huo huo wa *ORIO* ambao tunafanya nao *dola to dola*. Kwa hiyo, naomba atukubalie kama *repair* ndogo kwa pale tunaweza kushirikiana naye, naomba atukubalie sana, lakini kwa ile *repair* kubwa na wakaazi wa eneo lile lote zima basi tusubiri huo mradi mkubwa ambacho kitakuwa ni kituo cha kisasa na kitakuwa *upgraded*.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri. Hichi kimoja kwanza keshatoa ahadi kwamba kishakubalika kwenye masuala ya kuja kujengwa na wafadhili, lakini hichi kimoja niko tayari huo mfuko wake mdogo anambie shilingi ngapi atanisaidia ili tukiweke katika hali nzuri, huo mfuko mdogo anaosema wizara yake yenye uwezo nayo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, katika huu mfuko mdogo lazima nikae na Katibu Mkuu wangu, lazima nikae na Watendaji wangu na lazima tukae na *DMO* (*District Medical Officer*) wa *zone* yake ambae tulikwenda naye siku moja, siku hiyo tuliokwenda pale kwenye ziara. Kwa hiyo, hao lazima

tukae nao pamoja, pamoja na kamati ya afya ya Shehia, siku hizi kuna utaratibu ule tunagawana kwa sababu vile vituo tunaita vya *cummunity*, sisi tutabeba pale majukumu ambayo tunayoyaweza kubeba na watasema pale pale kutokana na bajeti yao na yeye Mwakilishi na pamoja kamati yake ya afya ya Shehia wataeleza pia wao wataweza kuchukuwa majukumu gani. Kwa hiyo, naomba nimuombe kwamba tukishamaliza hii turudi tena nikiwa na kamati yangu nzima pamoja na afisa *mas-ul* wa bajeti nzima twende naye pamoja na Katibu Mkuu mwenyewe, ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Mheshimiwa, nakubaliana naye.

Kifungu SH 010301 Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala
3,428,006,000
Kifungu SH 010302

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nilipokuwa ninachangia nilisema kuhusu *private hospital* hasa Al-Rahma. Naomba tutambue hizi *private hospitals* nyingi zao Zanzibar zipo kwa sababu ya biashara na sio kutoa huduma na ushahidi wa kwanza dawa unazoandikiwa ukenda hospitali nyengine hata hazina maana, kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri, awe *careful on that*. Lakini pili nilisema Al-Rahma; Mheshimiwa, nina ushahidi wa kutosha, huwa sipendi kusema kitu bila ya utafiti wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, Al-Rahma, mke wa rafiki yangu alikwenda kuzaa, kwenda kuzaa kule, alipofika akaruhusiwa kuzaa akiwa *pregnancy* yake iko *premature* kwa Kiswahili sijui miezi saba kujifunguwa, alipojifunguwa kumbe hawana *incubator* Al-Rahma na inaitwa hospitali. Alipomaliza ikabidi mbio mtoto achukuliwe kwenye *ambulance* apelekwe Mnazimmoja, baina ya Al-Rahma na Mnazimoja mtoto amefariki, mtoto yule amefariki kutokana na Al-Rahma inayoitwa hospitali kuwa na vifaa vya kutosha vya kuweza kumsitiri mtoto yule, hali ya kuwa anapokwenda kuzaa alijua huu ni *premature*. Kwa hivyo, ndio nikasema lazima tuangalie ili tuepushe mambo yasiyokuwa na maana, ipo kwa sababu ya biashara, hiyo moja.

Mhe. Mwenyekit, pili, Al-Rahma wanalazwa watu chungu mzima wanaotumia *insurance*, unapotaka kufa tu mbio unapelekwa Mnazimmoja, redio kila siku zinatangaza kifo kimetokezea Mnazimmoja, *not* Al-Rahma. Ombi langu Waziri namuomba aunde kamati anikubalie kuwa aunde kamati wizara kwake ichunguze pana watu Al-Rahma kwa ushahidi na utafiti ni *disqualified, unqualified to be there,* hawana sifa za kuwa pale na wapo, hivyo, aunde kamati maalum ya kuhakikisha anafuatilia hili jambo kwa umakini ili tusende

kupeleka watu wetu wakatumia pesa halafu hatupati huduma inayotakiwa, hali ya kuwa wapo pale *for business purpose*, kutengeza faida.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana sana sana Mhe. Hassan, kwa maelezo yake hayo na nashukuru sana leo bahati nzuri Mhe. Hassan, Mrajis wa *Private Hospitals Board* yumo humu ndani, yeye ndio mwenye sheria hakuna haja ya kuundwa kamati, yeye na Mwanasheria Mkuu yupo hapa atathibitisha, yeye ndiye mwenye sheria ya kufunga, kufungua, kutoa leseni kwa *private hospitals*, kuzichunguza, kuzi-*investigate* dawa zinazoandikwa kama za ovyo. Kwa sababu mimi na Mhe. Hassan, hatuna utaalamu huo, *I am engineer by profession, he is a diaspora by profession*, kwa hiyo, sisi hatuna utaalamu huo na yupo amekaa pale juu ndugu Shaaban anaitwa, naomba Mhe. Hassan, atukubalie humu ndani ya Baraza hili tukufu Mhe. Mwenyekiti, kuna vyombo mbali mbali vinafanya kazi zao, kila yanayozungumzwa yanafanyiwa kazi, maana na sisi vinatufata wakati mwengine hivyo vyombo vinataka taarifa kutoka kwetu, kuna vyombo vinafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo aliyoyaeleza asistaajabu vyombo vikimfata vitakwenda kumuhoji na bahati nzuri *registrar* mwenye Sheria ya *private hospitals* yumo humu ndani atamfata yeye Mhe. Hassan, kumuuliza ili ushahidi wote, kwa sababu katika *medical practissionals law* lazima kila kitu kiwe na ushahidi wake, huwezi kwa *hear say*, lazima kila kitu, ndio maana kuna *medical council*, kuna *nurses council*, *midwives council*, kuna na hii *private hospitals board* ambayo inafanya kazi hiyo na ina meno, hiyo bodi ina meno makali kweli kweli. Juzi walimkuta mtu mmoja anatibu tibu huko mitaani nadhani mliona kwenye *TV* wakati wa Kipindupindu walimfungia hospitali yake pale pale na walikwenda na polisi pamoja, kwa hiyo, ni sheria ambayo ina meno.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimuombe kwamba hakuna haja ya kuundwa kamati, ni *registrar* ndugu Shaaban atamfuata kwenda kumuuliza ampatie vielelezo vyote ili avifanyie kazi, pamoja na yale mengine mengine aliyoniuliza ya *oxygen* watayafanyia kazi wao. Ahsante.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, amejitahidi sana Mhe. Waziri, kupapatua, lakini mimi nina wenzangu hapa tuna ushahidi kabisa kwamba kunako Bodi yake mna wala rushwa, ndio wanaokula rushwa halafu wakaziweka hizi hospitali mbovu Zanzibar, tuna ushahidi kwenye Bodi yake mna wala rushwa, kwa maana hiyo atufate pembeni tutawataja na tutawathibitisha, hatutaki kuwataja majina hapa, tuna ushahidi, mimi nasema

kwa utafiti wanakula rushwa ndio maana hizi hospitali zinabakia kuwepo zinatuulia watu wetu, tuna ushahidi wa hili na sitapenda tu kuwataja hapa, nikitoa karatasi yangu nitawataja wote lakini leo ninawasemehe itafuata baadae, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ogfisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe, kazungumza suala moja zito sana kwamba, kuna wala rushwa na kitengo cha rushwa kiko chini ya Wizara ya Katiba, Sheria, Utawala Bora na Utumishi wa Umma. Hivyo, tutamuomba Mhe. Hassan na Mkurugenzi wangu atamfata ili atoe hiyo orodha na wote wanaohusika na kula rushwa hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafid: Ahsante nimefurahi sana Mheshimiwa, kwamba atufate tutawapa lakini nawaomba watu wako wa rushwa wafanye kazi isiwe wanatufata halafu *blaa blaa, no, I am not here for blaa blaa, I am here* wafanye kazi, maana yake niliuliza sitaki kwenda huko, tukishakuwapa majina na ushahidi wafanye kazi waje kutueleza yaliyofanyika, isiwe tumekuja kufanya kazi sisi wao hawamalizi, naomba kuwasilisha tuendelee.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunikumbuka tena. Mimi nilileta hoja moja huu utafiti au vigezo ambavyo vimemruhusu Mhe. Waziri wa Afya, pengine na Wizara nyengine kuruhusu kuleta peduu wa kuku, peduu nyama, peduu samaki, hawa kwa kweli hawana afya na sisi tuna vitu vyenye afya na tunao kuku, tunazo nyama, tunao samaki wa kutosha, ni vigezo gani waliowaruhusu hawa wakawa sasa hivi asilimia 90 ya wananchi wa Zanzibar wanatumia madude mabovu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru saana Mhe. Nadir, kwa suala lake zuri alilouliza na kweli aliniandikia kimaandishi lakini sikuwahi kutoa hoja hiyo. Sheria za nchi pamoja na sheria za kimataifa zinazokuwa *control* na *World Trade Organization* wanaruhusiwa kuleta biashara yoyote na ndio maana nikasema mpaka nguo za ndani hapa zinaletwa kama kibiashara, nguo za ndani nilizungumzia pia kwenye hotuba yangu nilipokuwa ninatoa pale. Hawa wanaoleta vyakula, wanaoleta vipodozi, kila *product* inaruhusiwa ili mradi iwe imekidhi sheria na imefata taratibu za nchi husika, sasa sisi katika Wizara yetu tuna Zanzibar *Food and Drug Board*, hii ndio inachunguza, huwezi kumkataza kwa sababu sheria yetu haijakataza mtu asilete kuku, asilete samaki, asilete nyama, asilete kitoweo, asilete mikate, asilete maziwa, hizi zote ni *products*, tukikataza hii maduka yetu yangekuwa

natupu na watu wasingepata kufanya biashara, wanaleta hawa wanaingia kwenye ushindani wa biashara.

Mhe. Mwenyekiti, kama tuna *local product* ama samaki wa *local* anaweza kushindana na samaki huyu anaeletwa *imported*, pale watu watashindana kibiashara, lakini hatuwezi kukataza, kisheria sisi haijatukataza tupinge na hii sheria haiko kwetu tu, Wizara ya Biashara inahusika, Wizara ya Kilimo inahusika, wote huwa tunakaa pamoja. Kwa hiyo, mfanyabiashara anaruhusiwa kuleta *product* yoyote iliyokuwa halali katika nchi ameruhusika kisheria ilimradi afate taratibu za kisheria zilizowekwa, kama *product* yake iko *approved* sisi hatuwezi kumzuia.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wanaoleta kuku peduu, hawa wanaoleta samaki, hawa wanaoleta nyama wote wanapasi mitihani wanayowekewa na *Zanzibar Food and Drug* ambayo wana *criteria* zao za *qualification* za kuleta hivyo vitoweo ndani ya nchi. Kwa hiyo, naomba ieleweke kwamba sheria haikatazi mfanyabiashara kuagizia *product* yoyote katika nchi, ahsante.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, jawabu lake zuri, lakini yeye kama Waziri wa Afya kuna vitu hata kama vinatuingizia mapato basi ana wajibu wa kuvikataa kwa afya ya wananchi wa Zanzibar. Wazanzibari watakapoletewa mapeduu ya ng'ombe, ya kuku, ya samaki inaonesha dhahiri kwamba tunawaumwa kiuchumi wananchi waliokuwa na mazingira ya chini, kwa sababu tuna uwezo tosha wa kuuza kuku.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir, hilo halihusiani, hicho unachokiongezea sasa hivi hakihusiani, kwa hiyo, umemaliza?

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Ah! Ninaongea kinachohusu sijamaliza, hii *ZBS Zanzibar Bureau Standard* inasumbuwa watu mtu anataka kuleta kuku, anataka watu watatu wapelekwe Marekani, wapelekwe wapi na hili nilimuuliza. Sasa ni sababu gani zinazowafanya wakati Zanzibar kuna hii *ZBS* ya kusimamia viwango vya vile vitu, kwa nini wasikamatie *container* hapa kama halifai wakaitaifisha wanataka lazima watu watolewe nchini Zanzibar wapelekwe Marekani, wapelekwe Norway, vigezo gani vinatumika hivyo wakati hii ipo hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hilo mbona ni suala jengine tena unaongezea?

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Hilo hilo namuuliza.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimsaidie ndugu yangu Nadir, Mhe. Muwakilishi wa wananchi Jimbo la Chaani. Hapo kidogo amekwenda upande, alichokusudia yeye ni *Zanzibar Food and Drug Board (ZFDB*) inaitwa, lakini ametaja *ZBS*, *Zanzibar Bureau of Standard*, kidogo amekwenda mchomo. *Zanzibar Bureau of Standard* iko chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masomo kwa Mhe. Amina Salum Ali, haiko kwetu sisi na wao hawafanyi kazi hiyo aliyoitaja Mhe. Nadir, kwa hiyo, kidogo naomba nimpe kijisemina kidogo tu cha kumuelimisha ili arudi kwenye mstari.

Mhe. Mwenyekiti, *Zanzibar Food and Drug* ndio wanaochunguza chakula, dawa na vipodozi, kazi zao tatu, wale wengine kitu chochote kinachozalishwa hapa Zanzibar wale wengine waliokuwa kwenye Wizara ya Biashara na Viwanda, *Zanzibar Bureau of Standard* wale *product* inayozalishwa kutoa ile nembo kwamba hii ni ya *approved*, kama vile *TBS*, wale ni *counter part of TBS*, lakini kwa upande wa *Food and Drug* na Bara pia kuna *TFBA* ina *Tanzania Food and Drug Agency*, kule wanaita *Agency* sisi hapa ni *Board* na bahati nzuri mwenyekiti wa *Food and Drug* yumo humu humu ndani sasa hivi ndani ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kumwambia Mhe. Nadir, hakuna kinachoingia nchini ikiwa kwa njia ya *Airport* au kwa njia ya Bandarini kinacholetwa kibiashara kwa ajili ya kuuzwa miongoni mwa chakula, dawa ama vipodozi bila ya kupata *certrificate* ya hawa *Zanzibar Food and Drug*. La pili, Maafisa wetu wapo saa zote kwenye njia kuu za kuingia, mpaka wale Maafisa wa *TRA* wanapokuwa Maafisa wetu hawapo kwenye *position* ile wakiona *product* ile inahusiana na mambo mambo yamekuwa *trained* wanaitwa Maafisa wetu kuja kukichunguza kile, kinaenda kuchunguzwa kama kinafaa ndio kinaingia,

Mhe. Mwenyekiti, na la tatu, wamekuwa wakati kiasi cha kwamba Jumuiya ya Wafanyabiashara imekuja kutuona sisi kwamba, watu wetu wasiwe wakati sisi tukawakatalia tukawambia kwamba hawa wanafanyakazi yao kunusuru maisha ya wananchi na kulinda afya zao, hilo hatuna *compromise*. Kwa hiyo, naomba mumuombe Mhe. Nadir, kwamba kila kinacholetwa nchini lazima kichunguzwe na hawa, hayo mengine ya *ZBS* sio ya kwentu sisi, lakini mtu yeyote akitaka kuleta kuku, akitaka kuleta samaki wanachunguzwa kuanzia ile *product* yenyewe mpaka kiwanda chao, lazima kichunguzwe, ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu kunifafanulia hivi vitengo viwili, lakini hii sehemu yake ya uchunguzi kwa nini

isifanye uchunguzi wake hapa hapa Zanzibar wakati wameshajiamini kwamba wao wanaweza kufanya uchunguzi kuliko kuwatia hasara wafanyabiashara kutoa watu wao wakaambiwa waende mpaka huko nje ya nchi wakachunguze kila kitu hapa hapa kwani haitoshi.

Mhe. Mwenyekiti: Ah! sasa hayo ni mengine Nadir utauliza tu kipindi kingine.

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Al-Wardy: Haya tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, humo kwenye *list* yangu ya hapa ulikuwa huko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa, wawili matatu hukuniona, labda hujaniona nimeinuka mara mbili hapa sasa hivi, hoja ya tatu hii.

Mhe. Mwenyekiti: Hukuwemo, ngoja nyengine halafu uta...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja ya tatu, Mheshimiwa hii, haki yangu ya msingi imo kwenye katiba hii.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana nikushukuru. Nilikuwa naomba kiokosi changu kwa Mhe. Waziri wa Fedha, baada ya kuokota milioni 7.5 angalau anisaidie hichi na hasa kwa Waziri wa Fedha. Suala la hii *X-ray* imekuwa mtihani katika hospitali ya Mnazimmoja tena kwa kipindi kirefu, naomba kauli ya serikali wala si ya Mhe. Waziri wa Afya, nataka kauli ya Serikali ya Waziri wa Fedha, kwamba serikali imeshindwa kutafuta milioni mia tatu mpaka mia nne hii ni hatari, wanionee huruma mimi nimeokoa 7.5 wanipe angalau kiokosi cha hizo shilingi 400 milioni ziende katiak *X-ray*.

Mhe. Waziri wa Fedha, kwa heshima na taadhima naomba kauli yako.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, unayemuuliza ni nani, waziri husika au...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nimemuomba Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti: Mwenye kutakiwa kukujibu masuala, wizara hii ni ya Waziri wa Afya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kauli ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ndio ninayoitaka, sio kauli ya Waziri wa Afya. Wanafanyakazi kama serikali, nataka kauli ya Waziri wa Fedha ya shilingi 400 milioni kufanya angalau *X-ray* ipatikane pale kwa muda wa mwaka mmoja. Kauli ya Waziri wa Afya nishaisikia kipindi kile, nataka kauli ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana namshukuru Mhe. Jaku Hashim, lakini Mhe. Mwenyekiti, labda nitoe rai tu kwa kiti chako, sidhani kama Mjumbe kutoka nyuma ana haki ya kusema nani ajibu kwenye serikali, serikali ndio inaamua. Kama nitakuwa nimekosea Mwanasheria Mkuu ataniongoza katika kauli hiyo. Kwa hiyo, naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa upande wa serikali asituchagulie nani na nani amuachie kazi hiyo mwenyewe Dkt. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza katika maelezo ya awali kwamba katika mradi huu wa *BADEA* bahati nzuri vitabu vyake hivi hapa, viko hapa vyote hii ni *feasibility study* yote, kuna *part 1, part 2, part 3* iliyofanyika ya Mnazi Mmoja na patakuwa na *X-ray.* Kule kwa Mchina Abdalla Mzee Pemba pia kutakuwa na *X-ray* na pale Mnazi Mmoja zaidi ya *X-ray* nne zitakuwepo katika mradi huu. Naomba asitu-*commit* sisi kama Wizara ya Afya kwa sasa hivi wala Wizara ya Fedha na Mipango kwa sababu bajeti yetu tuliyokuwanayo tunaiengaenga tuipeleke kwenye dawa na kumhudumia mwananchi moja kwa moja. *Unit* iliyokuweko pale ni *X-ray* ya *mobile* sasa hivi inafanya kazi iko *Unit.*

Mhe. Mwenyekiti, na mimi leo asubuhi wakati natoa maelezo hapa nilishasema kwamba hizo shilingi 32 milioni tutazitafuta kwa ajili ya ku-*repair* ile mashine kubwa kwa ajili ya *fluoroscopy*. Sasa kama itakuwa inaendelea hatuamini hili la Kuwait, Saudia, Qatar na *BADEA* na huku tunaendela kutumia hii *mobile unit* na huku tumeshakubali tutatoa hizo shilingi 32 milioni, naomba sana Mheshimiwa atukubalie tuweze kulifanyia kazi hili, Mhe. Jaku, yeye ni mwenzetu, anaweza kuja *any time* baina ya mimi na Waziri wa Fedha na Mipango tukakaa pamoja tukalifanyia kazi. Naomba atukubalie tu na hali itakuwa nzuri baada ya hapo Binguni tunatarajia nayo itakuja pia hivyo hivyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimfahamishe Mhe. Waziri, kwa mujibu wa Kanuni ya 37, kuhusu 'Wajibu wa Mipaka ya Kujibu Swali'.

Kifungu cha 37(1), kinasema kwamba:

"Waziri, au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa kikamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi. Isipokuwa kwamba, swali alililoulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu".

Hivi ndivyo kanuni zinavyotuongoza Mhe. Waziri, kidogo kauli yake angeirekebisha.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu huu Wimbo wa Taifa umekuwa wa muda mrefu, huu mwaka sasa, bajeti ile iliyopita nilizungumza suala hili, leo ananambia nisubiri mtu kutoka Kuwait, hakufika, ushahidi wa katika chombo hiki *DNA* imo kwenye meli Mheshimiwa, wewe ni shahidi, ndio nikasema pale nataka kauli ya Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha yuko makini na serikali hii, shilingi 400 bilioni wananchi wetu wamechagua Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi iko madarakani wanapata shida, wakifika pale katoka shamba anakwenda zake Al-Rahma kupima, iliyokuwepo hiyo ya *mobile* inatakiwa ipige picha 20 tu ikisha basi, inafosiwa kupiga picha 80, huoni ila unaona mawingu tu. Nataka kauli ya serikali, kwa hili niko tayari hata kupiga kura, kwa hili si langu, si la baba yangu, si la mjomba wangu, ni la wananchi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mweyekiti ahsante sana, kwa kanuni hiyo aliyoitaja Mhe. Jaku, kwamba swali linaweza kujibiwa na waziri mwengine tunaoamua ni sisi, huyo waziri mwengine tunaoamua ni sisi, atajibu nani, haamui yeye. Hiyo kanuni alivyosoma sawa sawa lakini kaitafsiri sivyo, tunaoamua ni sisi au wewe Mwenyekiti, unayo ruhusa ya kuamua kwenye kiti hicho. Kwa hiyo, naomba nimrekebishe kwa kanuni hiyo pia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri tumetoa amaelezo ya kutosha tuna *free option* za *X-ray*, bila ya kugusa ile shilingi 7.5 bilioni kuna *free option* za kwenye *X-ray*. Nimetoa *option* ya shilingi 32 milioni kwa ajili ya kutengeneza *fluoroscopy* ya *X-ray* hiyo tuliyokuwanayo, tumetoa *option* ya mradi wa *ORIO* ambayo inataka kufanyika, tumetoa *option* ya *BADEA* Kuwait, Saudia, tumetoa na *option* ya Pemba pia kwa Hospitali ya Abdalla Mzee. Sasa watendaji wangu wamenileta ki-*note* sasa hivi hiki hapa, katika mradi wa *ORIO* vifaa vyao sisemi kama hiyo *DNA*, aa, vifaa vyao vitakuwa njiani na kufika Zanzibar mnamo mwezi wa Novemba. Narudia tena, pamoja na hiyo *X-ray* vitafika mnamo mwezi wa Novemba.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Jaku, atukubalie ikishindikana Disemba tunakutana hapa Mwenyezi Mungu atuweke hai atakuja kunisuta kama anavyosuta kwenye hayo mambo mengine, atakuja kunisuta humu humu ndani.

Naomba atuamini, atukubalie, kamsifu sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuwa ni mtu mahiri na mimi nakubaliana naye ni mahiri, atatusaidia sisi kukifikisha hiki, lakini naomba atukubalie mwezi wa Novemba na kule pia kuna mradi wa China nao kwa Pemba itafika kwa wakati na huku sisi tunaendelea na hiyo *fluoroscopy* hatudharau. Kwa sababu na sisi tuko kwa lengo hilo hilo, nikisema tu kwamba upande mmoja ndio upo kwa ajili ya kumtumikia mwananchi, upande wa pili haupo kwa kweli tunaumia sana. Nashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tumeshafahamu tunaendelea. Mhe. Jaku Hashim, tuache tuendelee maelezo ya kutosha yameelezwa na Mhe. Waziri, wala usinisomee kanuni, usinisomee kanuni, naomba ukae tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Bado hoja ya tatu, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Umeshasema mara tatu naomba ukae tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naomba tupige kura basi, maana yake hii ni mara ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, nisikilize, hii ni mara ya tatu na kwa utaratibu wetu umeshasema mara tatu, sasa niache niendelee Mhe. Waziri, ameshakujibu vya kutosha lililobakia, unachotaka wewe ujibiwe haiwezekani alivyokujibu ni sahihi yeye. Umenifahamu?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimesema mara mbili, hii ndio itakuwa ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tuache tuendelee.

Kifungu SH010302 Program Ndogo ya Sera, Mipango na Utafiti 2,542,575,000
Kifungu HH010303 Program Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Afya Pemba

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza niwasibu Waziri na Naibu wake wa Afya kwa majibu yao mazuri. Mwanzo nilipozungumza hapa nilisema kwamba Mhe. Waziri, nilimuomba kwanza kabla ya yote nisemee Hospitali ya Chake Chake aje tena kwa siri asichukue ujumbe wowote, tuje tukate mzizi wa fitina pale Chake Chake. Kwa hivyo, ratiba yake na mimi nitampangia mimi akubali hilo tu kulisema kwamba, nimpangie sio atangaze programu Katibu Mkuu hapana, nataka kukata mzizi wa fitina, mbaya nani pale Chake Chake. Hilo lilikuwa la kwanza.

Pili, nilimumba mapema kwamba nilikuwa na mradi wa kusaidia watu pale kuwa wakapimwe watu majumbani kuhusu afya zao na watoto. Pia, anaweza akanisaidia madaktari, gharama za gari naweza nikazitoa. Kwa hiyo, kama akiweza mipangilio hiyo niweze kufanya kwa jimbo langu la Chake Chake, nilisema kwa nchi nzima ikiwezekana lakini kama haitowezekana hata jimbo la Chake Chake.

Tatu, nilizungumza suala la televisheni, lakini akanambia kule kwenye wale waliokuwa akili zao zina mashaka anaruhusu, huku kwa nini haruhusu? Naomba hili anitolee ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Suala la mwisho hakukusikia vizuri, naomba urudie la mwisho.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, alitaka kutoa hadithi ya kule kwenye wodi ya watu ambao kidogo akili zao zina mashaka na nilimuomba kwamba Chake Chake tutaweka televisheni kwenye ile wodi, akasema hatoruhusu baadhi ya maeneo isipokuwa kama Kidongo Chekundu. Sasa huku kwengine sijui kakwama kwa nini au kuna tatizo gani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana ndugu yangu Mhe. Suleiman Sarahan Mwakilishi wa wananchi, wenyewe wanamwita Meya. Kwanza kabisa anajua yeye mwenyewe kwamba mimi kwake yeye ni mwepesi sana, kwa hiyo, hilo la kwanza nimelikubali bila wasi wasi wowote. Na nitaomba siku hiyo niende mimi na yeye na Naibu Waziri pia tumchukue pamoja. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, kuhusiana na huduma za kwenda kupimwa nyumbani, hizo tunazo na tunaendelea nazo zinaotwa *Outreach Programme*, ni yeye tu anatakiwa apange na Afisa wake wa Wilaya ama Ndugu Mkasha ambaye yuko hapa Afisa Mdhamini, akishapanga naye atampangia mtu maalum kwa ajili ya *Outreach Programme* na yeye mwenyewe akiwepo anashiriki katika programu hiyo wanaweza kwenda kupata hizo huduma za majumbani.

La tatu, kuhusiana na televisheni. Televisheni kuna muongozo wake maalum, sio wodi yoyote tu inawekwa. Kwa sababu wakati mwengine zile zile televisheni zinatusababishia sisi kupata lawama. Kwa hiyo, naomba aseme wodi gani anataka kuweka na hizo televisheni alizokuwa kazitoa aina gani na king'amuzi gani atachagua Afisa Mdhamini yupo pale Pemba atampa muongozo sisi tutafurahi akienda kuweka kwenye wodi moja kwa moja. Kama

ukienda Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja utakuta Mapinduzi Kongwe katika vyumba vyote ziko televisheni, lakini sio kila pahala, kwa sababu kuna sehemu nyengine tunakataza na tuna sababu maalum za kiafya. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, wiki sita zilizopita nilikuweko Pemba kwenda kumtembelea m-diaspora mwenzangu ambaye ni daktari kule Pemba, nilimuomba kwa vile amechoka kukaa Ulaya akanambia narudi nyumbani kwenda kutoa huduma hii *regardless* pesa anazopata Ulaya ni nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipata bahati pia ya kuzungumza na watendaji pale Pemba yaliyojitokeza nilipochangia nilisema kuhusu maslahi ya wafanyakazi, nikamkuta mtu mmoja anafanya *internship* akanambia mimi Hassan niko hapa kuja kufanya *internship,* lakini sijaajiriwa na serikali kutoka Bara lakini tayari nalipwa shilingi 1,200,000 hajaajiriwa, akishaajiriwa atafika shilingi 1,600,000 wale watendaji wa Zanzibar wakasema ndio maana sisi tunakimbia, huyu hajaajiriwa mshahara mimi simuwezi tuna elimu sawa sawa akishaajiriwa ananizunguka mara mbili na tunafanya kazi kwa sababu ya maslahi. Kwa hivyo, na mimi nakubali, namuomba Mhe. Waziri, nawaomba watendaji wote waliangalie hili haiwezekani daktari apitwe na dereva wa Shirika la Bima, haiwezekani, aliyekaa miaka saba chuoni. Naliomba sana lazima tuwajali, kama *PBZ* tumeweza kuwapa *special package* ya mishahara hawa wanaotunusuru maisha yetu, je, lazima tuwaangalie, watatukimbia na watamalizika kutukimbia, tuwape *special package*.

Jengine hapo hapo kuhusu huduma. Kwenye kutoa *incentive* zile posho kwa ushidi kwamba Wizara ya Afya zinatolewa kwa upendeleo. Bibi mmoja anakiri kwamba mimi nina uzoefu wa siku fulani lakini ananipita mshahara mtu fulani na sote ni ma-*orderly*. Ushahidi huo ninao, wapo na wako tayari kusema. Kwa maana hiyo, naiomba wizara iliangalie hili, yote niliyoyasema nina ushahidi nayo, posho inatolewa kwa upendeleo kama unamjua mtu anakusaidia saidia unapata posho lako. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, la kwanza, naomba niseme tumelipokea na tutalifanyia kazi, lakini naomba kidogo ufafanuzi wake sijafahamu labda akili yangu ndogo. Amesema analipwa shilingi 1.2 milioni hajaajiriwa, akishaajiriwa analipwa shilingi 1.6 milioni. Sasa hiyo shilingi 1.2

milioni analipwa na nani na yeye hajaajiriwa. Ningependa kupata huo ufafanuzi sijafahamu hapo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, asikilize kwa makini sasa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaa kwanza Mhe. Waziri, alikuwa anaendelea.

Mhe. Waziri wa Afya: Mimi nilikuwa naendelea ndio. La pili kuhusu hii *incentive* hata mimi nasikia nikikaa ofisini, huyu analipwa zaidi kuliko huyu, ukimwambia mtu akuletee ushahidi wote wanaingia mitini hawakuletei ushahidi. Sasa kama Mhe. Hassan, anao ushahidi naomba humu humu ndani kama nilivyotoa ile *breakdown* ya bajeti humu humu auwasilishe kwako mimi niuchukue nikaufanyie kazi. Kwa sababu haya mambo ya *hear say* na majungu, fitna yashakuwa mengi kupita kiasi, kama lipo hilo aliwasilishe kwako mimi nitakuja kulichukua na nitakuletea matokeo nakuahidi Mwenyekiti nitakuletea matokeo mezani kwako yatafanyiwa kazi.*(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante mimi ni diaspora, sina *hear say* nina ushahidi, sina ushahidi wa maandishi nina ushahidi wa watu wako tayari kusema hayo na ni watendaji wake wa Wizara ya Afya, tukitoka hapa twende akawasikilize wanayoyasema na watamuonesha kesi, si ushahidi wa maandishi ni ushahidi wa watu ni bora zaidi kuliko wa maandishi.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, Tanzania Bara kuhusu madaktari kabla hujaajiriwa ukishamaliza *medical* tu...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa suala lako umeshajibiwa, sasa hiyo mifano ya Tanzania Bara tumemaliza hapa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kasema mwenyewe hajasikia, anataka ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Alichokitaka ni ushahidi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ushahidi tayari nimeshamwambia nitampa vipi kuwa watu wako tayari kusema, sasa hivi ni ufafanuzi.

Mhe Mwenyekiti: Ameuliza mshahara shilingi 1,200,000 analipwa na nani?

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Tanzania Bara Wizara ya Afya au Serikali ya Tanzania Bara ukishakuwa umesoma *medical* hata leo asubuhi nilikuwanaye mtu huyo kama hujaajiriwa hata Mnazi Mmoja yuko mtoto mmoja kama Mwarabu hivi yuko pale katoka huko jina lake nimemsahau, simtaji, analipwa na hajaajiriwa na Serikali ya Tanzania Bara shilingi 1,200,000; ananambia mwenyewe nikishaajiriwa niko hapa kwa *internship* tu nitalipwa shilingi 1,600,000. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Hassan Khamis Hafidh, mshahara wa Tanzania Bara na wa Zanzibar tofauti, sisi tulidhani unatoa mfano wa mtu ambaye yuko Zanzibar, lakini kama anaajiriwa Bara hilo ni suala jengine kabisa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Sasa Mhe. Mwenyekiti, ombi langu kwa hawa madaktari ili wasitukimbie, najua nchi yetu masikini, nchi yetu changa, tuwatengezee *special package* na wao ya mshahara. Kwa sababu wanatukimbia wengi na nimetoa hoja Shirika la Bima, *PBZ* wanalipwa mishahara mikubwa basi ije kuwa hawa wanaonusuru maisha yetu!

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Hassan, tunaifahamu na tunaielewa, lakini ajue tu kwamba kama kuna kada hapa Zanzibar ambayo inapata malipo mazuri na iliyopewa *priority* ni kada ya madaktari kuliko kada nyengine yoyote. Kwa sababu kazi zao zinaeleweka na zinaheshimika, lakini pia kuna utaratibu wa miundo ya utumishi hatuwezi kutoa mishahara kwa sababu ya kupendelea. Pia, haya mashirika hivi sasa tayari utaratibu wake umeshabadilika, zamani ilikuwa hivyo anavyozungumza walikuwa wanapeana wanavyotaka wenyewe maposho, wanafanya wanavyotaka; mashirika kama *PBZ, ZSTC, ZRB* na mengineyo, lakini sasa hivi Kamisheni ya Utumishi wa Umma tayari imeshaandaa utaratibu maalum wa kuyaweka mambo hayo yote katika utaratibu mmoja wa aina moja, hata hayo maposho sasa hivi yanakuwa yanaratibiwa kwa pamoja na kujua kwamba kuna utaratibu gani unaotumika kiserikali ili kusiwe na tofauti kubwa kama hizo ambazo zipo.

Kwa hivyo, hili jambo la maposho nalo vile vile tunaliangalia kwa sababu Kamisheni tayari imeshaangalia na tusiwe na wasi wasi haya mambo yote yameshaangaliwa tangu mwaka 2011 na bado Kamisheni inaendelea kuyafuatilia zaidi ili kuweza kutoa taarifa kamili na hatua za kufaa zichukuliwe kusiwe na tofauti hizo.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante namshukuru waziri husika kwa ku-*acknowledge* kwamba hili suala lipo na wanalifanyia kazi.

Lakini mimi nimewaombea wale wanaonusuru maisha yetu na hoja ipo, ushahidi upo kwamba mashirika yanapata pesa nyingi kuliko daktari haipendezi, inawavunja moyo ndio maana wanatukimbia.Ninalosema mimi tuwaongezee ili wasitukimbie. Ahsante.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupata fursa hii ya kuweka pingamizi niliyokuwa nimeweka. Katika kipindi cha maswali na majibu nilitaka kujua kuhusu *X-ray* iliyoko Micheweni ambayo imefungwa takriban muda wa miaka mitatu ambayo haijafanya kazi. Vile vile, leo katika kuchangia kwa maandishi pia nilitaka kupata ufafanuzi juu ya majibu ambayo yalitolewa kwa kipindi kile ambacho kilikuwa ni cha maswali na majibu, nilitaka tena kujua ufafanuzi kwa vile sasa hivi Waheshimiwa wengi kila anaesimama analalamikia jinsi ya kwamba kukosekana kwa vifaa tiba ikiwemo miongoni mwa *X-ray*.

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri, anipe ufafanuzi juu ya kina katika hatima ya *X-ray* ilioko Micheweni kwamba tayari imeshafanya kazi kama alivyosema ama kama haijafanya kazi ni lini itaanza kufanya kazi ili wananchi wa Jimbo la Micheweni na maeneo mengine ya wilaya waweze kuendelea kupata hii huduma ambayo wanaihitaji. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Shamata Shaame Khamis, kwa ufatiliaji wake wa karibu sana na Mheshimiwa Mwengine ni Mhe. Omar Seif Abeid, ataniwia radhi kaniletea masuala mengi sana kwenye masuala haya haya pia lipo yeye ndie Katibu wa Kamati ile ya pale kuhusu masuala ya Afya pale Micheweni.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili suala la *X-ray* kwa kule tatizo lake kidogo ni tofauti kule ni *Human Resource*, tunatafuta *staff* wa kupeleka ambaye ataweza ku-*operate* mashine, yaani anahitajika *radiologist* na hiyo ni *profession* kama nilivyosema awali ni *rare profession*. Kwa hiyo, tumo katika hatua za mwisho za kumpata *radiologist* ambaye tutampeleka pale Pemba na ataweza kuwa *situated* pale. Kwa sababu pale pia tunagenga *theater* mpya ya kisasa ambayo pia itakuwa inatoa huduma kwa kutumia mashine hiyo hiyo.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Shamata Shaame, atukubalie atuvumilie tunamtafuta huyo tukishampa kijana huyo na vijana wetu wengi wako masomoni kwa ajili ya masomo haya tutakwenda nae tu.

Pili, namuhaidi tukienda na Mhe. Suleiman Sarahani, siku hiyo ili iwe nzuri zaidi na yeye kwake tutakwenda kipindi hicho hicho. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Shaama Shaame Khamis: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe masikitiko yangu kuhusiana na majibu ambayo amenipa Mhe. Waziri, ambayo siku ya kipindi cha maswali na majibu niliambiwa kwamba huduma ile inafanyakazi na kuna baadhi ya siku ambayo kuna daktari anakwenda kule kutoa huduma. Lakini leo napata jibu jengine kwamba sasa anatafutwa mtaalamu.

Naomba sana Waheshimiwa, wanapokuwa wanatujibu maswali yetu kwa vile na sisi tunatekeleza majukumu ambayo tumepewa na wananchi wetu, basi naomba majibu yaende katika muelekeo uliokuwa sawiya ili na sisi kuepusha kuwaambia majibu ambayo hayako sawa.

Kwa hiyo, mimi nimuombe tu Mhe. Waziri, hiyo juhudi ambayo amesema kwamba anaifanya aendelee kuifanya ili wananchi waweze kupata huduma kule. Sina la ziada mimi nasema tu tuendelee.

Kifungu kidogo SH010303 Programu ndogo ya kuratibu shughuli za afya Pemba	7,798,150,000
Jumla ya Fungu	**3,768,731,000**
Jumla Kuu	**59,228,555,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Kifungu H0201 Kitengo cha Uongozi na Utawala	1,014,300,000
Jumla Kuu	**1,014,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PH0201 PROGRAMU YA HUDUMA ZA UCHUNGUZI NA MATIBABU
Kifungu SH02

Mhe.Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli si kawaida Mwenyekiti kupiga budi. Lakini mimi nimesimama kwa ombi maalum kabisa kwa Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla. Kwa kweli tulipotembelea Maabara ambayo ndio inayotoa huduma za uchunguzi tumekuta zinavujiwa sana. Tumekuta kwa kweli dari linaanguka, nondo zinaonekana tena kwenye vifaa vya *saver* pamoja na kule *clinical chemistry* na *Proctology*.

Namuomba sana Mhe. Waziri na serikali katuhakikishia Mhe. Waziri, kwamba kunakuja msaada mkubwa wa Kuwait. Lakini hivi sasa kunavujiwa na saruji inaanguka, baadhi ya hiyo *saver* imefunikwa hasa kuna *plastic* limefunika. Kwa hiyo, ninachoomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, anasikia.

Naiomba sana serikali iwapatie fedha lile paa lifanyiwe ukarabati wa haraka sana, ikija mvua za Vuli na kishindo chake litaporomoka lile paa na hasara tutapata zaidi ya Maabara ambayo kwa kweli inafanya kazi nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina ombi hilo tu kwa serikali. Nashukuru tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Afya na Elimu kwa *Intervention* yake hiyo. Kwa kuwa yeye tunamuheshimu sana na ni *senior member*, ameshakuwa *formar Minister of Health,* tunalipokea na tutalifanyia kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa nikichangia nilimuuliza Mhe. Waziri, juu ya kadhia kubwa tunayoipata juu ya matumizi mabaya ya *pampas*. Jambo ambalo huko nyuma wazee wetu walikuwa wakiwafunga watoto nusu nguo zile vipande vya kanga au nepi. Lakini sasa hivi wazee wanawafunga watoto *pampas* jambo ambalo wanarundika kinyesi, mikojo humo humo, mtoto anakaa nacho mpaka kufikia masaa 24, zikifunguliwa *pampas* zile zinawekwa kwenye ndoo mbovu au vipolo anasubiriwa Bwana Taka apite achukuwe, nzi wanaanza kuchukuwa, kuku wanapekuwa, pana ng'ombe anatafuta malaji.

Sasa nimuulize Mhe. Waziri, je, anawambia nini wananchi ambao wanatusikiliza juu ya kadhia hii ya *pampas* kupigiwa karantini ukizingatia inaendeleza maradhi ya mripuko ya kuharisha na kutapika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Ahsante sana namshukuru sana Mhe. Ali Bakar Khamis (Doholo), Kwa suali lake zuri sana. Mwenyekiti, naomba niseme katika Wizara ya Afya tulikuwa na mdahalo mkubwa sana katika kipindi kile tuko katikati ya Kipindupindu ya kwamba, tupige *pampas* marufuku au tusipige, tukawa tunajadiliana tuweka zile faida na hasara. Kwa sababu *pampas* nazo zina faida yake, kwanza wale wana-*import* wanalipa *tax* katika serikali moja kwa moja na kadhalika.

Lakini tatizo lake kubwa kabisa zikishatumika vipi tunatumia njia gani ku-*dispose* na tunajua sasa hivi wanawake wameshatetewa sana katika jamii wengi wanafanyakazi, wanakwenda maofisini. Kwa hiyo, pia nazo zile *pampas* zinawasaidia.

Zamani mimi nakumbuka mama yangu mzazi yeye yuko nyumbani toka nazaliwa mpaka nakuwa mkubwa yeye yuko nyumbani tu, kazi yake ni moja tu kulea mtoto ndio ilikuwa inatumika ile nepi ya kitambaa, ama ya kanga au ya taulo na mbele kunakuwa pini kubwa hapa inatiwa mbele, zile pini pia sikuhizi hazipatikani dukani hata ukizitafuta.

Kwa hiyo, tumejadiliana tukasema sasa hivi tukianza kutafuta pini na Kipindupindu hichi kiko katikati tutakuja kukosa pini zile za kanga zivuke iwe Kipindupindu dabali moja mara mbili iongezeke. Kwa hiyo, tukasema tusiende moja kwa moja kupinga vita *pampas,* tunachotakiwa sisi kufanya na naomba nimshukuru sana Wizara ya Mhe. Haji Omar Kheri na kumshukuru sana Mkurugenzi wa Manispaa pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri na Mazingira pamoja wameanzisha yale madepe ya taka yako sehemu mbali mbali ambayo sasa hivi wanafanya ile *collection point,* hata mjini hata Hospitali wamekuja nayo, yale ni ya *ZMC* na yameandikwa *ZMC.*

Tumeomba kwamba ni njia nzuri ni kutafuta pahala pa ku-*dispose*. Sasa tatizo lililokuweko huko maeneo ya Daraja Bovu na Mtopepo na kwengineko huko bado zinakuwa zinazagaa. Huko pia tutaanzisha programu ya kuhakikisha kwamba kwenye ile ile *Wash Programme* tunanzisha programu ya kupeleka mapipa maalum ya kutupia taka pamoja na yale mapipa ya Manispaa. Kwa hiyo, hapo itakuwa haina tatizo.

Lakini tukirudi kule kwenye kanga au kwenye nepi ya taulo ile tutakuja kupata matatizo kwa wakati huo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakari(Doholo): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri na majibu yake mazuri. Lakini tusimtafute mchawi, wachawi tutakuwa ni sisi

wenyewe. Lakini vile vile pesa ni kitu kizuri sana lakini tujue kwamba pesa ni kwa ajili ya kuingizia serikali mapato. Lakini tujue kwamba tunanunua vifo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kadri unavyopita kwenye mitaa basi unakuta marundiko ya ma-*pampas*. Jambo ambalo unaweza kutishika, *hish! pampas* zile sio tupu mna vinyesi. Sasa hebu hili pamoja na majibu yake mazuri aliangalie kwa kina, maradhi bado yapo.

Mimi pale zamani nilikuwa naona maradhi haya yanaingia sana Shamba kutokana na kwamba watu wa Shamba hawana vyoo. Lakini sasa hivi yakianza maradhi basi yanaanza Mjini kwa sababu ma-*pampas* na vinyesi yamechanganyika. Ahsante tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa Mhe. Rais, aliagiza kuwa huduma za wazazi ni bure. Sababu gani mpaka juzi wananchi wakafika pale Mnazi Mmoja wakachangia huduma na huwezi kumchukuwa mtoto wako kama hujapeleka chupa ya *JIK,* ndio maana Mhe. Waziri, akajisi ana *JIK* nyingi za kutosha.

Hebu awaeleze wananchi wapate kufahamu sababu gani ukanunue *drip*, ukanunue *cellular* wakati huduma Mhe. Rais, katangaza bure, hamuoni mnakiuka amri ya kiongozi wetu Mkuu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na namshukuru pia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwa suali yake hilo alilioliuliza katika kitengo hichi cha Mnazi Mmoja.

Ni kweli kuna agizo hilo la Mhe. Rais na ni kweli huduma hizo kila zinapokuwepo sisi hutoa bila ya malipo na juzi siku aliyokwenda yeye, baada ya kutoka yeye nikaingia mimi kwa bahati nzuri nilikuwa na kikao pale na madaktari na aliyoelezwa yeye na mimi nikaelezwa na alienieleza naomba nimtaje ni Bi Tatu Fundi, kwamba pale wagonjwa huambiwa walete pale tu inapokuwa fedha zimechelewa na vile vifaa vimekwisha, ndio wanaambiwa kwamba naomba ulete mpira uje na *JIK* yako.

Lakini panapokuwa na huduma hizo basi huendelea sisi kutoa kama kawaida. Hili hufanyika pale tunapokuwa tumechelewa kupa *other charges*, ama pesa haikutosha kwa huduma za Mnazi Mmoja au kumetokezea *emergence* nyengine ndio huwambiwa walete wao. Hakuna hata mmoja na hili nimethibitishiwa hakuna *staff* hata mmoja anaepokea pesa moja kwa moja kutoka kwa mgonjwa kwa ajili ya kuchangia huduma hizo.

Hilo naomnba tuwapongeze *staff* wetu wanafanyakazi vizuri sana, wanafanyakazi kwa umahiri sana madaktari wetu na manesi wetu wote wanafanyaka wakati mwengine kazi katika mazingira ambayo sisi tunatakiwa tuwapongeze wao, si kuwavunja moyo wala kuwashambulia mara kwa mara na si vizuri kuwataka wao kwa sababu wao hawawezi kuja hapa kujibu maswali hayo.

Naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, atukubalie pale tunapokuwa na kasoro wagonjwa huombwa wachangie na wachangie kwa *JIK* huwa wanaleta na si mara nyingi, kasoro hizo hutokea siku mbili tatu. Najua analalamika anataka kuongezea kulifanya liwe kubwa, lakini tuwahurumie na wale wanaofanya kazi kule. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwa kukiri hicho kitu kakiona na kipo. Lakini nilipokwenda mimi nilimkuta anatoka Shamba hata viatu hana na salama katika zile kazi zangu na huruma yangu na imani yangu ikabidi nijipapatue kujipapasa mfukoni kama haipo angeambiwaje.Maneno mazuri Mhe. Mwenyekiti, ukizungumza ni sadaka. Niombe tu wakunga wawe wanaendelea na maneno mazuri kutoa kwa wauguzi wetu. Maneno mazuri ni sadaka.

Lakini Mhe. Waziri, hili maneno yetu ya kisiasa hili suala si la juzi wala jana lipo linaendelea, sema tu ukiri kuwa hili suala lipo lakini pale ukienda humchukuwi mtoto kama hujatoa *JIK*, hiyo *drip*, *cellular* kitu chengine. Lakini *JIK* lazima uweke, utakuwa tayari mimi nikuthibitishie nikuletee hicho kitu na utakuwa uko tayari kujiuzulu kama sijakuthibitishia hivyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama niliposema hapo awali mamlaka ya kututeuwa sisi na mamlaka ya kutuondoa yapo kwa Mhe. Rais, yeye mwenyewe ambaye anaangalia kila tunachokifanya hapa. Mhe. Rais, anaona nani anafanya nini na nani anauliza nini na nani anae-*dramatize the situation* na nani anekejeli anaonekana.

Mimi naomba niseme hivi Mhe. Mwenyekiti, sisi tunafanya wajibu wetu kwa kadri Mhe. Rais, analivyotuteuwa na tunatimiza wajibu wetu na tumemuahidi, jana mimi nilitamka hapa kwa kauli na nimemuweka Mwenyezi Mungu mbele kwamba tutaendelea kutimiza malengo yake kwa kadri ya Mwenyezi Mungu na tumeshika msahafu mbele yake. Kwa hiyo, tusi-*dramatize* kwenye masuala hayo.

Suala hili la *JIK* hata wewe Mwenyekiti ulikuja ukatuchangia wewe mwenyewe uliekaa hapo ulikuja ukatuchangia. Ulituchangia kwa sababu gani, uliona wakati mwengine kunauwa na mapungufu umekuja pamoja na kina mama UWT Umoja wa Kina mama wa Chama cha Mapinduzi ulishajihisha. Ule ndio moyo wa kutoa, tupeane moyo na mimi hivyo hivyo ninapokuwa nacho sitaki kukitamka kila saa. Kwa sababu mimi nimeshachaguliwa waziri katika Wizara hii ni wajibu wangu ninapokuwa nacho na mimi nakitoa. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, pia na yeye anachangia, kila mmoja wetu anachangia kwa njia moja au nyengine.

Sasa hii tuki-*dramatize* katoka mtu kutoka Shamba hata viatu hana pale ziko *spares* mimi sitaki kusema mengi lakini ziko *spares* tunaweka za kuwasaidia watu wa namna hiyo. Kuna Afisi yetu pale ya Ustawi wa Jamii kuna *staff* wawili ambapo juzi nimezungumza nao tunaweka *stoke* ya aina hiyo. Si kila mtu anachajiwa, haachwi mtu akatike roho kwa sababu kitu hamna hatufanyi hivyo, kwanza kwa Muislamu hiyo ni dhambi kubwa sana.
Kwa hiyo, naomba tu wale madaktari wetu na wauguzi wetu tuwape moyo, naomba sana, kila tukiwapa moyo wale ndio wataweza kufanya uzalendo zaidi. Tayari wale wameshakuwa wazalende na sisi huku tunaendelea kuwadunda zaidi. Sasa unawavunja moyo kwa ufupi. Kwa hiyo, mimi naomba sana tuwape moyo, wanafanyakazi vizuri, wanafanyakazi katika mazingira ambayo sisi sote tunayaelewa, tuliokuwemo humu sisi sote tunayaelewa, mwenye pesa zake haendi pale kuzaa, anakwenda kwengine tuambizane ukweli, pale wanaokwenda ni hao hao tunaowazungumzia hapa wakulima na wakwezi na sisi tunawatumikia wao na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatupa nguvu zaidi sote kwa pamoja kuwatumikia wao zaidi. Naomba hilo tukubaliane.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, anachokizungumza huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani. Lakini nafikiri alichosema kwamba *nurses* wetu tuwape maneno mazuri, lakini na wao vile vile watoe maneno mazuri. Wanafanyakazi ngumu kwa kweli, tuwashukuru nakubaliana na wewe na tuwape moyo kweli.

Lakini narudia tena maneno mazuri ni sadaka mngewafahamisha tu wale, aaah! subirini utafanyiwa utaratibu gani. Lakini mtu ungemkuta ungelia machozi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Khamis Hafidh, tumeshamaliza wachangiaji watatu. Kwa hiyo, huna nafasi tena sasa hivi.

Kifungun kidogo SH020102 Programu ndogo ya Huduma za Matibabu 563,685,000

Jumla Kuu **563,685,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Mhe.Mwenyekiti: Kwa hiyo, Mheshimiwa, umechelewa, kifungu kimekubalika.

Kifungu PH0202 Programu Kuu ya Uongozi na Utawala
Kifungu SH

Mhe. Mwenyekiti: Mbona nimeona wengi halafu wengine wamekaa? Mhe. Ali Salum, nitampa Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na kama alivyotamka Mhe. Naibu Waziri, wakati anatoa majibu yake kwamba mimi nilikuwa nimezungumzia masuala mawili tu; Moja lilikuwa ni lile la wanafunzi, lakini la pili ni banda la kupumzikia watu wa kusubiri kwenda kutizama wagonjwa, ama mtu kama amepata huduma lakini hawezi kurudi nyumbani anatakiwa akae pahala asubiri familia ije imchukue na kumrejesha nyumbani.

Sasa niliyasikia majibu ya Mhe. Waziri kwamba, wameanza taratibu za kujenga vyoo na wametengeneza ma-*benches* kwa ajili ya watu kupumzikia. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hoja hii mara nyingi tulikuwa tunapiga kelele mimi na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Na mimi tangu nilianza katika masuala ya kawaida baadae nikawa ninatoa michango katika maeneo mbali mbali ya kibajeti na katika taarifa za Kamati.

Kwa kipindi chote cha miaka mitano. Sasa leo majibu ya Mhe. Waziri, alimwambia Mhe. Jaku, ameshamwita sana lakini hajenda ili kwenda kuzungumzia banda hili. Mimi ninataka kutoa masikitiko, sipendi sana kutumia lugha hii Mhe. Mwenyekiti. Kama kwamba tutaendelea kumsubiri Mhe. Jaku, serikali inamsubiri Mhe. Jaku, ndiyo aende Wizara ya Afya wakazungumze banda lijengwe hatuwatendei haki wananchi. (*Makofi*)

Na kajitetea zaidi kwamba anajenga vibaraza. Mimi masuala yangu yote na miaka yote ninazungumzia hali ya hewa mvua. Kukaa katika vibaraza na mvua athari zake zipo tofauti. Mtu anasubiri katoka Shamba, huyo mkwezi na

mkulima ambaye kaka yangu Hassan aliyemuona, anakuja kutizama mgonjwa amefika mapema.

Juzi tumemaliza mvua zilikuwa kubwa hapa, mafuriko kila pahala. Mtu baada ya kwenda kutizama mgonja, yeye mwenyewe atapata maradhi kutokana na mvua kama *Ammonia* na maradhi mengine kusubiri muda wa kutizama mgonjwa, nafasi inakuwa hamna.

Mhe. Mwenyekiti, na katika majibu yake ya miaka yote mitano kwa Mawaziri wote wawili waliokaa na Manaibu Mawaziri waliokaa. Mimi huko nyuma nilikuwa ninafikiria labda yeye Juma Duni na yule mzee wangu Seif labda nilikuwa nahisi wanafanya *sabotage* serikali makusudi, nilikuwa na wasi wasi huo mkubwa sana. Kwa sababu walikuwa kila siku wanapiga danadana. Mwanzo walikuja na *concern* kwamba Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe anawazungusha kuwapa kibali.

Babu Duni hapa alipiga kelele sana. Baada ya kupata kibali tukaambiwa mambo yote yameshakuwa tayari. Yeye Mheshimiwa, kwa leo anasema aah! mimi nina miezi mitano tu, ulikuwa Naibu Waziri katika Serikali hii hii ya miaka mitano iliyopita. Kila jambo unalifahamu, ukaja na maramani hapa, ukatuonesha kama tupo kwenye *TV*. Maramani tayari baada ya kipindi kifupi banda litajengwa, Mhe. Ali, tulia na mimi nikatulia.

Leo anasema anamsubiri Mhe. Jaku. Mimi ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, sitaki kusema sana, ninaiamini serikali, serikali ninajua ni sikivu, ina uelewa na ina uchungu na wananchi wake. Watutafutie taratibu za kuweza kujenga banda lile katika haraka ili tuwaondoshee wananchi wa nchi hii matatizo katika nchi yao. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji, mnadhimu wangu kwa heshimu zote. Kwanza ninamrekebisha mimi nimeteuliwa na Mhe. Rais mwaka 2014 kuwa Naibu Waziri.

Kwa hivyo, sikuwepo hapa miaka mitano. Naomba hiyo kauli kidogo irekebishwe. Katika Unaibu Uwaziri wangu nilionesha ramani mara moja hapa kweli na katika hiyo kuonesha ramani mara moja bajeti tumeitafuta na *priorities* zetu ni kubwa, huwezi kuacha *priority* ya dawa ukenda kuchukua *priority* ya muuguzi kumfunika mvua. Ki-*priority* ile inakuwa ina uzito zaidi kuliko hii. Tumefanya jitihada zetu wenyewe, tumefika hapo tulipofika na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha tutajenga banda, tutamaliza. Sasa

hivi mimi nimeapishwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 9 Aprili. Nimesema kweli kabisa zile rekodi zipo *right* na ukitaka cheti changu cha kuapishwa nitakileta hapa kuwa tarehe 9 nimeapishwa Aprili mpaka leo Juni.

Kwa hivyo, tumekuta *priorities* chungu nzima, tumekuta mambo yapo mengi sana. Hivyo, katika kipindi cha Unaibu hilo nimeweza kufanya na nilihamasisha na hili la Mhe. Jaku, mimi sijasema kwamba serikali nzima tumekaa kitako tunamsubiri Jaku aje kwetu, aah! Nimesema yeye huyo Mhe. Jaku, kasema anataka kuja kwetu mara chungu nzima kishasema, mbona hajaja na milango yetu ipo wazi, ndiyo nilivyosema hapa. Sijasema kwamba serikali inamsubiri Jaku. Serikali haiwezi kumsubiri Jaku mmoja. Serikali katika nchi yake ina Jaku zaidi ya elfu moja, wapo sehemu mbali mbali. Kwa hivyo, sijasema hivyo. Kwa hivyo, ninachoomba mimi bado hatujakuwa *allocated* katika bajeti kwa ajili ya banda. Hii tunafanya *initiatives* zetu wenyewe. Kuna wasamaria wema ambao hawataki kutajwa wanatoa vitu mbali mbali. Sadaka zao, zakka zao wanatoa pale ili kumfunika mtu hapa duniani, yeye apate kwenda kufunikwa Akhera. Kwa hivyo, hichi wanatoa wao kama mchango wao wenyewe. (*Makofi*)

Kwa hivyo, ndiyo maana tumeanza na *garden*, tumejenga na hodhi la maji, tumeshapata *pipes*, sasa hivi tunajengewa ma-*benches* yale. Leo piteni mutaona kuna *benches* zinajengwa. Tunakwenda kwenye vyoo, tunamaliza Ndugu Issa Sariboko tushakuja naye kufanya ziara pamoja Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe, tushakuja na Ndugu Serenge wameshatupa miongozo nini tufanye ili tusivuke kwa hicho hicho kidogo tulichokuwa nacho cha kwetu wenyewe tusivuke zile sheria.

Yaani tusivunje Sheria za Mamlaka ya Mji Mkongwe. Kwa hivyo, naomba mimi sana kama Waheshimiwa wanataka kuchangia, wasichangie kwa mdogo au kwa maneno.Tutie mkono mfukoni tuchangie.Kama wachangiaji wa kweli, tuchangie na zisiwasilishwe kwetu sisi, ziwasilishwe kwako wewe Mhe. Mwenyekiti, hapo ili iwe na rekodi kwenye Baraza. (*Makofi*)

Kwa hivyo, naomba hili niliweke wazi, kidogo limenigusa kwa sababu nimekuwa ninahamasisha wengi. Kama vile nilivyokuwa nikihamasisha wakati wa Kipindupindu watu wametuchangia maji, wametuchangia biskuti, mulikuwa mukiona kwenye *TV* siku zote wamejitolea. Na wote wale watu hamsini na tano nimewaandikia barua ya kuwashukuru mimi mwenyewe kwa saini yangu nimewapelekea na wamefurahi, wengine hawajawahi kushukuriwa hata siku moja. Na sisi tunajua kushukuru. Kwa hivyo, *stage* hii tuliyofika tunamshukuru Mwenyezi Mungu na tunawashukuru wale wote waliotusaidia. Kama wasemaji

kweli leo kwa ajili ya wananchi tushirikiane tutoe chochote tutafika pale lile banda tutajenga wenyewe, hatuna haja ya Jaku wala Mzee Hashim Ayoub mzee wangu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ninasema kelele zangu kubwa sana kwa serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, ina nidhamu kubwa sana. Lakini kuna vitu lazima tukiri kwamba *we are not serious about this*. Ninasema jambo hili nililiibua kwenye masuala ya kawaida. Nikaja kwenye ripoti ya Kamati, nikaja kwenye bajeti, *Hansard* zipo miaka mitatu na majibu kila siku yanabadilika.

Mhe. Mwenyekiti, jibu la mwanzo kama Mhe. Waziri, anakumbuka ilikuwa ni mvutano baina ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mamlaka ya Mji Mkongwe, na sote tukawa tunamlaumu Mhe. Sariboko, ikifika pahala pande hizi zikaafikiana. Hilo suala la kujenga katika mandhari ya Mji Mkongwe tukakubaliana.

Tukaja katika jawabu la pili ramani bado. Ikaletwa ramani hiyo ambayo Mji Mkongwe wameiridhia. Katika majibu yao kuna kipindi kukawa kuna tatizo nikawaambia kwamba ilikuwaje vibanda vilivyokuwepo pale vimepata mamlaka ya kujengwa, tushindwe kujenga banda la kupumzikia. Mazungumzo yalikuwa makubwa, mivutano ilikuwa mingi.

Awamu iliyopita imemalizika chini ya Mawaziri wawili, Manaibu wawili. Na yeye akiwa katika kipindi hicho kilichopita alikuwa Naibu Waziri analifahamu na akaja na ramani. Kama hatujawa tayari. Sasa kama anatwambia sasa hivi kwamba hizo *priorities,* kwa lugha nyengine vipaumbele madawa. Madawa mpaka tutakufa itakuwa kipaumbele na wananchi nao kupata huduma bora waepukane na maradhi, pia ni kipaumbele. Tutafute namna mimi ningemwambie hivyo.

Sasa ameleta namna ya kuturejeshea sisi. Niliyesimama hapa ni Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani na Mnadhimu wa Wawakilihi wote wa CCM. Mimi ninataka kutoa kauli tukubaliane hapa Mawaziri wachangie milioni, milioni, *back benchers* laki tano, laki tano tukajenge banda. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kukushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Ali Salum Haji na nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka kusema kwamba Sera ya serikali na dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kutoa huduma za afya bila ya malipo. Kwa msingi huo hapo hapo na utaendelezwa na ndiyo dhamira yetu kuu. (*Makofi*)

Hivyo, ninataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza hili na wananchi wote kwamba serikali yetu itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa huduma za afya zinapatikana bila ya malipo, ili wananchi wetu waweze kupata matibabu yaliyo sahihi. (*Makofi*)

Ninataka nimuhakikishie Mhe. Ali Salum Haji na Wajumbe wa Baraza hili kwamba banda lile pale, serikali itachukua hatua na litajengwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu. Na mtu yeyote ikiwa Wajumbe, Mawaziri kama wataamua kuchangia mikono yetu ipo wazi, fedha hizo zitapokewa kwa ajili ya mchango. Ninataka kuhakikishia kwamba serikali italijenga ili kuwaondolea bughudha wananchi wanaokuja kupata matibabu katika hospitali yetu.(*Makofi*) Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais na mimi tangu mwanzo nimesema kwamba serikali yangu ninaithamini, Rais wangu ninamthamini hata chama changu, na ndiyo maana mukanipa heshima hii kubwa sana, sina tatizo na hili.

Nitaipa muda serikali lakini naomba jitihada ziendelee, lakini pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza mwisho wa mwezi huu unaopita, maana yake huu mshahara umeshaingia ninafikiri. Basi ninaliomba Baraza likate laki tano nianze mchango huu, ninafikiri na wenzangu watafuatia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana tunakupongeza sana Mhe. Ali Salum Haji. Nilimtaka kwanza Mhe. Abdalla Maulid Diwani, baadae Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Katika mchango wangu nilizungumza kadhia nzima wanaopata baadhi ya wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Na hili Mhe. Waziri, wakati anafanya majumuisho yake hajanipa na bahati nzuri hili suala Mhe. Waziri, tushalizungumza naye chemba nje ya Baraza na hii leo nimelileta hapa Barazani.

Naomba anipe ufafanuzi mzima juu ya ile kadhia ambayo niliyomwambia kuwa baadhi ya watu wananyanyasika kutokana na imani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kuja nalo hilo. Bahati nzuri kweli aliniambia nje chemba na mimi nimezungumza na watendaji wangu, pia nimezungumza na Mwanasheria wa Wizara.

Tunaomba tu atuwasilishie ushahidi ili waufanyiekazi, tupo tayari kuufanyia kazi. Lakini atuwasilishie ushahidi kwamba fulani analipwa zaidi kuliko fulani na fulani analipwa zaidi kwa sababu yeye siyo CCM na huyu ananyimwa kwa sababu yeye ni CCM.

Akishatuletea tu yale majina, sisi wenyewe tutafanya kazi, kuna kamati ya uchunguzi ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuna Kamati ya Maadili, kuna Kamati ya Nidhamu itafanya kazi yake mara moja na matokeo pia naye tutampa apate kujua nini kinachoendelea.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri ulienda nje ya mada, sivyo nilivyokwambia hivyo. Nilikwambia juu ya kadhia nzima ya uhamisho. Ninafikiri ndiyo suala lenyewe, siyo suala la malipo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Masuala yenyewe yalikuwa mawili; Moja lilikuwa la malipo linaweza likawa limetokea kwake yeye au Mjumbe mwengine, kwa sababu nilisema michango ni mingi sana. Moja lilikuwa la malipo kwamba mmoja analipwa zaidi kuliko mwengine.

Na la pili, hilo la uhamisho anaondoshwa mtu kwa ajili ya kuadhibiwa na la tatu, lilikuja kwa ajili ya *mental*, kwamba mtu akipelekwa *mental hospital* kufanya kazi, ina maana ni adhabu ya aina fulani, amepelekwa kwa ajili ya adhabu. Sasa yote hayo Mhe. Mwenyekiti, yanahitaji ushahidi kwa sababu sisi

tuna Kamati yetu wenyewe ndani ya wizara ya mambo ya utumishi ambayo mwenyekiti wake ni Ndugu Kombo Mkurugenzi wa Utumishi na kuna Kamati za Nidhamu. Kwa sababu kuna nidhamu za madaktari, nidhamu za wauguzi. Tuna sheria nyingi sana.

Jumla ya sheria zote tulizokuwa katika wizara yetu ni sheria ni ishirini na mbili, za kwetu tu ndani ya wizara yetu ishirini na mbili peke yake. Sasa hivi vitu vyote vimo katika sheria hiyo. Tukishapata ushahidi wetu hata kama ile ya kuwasilishwa watu kama alivyosema Mhe. Hassan, watu bora kuliko *document*, tukiwasilishiwa wale pia tupo tayari kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo, tunalipokea hilo pamoja na hayo mengine kabla sijaulizwa pia yote jumla yake tunahitaji kuyafanyia kazi kwa ushahidi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri, ahsante sana naomba tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla sijachangia napenda kumkumbusha Mhe. Waziri, kauli mbiu;

Ya kwanza, Mhe. Rais wa Zanzibar anasema tubadilike, tuache kufanya kazi kwa mazoea. Ya pili, Mhe. Rais, anasema Mawaziri wawajibu Wawakilishi majibu yaliyo sahihi. Kauli ya Marehemu Mwalimu Nyerere inasema, ninanukuu, "Wabunge na Mawaziri, Wabunge wanatakiwa kuihoji serikali na serikali iwape majibu sahihi Wabunge na kama haiwapi majibu sahihi wawang'ang'anie mpaka wawape majibu yaliyo sahihi, kwa sababu Wabunge na Serikali wote wanafanya kazi moja ya kuhudumia wananchi wa Chama cha Mapinduzi".(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina ombi tu, ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja maabara, *X-ray* usiku hazifanyi kazi zile sehemu muhimu za vipimo. Na maradhi yanamtokezea mtu saa yoyote. Naomba sana zile huduma zote zinazopatikana mchana na usiku zipatikane kwa sababu tunasababisha maafa yasiyo ya lazima.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Ninashukuru Mhe. Mwenyekiti, tumelipokea na tutalifanyia kazi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kifungu SS 020201 Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala
Shs.8,042,115,000/-

Jumla Kuu

Shs.8,605,800,000.-

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa hapo juu na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba niseme maneno machache sana kabla sijatoa hii hoja. Naomba niwashukuru sana Wajumbe wote waliochangia kwa moyo safi kabisa, bila ya kinyongo chochote kabisa, bila ya kuweka jambo lolote moyoni. Wananchi wameyasikia kwamba wana Wajumbe mahiri kutoka CCM ambao wanawatetea. (*Makofi*)
Watu wengi au wananchi wengi walidhania tukiwa hivi wenyewe kwa wenyewe tutakuwa *bogus*. Lakini leo Wajumbe kwa kweli *back benchers* mumetuthibitishia kwamba siyo *bogus*. Nimetoka jasho kidogo lazima niseme ukweli wangu. (*Makofi*)

Naomba niwapongeze sana *back benchers,* kwa kweli Baraza limekuwa zuri hata tulipokuwa na ule upinzani wakati ule nikiwa Naibu Waziri wa Afya, hili limekuwa zaidi linatoa jasho sana. Naomba niwapongeze waliochangia wote, lakini naomba niwapongeze sana *front benchers* Dkt. Ali Mohammed Shein hakufanya kosa, amefanya uamuzi *superb* kabisa, amepata Mawaziri mahiri, Manaibu Waziri mahiri hata nyinyi *back benchers* kidogo tunakutoweni jasho, semeni ukweli. (*Makofi*)

Naomba nimpongeze Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa chaguo lake hilo na sote tupo katika kutekeleza majukumu kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar. Kwa kweli naomba kama kuna sehemu yoyote tumekoseana au tumekwazana ama tumekwaana, tafadhalini tusamehane huu ni mwezi wa Ramadhani, lakini yote hayo tulikuwa tukifanya kwa nia safi kabisa, kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, sasa natoa hoja. Mheshimiwa, muda hatuna.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, unawanyima faida kubwa Wajumbe wako. Ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu ya Afya bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liyakubali makadirio hayo yote.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri, tayari ameshatoa hoja, niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu na michango yenu pamoja na mabuti yenu muliyopiga, lakini kama alivyosema Mhe. Waziri wa Afya, lengo ni kujenga, tupo hapa kwa ajili ya kujenga na kila mmoja ambaye ameweza kuchangia, lakini vile vile ameweza kupiga buti, kuna kitu ambacho alikikusudia na amejenga.

Kwa hivyo, na mimi niwapongeze sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mhe. Waziri na Naibu wake niwapongeze sana kwa kupitisha bajeti hii. Hivyo basi nikutakieni kila la kheri na mafanikio katika utekelezaji kwenye mwaka huu mpaka 2017. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo sasa naahirisha Kikao hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 11.20 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22/06/2016 saa 3.00 asubuhi)